

**MASOMO YA BIBLIA YA KIKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA****NAMNA YA KUITUMIA KOZI HII YA BIBLIA****SOMO:** Zaburi 19

Kozi hii imeandaliwa ili kukusaidia uweze kuielewa Biblia, ambayo ni Neno la Mungu. Biblia, ambayo pia huitwa “Maandiko”, ndio kitabu pekee kinachoweza kuaminika, kutuambia juu ya Mungu na mpango wake kwa dunia, na kwa watu wanaoishi juu yake. Inatoa ahadi ya mbaraka kwa kila mtu anayeisoma, akiwa na nia ya dhati ya kuielewa.

**Utahitaji kuwa na Biblia yako mwenyewe**

Ni fursa ya bahati kuwa na nakala ya Neno la Mungu. Ili kuifuatilia vizuri kozi hii, utahitaji kuwa na nakala yako mwenyewe ya Biblia yote (na sio Agano Jipya tu). Kama bado hujawa nayo, unaweza kupata moja kwa bei ambayo sio kubwa, kutoka kwenye tawi la karibu la Chama cha Biblia, au katika maduka ya vitabu. Karibu kila nchi ina tawi la Chama hicho. Lakini, kama hili haliko chini ya uwezo wako, tafadhali mwambie mkufunzi wako haraka; anaweza kukusaidia pengine kupata hata iliyotumika.

Masomo haya kwa njia ya Posta yana mada 60, moja kwa kila juma. Kama mkufunzi wako (mtu anayekutumia masomo haya) anaishi mbali na wewe, inawezekana kuwa utapata masomo kadhaa pamoja, pamoja na karatasi za maswali, pengine mara moja kwa mwezi. Mkufunzi wako ni:

---



---



---



---



---



---

**Kumbukumbu yako itakuwa namba:** \_\_\_\_\_

Tafadhali utumie namba yako hii kwa mawasiliano yote, kwenye karatasi za majibu, n.k.

Tunakuomba utume majibu yako yote (na maswali uliyonayo) kwa mkufunzi wako. Ingekuwa vizuri zaidi umwandikie mkufunzi wako tu, hata kama unaona kuna anwani zingine kwenye machapisho yetu.

Kama utapenda pia kutumia Biblia ya Kingereza, nukulu zilizowekwa zipo katika Biblia ya Kingereza ya ‘Authorized Version’. Yapo machapisho mengine ya kisasa zaidi, kama ‘Revised Standard Version’ na ‘New International Version’, lakini yanaweza yasiwepo katika baadhi ya nchi. Hata hivyo yoyote ile utakayoitumia, utaona haitabadilisha maana au kuathiri kujifunza kwako Biblia.

Mafundisho haya tunayatoa bure. Gharama pekee utakayoingia ni kulipia gharama ya kutuma barua yako kwa mkufunzi wako, mara moja kwa mwezi. Lengo letu ni kukusaidia wewe kufurahia kuyasoma Maandiko, na tunatamani uweze kuugundua ujumbe wa maana sana na wokovu ulioko ndani yake, kupitia kwa Bwana Yesu Kristo. Hatutoi vyeti au hati yoyote kwa kuichukua kozi hii, ila mwishoni mwa masomo haya 60 tungependa bado tuendelee kukusaidia kuendelea kujifunza Biblia yako.

**Rejea za Biblia**

‘Rejea’ kutoka kwenye Biblia itakapokuwa imetolewa, itakuwa imeandikwa ifuatavyo:

Mwanzo 1 – hii ina maana ya Kitabu cha Mwanzo, Sura ya 1.

Mwanzo 1:1-7 ina maana ya Kitabu cha Mwanzo, Sura ya 1, msitari wa 1 mpaka wa 7 (msitari wa 7 unahusika).

### **Namna ya kujifunza masomo haya**

Jizoeze kufanya mada moja kila juma. Tungeonelea uhakikishe unaiielewa kila mada, kabla hujaendelea na nyingine inayofuata. Unaweza ukaona ni kitu cha manufaa kupitia kila mada **mara tatu**. Mara ya kwanza kwa kutaka kupata wazo la jumla la kile kinachosemwa, mara ya pili kwa kuifungua Biblia yako kwenye rejea zilizotolewa, na kuandika kwa kifupi kwenye kipande cha karatasi tatizo unaloliona au swali, na mara ya tatu kuisoma tena mada yote. Ni vizuri katika hatua hii kulisoma SOMO la Biblia lilitolewa mwanzoni mwa mada hiyo.

Mwishoni mwa kila mada utaona mistari ya manufaa ya kutazama kwenye Biblia yako, na Andiko moja tunalokutaka hasa kuliweka moyoni. Utaona kuwa, mistari hii itabakia kwenye kumbukumbu yako na itakusaidia katika maisha yako yote.

Pamoja na karatasi zako za mada za kwanza utakazopewa, utapewa pia na 'Mpango wa Kujisomea Biblia wa Kila Siku', tunaouita BIBLE READING PLANNER (kwa Kingereza). Kijitabu hiki kitakupa mfumo wa namna ya kusoma Biblia, kwa kusoma kifungu kimoja **kila siku**. Kama utakuwa na utayari wa kufanya hivyo, utapata ufahamu mzuri wa sehemu zote za Biblia baada ya muda.

Unaweza kupenda kuweka Mpango wako huo ndani ya Biblia yako, kwa ajili ya kuutumia wakati wa kusoma kila siku. Hili ni jambo jema. Kijitabu hiki kina maoni kinayokupa juu ya vifungu hivyo unavyosoma kila siku; na hasa ni muhtasari wa kile ulichosoma. Kina rejea za mistari mingine ya kwenye Maandiko, na ramani ndogo ndogo na michoro, inayoweza kukusaidia katika kujifunza kwako.

### **Kujibu maswali**

Tunakutaka utume majibu yako kwa mkufunzi wako kila mwezi. Unatakiwa ujibu kwa kutumia maneno yako, usinakili tu kile masomo yalichosema. Jaribu kusema kile unachoamini mwenyewe kuwa kweli. Kama hukubaliani na chochote unachosoma, au una maswali yoyote, tafadhali sema hivyo; hili ni jambo la muhimu sana. Kumbuka, tunaweza kukusaidia zaidi kama tukiwa tunajua unachofikiri. Kama kwa sababu yoyote huwezi kutuma majibu yako, basi mwandikie tu mkufunzi wako kumwambia unapenda kuendelea na masomo.

### **Matumizi ya muda**

Kwa vyovyote, kujifunza huku kutakuchukulia sehemu ya muda wako, pengine dakika 15 au 20 kila siku kwa kusoma somo lako la Biblia, na kama nusu saa kwa kujifunza mada uliyopewa. Utahitaji pia muda wa kujibu karatasi za maswali. Hata hivyo utagundua kuwa, Maandiko yanavutia kiasi kwamba utahitaji kutumia muda zaidi na zaidi katika kuyapitia.

Soma Biblia yako kwa kuomba. Anza kipindi cha kusoma Biblia au kujifunza kwa kumwomba Mungu, ukimwomba msaada wake uweze kuelewa. Hapa kuna ombi fupi kutoka katika Kitabu cha Zaburi:

“Uyafumbue macho yangu, niyatazame maajabu yatokayo katika sheria yako” (Zaburi 119:18).

Kama tukimwomba Mungu kwa dhati, atayafumbua macho yetu na kutusaidia kukielewa kitabu chake hiki cha muhimu sana kwetu.

### **Kama hatutasikia kutoka kwako**

Tuna hakika utakuwa unaelewa kuwa, kuna watu wengi duniani humu wanaotamani kuipata kozi hii ya Biblia. Kama tutakuwa hatupati mwitikio wowote kutoka kwako, kwa wewe kututumia majibu ya karatasi za maswali ulizopata, tutachukulia kuwa huhitaji tena kuendelea kupata masomo haya, na tutaacha kuendelea kuyatuma kwako.

Kama una matatizo yoyote katika kujibu, au katika kutuma karatasi zilizojibiwa, tafadhali wasiliana na mkufunzi wako umweleze. Itakuwa ni furaha kwetu kuendelea kukutumia masomo. Tunachohitaji tu ni kujua kama yanakufikia, na umekuwa ukiyatumia kukusaidia katika kujifunza kwako Neno la Mungu.

**Kozi kamili ya Biblia:** Ifuatayo ni orodha ya mada ya kila somo, katika kozi hii ya masomo 60.

1. Namna ya Kuitumia Kozi Hii ya Biblia
2. Wakristadelfia ni Watu Gani?
3. Mwongozo Wetu Biblia
4. Injili

Karatasi ya Maswali Na. 1

5. Mungu na Uumbaji
6. Mungu Aliupenda Ulimwengu
7. Kurudi kwa Bwana Yesu Duniani
8. Ishara za Kurudi kwa Yesu

Karatasi ya Maswali Na. 2

9. Ufalme Wako Uje
10. Mungu Anavyoiona Historia
11. Ufalme wa Mungu – Amani Duniani

Karatasi ya Maswali Na. 3

12. Ahadi za Mungu kwa Ibrahimu
13. Wayahudi katika Historia (Sehemu ya 1)
14. Wayahudi katika Historia (Sehemu ya 2)
15. Ahadi za Mungu kwa Daudi

Karatasi ya Maswali Na. 4

16. Baba na Mwana
17. Maisha ya Yesu
18. Kifo cha Yesu
19. Ufufuo na Kupaa kwa Yesu Kristo

Karatasi ya Maswali Na. 5

20. Roho Mtakatifu wa Mungu
21. Karama za Roho Mtakatifu
22. Dhambi na Matokeo yake (Sehemu ya 1)
23. Dhambi na Matokeo yake (sehemu ya 2)

Karatasi ya Maswali Na. 6

24. Kwa Neema Mmeokolewa
25. Ufufuo wa Wafu
26. Hukumu
27. Uzima wa Milele

Karatasi ya Maswali Na. 7

28. Malaika

29. Ibilisi, Mapepo, Shetani
30. Ibilisi na Dhambi
31. Ubatizo

Karatasi ya Maswali Na. 8

32. Ndoa ya Kikristo
33. Matatizo katika Ndoa
34. Wajibu Wetu kwa Taifa
35. Maombi
36. Kutembea katika Njia ya Uzima

Karatasi ya Maswali Na. 9

37. Usomaji wa Biblia wa Kila Siku
38. Ushirika na Walio wa Imani moja
39. Uwezo wa Ulimi
40. Kumega Mkate

Karatasi ya Maswali Na. 10

41. Maisha ya Kifamilia katika Huduma ya Yesu
42. Tatizo la Dhambi
43. Neno la Mungu katika Maisha yetu ya Kila Siku
44. Kanisa la Mungu

Karatasi ya Maswali Na. 11

45. Tunavyowafikiria Wengine ni Muhimu kwa Mungu
46. Kumpenda Jirani Yako
47. Biblia Inavyosema Juu ya Mateso
48. Kuishi kwa Hofu

Karatasi ya Maswali Na. 12

49. Ni Sawa Kupenda Makuu?
50. Uaminifu kwa Mungu na Mwanawe, Yesu Kristo
51. Matumizi na Udhibiti wa Hasira
52. Mfuasi na Nchi

Karatasi ya Maswali Na. 13

53. Kufanya Mapenzi; tuzo ya Mungu
54. Kuchagua Mwenza
55. Vipengere kuhusu Hukumu na Ufalme wa Mungu

56. Zawadi ya Thamani Kubwa ya Tumaini katika  
Maisha yako

Karatasi ya Maswali Na. 14

- 57. Imani na Kuufanyia Kazi Ukristo
- 58. Neema ya Mungu
- 59. Muhtasari wa Mafundisho ya Biblia
- 60. Hatua Inayofuata

Karatasi ya Maswali ya Mwisho

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

### WAKRISTADELFIA NI WATU GANI?

**SOMO:** Yohana 15

Lengo la kozi hii ya Biblia ni kuelekeza fikra zako kwenye Maandiko Matakatiifu. Lakini, unaweza ukajuliza Wakristadelfia ni watu gani, kwa hiyo tutakuambia machache juu yetu.

Wakristadelfia ni jumua pana kimataifa, ya wanaume na wanawake, wanaoisoma Biblia yote na kuikubali kuwa ni Neno lililotoka kwa Mungu. Wanaziamini ahadi zilizopo katika Agano la Kale na Agano Jipya zinazomhusu Bwana Yesu Kristo, na hatma ya ulimwengu. Wanasubiria kurudi kwa Yesu kutoka mbinguni, kuusimamisha Ufalme wa Mungu duniani.

Neno Kristadelfia linatokana na maneno mawili ya Kiyunani (Kigiriki), yenye maana ya '**Ndugu katika Kristo**'.

### Wakristadelfia wanaishi wapi?

Kuna Wakristadelfia kwenye nchi zaidi ya 50; wapo Uingereza na maeneo mengi katika Ulaya, wapo kwenye nchi zaidi ya 30 katika Afrika, wapo Mashariki ya Mbali- kutoka India hadi Indonesia, wapo Australia na visiwa vya Bahari ya Pasifiki, wapo Amerika ya Kaskazini na Kusini- kutoka Kanada kwenda chini mpaka Argentina, na katika visiwa vya Karibeani. Ni jumuiya yenye mchanganyiko wa watu wa rangi nyingi na tamaduni tofauti tofauti.

### Wanaamini nini?

Wakristadelfia wanachukulia imani yao katika mambo yaliyokuwa yakiaminiwa na kufundishwa na Yesu na wanafunzi wake kama miaka 2000 iliyopita. Ujumbe wa kweli wa Ukristo haujabadilika. Kwa bahati mbaya, katika karne zote hizi zilizopita, makanisa mengi ya Kikristo yameuacha ukweli na kufuata mafundisho yenye misingi yake katika imani za kipagani. Hata hivyo, kwa nyakati mbalimbali kumekuwa na vikundi vidogo-vidogo vilivyoishikilia imani ya kweli.

Kwa mfano katika Ulaya, zaidi ya miaka 400 iliyopita kulikuwa na watu wengi waliojifunza Injili ya kweli kwa kuisoma Biblia wenyewe, wakati ilipochapishwa katika lugha zao za kiasili. Watu hawa walijiita '**Ndugu katika Kristo**'. Cha kuhuzunisha, wengi wao waliteswa au kuuawa kutokana na imani yao. Wengi walilazimika kuzihama nyumba zao, na hata nchi, lakini waliibeba Injili na kuisambaza Ulaya na kwenye nchi za ng'ambo.

Haikuchukua muda, hata hivyo, ukweli ukawa tena umechanganywa na mafundisho potofu. Kuna fundisho katika hili: ukweli unadumu tu pale watu wanaompenda Mungu, wanapokuwa wanasoma na kujifunza wenyewe Neno la Mungu.

### Jumuiya ya Wakristadelfia ilianzaje?

Katika mwaka 1832 daktari mmoja wa Kingereza kwa jina la John Thomas, aliyekuwa mhudumu wa kanisa, alipanda meli iliyokuwa ikielekea New York, Amerika, kwa kuwa baba yake alitaka kuishi Marekani.

Meli hiyo ilipata msukosuko wa dhoruba kali baharini kiasi kwamba, dokta Thomas alifikiri wangeangamia. Alistukia hakujua vya kutosha juu ya kile hasa kinachomtokea mtu anapokufa. Alijiapia kuwa kama angepona na kuifikia nchi kavu, asingetulia mpaka aupate ukweli wote juu ya uhai baada ya kifo.

Kwa bahati aliweza kufika New York, na akawa mkweli kwa neno lake. Aliitumia miaka kumi na mitano iliyofuata kwa kujifunza Biblia kwa umakini sana, huku akiipima na kuilinganisha na madai ya makundi mbalimbali ya 'Ukristo'. Alipokuwa amejihakikishia kuwa ameelewa vizuri mambo yaliyoandikwa katika Agano la Kale na Agano Jipya, kumhusu Yesu Kristo na Ufalme wa Mungu unaokuja katika dunia, alifanya mpango akabatizwa kwa kuzamishwa kwenye maji. Alifanya mahubiri mengi ya hadharani katika Amerika na Uingereza, na kuandika vitabu na kuchapisha magazeti ya kidini.

Kati ya wale waliopata mafundisho yake na kujiunga na John Thomas katika kazi yake ya kuhubiri, kulikuwa na bwana mmoja wa Scotland aliyeitwa Robert Roberts. Huyu alisaidia sana katika kuwaweka pamoja walioamini katika vikundu vya wafuasi tunavyoviita 'Eklezia'. Hili ni neno la Kibiblia lenye maana ya 'kusanyiko la watu walioitwa'. Wakristadelfia wanapenda kulitumia neno **Eklezia** zaidi badala ya neno 'Kanisa'; neno ambalo mara nyingi linatumiwa na wengi kumaanisha jengo, **badala** ya watu.

### **Jina Kristadelfia linaweza kuonekana la ajabu kidogo mwanzoni**

Jina 'Mkristadelfia' au 'Wakristadelfia' lilianza kutumiwa kwa mara ya kwanza mwaka 1862, wakati walioamini katika Amerika walipoitaka serikali yao ya Marekani iwasamehe kujiunga na jeshi, wakati wa vita vya wenyewe-kwa-nyenye vya Marekani. Wakristadelfia hawapambani au kukubali kuuu. Wakiwa wameona haja ya kuwa na jina la kuweza kujitambulisha kama washiriki wa kundi moja (lililo tofauti na madhehebu zingine), John Thomas aliwakumbuka wale Ndugu katika Kristo wa miaka 300 nyuma, hivyo akalibuni jina 'Christadelphian' ambalo ni namna ya Kiyunani ya kusema 'Ndugu katika Kristo'.

Hawa Wakristadelfia wa karne ya 19 walikuwa wakisafiri sana, na walihubiri katika maeneo mengi ya dunia walipokwenda, na ilipofika mwishoni mwa karne hiyo kulikuwa na vikundi vingi vya waumini katika nchi nyingi.

### **Wakristadelfia wanajipangaje?**

Kuna kamati kadhaa zinazopanga mambo kuhusiana na kazi ya kueneza Injili, na zingine za kuwaangalia wagonjwa, wazee na wale walio katika mazingira ya upweke. Tunazo pia ofisi katika nchi chache kwa ajili ya kuchapisha magazeti, vitabu na majalida mbalimbali. Lakini, hatuna wahudumu wa kulipwa, wala Makao-makuu. Mahitaji yetu ya kifedha yanashughulikiwa kwa michango ya hiari inayotoka kwa wanajumuia wetu. Hatuna 'wachungaji'.

Lakini utapenda kuuliza: kama hakuna mfumo wa uongozi unaotoka Ofisi-Kuu unaowaunganisha waumini, Wakristadelfia wanajiendesha? Jibu ni kwamba, imani ya namna moja tuliyonayo na mambo ya pamoja tunayofanya, ndivyo vitu vinavyotuweka katika ushirika wa namna moja, unaotuunganisha wote.

Kila Eklezia ilipo, inajiendesha yenyewe kwa kuchagua 'wazee' wake wanaoongoza mambo. Hao wanapatikana kwa kupiga kura (kwa kawaida) mara moja kwa mwaka. Wale wanaochaguliwa wanalitumikia kusanyiko lao katika kutekeleza majukumu mbalimbali kama ya Ukatibu, Uweka Hazina, au kuwa Mwenyekiti wa mikutano (kuwa Mwongoza-Ibada).

Hawalipwi kwa kazi wanayofanya na sio 'makuhani'. Tunaamini ya kuwa, Bwana Yesu, akiwa sasa mbinguni, ndiye aliye pekee Kuhani wetu, ambaye kupitia kwake waumini wote waliobatizwa, wanaweza kutubia dhambi zao kwa njia ya maombi. Wakristadelfia hawajengi majengo makubwa yanayoonekana ki-kanisa. Hata hivyo, kuna baadhi ya Eklezia katika sehemu mbalimbali zenye kumbi zao wanapokutania, na kutangazia imani yao. Kwingineko wanatumia nyumba zao, vyumba vya kupanga, madarasa ya shule, au kumbi za kijamii.

### **Imani moja**

Wakristadelfia, bila kujali walipo ni wapi katika dunia, wamesoma na kujifunza Biblia zao wenyewe au kuhubiriwa, na kuja kuamini mambo yanayofanana na ya kuaminika. Kwa zaidi ya miaka 100 tumekuwa na Tamko la Kiimani ambalo kila muumini analikubali kuwa ni msingi wa ushirika wake na waumini wengine.

Tamko hilo ni muhtasari ya mafundisho ya Kibiblia waliyojifunza. Kabla mtu yeyote hajibatizwa kuweza kuwa Mkristadelfia, ni lazima ajiridhishe mwenyewe kuwa ameelewa mafundisho ya muhimu ya Biblia, na ni sharti akubaliane kabisa na imani yetu iliyojengekea kwenye Biblia, na aridhie yale yanayofanyika. Hili ndilo linalowaunganisha Wakristadelfia pamoja. Andiko linasema, kuna: "Mwili mmoja...Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja" (Waefeso 4:4-5).

Hili limetuwezesha Wakristadelfia popote pale tulipo, kuwa na ushirika wa kufurahia na wa maana sana, mmoja kwa mwingine.

### **Tunataka kuwaje?**

Sisi wote tunahitaji msaada wa Mungu. Kitu kimoja tunachokifanya kila siku ni kusoma Biblia. Hili ni jambo la maana kama kupata chakula chetu cha kila siku. Mara moja kila juma tunakutana **Kumega-Mkate** (kula kipande kidogo cha mkate na kunywa divai kidogo) kwa kuyakumbuka mauti ya Bwana Yesu Kristo. Kwa kufanya hivi tunakuwa tukitekeleza amri ya Yesu, kama alivyotuagiza akisema tufanye hivyo kwa kumkumbuka.

Tunajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu, kuweka imani yetu katika matendo kwa kuangalia sana jinsi tunavyoishi. Kwa kuwa Yesu anarudi hivi karibuni, tunapenda tuwe tayari kwa ujio wake. Hili lina maana ya kuishi maisha yaliyo safi katika KWELI; lina maana ya kujiepusha na ulevi, zinaa, kucheza kamari na mambo mengine maovu.

Wakristadelfia ni raia wema katika nchi zao. Wanajitahidi kufanya mema wanayoweza, na hawapambani au kuwapeleka watu mahakamani. Wanakuwa na mke mmoja, na ni kinyume kwao kufanya ngono kabla ya kuoa au kuolewa, au nje ya ndoa. Tunatambua kuwa, wapo wanaojiunga nasi wakiwa walishakuwa na wake zaidi ya mmoja kabla ya kubatizwa; jambo hili limejadiliwa katika Somo la 33.

### **Ushirika wa Kibiblia wa Kikristadelfia (Christadelphian Bible Mission)**

Ushirika huu, CBM (kama tunavyouita), upo kwa ajili ya kuihubiri Injili ya Ufalme wa Mungu duniani pote. CBM inatangaza kozi za mafunzo na inachapisha machapisho mbalimbali kuwasaidia watu waelewe Biblia. Ni ushirika wenye watumishi wa kujitolea wa Kikristadelfia wanaoifanya kazi hii pamoja na kazi zao zingine. Kusudi lake ni kuwasaidia watu, wanaume kwa wanawake, kujifunza Injili, na kuwatia moyo watubu na kubatizwa, na kuufuata mfano wa Yesu na mitume wake.


### **Tunataka kukushirikisha imani sahihi, tumaini na furaha**

Wakristadelfia wanaamini kikweli kuwa, imani yao ni kielelezo cha INJILI ya KWELI, kama ilivyo katika Biblia. Tunatumaini kuwa, wewe nawe unaweza kufurahia kuigundua KWELI. Inaridhisha sana; sio tu kwa sababu ya ukweli uliomo ndani yake, bali inaleta pia tumaini, furaha na upendo katika maisha yako. Mungu akubariki sana katika kumtafuta. Mafundisho kadhaa ya Kibiblia yameandikwa hapo chini.

**Mistari ya kusoma:** Zaburi 119:130, Mathayo 28:19-20, Yohana 17:3

**Jifunze kwa moyo:** Yohana 15:13-14

“Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake. Ninyi mmekuwa rafiki zangu, mkitenda niwaamuruyo”.



### **Baadhi ya mafundisho ya muhimu ya Biblia:**

- ✚ Biblia ni ujumbe wa kweli kutoka kwa Mungu.
- ✚ Kuna Mungu mmoja tu, Muumbaji, ambaye anaongoza mambo yote ya dunia hii.
- ✚ Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, aliyezaliwa na Mariamu. Alikuwa mtu pekee ambaye hakufanya dhambi. Alikufa msalabani kuwaokoa wale wanaomwamini. Alifufuliwa kutoka kaburini na sasa yupo mbinguni.
- ✚ Yesu atarudi hivi karibuni kutoka mbinguni. Akirudi atausimamisha Ufalme wa Mungu duniani. Atatawala kama Mfalme, na Makao Makuu yake yatakuwa Yerusalemu katika Nchi ya Israeli.
- ✚ Wayahudi ni mashahidi wa Mungu wa kusudi lake, hata kama wapo kati yao ambao hawalitambui hili. Mungu alifanya maagano na Ibrahimu na Daudi ambayo yatatimizwa Yesu atakaporudi.

- ✚ Kifo ni adhabu kutokana na dhambi, na watu wote ni wadhambi. Tumaini pekee la uhai baada ya kifo ni katika miili kufufuliwa kutoka kwenye makaburi katika kurudi kwa Yesu.
- ✚ Kutakuwa na hukumu. Wale walio wafuasi waaminifu wa Yesu watapewa uzima wa milele, na watamsaidia Yesu katika kutatua matatizo ya dunia, na kuleta amani na mibaraka kwa mataifa yote.
- ✚ Ni lazima tuiamini Injili, tutubie dhambi zetu, na tubatizwe. Kama tukiendelea kujitahidi kuzitii amri za Mungu, na kuomba msamaha tunaposhindwa, ndipo tutakapookolewa.
- ✚ Unabii wa Biblia kuhusu matukio duniani kwa nyakati za nyuma na sasa, umetimia na unatimia wote. Ishara zinaonesha kuwa, kurudi kwa Yesu Kristo duniani kumekaribia sana. Ndio maana unapaswa kujifunza Biblia yako sasa.



**MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA****BIBLIA-MWONGOZO WETU**

**SOMO:** Zaburi 119:1 – 40

**Madai ya Biblia**

Biblia inadai kuwa ni Neno la Mungu; ni neno lenye ‘pumzi’ ya Mungu (2 Timotheo 3:16). Mungu aliwaongoza watu waliochangia kuiandika, kwa hiyo walichoandika ni ujumbe wake Mungu. Mara nyingi katika Agano la Kale, manabii wanasema: “Bwana Mungu asema.....”

Kama Biblia sio Neno la Mungu, basi haina umuhimu sana. Lakini, kama ni kweli ni ujumbe wa Mungu kwa mwanadamu, basi ni muhimu sana kuisoma na kujaribu kufanya kile inachosema. Kama tunaudharau ujumbe wa Biblia, tunamdharau Muumba wa Enzi yote.

**TUNAJUAJE KUWA BIBLIA NI YA KWELI?****Biblia inatabiria mambo yajayo**

Hatuwezi kujua litakalotokea kesho. Biblia imesemea katika sehemu nyingi mambo ambayo yangetokea mbeleni, mamia ya miaka kabla hayajatokea. Unabii wa namna hii umetimia kama ilivyosema, hata kwa vitu vidogo-vidogo sana. Hapa kuna mifano michache.

**Kuzaliwa kwa Yesu**

Katika Mathayo 2 tunasoma kuwa Mamajusi walikuja kwa Herode na kuuliza, “Yuko wapi yeye aliyezaliwa, Mfalme wa Wayahudi?” Sasa Herode aliwauliza wakuu wa Makuhani hili swali, na wakamjibu, ni: “Katika Bethlehemu ya Uyahudi”. Walijuaje? Ni kwa kuwa, mamia ya miaka nyuma, ilikuwa imetabiriwa hivyo na kimojawapo cha vitabu vya Agano la Kale (Mika 5:2).

**Kifo cha Yesu**

Fungua Zaburi ya 22 na isome kwa uangalifu. Katika Zaburi hii kuna maelezo ya kifo cha Yesu kwa kuwambwa msalabani. Hebu uangalie zaidi msitari wa 16, “Wamenizua (wamenipigilia) mikono na miguu”. Angalia tena msitari wa 18, “Wanagawanya nguo zangu, na vazi langu wanalipigia kura”.

Sasa, kama unaisoma Injili ya Yohana 19:23,24 utaona kuwa hivyo ndivyo wale askari walivyofanya; baada ya kumpigilia Yesu msalabani, waligawana nguo zake kwa kura. Mwandishi wa Zaburi aliwezaje kusemea vile ambavyo kifo cha Yesu kingetokea mamia ya miaka nyuma, kama aliloandika halikutoka kwa Mungu? Hili ni jambo la ajabu hata zaidi tukizingatia kuwa, katika enzi hizo za mwandika-Zaburi, Wayahudi hawakuwa wakijua chochote kuhusu kuua au kuuawa kwa kupigiliwa msalabani; wahalifu wao waliuawa kwa kupigwa mawe.

**Matukio makuu yalitabiriwa**

Soma Isaya 13:19,20. Katika wakati nabii Isaya alipoyaandika maneno haya kuihusu Babeli, Babeli lilikuwa ni taifa kubwa kuliko yote duniani, lenye nguvu na utukufu. Sasa, pale kulipokuwa Babeli nyakati hizo, kumebakia tu mahame kwenye eno ambalo ni nusu-jangwa.

Imekuwa vile vile kama nabii Isaya alivyosema, mamia ya miaka baada ya unabii huo kutoka. Ni Mungu peke yake ambaye angeweza kujua kuwa mabadiliko makubwa kiasi hicho yangetokea. Kuna mifano mingi kama hii. Ni Mungu pekee awezaye kuyaona ya mbele, na unabii ulioandikwa katika Biblia unathibitisha kuwa, ni Mungu aliyewaambia hao walioandika kitu cha kuandika.

Wataalam wa Kihistoria wanaochimbua chini (Archaeologists), wamevumbua uthibitisho wa vitu vingi vinavyozungumzwa kwenye Biblia. Kwenye mabaki ya kale wamegundua kuwa, miji ya Sodoma na Gomora ni

kweli ilikuwapo (Mwanzo 19). Wameigundua pia miji ya Ai, Ashkeloni, Betheli, Bethshemeshi, Gibe, Hazori, Yeriko, Lakishi, Megido, Samaria, Shechemu na mingine mingi iliyotajwa katika Biblia.

### **Biblia haijabadilika karne zote hizi**

Kati ya vitabu vya kale vilivyogunduliwa katika eneo la Dead Sea mwaka 1947 ni gombo la nabii Isaya. Liliikuwa limeandikwa kama miaka 2,000 nyuma. Maandiko ni kama yalivyo kwenye kitabu cha Isaya leo. Ujumbe wa Biblia haubadiliki kufuatana na wakati!



Kitabu cha kale  
(Gombo)

### **Yesu aliamini Agano la Kale**

Wapo watu leo wanaolicheka wazo kuwa Adamu na Hawa walikuwa watu kikweli, na kwamba Nuhu alijenga kweli Safina na kuwaweka wale wanyama wote ndani yake. Wanafikiri wanajua zaidi, kuliko kuamini hadithi kama ile ya Yona kumezwa na samaki mkubwa. Lakini, Yesu aliviamini vitu hivi!

Yesu aliamini mafundisho ya Agano la Kale kuwahusu:

- |                             |                           |
|-----------------------------|---------------------------|
| ◆ Adamu na Hawa             | (Tazama Mathayo 19:4,5)   |
| ◆ Nuhu na gharika           | (Tazama Luka 17:26, 27)   |
| ◆ Lutu na mkewe             | (Tazama Luka 17:29-32)    |
| ◆ Ibrahimu, Isaka na Yakobo | (Tazama Mathayo 8:11)     |
| ◆ Daudi na Sulemani         | (Tazama Mathayo 12:3, 42) |
| ◆ Yona na nyangumi          | (Tazama Mathayo 12:40)    |

Hatuwezi kupuuza alichosema Bwana Yesu Kristo. Alifufuliwa na Mungu baada ya kufa kwa siku tatu. Hili ni tukio la kweli katika historia, ambalo watu wenye busara walio wengi wanalikubali. Muujiza kama huo ungeweza tu kufanywa kwa uweza wa Mungu.

### **Hakuna ambaye ameweza kuithibitisha Biblia kusema uongo**

Wengi wanaoipinga Biblia, wakiwepo baadhi ya watu wajanja sana, wamejaribu kuthibitisha kuwa haisemi ukweli, lakini wote wameshindwa. Kama ni hivyo, ni lazima tukubali kuwa **sio** kitabu cha kawaida.

### **Je, unajua kuwa:**

- ✚ Biblia ilichukua karibu miaka 2,000 kuandikwa?
- ✚ Iliandikwa na wachunga-kondoo, wavuvi, daktari, mtengeneza mahema na wengineo?
- ✚ Ina jumla ya vitabu 66, na kwamba 39 kati yake ni vya Agano la Kale na 27 ni vya Agano Jipya?
- ✚ Waandishi hao wote kwa pamoja wanatupa hadithi moja iliyokamilika; habari ya **kusudi la Mungu kwa wanadamu**?
- ✚ Karibu waandishi wote walikuwa Wayahudi?
- ✚ Sehemu kubwa ya Biblia ni juu ya Wayahudi?

Ufuatao ni mwongozo wa juu-juu kukuonesha yaliyomo katika sehemu mbalimbali za Biblia:

## AGANO LA KALE

KITABU	YALIYOMO
MWANZO	Mwanzo wa dunia na mahusiano ya Mungu na wanadamu wa kwanza.
KUTOKA, MAMBO YA WALAWI, HESABU, KUMB. LA TORATI	Vitabu hivi vinatuambia jinsi Mungu alivyowateua Wayahudi kuwa watu wake na kuwatoa Misri, na kuwapa nchi ya Kanaani (Israeli).
YOSHUA---ESTA	Historia ya Wayahudi inaendelea kuzungumziwa katika vitabu hivi.
ZABURI---WIMBO ULIO BORA.	Hivi ni vitabu vya ushairi na hekima.
ISAYA---MALAKI	Hivi ni vitabu vya manabii. Waliwaambia na kuwakumbusha Wayahudi walivyopaswa kumtii Mungu. Wanaongelea pia matukio mengi ya muhimu ambayo yalipaswa kutokea katika historia ya ulimwengu. Baadhi ya haya yanaendelea kutokea katika nyakati zetu hizi, na mengine ni ya mbele zaidi.

## AGANO JIPYA

KITABU	YALIYOMO
MATHAYO, MARKO, LUKA, YOHANA	Hivi ni vitabu vinne tofauti-tofauti vya maelezo ya maisha ya Kristo, kifo na kufufuka kwake kutoka kwa wafu.
MATENDO YA MITUME	Hiki ni juu ya kuanzishwa kwa makanisa ya kwanza, na jinsi Wakristo wa karne ya kwanza walivyokuwa. (Wanapaswa wawe ndio mwongozo wetu leo!)
WARUMI ---YUDA	Ni nyaraka (barua) mbalimbali zilizoandikwa na mitume, ili kuziongoza na kuzifundisha hizo eklesia changa za awali.
UFUNUO YA YOHANA	Ni kitabu cha unabii.

(Kama unahitaji orodha kamili ya vitabu vya Biblia, utaipata katika ukurasa wa mwanzoni wa Biblia yako)

### **Kuna Maandiko mengine Mungu aliyojifunua kwayo?**

Jibu kwa swali hili ni, "Hapana". Kuna dini nyingi katika dunia, na nyingi zina vitabu vyake 'vitakatifu'. Waislamu, kwa mfano, wana Kuruani, wanayoichukulia kuwa ni Neno la Mungu. Wamormoni wana Kitabu cha Mormoni, wanachosema wametumiwa na Mungu. Zipo sehemu katika vitabu hivi zinazochukulia baadhi ya mafundisho yake kwenye Biblia, na zinatoa nasaha za maana na za hekima. Lakini, katika maeneo mengi, vitabu hivi havikubaliani na ujumbe wa Biblia.

Sasa si kitu kinachoweza kueleweka, kama Mungu angeweza kusema kitu hiki katika kitabu kimoja, na kitu kingine tofauti katika kitabu kingine. Ni **kimoja tu** kinachoweza kweli kuwa Neno lenye pumzi ya Mungu, na Biblia inadai ndio hilo Neno.

### **Biblia – Mwongozo wa maisha ya mwanadamu**

Mungu aliona hali ya kusikitisha iliyoko kwa mwanadamu, mdhambi, na akamtuma mwanawe, YESU, kufa, watu waweze kuwa na tumaini la uzima wa milele. Yesu Kristo naye ametuonesha jinsi tunavyoweza kuishi maisha yanayoweza kumpendeza Mungu. Biblia inayo mifano mingine ya 'watu wa imani', na inatuonesha jinsi baadhi yao walivyoshindwa. Habari za Wayahudi zinatuzesha kujifunza mengi kutoka katika makosa yao.

## HITIMISHO

Ni wazo kubwa kuwa, Mungu wa mbinguni ametupa kitabu kusudi tuweze kumjua, na kuishi kwa namna anavyotutaka tuishi. Amewaambia kiuhakika wanaume na wanawake katika kitabu chake hiki, sababu ya kuiumba dunia, na vile historia yake itakavyokuwa, mpaka wakati Injili itakapotimizwa, na Mungu kuwa 'yote katika wote'.

Biblia ni mwongozo ambao Mungu ametupa, unaotonesha njia ya Uzima wa Milele katika Ufalme wake. Hakuna kitabu kingine kama hiki; sio maandiko yaliyokufa, ni Neno la Uzima. Kama tukikisoma kila siku kwa umakini na kwa kuomba, kitayabadili maisha yetu, na kuyafanya yawe ya kumpendeza Mungu.

### Muhtasari

1. Biblia ni kitabu cha kipekee. Kinadai kuwa ni Neno la Mungu kwa mwanadamu.
2. Biblia inatoa kwa watu tumaini la uzima.
3. Yesu aliyaamini Maandiko ya Agano la Kale.
4. Kuna ushahidi mwingi kuwa Biblia ni ya kweli, historia yake imethibitishwa pia na uvumbuzi wa kisasa. Inayo ndani yake unabii mwingi ambao umetimia.
5. Biblia inatupa historia ya Mungu anavyoshughulika na mwanadamu, tangu alivyomuumba mtu wa kwanza, mpaka hapo ulimwengu utakapojazwa na Utukufu wake.
6. Biblia ni hazina ya Mungu kwetu, inayotonesha namna ya kusihhi. Tunapaswa kuisoma kila siku.

**Mistari ya kusoma:** Zaburi 1, Zaburi 22, 2 Timotheo 3


**Jifunze kwa moyo:** 2 Timotheo 3: 16 – 17

“Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema”.

**MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA****INJILI****SOMO:** Isaya 55**Habari Njema**

Kila mtu anafurahi kusikia 'habari njema'. Na hivi ndivyo hasa habari ya Injili ilivyo. Neno Injili maana yake ni **"Habari Njema"**

Vitabu vinne vya kwanza vya Agano Jipya mara nyingi vinaitwa 'Injili', kwa sababu ya habari njema iliyopo ndani yake. Ni habari njema inayomhusu Bwana Yesu Kristo. Alikuwa ni Mwana wa Mungu, na alizaliwa na bikira Mariamu.



Hivi ni sehemu tu ya  
habari njema!

Yesu hakutuonesha tu jinsi Mungu alivyo, na upendo na wema wake, bali ametuonesha pia uweza wake katika miujiza aliyofanya. Lakini kitu cha kushangaza kuliko vyote ni kwamba, Yesu hakuwahi kutenda dhambi. Kwa kuwa hakukosa, alifufuliwa katika wafu. Ni mtu pekee ambaye amewahi kufufuliwa kutoka kwa wafu, anayeendelea kuishi.

Hii sio Habari Njema kwa Bwana Yesu Kristo tu, ni Habari Njema kwetu sisi wote. Kwa kufa na kufufuliwa kwake, Yesu ameifungua njia kwetu sisi wanadamu wadhambi, ya kuweza kusamehewa dhambi zetu. Ametupa tumaini la uzima baada ya kufa. Kwa hiyo habari njema ni kwamba, sio lazima kwetu sisi kuendelea kuishi katika hali hii mbaya tuliyonayo. Mungu ametuonesha njia ya kutuwezesha kuiepuka dhambi na hatma ya mauti ya milele.

**Lakini kuna zaidi ya hilo**

Bwana Yesu Kristo yupo mbinguni kwa sasa, lakini muda si mrefu atarudi tena duniani. Katika Ufunuo tunaambiwa: "Tazama, yuaja na mawingu, na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma, na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake. Naam, Amina" (Ufun.1:7).

Atakaporudi katika dunia hii, Yesu Kristo atausimamisha Ufalme wa Mungu hapa ulimwenguni. Dunia itakuwa wakati huo mahali tofauti kabisa. Tunaambiwa kutakuwa:

- Hakuna tena vita
- Hakuna tena njaa
- Hakuna tena majonzi
- Hakuna tena dhambi
- Hakuna tena mauti

Bwana Yesu Kristo atakapokuwa ndiye Mtawala-Mkuu wa dunia, haki itastawi na kutakuwa na amani. Ardhi itakuwa ikizalisha sana, hivyo kwamba njaa itatokomea moja kwa moja. Mauti itamezwa na ushindi. Nabii Isaya, akiusemea wakati huo, anasema:

"BWANA Mungu atafuta machozi katika nyuso zote, na aibu ya watu wake ataiondoa katika ulimwengu wote, maana BWANA amenena hayo" (Isaya 25:8).

Mungu atatupa nafasi katika Ufalme wake huo duniani. Ni zawadi kubwa sana hii anayoitoa kwetu. Kwa vyovyote kuna masharti yake, na ndio maana tunahitaji kulisoma Neno la Mungu, Biblia, ili tuweze kujua kile Mungu anachokitaka tufanye kwa sasa katika maisha yetu.

### **Injili ilifahamika kwa watu wakati wa Agano la Kale**

Tunaambiwa kuwa, Injili ilihubiriwa kwa Ibrahimu! (Wagalatia 3:8). Kutokana na imani na utii aliokuwa nao, Mungu alifanya 'maagano' naye ya muhimu sana. Alimuahidia urithi wa nchi ya Israeli **milele**. Ibrahimu alizeeka na kufa bila ya kurithi kipande chochote cha ardhi Mungu aliyomuahidi.

Hata hivyo tunajua ya kuwa, Mungu huwa anazitimiza ahadi zake zote. Kwa hiyo, ili Ibrahimu aishi katika nchi Mungu aliyomuahidia, ni lazima Ibrahimu afufuliwe kutoka kwa wafu. Ibrahimu aliamini juu ya ufufuo, kwa hiyo aliahidiwa uzima baada ya kufa (Waebrania 11:19).

Nchi hiyo ambayo Ibrahimu aliahidiwa, ndiyo itakayokuwa kitovu cha Ufalme unaokuja. Ibrahimu atafufuliwa kutoka kwa wafu, na kuwa katika Ufalme wa Mungu katika dunia, Bwana Yesu Kristo atakaporudi. Kwa hiyo Ibrahimu aliifahamu Habari Njema ya Ufalme unaokuja na aliutazamia (Waebrania 11:10).

Mfalme Daudi naye aliutazamia wakati ambao 'mzao' wake angetawala kutoka katika Yerusalemu. Utajifunza mengi zaidi kuzihusu ahadi za Mungu kwa Ibrahimu na Daudi katika masomo ya mbele.

### **Bwana Yesu Kristo atarudi lini?**

Hatuifahamu siku ya kurudi kwa Yesu. Lakini tunajua, kutokana na matukio yanayotokea duniani leo, kuwa muda sio mrefu atarudi. Kwa miaka kama 2000 iliyopita, Wayahudi hawakuwa na nchi ya kwao wenyewe. Sasa wamerudi katika nchi yao ya kale, na katika mwaka 1948 walianza kuwa na **taifa** lao tena. Hiki ni kitu kilichoahidiwa kutokea kabla ya kurudi kwa Bwana Yesu.

Dunia leo imejaa machafuko na uovu ni mwingi; watu wengi wanajifanyia tu wanavyopenda; hawataki kujizuia. Kuna vita, njaa na magonjwa ya kutisha duniani kote. Ugaidi nao umekuwa tatizo lililo katika kuongezeka. Watu wanahofia maisha yao, kama Yesu alivyosema ingetokea. Alisema, watu wangevunjika: "Mioyo kwa hofu, na kwa kutazamia mambo yatakayoupata ulimwengu" (Luka 21:26).

Yesu aliendelea kusema mambo haya yote yatakapokuwa yakitokea, ujio wake utakuwa karibu sana. Utajifunza zaidi juu ya hili katika masomo yanayokuja.

### **Yesu atarudi na kuwa Mfalme wa dunia**


Yesu alimwambia Pontio Pilato kuwa, alizaliwa kuwa Mfalme. Juu ya msalaba wake waliandika: "Yesu wa Nazareti, Mfalme wa Wayahudi". Lakini hawezi kuwa Mfalme wa Wayahudi tu. Atakuwa Mfalme wa dunia nzima. Mungu alisema hili miaka mingi nyuma: "Na awe na enzi toka bahari hata bahari, toka mto hata miisho ya dunia" (Zaburi 72:8).

### **Nini kitatokea wakati Yesu Kristo akirudi hapa duniani?**

Atawafufua waliokufa na kutoa hukumu. Ni wale tu walio vile Mungu anavyotaka, watakaopewa uzima wa milele na sehemu katika huo Ufalme wa Mungu. Hao watamsaidia Yesu katika kuitawala dunia.

Katika wakati huo, Yerusalemu itakuwa ni Mji Mkuu wa dunia, na Yesu Kristo atakuwa Mkuu wa dunia yote. Utakuwa ni wakati wa furaha kuu. Yesu aliwaambia wanafunzi wake wauombe wakati huo kwa Mungu, wakisema: "Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni....kwa kuwa Ufalme ni wako, na nguvu na utukufu, hata milele" (Mathayo 6:9-13).

Baada ya miaka elfu moja, hakutakuwa tena na dhambi wala mauti. Mungu atakuwa, 'yote katika wote' – kama alivyopanga tangu mwanzo, kwa maana: "Dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa BWANA, kama maji yanavyoifunika bahari" (Habakuki 2:14).



Ujumbe wa maana sana kipekee ni kwamba, tunaweza kuwa na nafasi katika Ufalme huo.

### **Tunawezaje kupewa sehemu katika Ufalme huo wa Mungu unaokuja duniani?**

Tunahitaji kutambua jinsi watu wote walivyo wadhambi, na kuchukua hatua kibinafsi juu ya hali yetu hii. Wakati mtume Paulo alipokuwa Athene, alisema:

“(Mungu) Anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu, kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua, naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu” (Matendo 17:30,31).

Mungu anawaamuru watu wote kutubu. Kutubu ni kuacha kujipendeza mwenyewe na kujaribu kumpendeza Mungu. Sisi wote ni wadhambi, kwa hiyo tuna wajibu wa kutubu na kubatizwa katika maji. Ni lazima tujaribu kuishi kwa namna alivyosema Yesu. Kwa wale watakojitahidi kufanya hivyo, Yesu Kristo atawapa uzima usio na mwisho atakaporudi.

(Utakuwa umegundua kuwa, Injili haihusu kwenda mbinguni, hilo sio Biblia inalofundisha. Injili inahusu uzima wa milele katika Ufalme wa Mungu **katika** dunia)

#### **Muhtasari**

1. Biblia yote inahusu Injili (au **Habari Njema**). Watu waaminifu katika Agano la Kale na Agano Jipya walielewa maana ya Injili.
2. Ili kuwaokoa watu, Yesu aliishi maisha makamilifu na kufa kwa hiari.
3. Mungu alimfufua Yesu kutoka kwa wafu, na baadaye kidogo Yesu alipaa mbinguni.
4. Bwana Yesu atarudi kuusimamisha Ufalme wa Mungu hapa duniani.
5. Yesu atawafufua waliokufa na kuwahukumu. Wale watakaokubalika watapewa uzima wa milele katika Ufalme wake hapa duniani.

**Mistari ya kusoma:** Isaya 45:18, Zekaria 9:9, Mathayo 25:31-34, 1 Wakorintho 15:28.

**Jifunze kwa moyo:** Mwanzo 12:1-3

“BWANA akamwambia Abram, toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, nenda mpaka nchi nitakayokuonyesha, nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako, nawe uwe baraka, nami nitawabariki, wakubarikiyo, naye akulaaniye nitamlaani, na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa”.

**MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA**

***Karatasi ya maswali: namba 1***

Jaribu kujibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa “Kazi ya ziada” unaweza kujibu swali kama ukipenda, au kuliacha kama ukiona huliwezi. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

**MASOMO: 1 – 4**

- A. Andika angalau mambo matatu unayoyajua au uliyojifunza:
  - a) kumhusu Ibrahimu
  - b) kumhusu Yesu Kristo
  - c) kuuhusu Ufalme wa Mungu
- B. Daudi aliahidiwa nini?
- C. Neno ‘Injili’ maana yake ni nini?
- D. Tunawezaje kuwa marafiki wa Yesu? (Yohana 15)
- E. Ni kwa nini inatupasa kutubu?
- F. Kwa nini Biblia ni tofauti na vitabu vingine vyote?

*Kazi za ziada:*

- G. Zaburi ya kwanza **inatuambia nini** juu ya hatma ya watu walio ‘wa haki’ na wale wasiomjali Mungu?
- H. Katika 2 Timotheo 3 tunasoma nini kuhusiana na ‘siku za mwisho’? (nyakati tunazoishi sasa)

Tuma majibu yako kwa:

.....  
.....  
.....  
.....

Kumbukumbu yako ni namba: .....










## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## MUNGU NA UUMBAJI

**MASOMO:** Mwanzo 1, 2 : 1 – 7

**Uumbaji**

Katika kifungu cha kwanza cha Biblia, Mwanzo 1, umeshasoma juu ya siku saba za uumbaji. Jedwali hapa chini linaonesha kazi ya kila siku:

Siku	Tukio	Kilichofanyika
1.		Nuru inatokea; kunakuwa na mchana na usiku
2.		Maji yanajitenga, anga linajitanda
3.		Nchi kavu inatokea; majani, miti na mimea inaota
4.		Jua, mwezi na nyota vinatokea
5.		Samaki wanatokea baharini, ndege angani
6.		Wanyama wanaumbwa, na mwisho kabisa mwanadamu
7.		Mungu anapumzika.

Kila kitu kilifuata utaratibu wake. Kwa mfano: mimea na miti haikuwekwa mpaka siku ya tatu, wakati nchi kavu ilipokuwa imewekwa tayari kwa ajili yao. Wanyama waliumbwa siku ya sita, wakati chakula kikiwa kimeshapatikana kwa ajili yao.

“Munqu akaona kila kitu alichokifanva. na tazama. ni chema sana”.

Popote pale tulipo, kila siku tunaona uzuri wa kazi ya Mungu. Mwanadamu amegundua vitu vya ajabu kama ndege za kusafiria angani, na madawa, lakini utaalamu unaotumika kuvibuni na kuviunda vitu hivi, si chochote ukilinganisha na ustadi na uweza uliovumba vitu hivi vyote kwa umahiri mkubwa.

Mchana unafuata usiku, misimu inafuatana, na hatuwi na mashaka kama mambo hayataendelea kuwa hivyo. Kazi anayoifanya mtu anaweza kuikosea, lakini kazi ya Mungu haikosewi.

Wakati kazi nyingi wanazofanya watu zinakuwa na kasoro nyingi, kila anachokiumba Mungu, sio tu kama kinafaa kwa lengo alilolikusudia, bali pia kinapendeza. Ua dogo kabisa la rangi na kwa umbo lake, uwezo wake wa kujizalisha ni muujiza. Ni hivyo hivyo kwa kindege kidogo na vibawa vyake vinavyokiwezesha kuruka. Kinaweza kuruka kwa kujua njia yake kwa maelfu ya kilometa, kikizunguka kwenda kwenye makazi yake ya msimu wa baridi kali.

“Wewe Mungu, BWANA wetu, jinsi lilivyo tukufu jina lako duniani mwote!”

### **Miungu isiyo miungu**

Katika nyakati zote tangu kale, mwanadamu amekuwa akiona maajabu ya asili, lakini, badala ya kumuabudu Mungu aliyevumba vitu vyote, wamekuwa wakiviabudu vitu alivyoviumba! Hata watu wa Mungu, Wayahudi, wamefanya hivyo kwa nyakati mbalimbali. Watu wameliabudu jua, mwezi na nyota, na kufikiri kuna mizimu inayoishi kwenye maji na upepo, kwenye miti na mawe. Hili ni jambo ovu sana kufanya, na Mungu analilaani. Hebu soma kitu mtume Paulo anachokisema juu ya hili katika Warumi 1:20–23. Anasema:

“...wakaubadili utukufu wa Mungu asiye na uharibifu kwa mfano wa sura ya binadamu aliye na uharibifu (‘anayekufa’), na ya ndege, na ya wanyama, na ya vitambaavyo” (ms.23).

Kwa vyovyote, watu walipoimba miungu hiyo ya uongo haikuweza kujibu kamwe. Iwezeje kujibu wakati sio miungu lolote? Kuabudu miungu ya uongo ni jambo ovu sana, na kumeleta matukio mabaya sana kufikia hata kuwapitisha watoto kwenye moto. Hata Wayahudi, ingawa walikuwa wamepeva mafunuo ya Mungu pekee aliye wa Kweli kwa Sheria yake ya Haki, walikuwa na hatia ya kuabudu sanamu; kuabudu miungu ya uongo. Mungu alikuwa amewaonya dhidi ya hili, katika Kumbukumbu la Torati 4:15-19.

Sasa tazama Ezekieli 14:1-5. Ona vile Mungu aliyosema juu ya hawa ‘waabudu sanamu’ katika mstari wa 3, kuwa, walikuwa: “Wametwaa vinyago vyao na kuvitia mioyoni mwao”. Nasi tutaendelea kufanya hivi tusipoangalia. Kama kuna kitu katika maisha yetu tunachokifiri ni cha maana zaidi kumpita Mungu aliyetuumba, kitu hicho ni ‘sanamu’; ni kinyago mioyoni mwetu. Imani mtu aliyo nayo inaweza kuwa kinyago chake, kama haiendani na mambo Mungu aliyosema, na anaing’ang’ania. Inahesabiwa kama ni kuasi! Kama tunataka kumpendeza Mungu, inatubidi kuachana na sanamu; inatubidi tujitenge na wanaoabudu miungu ya uongo. Paulo analiongelea hili katika waraka wake wa pili kwa Wakorintho, ambapo anasema:

“Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa, kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana ushirika gani kati ya nuru na giza?” (2 Wakorintho 6:14).

Endelea kusoma mpaka mwisho kifungu hiki kwa Wakorintho, kisha fungua waraka wake kwa Wathesalonike. Waumini Wakithesalonike, walimgeukia Mungu na kuziacha: “...sanamu, ili kumtumikia Mungu aliye hai, wa kweli. Na kumngojea Mwanawe kutoka Mbinguni, ambaye alimfufua katika wafu, naye ni Yesu, mwenye kutuokoa na ghadhabu inayokuja” (1 Wathes.1:9,10).

## **Ulimwengu wanadamu waliouchafua**

Watu wanafanya uovu mkubwa wanapoabudu sanamu, na watu wanafanya uovu wanapoichafua dunia iliyoumbwa na Mungu. Hapo mwanzo, dunia yetu ilikuwa ni mahali pazuri zaidi kuliko ilivyo leo. Wanadamu wamefanya mengi kuharibu uzuri wake. Wanakata miti ovyo ovyo na kusababisha majangwa palipokuwa pameota misitu. Wameichafua hewa kwa mioshi ya sumu, na kuchafua chemchemu na mito kwa takataka za sumu kutoka kwenye viwanda vyao. Kwa njia hizi na zingine, dunia yetu inaharibika.

Lakini bado ni dunia ya Mungu, na hataruhusu watu waendeleo kuiharibu moja kwa moja. Katika Matendo ya Mitume, mtume Paulo anasema, Mungu: “Ameweka siku atakayowahukumu walimwengu” (Matendo 17:31).

Siku inakuja ambapo Mungu atamtuma Yesu arudi kuyaweka mambo sawa; kuitawala dunia. Utawala wake wa busara na miongozo yake ya haki, itairudisha dunia katika uzuri wake wa kwanza. Mungu amesema: “Hakika yangu, kama niishivyo, ndivyo dunia hii nzima itakavyojawa na utukufu wa BWANA” (Hesabu 14:21).

## **Mungu, Mwenye Uweza Wote**

Zaburi ya 90:2 inasema: “Tangu milele hata milele, ndiwe Mungu”. Hiki ni kitu ambacho akili zetu haziwezi kukielewa. Tunajua kutokana na namna tunavyoishi maisha yetu kuwa, mambo yote yana mwanzo na mwisho, na tumezoea kuna kuzaliwa na kufa. Lakini, Bwana Mungu yeye amekuwako nyakati zote na ataendelea tu kuwako. Tunapaswa tuwe na imani kuwa, hivi ndivyo ilivyo. Mwandishi kwa Waebrania anasema: “Mtu amwendeaye Mungu (‘anayemwamini Mungu’) lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao” (Waebr. 11:6).

Tunaweza kuangalia vitu vya ajabu tunavyoviona katika mazingira tulimo, na kujifunza kitu kuhusu uweza wa Mungu na hekima yake. Lakini, hatuwezi kuona katika dunia inayotuzunguka, jibu la kusudi la Mungu katika kuiumba dunia, na mipango aliyonayo kwa mambo yake ya mbeleni. Hatuwezi kujua anavyowataka wanadamu waishi.

Ni kwa **Neno** lake tu tunavyoweza kuyajua mambo haya. Ili kumjua Mungu, ni lazima tuje kwenye Biblia. Biblia inatuambia ya kwamba, YEYE ni Mkuu sana na ni mwema. Inatuambia kuwa anao mpango na dunia yake. Katika kujifunua kwa Musa, alijitambulisha kuwa, YEYE ni:

“BWANA, BWANA, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli, mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi, wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe” (Kutoka 34:6,7).

Mungu ana rehema na upendo, lakini pia ni wa kweli na haki. Anatutegemea tumtukuze na kumtii.

## **Hapo mwanzo**

Kuna watu wengi wanaoamini kuwa, dunia yetu hii ya ajabu ilitokea hivi hivi tu. Wanafikiri uhai ni kitu kilichoanza tu, na tokea hapo, baada ya mamilioni ya miaka, mambo yakajipanga yenyewe katika utaratibu na uzuri wa dunia tunayoiona leo. Kwa hiyo wanasema, viungo vyenye uajabu kama macho yanayoona na masikio yanayosikia, vilitokea kwa bahati-bahati tu.

Miaka si mingi iliyopita, wana-sayansi karibu wote waliamini katika “mabadiliko ya pole pole” yaliyotokea yenyewe tu (Evolution, kama nadharia hiyo inavyoitwa). Walisema dunia hii tunamoishi leo ni matokeo ya mpasuko na mabadiliko ya taratibu kwa mamilioni ya miaka. Kwa siku hizi, hata hivyo, wana-sayansi wengi maarufu wanarudi kwenye mawazo ya kwamba, hayakutokea tu. Kuna Muumba wa yote. Biblia inasema:

“Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi”.

Biblia haituambii namna alivyofanya, na kama ingetuambia, inawezekana tusingeelewa. Tuna wajibu wa kulipokea Neno la Mungu kwa imani. Kitu kimoja ni hakika: hatuwezi kuamini Biblia inachofundisha kumhusu Mungu aliyeviumba vitu vyote, na wakati huo huo tukaamini kuwa dunia hii ilitokea tu:

“Kwa neno la BWANA mbingu zilifanyika, na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake” (Zaburi 33:6).

Tuliona katika Mwanzo 1 jinsi Mungu alivyoiumba dunia, na kuwaumba mwanamume na mwanamke. Sasa hebu soma Mwanzo 2:15 mpaka Mwanzo 3:24. Mistari hii inatoa hadithi ya kusikitisha; jinsi mambo yalivyokwenda vibaya. Hapo mwanzo kila kitu baada ya kuumbwa kilikuwa 'chema sana'. Baada ya hapo Adamu na Hawa hawakumtii Mungu, na kutomtii kwao kukaleta dhambi na mauti duniani.

Kwa upendo wake kwa wanadamu, miaka mingi baadaye Mungu alimtoa Mwanawe, Bwana Yesu Kristo. Yesu aliweza, kwa maisha yake makamilifu na kwa kifo chake msalabani, kuifungua njia kwa Mungu kuweza kusamehe dhambi. Yesu ametuletea tumaini la uzima. Utasoma juu ya hili katika somo litakalofuata.

### **Sisi ni sehemu ya uumbaji wa Mungu**

“Njoni, tuabudu, tusujudu, tupige magoti mbele za BWANA aliyetuumba” (Zaburi 95:6).

Kuweza kuja mbele ya Mungu kumwabudu na kumsifu, ni fursa ya kipekee iliyo ya maana sana. Yesu anaongelea wale wanaokuja kumwabudu Mungu **‘katika roho na kweli’**, na kusema, **“Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu”** (Yohana 4:23). Mungu anataka awabariki watu wanaompenda; wanaopenda kumwamini na kumtii, waifurahie dunia hii aliyoiumba.

Mungu anawataka watu wamruhusu YEYE ayaongoze maisha yao. Anawaandaa watu kama hao kwa ajili ya wakati watakapoweza kumtumikia milele katika Ufalme wake, Yesu atakaporudi duniani. Kama tukilisoma Neno lake na kumtukiza na kumtii sasa, katika siku hiyo inayokuja tutakuwa kati ya wale watakaosema:

“Tazama, huyu ndiye Mungu wetu, ndiye tuliyemngojea.....tushangilie na kuufurahia wokovu wake” (Isaya 25:9).

#### **Muhtasari**

1. Hii dunia iliumbwa na Mungu.
2. Ni YEYE pekee astahiliye kuabudiwa.
3. Nadharia zote za watu juu ya dunia ilivyoanza ni uongo, kama zinamkana Mungu kuwa siye Muumbaji.
4. Tunaweza tu kufahamu juu ya Mungu na kusudi lake kwa dunia hii kwa kuisoma Biblia.
5. Biblia inatufundisha tunavyoweza kuishinda dhambi na mauti kwa kupitia kwa Yesu, na kuwa na sehemu katika Ufalme wa Mungu unaokuja.

**Mistari ya kusoma:** Zaburi 24 , Zaburi 102:25–28, Warumi 1:18-23, Mwanzo 2:15, 3:24.

**Jifunze kwa moyo:** Waebrania 11:3

“Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri”.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

### MUNGU ALIUPENDA ULIMWENGU

**SOMO:** Isaya 53

#### **Dunia ina matatizo gani?**

Ni kweli kuna matatizo katika dunia tunamoishi. Kila siku tunasikia habari za kutisha za ukatili na vurugu duniani kote, na matishio ya vita. Magonjwa ya ajabu-ajabu yanasambaa kwa haraka, na wengi wanakufa kwa njaa wakati wengine wana chakula kingi zaidi ya mahitaji yao. Wafalme na watawala wengine hawaonekani hasa kuguswa na matatizo ya wale wanaowaongoza.

Maisha ya dhiki kwa watu yamekuwepo wakati wote, kwa sehemu kubwa. Tumeyazoea, tunachukulia kama ndivyo ilivyo, lakini, kama tukitulia na kufikiri, tunajikuta tukijiuliza, 'Ni kwa nini?'

Kwa hakika, hapo Mungu alipoiumba dunia na kuifanya iwe mahali pazuri sana pa watu kuishi, alikuwa amekusudia pawe mahali bora zaidi, kuliko dunia hii ya shida na mashaka tunamoishi ndani yake leo.

#### **Mwanzo wa shida**

Hapo mwanzo Mungu alipomuumba mtu wa kwanza, aliyeitwa Adamu, alimfundisha Njia zake. Alimpa pia Adamu amri ndogo, na kama ambavyo baba yeyote anavyotazamia wanawe wamtii, naye Mungu alitegemea utii kutoka kwa Adamu. Mungu alimwambia:

"Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika" (Mwanzo 2:16,17).

Adamu hakumtii Mungu; alianguka kwenye dhambi. Kutokumtii kwake hatimaye kulileta mauti, kama Mungu alivyosema. Dhambi ya Adamu ilimpa urahisi baada ya hapo wa kuendelea kukosea, na tangu hapo kila mwanadamu ameona rahisi kumkiuka Mungu. Katika Warumi 5:12 tunaambiwa:

".....kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti, hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi".

Kwa hiyo Adamu alifanya dhambi, na kwa kuwa mdhambi, alikufa. Ni vizuri kugundua hapa ya kuwa, Mungu **hakuwaahidia** Adamu na Hawa kuwa wangekwenda mbinguni baada ya kufa. Kuwaahidi hivyo ingekuwa kuwazawadia. Walichopewa ilikuwa ni hukumu ya kifo; **adhabu**, sio tuzo.

#### **Inatokea na sisi, pia**

Nasi tunamkiuka Mungu na tunakufa. Uliposoma Sura ya Isaya 53, uligundua maneno katika msitari wa 6, yanayosema: "Sisi sote kama kondoo tumepotea, kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe".

Nabii Yereimia naye anatuambia kitu hicho-hicho kwa maneno mengine, anaposema: "Moyo (wa mwanadamu) huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha" (Yereimia 17:9). Tunayasoma mambo haya katika Biblia, na tunajua kutokana na tunavyojisikia wenyewe, kuwa ni kweli.

Mtume Paulo alisema: "Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani, ndani ya mwili wangu halikai neno jema" (Warumi 7:18). Wote sisi tunastahili kukubaliana na Paulo. Kwa namna fulani sisi wote tunakuwa tunashindwa kuwa wema kama tunavyotaka. Wapo wengi pia ambao hawataki hata kule kuwa wema.

#### **Ufumbuzi ni nini?**

Kabla ya kuanguka kwenye dhambi, Adamu aliishi kwa mahusiano mema na Mungu. Sasa, urafiki huo ulivunjika baada ya kuwa mdhambi. Ushirika wake na Muumba wake usingeweza kuendelea; Mungu ni Mtakatifu sana.

Adamu inawezekana hakujua ni balaa gani alikuwa analianzisha. Kuanzia hapo aliendelea kumkiuka Mungu, na mpaka sasa kila anayetokana naye (ukiwepo wewe na mimi), amezifuata nyayo zake na kufanya dhambi (ukimweka pembeni Yesu tu). Na kwa kuwa sisi wote tumekuwa wadhambi kiurithi, wote tumefarakana na Mungu.

Tokea hapo, tunapozaliwa, tunakuwa ni uzao wa Adamu na tunarithi matokeo ya dhambi yake. Tu-viumbe wa kufa tangu tunapotungwa mimba, na tunapozaliwa tunafanya mambo yawe mabaya zaidi kwa kuongeza dhambi zetu wenyewe. Hii ni hali mbaya sana! Hakuna anachoweza kufanya mtu kujiokoa mwenyewe.

### **Wokovu ni kwa neema ya Mungu**

Mungu kwa upendo na huruma yake, hakuwaacha wanadamu waishie wote kwenye kufa kwenye dhambi zao tu. Ameweka njia ambayo watu wanaweza kumjea na kuwa na uzima. Tunasoma katika Yohana 3:16 kuwa: “Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele”.

Mtume Paulo anasema: “Mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani” (Waefeso 2:8).

Neema ya Mungu ni upendo wake anaotupa bure, wa kutusamehe dhambi zetu, kwa ajili ya Kristo. Ametimiza hilo kwa upande wake kwa kutupa Yesu; ametufungulia njia, tusipotee. Hili linawezekana, kwa njia ya imani.

Biblia inapoongelea **kwa njia ya imani**, inamaanisha **kuamini na kuweka tumaini**. Kama hatuliamini Neno la Mungu, ni kwamba haiwezekani tukawa na imani inayolitumaini. Katika hali hiyo, hatuwezi kuwa na ushirika katika hiyo neema ya Mungu. Neno linasema:

“Pasipo imani haiwezekani kumpendeza (Mungu), kwa kuwa mtu amwendeaye (‘amwaminiye’) Mungu, lazima aamini kwamba yeye yuko na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao” (Waebrania 11:6).

### **Yesu na msalaba**

Yesu hakutenda dhambi. Alifanya wakati wote mambo yale yanayompendeza Mungu. Hata hivyo walimsulubisha! Mungu hakumwokoia kisimpate kifo hicho cha kutisha. Msitari tuliounukulu kutoka Isaya 53 unaendelea kusema: “Na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote”.

Biblia inatufundisha wazi-wazi kuwa, kupitia katika kifo cha Yesu msalabani, kwa kuyatii mapenzi ya Baba yake, tunaweza kusamehewa dhambi zetu, na kuwa na tumaini la uzima.

Kuna kitu kizuri sana cha ajabu katika hili; katika huo upendo wa Mungu katika kumtoa Mwanawe, na katika upendo wa Yesu wa kutii mapenzi ya Baba yake. Kwa kuiamini **Habari Njema** iliyoko ndani yake, tunaweza kuwa na uzima. Watu hawalishiki hili vizuri; tualirudia tena na tena katika uchunguzi wetu wa Kimaandiko, kwa maana dhana hii ndiyo iliyo kiini cha tumaini la wokovu; tumaini la Mkristo.

### **Uko upande upi?**


Namna moja ya kuutafakari wokovu ni kuifikiria **familia**. Adamu alikuwa kiongozi wa familia ya ‘wanadamu’ na kutokana naye (na mke wake, Hawa), sisi wote tumezaliwa. Adamu alifanya dhambi na kuleta mauti kwa jamii ya wanadamu, na kwa hiyo watu wote tunakufa.

Bwana Yesu Kristo, akiwa naye na mwanadamu, alifanya jambo la ajabu. Alichepuka na kuanzisha familia nyingine. Aliweza kufanya hili kwa kuivunja nguvu dhambi. Ilihitaajika dhabihu kamilifu kuweza kuishinda laana ambayo Adamu na Hawa walikuwa wameileta kwa wanadamu. Yesu alikuwa ndio hiyo dhabihu kamilifu.

Kwa hiyo familia ziko mbili: familia ya Adamu na familia ya Kristo. Sisi wote tunakuwa tumezaliwa katika familia ya Adamu, na tunapokufa tukiwa ndani ya familia hiyo ya Adamu, tunapotea milele. Inatubidi tufanye kitu; inatubidi nasi tuchepuke!

Kristo anatutaka tujiunge na familia yake yeye, na tunaweza kufanya hivyo kwa kujifunza juu yake tunapolifahamu kusudi la Mungu, na kubatizwa. Ubatizo (kama utakavyojifunza baadaye), ni ishara ya kufa kwake Yesu na kufufuka tena. Kwa hiyo tunakufa ili kujitoa katika familia ya Adamu, na kujiunga na familia ya Kristo tunapoibuka kwenye maji ya ubatizo.

Kama ukisoma Warumi 6:12, 18-21, utaona vile mtume Paulo anavyolitumia wazo hili la familia. Tunapaswa kumshukuru sana Mungu na Bwana Yesu kwa kutuwezesha kutoka katika familia hiyo ya Adamu.



### **Kumwamini**

Tumeshaona kuwa, kama tunapenda kumpendeza Mungu, ni lazima tuamini yale Mungu aliyofanya kwa ajili yetu kupitia katika kifo cha Yesu Kristo. Katika Yohana 3:16 tumeambiwa ni: “Ili kila (mtu) amwaminiye (Yesu) asipotee, bali awe na uzima wa milele”.

Hili halina maana ya kusema tu kwamba, ‘Nimemwamini Yesu’, kwa hiyo nitaokolewa na dhambi na mauti. Inaweza ikaonekana kihivyo unapoanza kufikiri, lakini hebu tulia na kulifikiria jambo hili vizuri. Tunapokuwa kikweli tumeamini kitu, tunakifanyia kazi! Kama tunauguliwa na mtoto, na tunaamini daktari anaweza kutusaidia kumponya, hatusemi tu, ‘Namwamini daktari’, na kuishia hapo. Tunampeleka mwanetu kwa daktari, na kwa kuwa tunamwamini daktari wetu, tunafanya lolote analotuambia.

Sasa, ni hivyo ilivyo kumwamini Yesu. Kama ni kweli tumemwamini, tutajitahidi kujua kile anachotutaka tufanye na tutakifanya kwa uwezo wetu wote. Kumwamini Mungu kunaanzia katika kubatizwa kwa kuzamishwa kwenye maji, kama Kristo alivyoamuru. Ni pale tu tunapofanya hili, ndipo tunapoweza kuwa miongoni mwa wale ambao hawapotei; miongoni mwa wale watakaopata ‘uzima wa milele’.

### **Tuzo ya Uzima wa Milele**

Maisha katika Ufalme wa Mungu ni tuzo ya Mungu kwa wale wanaoliamini Neno lake, na kujitahidi kumtii. Hawa ni watu wanaomuomba Mungu kila siku wakisema, ‘Ufalme wako uje’. Yesu atakaporudi, atausimamisha huo Ufalme wa Mungu. Atakikalia ‘kiti cha enzi cha Daudi’, baba yake, na kuitawala dunia nzima. Hapo ndipo wanaume kwa wanawake waliomngoja wakijitahidi kuishi kwa namna walivyoamuriwa, watakapopewa zawadi kubwa kuliko zawadi yoyote mtu anayoweza kupewa, ya uzima usio na mwisho katika Ufalme wa Mungu. Hawatakufa tena.

Hao wataishi milele na kumsaidia Bwana Yesu katika jukumu lake la kuitawala dunia. Ndipo watakapoimba maneno haya tunayoyasoma katika Ufunuo, wakisema:

“Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu, kwa damu yako, watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu, nao wanamiliki juu ya nchi” (Ufun. 5:9,10).

#### **Muhtasari**

1. Matatizo yote yaliyoko katika dunia yanatokana na dhambi ya mwanadamu, iliyorithiwa kutoka kwa Adamu na Hawa.
2. Kwa ajili ya dhambi, wote tunakufa, na kifo ni adhabu.
3. Injili, ambayo ni Habari Njema, ni kwamba Mungu ametufungulia njia ya watu wote kuweza kuokolewa na matokeo ya dhambi.
4. Hatuwezi kujiokoa wenyewe, hata tukijitahidi namna gani. Tunaokolewa kwa neema; wokovu ni tuzo.
5. Njia ya wokovu ni kupitia kwa Bwana Yesu Kristo tu, na imewezeshwa na dhabihu yake msalabani.
6. Ni wajibu wetu kumwamini Yesu na kumwekea tumaini.
7. Wale wanaoonesha imani, wataitikia kwa kubatizwa na kujitahidi kumtii na kumfuata Bwana Yesu.
8. Mungu anaahidi kuwa, wale wanaomwamini na kumfuata Bwana Yesu, wataishi milele katika Ufalme wake hapa duniani, Yesu akiwa ndiye Mfalme wao.

**Kifungu cha kusoma:** Waefeso 2

**Jifunze kwa moyo:** Yohana 3:16

“Kwa jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele”.



## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

### KURUDI KWA BWANA YESU DUNIANI

**SOMO:** Matendo 1

#### Miaka 2000 iliyopita

Bwana Yesu alisulubiwa miaka elfu mbili iliyopita. Wafuasi wake walivunjika moyo na kuchanganyikiwa. Matumaini yao yote kwake yalivunjika, alivyokuwa amekufa na kulazwa kaburini.

**Lakini:**

Siku ya tatu, Yesu alitoka kwenye kaburi lile akiwa hai!

Lilipotokea hili, wafuasi wake waliyakumbuka maneno aliyokuwa amewaambia kabla ya kufa: “Ninyi mtalia na kuomboleza, bali ulimwengu utafurahi....lakini huzuni yenu itageuka kuwa furaha” (Yohana 16:20).

Watakuwa walifurahi kiasi gani kumwona Bwana wao mpendwa tena! Tunaambiwa: “Basi wale wanafunzi wakafurahi walipomwona Bwana” (Yoh. 20:20). Kwa hakika, furaha yao ilikuwa kubwa sana.

#### Yesu alipokwenda mbinguni

Sasa hebu soma tena mistari nane ya kwanza ya Matendo 1. Jaribu kupata picha jinsi mitume walivyokuwa katika hizo siku arobaini, Yesu alipokuwa yupo nao tena kwa mara nyingine. Wafikirie tena mwishoni mwa siku hizo arobaini, wakiwa wamesimama juu katika miteremko ya kijani ya Mlima wa Mizeituni, wakiwa na Yesu katikati yao. Ghafila anatwaliwa pale walipo na kuanza kupaa mbinguni.

Watakuwa walimtazama sana kwa jinsi alivyoondoka duniani, na kutokomea mwinguni, wasimwone tena. Walikuwa wameachwa ukiwa tena.

Hata hivyo, safari hii hawakufadhaika wala kujiuliza; hapana! Luka anatuambia tu: “..... alijitenga nao, akachukuliwa juu mbinguni. Wakamwabudu, kisha wakarudi Yerusalemu wenye furaha kuu” (Luka 24:51,52).

#### Siri ya furaha yao

Ni kwa nini baada ya kutengana nao mara hii ya pili walikuwa na furaha kubwa?

Sababu moja ni kwamba, Yesu alikuwa amewaahidi kitu. Alikuwa amewaambia: “Tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari” (Mathayo 28:20). Hili lilikuwa na maana kuwa, ingawa walikuwa hawawezi tena kumwona, yeye alikuwa pamoja nao na angeendelea kuwajali siku zote.

Lakini, hiyo haikuwa sababu pekee ya furaha yao. Walipokuwa wakimwangalia akipaa kwenda mbinguni, kuna malaika wawili waliowajea na ujumbe na kuwaambia:

“Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi hiyo hiyo mliyomwona akienda zake mbinguni” (Matendo 1:11).

Wanafunzi wale wote walipokuwa wakirudi Yerusalemu kwa kutii maagizo ya Bwana wao, walikuwa na **uhakika kabisa** ya kuwa, Yesu mwenyewe angerudi duniani. Hiki kilikuwa ni kitu cha kuwafaraji na kuwatia furaha.

#### Maneno ya Yesu

Yote haya yalitokea miaka 2000 iliyopita, na Yesu bado hajarudi. Lakini tunajua atarudi kwa kuwa ndivyo alivyosema. Katika Luka 21:27 anaongelea kurudi kwake mwinguni, akiwa na ‘nguvu na utukufu mwingi’. Utakuwa umegundua kuwa, alipokuwa akipaa aliinuliwa, na “wingu likampokea” (Matendo 1:9), na kwamba malaika walisema atarudi, “...jinsi hiyo walivyomwona akienda zake” (ms.11).

Mifano mingi aliyotoa Bwana Yesu iliongelea pia kurudi kwake. Chukua kwa mfano, mfano katika Mathayo 25:1-13. Huu unamsema 'bwana-harusi', na hatuna tatizo katika kuuelewa. Bwana harus huyo, hakuna shaka, ni Bwana Yesu Kristo, na simulizi hilo linatutahadharisha kuwa, atakapokuwa akirudi, watakuwepo watu watakaokuwa hawajajiandaa kumpokea. Kwenye msitari wa 13 tutambue kuwa hasemi, 'hamjui kama Bwana wenu atarudi au la'. Hakuna mashaka juu ya hili, ujio wake ni kitu cha uhakika. Analosema ni: "Hamwujui siku wala saa".

### **Ushuhuda wa Petro**

Siku chache baada ya Yesu kupaa mbinguni, tunasoma juu ya Petro, akiwa hekaluni, Yerusalemu, akihutubia kwa kishindo Wayahudi waliohusika katika kumsulubisha Yesu. Katika Matendo 3:19,20 anawaambia:

"Tubuni basi mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakazi za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana; apate kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani".

Petro alisemea tena ujio wa mara ya pili wa Kristo, katika barua aliyoandika baadaye kwa waumini. Akiwasemea wale wasioamini katika 2 Petro 3:4 anasema kuwa, watahoji wakisema: "Iko wapi ahadi ile ya kuja kwake? Kwa maana, tangu hapo babu zetu walipolala, vitu vyote vinakaa hali hiyo hiyo, tangu mwanzo wa kuumbwa".

Unaweza ukawa umewasikia watu wakidharau, wakitumia maneno kama hayo. Lakini ni Mungu mwenyewe aliyeahidi kumtuma Bwana Yesu, na tunajua ya kuwa ataitimiza ahadi yake. Petro anaendelea katika mstari wa 9 na wa 10 kusema:

"Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie ('waifikie') toba. Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi".

### **Ushuhuda wa Paulo**

Yesu mwenyewe alimtokea mtume Paulo na kumtuma aende kuwahubiri wengine. Paulo anadai kuwa Injili aliyokuwa akihubiri alipewa na Yesu Kristo. Paulo alifundisha juu ya ujio wa mara ya pili wa Bwana Yesu Kristo. Katika 2 Timotheo 4:1 tunasoma Paulo akimwambia Timotheo:

"Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa kwa kufunuliwa kwake....."

Aliandika pia barua mbili kwa eklesia katika Thesalonike. Utazona nyaraka hizi ndani ya Biblia yako. Ndani yake kuna vifungu vinane vifupi-vifupi, na kuna kitu cha kushangaza ndani yake katika **kila** kifungu; Paulo anataja **ujio wa Yesu**.

Katika 1 Wathesalonike 4:16, anaongelea ufufuo wa wafu katika ujio wa Yesu:

"Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu, nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza".

Katika 2 Wathesalonike 1:7,8 Paulo anazungumzia:

"Kufunuliwa kwake Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake, katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana Yesu Kristo".

Hapa anamwongelea Yesu akirudi kuwaadhibu watu, lakini kama tukiendelea kusoma tutaona kuwa, anawaongelea pia watu wengine ambao, ujio wake utakuwa tukio kubwa la shangwe kwao, kwa kuwa atakuwa amekuja, "Kustaajabiwa katika wote waliosadiki katika siku ile" (ms. 10).

### **Yesu atafanya nini atakaporudi?**

Ujio wa Yesu utayabadili maisha ya kila mtu, atakayekuwa akiishi wakati huo. Litakuwa ni tukio kubwa sana kwa:

- (a) Waumini wanaomsubiri na kumtazamia.
- (b) Wote watakaokuwa wanaishi wakati huo, wasiojua Injili ya kweli.
- (c) Taifa la Wayahudi.

Tuyaangalie haya moja baada ya jingine:

**(a) Waumini wa kweli wanaomtazamia na kumngojea (Watu walio katika Kristo):**

Yesu atawafufua katika wafu wale wote waliokufa katika imani, na kuwakusanya pamoja waumini walio hai:

“Angalieni, nawaambia ninyi siri, hatutalala sote, lakini sote tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho, maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika” (1 Wakorintho 15:51,52).

Wale ambao wamekuwa si waaminifu watakataliwa, lakini kwa waliokuwa waaminifu, kutakuwa ni shangwe kuu; Yesu atawapa uzima wa milele. Paulo anatuambia katika Wafilipi, Yesu ataubadili: “Mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu” (Wafilipi 3:21).

Kama ilivyo kwake, watashirikishwa uzima usio na mwisho; usio na maumivu na machungu yoyote. Watamsaida Yesu katika kazi kubwa ya kuyafundisha mataifa yote juu ya Mungu, na kuwaongoza watu wa dunia waweze kuitikia upendo wake, na kwenda katika njia zake.

**(b) Watu wa dunia:**

Wakati atakapokuwa akirudi Yesu, hukumu za Mungu zitamwagwa juu ya watenda maovu, na kutakuwa na dhiki kubwa duniani. Hili linasikitisha, lakini haliyekubwa. Bila ya Mungu kuitikisa dunia, dunia haitaweza kamwe kumgeukia YEYE na kumkubali Bwana Yesu kuwa Mfalme wake anayemweka.

Baada ya hukumu hizo za Mungu kumwagwa, watu wa dunia watakuwa tayari kumkubali Yesu kuwa Mfalme wao. Naye atausimamisha utawala wa Mungu katika dunia; Ufalme wa Mungu. Uongozi wake utakuwa wa upendo na hekima, wenye kuwajali maskini na wanyonge. Hebu ifungue Zaburi ya 72 na uisome yote. Itakupa picha ya utawala wake. Inasemea vile atakavyowahurumia wenye shida, na wale wasio na msaada.

Watu wa dunia watakaopona katika hukumu hizo za Mungu, wataishi katika Ufalme wa Mungu na kupata mibaraka mingi. Watakuwa, hata hivyo, wakitutwa bado na dhambi, na hatimaye watakuwa kama inavyowatokea watu leo. Hata hivyo maisha yao yatakuwa marefu zaidi, na wakati wakiishi watakuwa wakizifundishwa Njia za Mungu. Fursa itakuwapo bado kwao ya kuipokea miongozo ya Bwana Yesu, au kuikataa.

Itakapofikia mwisho wa kipindi cha miaka 1000 cha utawala wa Yesu, kutakuwa na ufufuo wa pili na hukumu kwa wale walioishi katika dunia katika kipindi hicho cha miaka elfu moja. Wengi wao watapewa uzima wa milele, na wengine watakataliwa milele. Hatimaye, mauti yatakuwa yametokomezwa; hakutakuwa tena na kufa.

**(c) Itakuwaje juu ya Wayahudi?**

Yesu atarudi katika wakati ambao Taifa la Israeli wapo kwenye hekaheka kubwa. Watakuwa wamezungukwa na maadui pande zote. Yesu, kwa uweza wa Kimungu, atawashinda hao wanaopigana nao. Ndipo Wayahudi walio wengi watakapotambua hatimaye ya kuwa, Yesu alikuwa ndiye Mfalme na Mwokozi wao kweli waliyehidiwa, na ambaye walimsulubisha! Nabii Zekaria anasema: “Watamtazama yeye ambaye walimchoma, nao watamwombolezea” (Zekaria 12:10). Ndipo sasa watakapomkubali kwa furaha awe Mfalme wao.

Bwana Yesu atausimamisha Ufalme wa Mungu, na Wayahudi watakuwa wakati huo ‘Taifa Kiongozi’ juu ya mataifa yote. Mji wao mkuu, Yerusalemu, utakuwa ‘Makao Makuu’ ya dunia, na kuwa ‘kitovu’ cha Ibada ya Kweli kwa watu wote. Utakuwa ni wakati wa furaha sana kwa Wayahudi, baada ya mateso yao yote ya miaka

mingi. Upendo, furaha na amani ya hali ya juu vitatiririka kwa dunia kutoka katika Makao hayo Makuu mapya!

### **Kitatokea nini kwako wewe na mimi?**

Usume tena mfano ule wa wanawali kumi katika Mathayo 25:1-13. Kama tuna akili nzuri kama wale wanawali wenye busara katika kielelezo hicho, tutajifunza Neno la Mungu, na kujiandaa sasa kwa ujio wa Yesu. Bwana Yesu alipomwambia mtume Yohana, “Naam, Naja upesi” (Ufunuo 22:20), Yohana alimjibu, “Na uje, Bwana Yesu”.

Tujiulize, tutakuwa kama mtume huyu na kulifanya jambo hili la kurudi kwa Bwana Yesu liwe jambo la kuombea?

#### **Muhtasari**

1. Yesu Kristo anarudi duniani.
2. Tunaweza kuwa na uhakika juu ya hili, kwa kuwa alisema hivyo mwenyewe, na malaika na mitume walisema hivyo pia.
3. Atakapokuja atawapa wafuasi wake waaminifu uzima wa daima.
4. Ataifanya Israeli kuwa Taifa Kuu kati ya mataifa.
5. Atawafundisha watu wote wa ulimwengu Njia za Mungu.
6. Kama tuna busara, tutajiandaa sasa kwa ujio wake huo.

**Vifungu vya kusoma:** 1 Wathesalonike 4, Danieli 12:1-4, Mathayo 25:1-13

**Jifunze kwa moyo:** Matendo 1: 11

“Malaika wakasema: Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi hiyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni”.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

### ISHARA ZA KURUDI KWA YESU

**SOMO:** Luka 21

Yesu atarudi tena hapa duniani. Biblia inatuambia hili waziwazi sana, kama tulivyoona katika somo lililopita. Kuja kwake ni sehemu ya mpango wa Mungu kwa dunia yetu. Yesu atakuwa 'Mfalme wa Wafalme', akiiongoza dunia kutoka katika Kiti chake cha Enzi katika Yerusalemu.

Hii ilikuwa ahadi ya Mungu kwa Wayahudi katika Agano la Kale, na ni ujumbe muhimu sana wa Agano Jipya kwa watu wote. Wafuasi wa mwanzo wa Bwana Yesu waliutazamia wakati wa kuja mbeleni, wa: **"Kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana,"** atakapomtuma **"Yesu Kristo"** (Matendo 3:19,20).

Neno lililotafsiriwa 'kuburudishwa' hapa, maana yake hasa ni **'kurudishiwa-upya'** ('refreshing'-kwa lugha ya Kingereza). Ni kurudishiwa mambo upya au kuwekwa mwanzo-mpya, kutakakotokana na kurudi kwa Bwana Yesu.

Kurudi kwa Yesu kutakuwa ni tukio kubwa kuliko yote yaliyotokea, tangu kuumbwa kwa dunia. Kutayabadili maisha ya wote wanaoishi katika dunia hii. Kwa hiyo tunaweza kujiuliza, "jambo hili litakuwa lini?"

Hatuijui siku yenyewe. Yesu mwenyewe alisema: "Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake" (Mathayo 24:36). Lakini Mungu ametupa ishara zilizo wazi sana katika Neno lake. Yesu anatupa baadhi ya hizi katika Sura hiyo ya Mathayo 24, anazozihitimisha akisema: "...Myaonapo hayo yote, tambueni ya kuwa yu karibu milangoni" (Mathayo 24:33), yaani Ufalme wa Mungu umekaribia sana.

Mtu aliye safarini, anatambua anapona alama fulani njiani au kibao kuwa, anakaribia mwisho wa safari yake. Kwa namna kama hiyo, ishara tunazoziona katika dunia zinatutambulisha kuwa, tunakaribia kabisa wakati wa kurudi kwa Kristo.

Wanafunzi wa Yesu walipomuuliza Yesu: "Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?" (Mathayo 24:3), Yesu aliwapa ishara kadhaa. Aliwaambia kuwa Yerusalemu ingeharibiwa, na Wayahudi kutawanywa. Hili lilitokea miaka kama 40 tu baadaye, katika mwaka wa 70 (Baada ya Kristo). Aliendelea kuongelea juu ya kurudi kwake kwa kuwapa 'ishara' za kuchunguza. Zote zipo pia kwa ajili yetu leo.

**Ishara kwamba tunaishi katika siku za mwisho:**

### ISHARA KUHUSU WAYAHUDI

Biblia inasema kuwa, katika siku za mwisho:

- (a) Wayahudi watarudi katika nchi yao ya Israeli.
- (b) Waisraeli watakuwa ni taifa tena.
- (c) Jiji la Yerusalemu litawekwa huru kutoka kwa maadui zake.

### Maelezo:-

- (a) Wayahudi walikuwa wametawanywa dunia nzima katika mwaka wa 70 B.K. Tokea wakati huo, kwa karibu miaka 2000, hawakuwa na nchi iliyokuwa yao wenyewe. Lakini katika nyakati zetu hizi tumewaona wakiirudia Nchi ya Israeli, na kwa kufanya hivyo unabii wa Biblia kutimbia:

"Tazama, siku zinakuja, anasema BWANA, nitakapowarejeza watu wangu wa Israeli na Yuda waliofungwa, asema BWANA, nami nitawarudisha hata nchi niliyowapa baba zao, nao wataimiliki" (Yer.30:3).

- (b) Katika mwezi Machi 1948, ingawa kulikuwa na upinzani mkali sana kutoka kwa Waarabu, Taifa la Israeli lilianzishwa. Hakuna vikwazo vilivyoweza kuzuia hili lisitokee. Nchi hiyo tangu hapo imechukua nafsi yake kati ya mataifa ya ulimwengu. Mungu alisema hili lazima lingetokea, kupitia kwa nabii Ezekieli, zamani sana:

“Tazama, nitawatwaa wana wa Israeli toka kati ya mataifa walikokwenda, nani nitawakusanya pande zote, na kuwaleta katika nchi yao wenyewe, nami nitawafanya kuwa taifa moja katika nchi hiyo, juu ya milima ya Israeli” (Ezek. 37:21,22).

- (c) Yerusalemu sasa ni Makao Makuu ya Wayahudi. Soma maneno ya Yesu katika Luka 21:24, yanayoongelea kutawanywa kwa Wayahudi. Tambua hapa ya kuwa, Yesu alisema, mji wa Yerusalemu ungekanyagwa na mataifa, hata **‘majira ya mataifa yatakapotimia’**. Unaona vile msitari huu unavyosisimua?

Sasa, katika mwezi Mei 1967, Wayahudi walipambana katika Vita Ya Siku Sita, na kuiweka Yerusalemu huru kutoka kwa maadui zake. Jiji hilo ‘halikanyagwi’ tena na mataifa (halimilikiwi); liko tena mikononi mwa Wayahudi wenyewe. Hakika ni ishara kali kabisa ya kuwa ujio wa Bwana umekaribia.

### ISHARA KATIKA DUNIA TUNAMOISHI

Kila mahali duniani kuna matatizo; matatizo ambayo viongozi wa mataifa hayo wanashindwa kuyatatua:

- Mamilioni ya watu wanateseka kwa njaa, na wengine kufa, wakati wengine wanashiba na kusaza na kutupa.
- Kuna matatizo ya uchafuzi wa mazingira. Watu wanaiharibu dunia wanayoishi ndani yake kwa choyo na uzembe.
- Kuna matatizo ya ukuaji wa idadi ya watu. Ukuaji kwa baadhi ya nchi ni mkubwa mno kuliko uwezo wa serikali zake kumudu.
- Kuna miogogoro ya kivita kila mahali inayoleta mateso makubwa na vifo.

Yesu aliyaona haya mapema. Alisema, “Kutakuwa na ishara katika jua, na mwezi, na nyota, na katika nchi dhiki ya mataifa wakishangaa kwa uvumi wa bahari na msukosuko wake” (Luka 21:25).

Hili limekuwa kweli tukiangalia matatizo yanayoikabili dunia leo. Watu wanashindwa kujua wafanyeje. Katika msitari uliofuata Yesu anaendelea kusemea mioyo ya watu kuvunjika kwa hofu, “...na kwa kutazamia mambo yatakayoupata ulimwengu” (Luka 21:26). Siku hizi watu wanaogopa: wanahofia vita vya kinyuklia, na ajali za kinyuklia kama ile iliyotokea Japani mwaka 2011. Kuna hofu kubwa juu ya sunami, ugaidi, utekaji nyara, ujambazi, ukatili, uharibifu wa mali n.k. Viongozi wanababaika tu; wanashindwa kujua hasa la kufanya!

Imekuwa kama vile hakuna suluhu juu ya matatizo haya, lakini hebu ona kile Yesu anachosema katika msitari uliofuata tena:

“Hapo ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika wingu pamoja na nguvu na utukufu mwingi” (Luka 21:27).

Ni hakika tunaikaribia sana siku ya kurudi Bwana Yesu.

### Kutokumwamini Mungu na Neno lake

Mtume Paulo, akiwasemea watu wa wakati wake, alisema: “Kumcha Mungu hakupo machoni pao” (Warumi 3:18). Hivi si ndivyo ilivyo kwa watu hivi leo? Watu walio wengi hawataki kuusikia UKWELI ulio katika Neno la Mungu, na hawataki kufahamu habari ya Yesu kurudi kuusimamisha Ufalme wa Mungu.

Wanapendezwa zaidi na kwenda njia zao wenyewe, na kumsikiliza yeyote anayewaambia, sio lile lililo **kweli**, bali lile **wanalopenda** kusikia. Imeandikwa, watu kama hao wana ‘masikio ya utafiti’. Tafsiri hii ya Kiswahili

sio sahihi sana hapa. Tafsiri sahihi ingekuwa, “wana masikio yanayowawasha” (kwenye Kingereza ni ‘itching ears’). Paulo anasema:

“Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima, ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana *masikio ya utafiti* (‘masikio yanayowawasha’); nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo” (2 Timotheo 4:3,4).

Mtume Petro naye alisema, katika siku za mwisho watu watalibezwa Neno la Mungu. Anasema watalidhihaki wakisema, “Iko wapi ahadi ile ya kuja kwake?” (2 Petro 4:3,4). Naona kama ni hivi ndivyo hasa watu wanavyosema siku hizi.

### **Ukiukaji wa sheria**

Katika wakati Israeli walipokuwa wakiongozwa na Waamuzi, tunaambiwa: “Siku hizo hapakuwa na mfalme katika Israeli, kila mtu alifanya hayo aliyoyaona kuwa ni mema machoni pake mwenyewe” (Waamuzi 17:6). Matokeo ya hili yalikuwa ni mauaji, uporaji, ubakaji na vurugu za aina zote. Ni hivyo ilivyo leo. Watu hawajali Sheria za Mungu na wanazivunja sheria za mataifa yao kila siku. Kujizuia na kujidhibiti kimienendo ni kudogo sana.

Watu wamekuwa wachoyo sana, na kuwa wapenda fedha. Hawajali wengine wanavyoteseka, mradi wanapata kile wanachokitaka, iwe mali au madaraka. Paulo alisema ndivyo ambavyo ingekuwa katika ‘siku za mwisho’:

“Lakini ufahamu neno hili ya kuwa, siku za mwisho kutokuwako nyakati za hatari. Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha. Wasiowatii wazazi wao, wasio na shukrani..... wasiojizuia... wapedao anasa kuliko kumpenda Mungu” (2 Timotheo 3:1-5).

### **Wakati wa taabu**

Nabii Danieli aliongelea ujio wa wakati wa taabu ambao mfano wake haujakuwapo duniani. Huo ndio wakati tulio nao. Tunasikia mengi kuhusu ‘uchumi’ siku hizi. Ni uchumi imara unaoweza kuboresha maisha ya watu katika jamii. Unapodorora, hali za watu zinakuwa mbaya.

Katika mwaka 1973 Waarabu waliishambulia Israeli, lakini hawakuweza kuiangamiza. Baada ya hapo walipandisha sana bei ya mafuta yao na kuzorotesha uchumi wa mataifa mengi. Mataifa mengi bado yanategemea mafuta ya Mashariki ya Kati kwa uchumi wake. Matokeo, matajiri wameendelea kutajirika wakati maskini wakiendelea kudhoofika zaidi.

Kila taifa linaumia kunapokuwa na mitikisiko ya kiuchumi. Inasababisha watu kupoteza kazi na masononeko kila mahali. Inaonekana matatizo yaliyo mengi hayana ufumbuzi; kumekuja wakati wa taabu aliousema Danieli:

“Kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati huo huo.....Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele” (Danieli 12:1,2).

Taabu zilizopo zinaonesha tulivyo karibu na kurudi kwa Yesu.

### **Israeli na mataifa**

Waisraeli wanazungukwa na maadui. Mataifa ya Kiarabu yamekuwa yakinuia kuliangamiza Taifa la Kiyahudi na kuitwaa tena nchi ile, ambayo wanaihesabia kuwa ni yao. Kuna mivutano isiyoyisha na vita katika mipaka ya Israeli wakati wote.

Waarabu wanadai ndio wenye haki ya nchi hiyo, lakini ni Mungu aliyemuahidia Ibrahimu, Isaka na Yakobo hapo kale, na uzao wao kuwa, nchi hiyo ingekuwa urithi wao wa milele. Migogoro itaendelea na mataifa yote hatimaye yatafutwa kwenye vita vitakavyotokea.

Hapo ndipo Kristo atakaporudi. Yapo karibu kutokea haya; ujio wa Kristo u-karibu. Akiongelea nyakati hizi, mtume Petro anawaasa wale wanaoyafahamu mambo haya, akihoji: “Imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa?” (2 Petro 3:11).

Ni kitu ambacho sisi wote tunapaswa kujihoji wakati wote.

#### **Muhtasari**

Hatujui siku wala saa Bwana Yesu atakaporudi duniani kutoka mbinguni, lakini kuna ishara nyingi zinazoonisha atarudi karibuni. Baadhi yake ni hizi:

- ✚ Kurudi kwa Wayahudi kwenye nchi yao.
- ✚ Kuanza upya kwa Taifa la Israeli, mwaka 1948.
- ✚ Yerusalemu kuwa mji mkuu wa Israeli tangu mwaka 1967.
- ✚ Uwepo wa matatizo mengi duniani.
- ✚ Watu kuwa na hofu ya yanayoipata duniani.
- ✚ Vurugu na kuongezeka kwa ukatili.
- ✚ Uwepo wa taabu ambazo hazijatokea nyuma.
- ✚ Maadui wa Israeli kujiandaa kuipiga.

**Mistari ya kusoma:** Yeremia 31:10, Ezekieli 5:5, Yoeli 3:1, 2, 9-18

**Jifunze kwa moyo:** Luka 12:40

“Ninyi jiwekeni tayari kwa kuwa, saa msiyodhani ndipo ajapo Mwana wa Adamu”.



## MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

### *Karatasi ya maswali: namba 2*

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa 'Kazi ya ziada' unaweza kulijibu swali kama ukipenda, au kuliacha kama unaona huliwezi. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

#### **MASOMO: 5 – 8**

5. A. Uhai ulianzaje duniani?
- B. Eleza jinsi mwanadamu wa kwanza, Adamu, alivyoumbwa.
- C. Kumbukumbu la Torati 4: 15 – 19 linatuambia nini?
- D. Ibada za sanamu kwa sasa zipo kwa namna gani?

6 A. Sema kama semi zifuatazo ni Kweli au ni Uongo

- a) Sisi wote tunao wema fulani ndani yetu.
- b) Imani maana yake ni kuamini kwa kutumaini.
- c) Adamu alibidi afe kwa kuwa alitenda dhambi.
- d) Yesu hakufanya dhambi yoyote.
- e) Adamu alikwenda mbinguni alipokufa.

*Kazi ya ziada:*

6 B. Katika Isaya 20 kuna maelezo juu ya mateso na kifo cha Yesu. Andika mambo matatu yanayosemwa kumhusu Yesu na mawili yanayosemwa kutuhusu sisi.

7 A. Yesu Kristo yupo wapi sasa?

7 B. Yesu atakaporudi hapa duniani:

- a) Nini kitawatokea waumini wa kweli waliokwisha kufa?
- b) Nini kitawapata waovu?

8 A. a) Ni nini unafikiri ni ishara ya maana kuliko zote inayoonesha kuwa Yesu karibu atarudi hapa duniani?

b) Eleza kwa nini unafikiri ni ya muhimu sana.

8 B. Hebu iandike Yeremia 31:10. Ina maana gani?


*Kazi ya ziada:*

8 C. Katika Yoeli 3 tunasoma juu ya wakati ambao mataifa yote yatainuka kuipiga Israeli. Katika msitari wa 16 na 17 tunaambiwaaje?

**MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA****UFALME WAKO UJE****SOMO** : 1 Nyakati 29**“Ufalme wako uje. Mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni”.**

Ni mara ngapi umeyasema maneneo haya, au kuyasikia yakitamkwa na wengine? Yapo yakiwa ni sehemu ya maombi, ambayo Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuomba. Unaweza kuyasoma katika Luka 11:2-4. Tunayafahamu maneno haya vizuri, lakini unajua yanachokimaanisha?

Yaangalie tena. Ni maombi kwamba Ufalme wa Mungu uweze kuja ili mapenzi yake Mungu yaweze kutendeka katika dunia hii, kama yanavyofanywa wakati wote huko mbinguni. Kwa hiyo tunaona moja kwa moja kuwa, Ufalme ambao tunauomba ni wa kuwa hapa duniani, na kwamba, Ufalme huo wa Mungu ukija, ndipo watu watakapoyatimiza anayoyapenda Mungu, katika dunia hii.

**Nchi kwa ajili ya Ufalme**

Ufalme ni lazima uwe na mahali, na miaka elfu kadhaa iliyopita Mungu aliichagua nchi ambayo itakuwa Makao-Makuu ya Ufalme wake; ni nchi ya Israeli.

Yerusalemu ni Mji-Mkuu wa Israeli, na ndio utakaokuwa ‘kitovu’ cha utawala wa dunia, wakati Yesu Kristo akiwa Mfalme. Yesu mwenyewe alisema:

“Usiape kabisa, hata kwa mbingu, kwa maana ndicho kitu cha enzi cha Mungu; wala kwa nchi, kwa maana ndiyo pa kuwekea miguu yake; wala Yerusalemu, kwa maana ndio mji wa Mfalme mkuu” (Mathayo 5:34,35).

Yesu aliyapata maneno haya kwenye Zaburi ya 48; kitu kinachotudokezea kwamba, tunapaswa kulisoma Agano la Kale nalo vizuri. Msitari wa pili wa Zaburi hiyo unasema hivi juu ya mlima Sayuni, mahali Yerusalemu ilipo:

“Kuinuka kwake ni mzuri sana, ni furaha ya dunia yote, mlima Sayuni pande za kaskazini; mji wa Mfalme mkuu” (Zab.48:2).

Mlima Sayuni ni sehemu ya Yerusalemu na hapa unaelezewa kuwa, “Ni furaha ya dunia yote”. Zaburi ya pili nayo inasema: “Nami nimemweka mfalme wangu juu ya Sayuni, mlima wangu mtakatifu”. (Zab.2:6).

Zaburi hii ni unabii unaohusu wakati Yesu atakapokuwa akitawala kutoka katika mlima Sayuni. Mungu alichagua ‘kuliweka Jina lake’ katika jiji la Yerusalemu miaka mingi nyuma. Katika 2 Nyakati 6:5;6 alishasema: “...Lakini nimeuchagua Yerusalemu, jina langu liwe humo”.

Hapa kuna vifungu vingine viwili kwa ajili yako kuvisoma kiuangalifu:

- a) Isaya 62:1-7: Tunatakiwa kumwomba Mungu aifanye Yerusalemu kuwa mahali pa sifa duniani ('taji ya uzuri').
- b) Isaya 65:17-25: Mungu anaweka mpango wake juu ya Yerusalemu, na anatumia tuufurahie.

Kuliwahi kuwa na Ufalme wa Mungu katika dunia hii miaka mingi iliyopita, katika Agano la Kale. Je, unalifahamu hilo? Fungua sasa 1 Nyakati 29, na soma msitari wa kwanza, na wa 10 mpaka wa 13. Msitari wa 11, unasema:





“Ufalme ni wako, Ee BWANA, nawe umetukuzwa, u mkuu juu ya vitu vyote” (1 Nyakati 29:11).

Ufalme unaoongelewa, kama utakavyoona unavyoendelea kukisoma kifungu hiki, ni Ufalme wa Israeli, katika nchi ya Israeli, kwani tunasoma:

“Ndipo Sulemani akaketi katika kiti cha enzi cha BWANA, awe mfalme badala ya Daudi babaye” (1 Nyakati 29:23).

Kiti cha enzi alichokikalia Daudi na ambacho mwanawe Sulemani alikikalia baada yake, kilikuwa ni mamlaka katika **Yerusalemu**, mji uliokuwa mkuu katika nchi ya Israeli. Ufalme ambao aliutawala akiwa mfalme ulikuwa **Ufalme wa Israeli**.

Ni kwa nini Ufalme wa Israeli uliitwa Ufalme wa Mungu, na 'kiti chake cha enzi' kiliitwa, “Kiti cha Enzi cha BWANA?” Sababu ni kwamba:

-  Ni Mungu mwenyewe aliyewapa Waisraeli Ufalme huo.
-  Ni Mungu mwenyewe aliyeteua Yerusalemu kuwa Makao Makuu (1 Wafalme 11:13).
-  Ni Mungu mwenyewe aliyetoa Sheria za kuuongoza Ufalme huo (Zipo katika vitabu vya Mambo ya Walawi, Hesabu, na Kumb. La Torati).
-  Mfalme alikuwa akitawala **kwa niaba ya Mungu**.

### **Ufalme wa Mungu ulipinduliwa**

Mamia ya miaka yalipita. Wafalme mmoja baada ya mwingine waliitawala Israeli katika Yerusalemu. Baadhi yao walikuwa wafalme wazuri waliowaongoza watu wao kwa kumcha Mungu, na wafalme wengine walikuwa waovu; wasiozingatia Sheria za Mungu.

Mwisho ulifika wakati ambao Taifa la Israeli liliziacha mno njia za Mungu na mfalme katika Yerusalemu alikuwa mwovu mno. Mwenyezi Mungu aliamua kuuvunjilia mbali Ufalme huo.

Soma Ezekieli 21:25 – 27, na hasa msitari wa 27 unaosema: “Nitakipindua, nitakipindua, nitakipindua (Kiti cha Enzi cha Israeli katika Yuda); hiki nacho hakitakuwa tena, hata atakapokuja yeye ambaye ni haki yake, nami nitampa”.

### **Yeye ambaye 'ni haki yake'!**

Tunaweza kuona kutoka katika mistari hiyo ya Ezekieli kuwa, kulikuwa na mtu 'wa kuja' ambaye Kiti hicho cha Enzi cha Ufalme wa Mungu kilikuwa ni 'haki yake'. Huyu alikuwa awe ndiye mrithi wa kukifaa, na Mungu alikuwa amepanga kukimpa.

Tokea wakati huo wa mfalme huyo wa mwisho aliyeng'olewa kutoka katika kiti-hicho-cha-enzi, mpaka sasa, hakujawa na mfalme wa Kiyahudi aliyetawala katika Yerusalemu tena. Lakini fungua Biblia yako kwenye Luka 1:31 – 33 na usome maneno yaliyosemwa na malaika kwa Mariamu, mama yake Yesu. Akisemea malaika juu ya jina la Yesu, alisema:

“Huyo atakuwa Mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye Juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake” (Luka 1:32).

Ni nani aliyekuwa na ‘haki’ ya Kiti cha Enzi cha Ufalme wa Mungu? Hakika ni Yesu, Mwana wa Mungu. Haki yake ina sura mbili:

1. Alikuwa ni Mwana wa Mungu.
2. Mama yake Mariamu alikuwa wa uzao wa Daudi.

Kuna kutokuelewa kwingi kunakohusu utawala wa Yesu katika Ufalme wa Mungu. La muhimu kutambua ni kwamba:

- ✚ Yesu atakuwa mtawala katika dunia.
- ✚ Kiti chake cha enzi kitakuwa ni Kiti cha Enzi cha Daudi katika Yerusalemu.
- ✚ Yerusalemu itakuwa Makao Makuu ya Ufalme wa Mungu duniani.

Hii ndio sababu ya Yesu kurudi duniani. Kusudi la Mungu linawahusu wanadamu katika dunia yake hii, na atalitimiza, ndio maana Mwenyewe anasema: “Dunia hii nzima itajawa na utukufu wa BWANA” (Hesabu 14:21).

Kufikiri kwamba mtu anakwenda mbinguni anapokufa, hakwendani na Maandiko; hakukubaliani na kile Maandiko yanachofundisha. Ufalme unaoanzishwa ni wa hapa katika dunia. Mungu anaongoza kutoka katika mbingu, lakini mpango wake ni kumtuma Yesu kuitawala dunia. Wafuasi wake walio waaminifu wa enzi zote watakuwa watu wa kumsaidia katika jukumu hili kubwa.

Yesu alidai kuwa ni Mfalme. Kwenye kesi yake wakati Pilato alipomuuliza, “Wewe u mfalme basi?”, yeye alijibu, akisema: “Wewe wasema, kwa kuwa mimi ni mfalme” (Yohana 18:37). Hii ni namna ya Kiyahudi ya kusema, “Ndiyo!”

Juu ya msalaba Yesu aliosulubiwa, iliandikwa, “HUYU NI YESU, MFALME WA WAYAHUDI” (Mathayo 27:37). Maadui zake walidhani wanamdhahiki; hawakujua kuwa wanachosema ni KWELI.

Injili aliyoihubiri Yesu ilikuwa ni Habari Njema ya huo Ufalme wa Mungu. Katika Luka 8:1, tunasoma kuwa: “Alikuwa akizunguka-zunguka katika miji na vijiji, akihubiri na kuitangaza **habari njema ya Ufalme wa Mungu**”.

Sasa unajua sababu ya kurudi kwake Yesu. Anarudi kuusimamisha tena Ufalme wa Mungu katika dunia.

#### KITI CHA ENZI CHA DAUDI KATIKA YERUSALEMU

<b>UFALME WA ISRAELI</b> Wafalme wakiwa katika Kiti cha Enzi: Daudi, Sulemani.....kuanzia kama mwaka 1000 (kabla ya kuzaliwa Kristo). <b>VITABU:</b> Samweli na Wafalme.	<b>KITI CHA ENZI KITUPU</b> Hakuna wafalme kuanzia kama mwaka 600 (kabla ya kuzaliwa Kristo hadi leo; tulipo). <b>KITABU:</b> Ezeieli 21:27	<b>YESU: KURUDI KUTOKA MBINGUNI</b> Kusimamishwa kwa Ufalme wa Mungu katika dunia. Mbeleni ..... <b>KITABU:</b> Luka 1:32
---	---	--

### **Ufalme huo na sisi**

Pengine unaweza kufikiri, kwa nini, basi, tuombe ‘Ufalme wako uje’, wakati Ufalme wenyewe ni wa Kiisraeli? Unatuhusu nini sisi?

Unavyoendelea kujifunza utagundua kuwa, Ufalme huo ambao Yesu atauongoza, utapanuka sana na kuenea maeneo ya mbali, kuliko ilivyokuwa kwa ule Ufalme wa Mungu wa kwanza. Utaenea dunia yote, na kuleta amani kwa watu wote.

Kwa hiyo tunauomba Ufalme wake uje, na tunaomba pia kwamba, Yesu atakaporudi aweze kutuambia: “Njoni mliobarikiwa na Baba yangu, urithini Ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu” (Mathayo 25:34).

#### **Muhtasari**

Ona vile kila sehemu ya Biblia inavyosaidia kuelezea sehemu nyingine. Sasa tumejifunza kuwa:

1. Ufalme wa Mungu uliwahi kuwepo katika nchi ya Israeli.
2. Mungu aliusitisha Ufalme huo, lakini aliahidi kuurudishia upya na kumpa anayeustahili kuurithi.
3. Mrithi huyo ni Yesu; atakikalia hicho Kiti cha Enzi cha Daudi katika Yerusalemu, akiwatawala Wayahudi na ulimwengu wote.
4. Waaminifu wote wataishiriki mibaraka ya Ufalme huo katika dunia.

**Vifungu vya kusoma:** Mwanzo 22, Wagalatia 3

**Jifunze kwa moyo:** Ufunuo 11:15

“Malaika wa saba akapiga baragumu, pakawa na sauti kuu katika mbingu, zikisema, Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atamiliki hata milele na milele”.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

### MUNGU ANAVYOIONA HISTORIA

**SOMO:** Danieli 2

Mungu hatazami historia kwa namna tunavyoitazama sisi. Ie watu wanayoiona kama dola yenye nguvu sana, inaweza kuwa si chochote machoni pake. Kwa upande mwingine, mtu anayeonekana mkimya, mwenye unyonge, anayedharauliwa na wenzake, anaweza kuwa wa thamani kubwa machoni pa Mungu.

Biblia ni kitabu cha historia cha Mungu, na Wayahudi ni watu wake. Mpango wa wokovu wa Mungu kwa wanadamu umejengekea kwa Wayahudi, ingawa kwa njia ya Kristo umetanuka kuyafikia mataifa yote. Kwa sababu hiyo, basi, historia katika Biblia inawahusu zaidi Wayahudi.

Katika Biblia kuna maelezo mafupi ya watu kadhaa wa muhimu:

**ADAMU:** Adamu alikuwa mtu wa kwanza. Mungu alimuumba akiwa mwema kabisa, lakini hakumtii Mungu. Tangu wakati huo, watu wote wamemkiuka Mungu na wanaendelea kumkiuka kwa namna moja au nyingine, na wote wanakufa.

**NUHU:** Nuhu alizaliwa zaidi ya miaka elfu moja baada ya Adamu. Katika siku zake, wanadamu walikuwa wamekuwa waovu mno kiasi kwamba, Mungu alituma gharika na kuwaangamiza wote, akibakia Nuhu na familia yake tu. Nuhu alimwamini Mungu na kumtii (Mwanzo 6).


**IBRAHIMU:** Ibrahimu anaitwa katika Biblia 'Rafiki wa Mungu'. Mungu alimwambia aiache nyumba yake kule Uru, aende kuishi Kanaani, na Ibrahimu alimtii. Mungu alifanya naye Maagano ya muhimu sana (Mwanzo 12).

**ISAKA:** Isaka alikuwa mwana wa Ibrahimu, aliyezaliwa ki-muujiza wakati Ibrahimu na mke wake, Sara, wakiwa wazee sana kuweza kupata mtoto (Mwanzo 21).

**YAKOBO:** Yakobo alikuwa mwana wa Isaka. Mungu alimbadilisha jina na kumwita 'Israeli', maana yake, 'Mkuu pamoja na Mungu'. Yakobo alipata wana kumi na wawili.

**YUSUFU:** Yusufu alikuwa mmojawao wale wana kumi na wawili wa Yakobo. Kaka zake walimuonea wivu, na kumuua apelekwe Misri kuwa mtumwa. Yalimpata majaribu mengi, lakini Mungu alimbariki akawa wa pili kwa ukuu, kimamlaka Misri.

Baada ya hapo, familia yote ya Yakobo ilijiunga na Yusufu kule Misri (Mwanzo 46). Miaka mingi baadaye, wakiwa wameongezeka na kuwa taifa la Kiyahudi, walifanywa kuwa watumwa na Wamisri.



**MUSA:** Wazazi wa Musa walikuwa Wayahudi, lakini alilelewa na kuwa mwana wa binti Farao, mfalme wa Misri. Mungu alimtumia Musa kuwatoa Waisraeli Misri, na kuwaleta katika nchi ya Kanaani, aliyokuwa amewaahidia.

Mungu aliwapa watu hawa Sheria za hekima na haki, lakini hawakupenda kuzitii. Walizipenda zaidi ibada za Kimisri; ibada za sanamu.

#### **SANAMU**

Sanamu ni kitu chochote kinachoabudiwa; badala ya Mungu wa Kweli. Watu wameabudu vitu vingi- jua, miti, vinyago, mawe, picha za vitu, mali n.k. Vyote hivi ni **miungu ya uongo**; haviwezi kusaidia, haviwezi kuokoa.

Baada ya miaka 40 ya kuzagaa-zagaa nyikani, ambapo waliokuwa watu wazima karibu wote walikufa kwa kukosa imani, uzao wao ulifika katika nchi Mungu aliyokuwa amewaahidia.

**YOSHUA:** Ndiye aliyewaingiza watu hao katika nchi ya ahadi, nchi ya Kanaani.

#### **Waamuzi ulingoni**

Kwa miaka kama 400 Wayahudi waliongozwa kwa vipindi tofauti-tofauti na Waamuzi, lakini Mungu ndiye aliyekuwa Mfalme wao. Mara kwa mara walizivunja amri zake, na aliwaadhibu kwa kuleta mataifa ya nje kuwapiga. Matatizo yalipowazidia, walimgeukia Mungu na aliwaokoa kwa kutuma Waamuzi.

#### **Watu wataka Mfalme**


Badala ya kuishi kwa furaha wakimtii Mungu, Wayahudi waliomba wapatiwe mfalme. Hawakuwa wakimtaka Mungu. Walitaka mfalme wanayeweza kumwona, kama ilivyokuwa kwa mataifa mengine.

**SAULI:** Alikuwa ndiye aliyekuwa mfalme wa kwanza. Hakumpendeza Mungu; hakuwa mtiifu. Mfalme wa pili, Daudi, anaitwa katika Biblia 'Mtu anayefanana na moyo wa Mungu'. Huyu alikuwa mtiifu sana. Alipewa ahadi za kipekee sana na Mungu, za kutimizwa na Bwana Yesu Kristo (2 Samweli 7).

Daudi alifuatiwa katika kiti chake cha enzi na mwanawe, Sulemani, lakini Israeli walikuwa bado ni Ufalme wa Mungu, kama tulivyoona katika 1 Nyakati 29: 23.

#### **Ufalme unagawanyika**

Baada ya Sulemani, Ufalme ulijigawa sehemu mbili. Ufalme wa Kaskazini ukaitwa Ufalme wa Israeli na ule wa Kusini ukaitwa Yuda. Watu wa Israeli upande wa kaskazini walikuwa waovu sana kiasi kwamba, Mungu aliwaleta Waashuru juu yao. Waliwachukua mateka, na hawakuirudia tena nchi yao.



Ufalme wa Yuda, kusini, hawakuwa na unafuu wa maana. Baada ya muda walibebwa nao mateka kupelekwa Babeli. Tokea wakati huo hakujawa na mfalme tena katika nchi takatifu. Baadhi ya watu wa Yuda waliirudia nchi yao ya Israeli baada ya miaka 70.

#### **Agano Jipya**

Hatimaye, kama miaka 400 baada ya Yuda kurudi na Agano la Kale kufungwa, Mungu alimtumia Mwanawe mwenyewe, Bwana Yesu Kristo. Agano Jipya linatupa simulizi juu ya Yesu, na jinsi kanisa la Kikristo lilivyoanza.



Ndugu zake wa Kiyahudi karibu wote walimkataa Yesu. Baada ya hapo Mungu alitoa 'ofa' ya uzima kupitia kwa Yesu kwa mataifa yote, kwa njia ya Agano Jipya. Humo tunasoma vile hao Wakristo wa kwanza walivyosafiri mbali wakihubiri juu ya 'namna mpya' ya maisha. Kuhubiri kwa namna hiyo bado kunaendelea kufanywa hata sasa.

### **Picha ya Falme za Dunia**

Kabla hujajifunza somo linalofuata, hebu jaribu kuichunguza kwa makini picha inayofuata.



Kichwa cha **Dhahabu**  
**BABELI**

Kama miaka 600 (Kabla ya Kristo)

Kifua na mikono ya **Fedha**  
**WAMEDI – WAAJEMI**

Kama miaka 450 (Kabla ya Kristo)

Tumbo na kiuno cha **Shaba**  
**UYUNANI (UGIRIKI)**

Kama miaka 300 (Kabla ya Kristo)

Miguu ya **Chuma**  
**RUMI**

Mwanzo wa Enzi ya Ukristo  
Nyayo: **Nusu chuma/ Nusu udongo.**

Maono yanayoihusu picha hii, ni historia inayohusu ulimwengu kuanzia wakati wa Dola ya Babeli, kushuka mpaka nyakati zetu hizi, na kuendelea mbele. Yanaonesha vile Mungu anavyotambua mataifa na kuziongoza nchi, na ameelekeza lini Ufalme wa Mungu utakuja.

Unakumbuka vile Waisraeli (wa Yuda) walivyochukuliwa mateka kwenda Babeli? Miongoni mwao alikuwapo kijana mmoja aliyeitwa Danieli.

Usiku mmoja, Nebukadreza, aliyekuwa mfalme wa Babeli, alipata ndoto moja ya ajabu sana. Ndoto hiyo ilitumwa kwake na Mungu, na Danieli, kwa hekima aliyopewa na Mungu, alimfafanulia maana yake.

Mfalme aliona sanamu kubwa sana, iliyokuwa ikifanana na picha ya mtu. Sanamu hiyo ilisimama badala ya dola nne kubwa: Dola ya Babeli, Dola ya Wamedi na Waajemi, Dola ya Wayunani, na Dola ya Warumi. Zote hizi katika historia ya dunia zilishamiri kwa vipindi fulani, moja baada ya nyingine, na kupita. Tunaweza kusoma habari zake katika vitabu vya Historia vya kawaida.

Kile kichwa cha dhahabu kiliwakilisha ufalme wa Babeli, ambao ulikuwa umenawiri sana. Kifua na mikono katika sanamu yalikuwa ni madini ya fedha, na yaliwakilisha dola ya Wamedi na Waajemi. Chini yake tumbo na kiuno ilikuwa shaba, ikiwakilisha dola ya Wayunani.



Hatimaye ilikuja dola ya Warumi iliyokuja kuutawala ulimwengu. Iliwakilishwa na miguu ya chuma; chuma kwa sababu ilikuwa kali na ya kikatili, yenye nguvu sana. Dola hii ilipanuka na kuenea maeneo ya mbali zaidi kuliko dola zote, na miongozo yake ya kisheria ni msingi na sheria za mataifa mengi hata leo. Ni katika wakati huu wa dola ya Kirumi alipozaliwa Bwana Yesu na ni askari wa Kirumi waliomsulubisha.

Baada ya mamia ya miaka, dola ya Kirumi nayo ilisambaratika. Hakujatokea tena dola inayojulikana kuwa juu ya mataifa, kwa namna ilivyokuwa.

Kwa miaka kama 1500, historia ya dunia imekuwa kwenye nyayo za sanamu ile ya Nebukadreza. Ni mchanganyiko wa chuma na udongo; mataifa yenye nguvu na mataifa dhaifu. Ndivyo ilivyo leo.

Alafu, katika ndoto, Nebukadreza aliona jiwe dogo ambalo, “Lilichongwa mlimani bila kazi ya mikono” (Dan. 2:45). Hilo lilipiga sanamu hiyo kwenye miguu yake, na kuivunja vipande vipande. Kisha jiwe hili dogo lilikua likawa mlima mkubwa, uliojaza dunia yote. Jiwe hilo lililotoka juu, lililokatwa ‘bila ya kazi ya mikono’ linamwakilisha Yesu, ambaye hakuwa na baba wa kibinadamu. Atakaporudi duniani, atazivunja-vunja falme za kibinadamu, na kuusimamisha Ufalme wa Mungu, utakaokua na kuijaza dunia yote.

Historia ya dunia kwa sasa tupo katika nyakati za hicho chuma na udongo; ni wakati wa mitengano. Baadhi ya mataifa ni tajiri na yenye nguvu, na yaliyo mengi ni madhaifu. Hakuna dola moja. Yanaridhiana katika baadhi ya mambo tu, hayawezi kuwa na umoja wa maana, kama ambavyo vipande vya chuma visivyoweza kuungana na udongo. Hayawezi kushikamana. Muda si mrefu Yesu atarudi. Atazivunja tawala za kibinadamu, na kuusimika utawala wa Mungu, yeye akiwa ndiye Mfalme, na Ufalme wake utakua na kuenea ulimwenguni pote.

Mengi ya yale yaliyoelezwa kuihusu ndoto ya Nebukadreza, yametimia na sasa ni historia. Tunaweza kuwa na uhakika ya kwamba kipande kilichobaki cha mwisho (cha wakati tulio nao), nacho kitatimia. Kumbuka: Ufalme unaozungumziwa ni wa hapa duniani.

#### **Muhtasari**

1. Agano la Kale linazungumzia juu ya historia ya taifa la watu walioteuliwa na Mungu; Waisraeli.
2. Agano Jipya ni juu ya Yesu, na linatuambia vile Injili ilivyohubiriwa kwa mataifa baada ya kufufuka kwa Yesu.
3. Ndani ya Agano la Kale na Agano Jipya tunasoma juu ya kurudi kwa Kristo duniani kuusimamisha Ufalme wa Mungu.
4. Unabii wa Danieli unaonesha jinsi dola nne kubwa zilivyopokezana katika historia ya ulimwengu. Tunaishi katika nyakati za ‘uayo’, na tupo kwenye ‘vidole’, tukilingojea ‘jiwe’ kurudi kuvunja serikali za kibinadamu.

#### **Vifungu vya kusoma:**

Kuna vifungu vingi vinavyotajwa katika somo hili. Jaribu kuvisoma vyote; vitakuza uelewa wako. Baada ya hapo soma Matendo 7.

#### **Msitari wa kuushika:** Danieli 2:44

“Na katika siku za wafalme hao, Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake, bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele”.

**MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA****UFALME WA MUNGU – AMANI DUNIANI**

**SOMO:** Isaya 35

**Amani Duniani – Lini?**

Yesu alipozaliwa, malaika waliimba kwa shangwe. Maneno ya wimbo wao yameandikwa katika Luka 2:14: “Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia”.

Hata hivyo tangu wakati huo hadi sasa, hakujawahi kuwa na amani ya sawasawa inayodumu katika dunia. Haitaweza kuwapo, mpaka hapo Yesu atakaporudi duniani kuusimamisha Ufalme wa Mungu. Agano la Kale linatambia mengi kuhusu Ufalme huo, na linatupa vidokezo vingi vya wakati wa amani na neema utakaoletwa na Ufalme huo.

**Ukubwa wa Ufalme huo**

Hebu iangalie Zaburi ya 72. Katika Zaburi hii tunapewa picha kwa njia ya maneno, ya wakati Ufalme wa Mungu utakaposimamishwa katika dunia. Lakini, kwa sasa, angalia hasa msitari wa 8 unachosema:

“Na awe na enzi toka bahari hata bahari, toka mto hata miisho ya dunia”.

Hapa tunaambiwa kuwa, Ufalme atakaousimamisha Yesu, wenye chimbuko lake katika Israeli, utaenea dunia nzima. Tunaona kitu kama hicho katika Zaburi 2:8 ambapo Mungu anasema na Yesu, akimwambia:

“Uniombe, nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako, na miisho ya dunia kuwa milki yako”.

Hebu tutazame msitari mmoja zaidi. Katika Zekaria 14:9 tunaambiwa:

“Naye BWANA atakuwa Mfalme juu ya nchi yote, siku huyo BWANA atakuwa mmoja, na jina lake moja”.

**Utawala wa Kristo**

Yesu Kristo atatawala kutokea Yerusalemu, ‘makao yake makuu’, ambayo kuna wakati aliyaita, ‘Mji wa Mfalme Mkuu’ (Mathayo 5:35). Sheria zake ndipo zitakapotokea, na kuenea duniani mwote. Katika Isaya 2, tunaambiwa: “Katika Sayuni itatoka sheria, na neno la BWANA katika Yerusalemu” (Isa 2:1-4).

**Ufalme mzuri**

Kama ungetakiwa kusema ni hali gani ungependa kuiona kwenye dunia iliyo bora kabisa, ungesemaje? Natumaini, kati ya mambo ambayo ungeyatamani sana yangukuwa ni: mazingira ya amani; kusiwe na hofu, kuwe na ufanisi na utulivu wa kuweza kuyafurahia matunda ya kazi zako, n.k. Ungeweza pengine kuwa na mawazo ya kitu kama kile nabii Mika anachotupa, akisema:

“Naye (Yesu Kristo) atafanya hukumu kati ya watu wa kabila nyingi, naye atawakemea mataifa wenye nguvu walio mbali, nao watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe mundu, taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine, wala hawatajifunza vita tena kamwe. Bali wataketi kila mtu chini ya mzabibu wake, na chini ya mtini wake, wala hapana mtu atakayewatia hofu; kwa kuwa kinywa cha BWANA wa majeshi kimesema hivi” (Mika 4:3,4).

Lakini kabla hakujawa na amani, itakuwa lazima kuwe na jitihada ya makusudi kati ya watu, ya kutembea katika njia za Mungu. Wakati wote watu wanapokuwa wakiziendea njia zao wenyewe, ni lazima kuwe na matatizo. Kwa hiyo jambo kubwa la kwanza atakalofanya Bwana Yesu litakuwa kuyafundisha mataifa yote njia za Mungu.

Lakini unaweza kusema, wapo tu ambao hawatakuwa tayari kumsikia. Hilo ni kweli, lakini, hao wasiomtii wataadhibiwa. Tunasoma katika Isaya 11:4 kuwa: “Kwa pumzi ya midomo yake atawaua wabaya”.

Kumbuka, Yesu atakapokuja tena, atakuwa na uweza wote.

### **Ni nani watakaokuwa katika Ufalme huo?**

1. Kwanza kutakuwa na **watawala**. Hawa watakuwa ni wanaume na wanawake ambao wamekuwa **wafuasi**. Hawa ni wote waliomfuata Yesu katika nyakati zote mpaka anaporudi. Sasa watakuwa wamepewa uzima usio na mwisho na Yesu katika kuja kwake. Watakuwa **Wafalme** na **Makuhani**, wakimsaidia Yesu kuitawala dunia. Watakuwa watu ambao hawafi; watu wasioweza tena kufa:

“Nao waimba wimbo mpya wakisema, Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake, kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu, nao wanamiliki juu ya nchi” (Ufunuo 5:9,10).

2. Watakuwapo pia Wayahudi waliompokea Yesu kuwa Mfalme wao. Yerusalemu itakuwa ni Makao Makuu ya dunia nzima. Mataifa yote yataielekea, kwa kuwa ndipo Sheria ya Mungu itakapokuwa ikitokea:

“Wakati ule utauita Yerusalemu kiti cha enzi cha BWANA, na mataifa yote watakusanyika huko Yerusalemu, kwa ajili ya jina la BWANA, wala hawatakwenda tena kwa ukaidi wa moyo wao mbaya” (Yeremia 3:17).

Kristo atakuwa miongoni mwao na watakuwa wamebarikiwa sana. Lakini watakuwa bado wakifa; watakuwa hawajapata uzima wa milele.

3. Kristo atakapokuja, hukumu za Mungu zitakuwa kali, na watu wengi watakuwa. Wale watakuoachiwa kuendelea kuishi popote pale walipo katika dunia, watakuwa chini ya mamlaka ya Yesu, wakijifunza kufanya yale yanayompendeza Mungu. Neno la Mungu kwa Isaya linasema:

“Hukumu zako zikiwapo duniani, watu wakao duniani hujifunza haki” (Isaya 26:9).

### **Neema kwa wote**

Kutokana na mazingira bora kabisa yatakyokuwapo, kutakuwa na mibaraka kwa kila mtu. Zaburi ya 72:16 inasema:

“Na uwepo wingi wa nafaka juu ya milima, matunda yake na yawaye-waye kama Lebanoni”.

Juu ya milima kwa kawaida huwa hakuna kitu. Kama kunaweza kuwa na nafaka nyingi katika vilele vya milima, tunaweza kujua kwa kiasi gani mavuno yatakuwa mengi mabondeni. Zaburi ya 67:6 inatoa picha ya wakati huo, ikisema: “Nchi imetoa mazao yake, MUNGU, Mungu wetu ametubariki”.

Hata majangwa yatakuwa kijani siku hizo. Soma mistari miwili iliyopo tena katika Isaya, inayosisimua, inayotuambia:

“Nyika na mahali palipo ukiwa patafurahi, jangwa litashangilia na kuchanua maua kama waridi. Litachanua maua mengi, na kufurahi, naam, kwa shangwe na kuimba” (Isa 35:1, 2).

### **Kuponywa kwa akili na mwili**

Pamoja na mibaraka hii, kutakuwa na mibaraka ya afya bora na nguvu.

Yesu alipoishi duniani miaka 2000 iliyopita, aliwapa afya wengi waliokuwa wagonjwa, kwa kutumia uweza aliopewa na Mungu. Katika Ufalme wa Mungu, uweza huo utaonekana tena. Endelea kusoma Isaya 35 msitari wa 6:

“Ndipo mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kulungu, na ulimi wake aliye bubu utaimba”.

Tunaweza pia kuona kwamba, watu wale wanaokufa (wasiopata uzima wa milele) wataishi maisha marefu zaidi kuliko wanavyoishi sasa. Nabii Zekaria anatuambia hivyo ndivyo itakavyokuwa. Anasema:

“Wazee wanaume na wazee wanawake watakaa tena katika njia za Yerusalemu, kila mtu ana mkongojo wake mkononi, kwa kuwa ni mzee sana. Na hizo njia za mji zitajaa wavulana, na wasichana, wakicheza katika njia zake” (Zek. 8:4,5).

Mistari hii inaiongelea Yerusalemu, lakini, kama tulivyoona, mibaraka ya Ufalme huo itaenea maeneo yote ya dunia.

### **Neno thabiti la Mungu**

Pengine utasema: “Haya yote yanaonekana mazuri sana, lakini nina shaka hayawezi kutokea”. Kama ahadi hizi tunazosisoma zingewategemea wanadamu, kwa hakika tusingeweza kuziwekea tumaini. Hata mtu anayeonekana kuwa mkweli sana, anaweza kushindwa kutekeleza anayowaahidi wengine kwa sababu ya udhaifu wa kibinadamu.

Lakini ahadi hizi zinatoka kwa Mungu, na kwa sababu hiyo tunaweza kuzitumainia kabisa. Hebu soma Isaya 55:6-11. Katika msitari wa 11 Mungu anasema: “Ndivyo litakavyokuwa neno langu, litokalo katika kinywa changu, halitanirudia bure, bali litatimiza mapenzi yangu, nalo litafanikiwa katika mambo yale niliyolituma”.

Kwa hiyo tunaweza kuutazamia kwa matumaini mema wakati huo unaokuja wa utukufu, unaoletwa na Mungu aliye juu mbinguni. Utakuwa kweli wakati wa furaha na, “Amani duniani, kwa watu aliowaridhia” (Luka 2:14).

### **Utimilifu mkubwa zaidi**

Kipindi cha Ufalme kitakachochukua miaka elfu moja, kitakuwa kipindi kizuri ajabu, lakini hakitakuwa kikamilifu. Mtu wa kawaida anayeishi katika enzi hiyo ya Ufalme, bado atakuwa na hulka ya ubinadamu-wake, inayopata urahisi kukosea na kushindwa. Bado watu watazeeka na kufa. Tunaambiwa pia kwamba, yapo mataifa yatakayofanya uasi dhidi ya utawala wa Bwana Yesu, utakapokaribia mwisho wa kipindi hicho.

Bwana Yesu atawashinda vibaya; hakuna shaka juu ya hili. Waliokufa watafufuliwa na Yesu, na hukumu itapita. Wakati huo, wale ambao wamekuwa waaminifu katika wakati huo wa Ufalme, watapelelewa nao tuzo yao ya uzima wa milele.

Baada ya hapo, dunia yote itajazwa utukufu wa Mungu, naye Muumba Mkuu wa yote atakuwa ‘yote katika wote’ (1 Wakorintho 15:28).

#### **Muhtasari**

1. Yesu atakuja tena na kuwa Mfalme wa dunia.
2. Makao yake makuu yatakuwa Yerusalemu.
3. Dunia itakuwa mahali pa amani na neema, afya bora na furaha.
4. Katika Ufalme wa Yesu, kila mtu atajifunza kuzitii amri za Mungu.
5. Katika Ufalme huo kutakuwa na:
  - (a) Watu wasiokufa: Ni wale waliomfuata Yesu na kumtii Mungu katika maisha yao ya sasa. Wakiwa wamepelelewa uzima usio na mwisho, hawatapatwa na machungu, wala kulazimika kupambana na dhambi tena. Ndio watakaomsaidia Yesu kutawala na kuiweka sawa dunia na watu wake, katika Ufalme wa Mungu.
  - (b) Watu wa kawaida (wanaokufa), watakaokuwa wameokoka kwenye zile hatari na hekaheka za hukumu za Mungu juu ya dunia iliyojaa uovu, watajifunza kumtumikia Mungu na kumcha na kumwabudu.

**Vifungu vya kusoma:** Zaburi 72; Mika 4: 1-7

**Kujifunza kwa Moyo:** Zaburi 22: 27, 28

“Miisho yote ya dunia itakumbuka, na watu watamrejea BWANA, jamaa zote za mataifa watamsujudia. Maana ufalme una BWANA, naye ndiye atawalaye mataifa”.

KURUDI KWA KRISTO DUNIANI		KRISTO ANAUKABIDHI UFALME KWA BABA YAKE
WAKATI TULIO NAO	UFALME WA MUNGU DUNIANI (Miaka 1000)	MUNGU ANAKUWA “YOTE KATIKA WOTE”
Falme za wanadamu	KRISTO ANAITAWALA DUNIA AKIWA NI MFALME	Watu wasiokufa tu!
Mwisho wa falme za wanadamu; wanafufuliwa.	Watu wasiokufa na watu wanaokufa.	Mwisho wa dhambi zote na mauti.
<b>Jedwali la falme za wanadamu na Ufalme wa Mungu.</b>		

## MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

### *Karatasi ya maswali: namba 3*

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa 'Kazi ya ziada' unaweza kulijibu swali kama ukipenda, au kuliacha kama unaona huliwezi. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

#### **MASOMO: 9 – 11**

9 A. Ufalme wa Mungu enzi za kale:

- a) Ulikuwa wapi?
- b) Mfalme wake wa kweli aliyetoa sheria zake alikuwa ni nani?

B. Ufalme wa Mungu ujao:

- a) Utakuwa wapi?
- b) Ni nani atakayekuwa Mfalme?
- c) Makao yake makuu yatakuwa wapi?
- d) Itakuwa lini?

10 A. Mwandike huyo mtu! (Majina yao yote yapo katika Somo la 10)

- a) Aliokolewa kufa maji kwa sababu ya kumtii Mungu.
- b) Malaika wa Mungu alimtokea katika kichaka kilichokuwa kikiungua moto.
- c) Kuna nchi iliyoitwa kwa jina lake.
- d) Alikuwa mfalme wa kwanza wa Israeli.
- e) Huyu mfalme alikuwa na ndoto kuhusiana na dola zilizokuwa zikifuata duniani.
- f) Aliacha nyumba yake, nchi na jamaa zake kwa kuwa Mungu alimuagiza afanye hivyo.
- g) Aliwakilishwa na jiwe katika ile ndoto ya sanamu kubwa.
- h) Mara baada ya utawala wake, ufalme wa Israel uligawanyika makundi mawili.
- i) Alikuwa mtu wa kwanza kumkiuka Mungu.

B.

- a) Ni sehemu gani ya sanamu ile Nebukadreza aliyoiona katika ndoto yake inayozungumzia wakati tulio nao?
- b) Ni kwa nini sehemu hiyo ni kielelezo kizuri cha wakati huu?

11 A. a) "Kutokufa" maana yake ni nini?

- b) Ni nani watakaopewa kutokufa?
- c) Watu watakaopewa "kutokufa" watafanya nini kumsaidia Bwana Yesu Kristo?
- d) Katika nyakati hizo za Ufalme unaokuja, watu watakuwa wakiishi wapi- mbinguni au duniani?

*Kazi ya ziada:*

11 B. Unafikiri Ufalme huo wa Mungu duniani utakuwaje?

(Tumia Zaburi ya 72 na Isaya 35 kukusaidia)


## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## AHADI ZA MUNGU KWA IBRAHIMU

**SOMO:** Mwanzo 13

Miaka ipatayo 2000 kabla ya kuzaliwa kwa Yesu, aliishi mtu mmoja aliyeitwa Abram, anayezungumziwa katika Biblia kuwa alikuwa 'rafiki wa Mungu' (Isaya 41:8). Aliishi Uru, mji uliokuwa katika Mesopotamia, katika nchi tunayoiita leo Iraki, kama maili 800 mashariki ya nchi ya Israeli.

Watu wa Uru hawakujua lolote kuhusu Mungu wa Kweli; waliabudu miungu mingi ya uongo, mkubwa kati yao akiwa ni mungu-mwezi. Mabaki ya hekalu alilojengewa yamegunduliwa katika eneo hilo.



### Ujumbe kutoka kwa Mungu

Siku moja Abram alipokea ujumbe kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Tunaweza kuusoma ujumbe huo katika Mwanzo 12:1 ambapo Neno linasema: “BWANA akamwambia Abram, Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha”.

Alikuwa anaambiwa aiache nchi alimozaliwa, aende kuiendea nchi asiyojua ambayo Mungu angemuonesha. Sijui tungejisikiaje tungepewa amri kama hilo, na hasa tukizingatia kuwa, usafiri nyakati hizo ulikuwa kitu kigumu sana na cha hatari kuliko ilivyo sasa.

Mungu alipomwagiza Abram afanye hilo, alimwambia pia: “Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka. Nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa” (ms.2,3).

Abram aliziamini ahadi zile Mungu alizompa, na kumtii. Mwandishi kwa Waebrania anatuambia, Ibrahimu: “Akatoka asijue aendako” (Waebr.11:8). Ibrahimu ni jina lingine Abram alilopewa.

Baada ya siku nyingi, Ibrahimu aliifikia nchi ya Israeli, wakati huo ikiitwa nchi ya Kanaani, akiwa na mke wake, Sara, na mwana wa ndugu yake, aliyeitwa Lutu. Sasa isome Mwanzo 13. Utaona vile Lutu alivyochagua nchi iliyokuwa bora zaidi, na Abram kubakia akitafuta malisho kwa shida kwa ajili ya mifugo yake katika sehemu ya nchi iliyokuwa kame zaidi. Lakini Mungu alikuwa na Abram, na akaipanua ahadi ile aliyompa awali kule Uru, na kumwambia:

“Nchi hii yote uionayo, nitakupa wewe na uzao wako hata milele. Na uzao wako nitaufanya uwe kama mavumbi ya nchi” (Mwanzo 13:15,16).

Hapa Mungu alikuwa akimwahidia Ibrahimu kuwa, nchi hiyo yote ingekuwa urithi wake wa milele. Ili Ibrahimu aweze kuimiliki nchi hiyo milele, ilibidi awe anaishi milele; kwa hiyo Mungu alikuwa hapa akimwahidia uzima wa milele. Nchi aliyokuwa akiahidiwa ilikuwa ni nchi aliyoiioneshwa; nchi kwa sasa tunayoiita Israeli.

Pamoja na hilo, Mungu aliahidi urithi wa nchi hiyo pia kwa ‘uzao’ wake. Kwa wakati huo, Ibrahimu na Sara hawakuwa na watoto. ‘Uzao’ huo ulikuwa ukimhusu ‘Mwana’ mmoja maalumu, ambaye angeimiliki nchi hiyo pamoja na Ibrahimu. Mungu aliahidi pia kwamba, uzao ambao ungetokana na Ibrahimu ungekuwa **taifa kubwa**.

### **Mungu afanya Agano na Ibrahimu**

Fungua Mwanzo 15. Hapa utaona kuwa, Mungu anazirudia tena ahadi zake kwa Ibrahimu na kuziongezea.

Miaka ilikuwa inakwenda, na Ibrahimu alikuwa akizeeka. Mwana aliyeahidiwa alikuwa hajampata. Kwa mara nyingine tena Mungu anamhakikishia kuwa angepata mtoto, na kwamba wazaliwa wake wangekuwa wengi kama nyota za mbinguni. Katika msitari wa 6 tunaambiwa, Ibrahimu: “Akamwaamini BWANA, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki”.

Ibrahimu, kama tulivyo nasi, hakuwa mkamilifu. Hata hivyo, alimwamini na kumtumaini Mungu, na kwa sababu hiyo Mungu alimfurahia. Mungu alifanya sasa Agano na Ibrahimu; mapatano yasiyoweza kamwe kubatilika. Agano hili lipo katika Mwanzo 15:8-18.

Kwa nyakati hizo za Ibrahimu, Agano lilikuwa likifanywa kwa mnyama kuchinjwa. Mnyama huyo aligawanywa vipande vipande, na watu wawili waliokuwa wakifanya Agano walitembea kati ya hivyo vipande. Katika tukio hili, utukufu wa Mungu ulipita kati ya vipande hivyo, na kwa hiyo Ibrahimu alitambua ya kwamba Agano hilo lingekuwa thabiti.

### **Mwana aliyeahidiwa**

Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka 100 na mke wake 90, wakati hatimaye Mungu alipomtimizia mojawapo ya ahadi zake. Walimpata mwana, waliyemuita Isaka.

Katika Mwanzo 22 utaona kielelezo cha ajabu cha imani aliyokuwa nayo Ibrahimu kwa Mungu. Soma mistari 14 ya kwanza, ambapo Mungu anamtaka Ibrahimu amtoe mwanawe, Isaka, awe sadaka. Hili lilikuwa ni jaribu kubwa sana maana, Mungu alikuwa ameahidi kuwa kupitia kwa Isaka, uzao wa Ibrahimu ungekuwa taifa kubwa.

**Ibrahimu alifanyaje?** Alijua kuwa Mungu angeweza bado kuzitimiza ahadi zake, na kwa hiyo mwandishi wa Waebramia anatuambia:

“Kwa imani Ibrahimu alipojaribiwa, akamtoa Isaka awe dhabihu; na yeye aliyezipokea hizo ahadi alikuwa akimtoa mwanawe, mzaliwa pekee; naam, yeye aliyeambiwa, katika Isaka uzao wako utaitwa, akimhesabu ya kuwa Mungu aweza kumfufua hata kutoka kuzimu; akampata tena toka huko kwa mfano” (Waebr. 11:17-19).

Ibrahimu alikuwa tayari kumtoa mwanawe mpendwa, akijua ya kuwa Mungu angeweza bado kumrudishia uhai. Ndio maana tunaona jinsi Mungu alivyopendezwa na Ibrahimu, kwa jinsi alivyomtumaini na kumtii. Katika Mwanzo 22:15–18 Mungu anampa tena ahadi ya ziada.

### **Mzaliwa Mkuu kuliko Isaka**

Haya mambo yalitokea kama miaka 4,000 iliyopita, na juu-juu hayaonekani kama mambo ya sisi kuyajali sana. Lakini, Ibrahimu alipata ‘Mwana’ baadaye ambaye alikuwa ‘Mkuu’ zaidi kuliko Isaka. Msitari wa kwanza wa Agano Jipya unamzungumzia, ukimtaja. Ni “Yesu Kristo, Mwana wa Daudi, Mwana wa Ibrahimu” (Mathayo 1:1).



Kwa hiyo, Yesu naye alikuwa ‘Mwana’ aliyeahidiwa kwa Ibrahimu. Paulo anatuambia hili katika Wagalatia 3:16, akisema:

“Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake. Hasemi, kwa wazao, kana kwamba ni wengi, bali kana kwamba ni mmoja: kwa mzao wako, yaani, Kristo”.

Kwa hiyo, ahadi alizopewa Ibrahimu kwamba angeishi milele katika nchi ya Israeli na kuwa ‘mbaraka kwa mataifa yote’, zilikuwa pia ni ahadi zilizofanywa kumhusu Bwana Yesu Kristo.

Atakapokuja tena kuitawala Israeli na dunia kutokea Yerusalemu, tutaona ahadi hizi zikitimilika, na kubwa zaidi ni kwamba, nasi tunaweza kuwa na sehemu katika ahadi hizo. Kama tukimwamini Yesu na tukafanya kile anachotutaka tufanye, tunaweza nasi kuwa washiriki wa ahadi hizi, kwa kuwa tunaweza kuwa ‘wana’ wa Ibrahimu pia.

Katika msitari wa mwisho wa Wagalatia 3 tunaambiwa: “Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi” (Wagalatia 3:29).

Kuwa na sehemu katika ahadi hizo ni kuweza kupata uzima wa milele, na kumsaidia Yesu Kristo katika kazi kubwa inayokuja ya kuleta ufanisi, amani na furaha duniani. Tunawezaje kuwa watu wa ‘uzao wa Ibrahimu’? Jibu ni- kwa kuamini na kubatizwa katika Yesu Kristo. Hiki ndicho hasa Paulo anachosema katika Wagalatia 3:26–29, anaposema:

“...Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu. Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi”.

Utakumbuka kuwa, mojawapo ya ahadi ya ziada aliyopewa Ibrahimu ilikuwa kwamba:

“Na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia” (Mwanzo 22:18).

Ahadi hii itatimia hapo Yesu atakaporudi kuusimamisha Ufalme wa Mungu.

### **Ibrahimu je?**

Lakini unaweza ukawa unafikiri, Ibrahimu je, itakuwaje juu yake? Hakuwahi kuzitimiziwa zile ahadi na alikufa! Hilo ni kweli. Lakini ahadi za Mungu haziwezi kushindwa. Yesu atakapokuja, atamfufua Ibrahimu na Isaka kutoka kwa wafu, na wengi wengineo, na wataishi milele katika dunia, wakiifurahia hiyo mibaraka Mungu aliyowaahidia zamani hizo.

Utambue hapa ya kuwa, Mungu hakumwahidia Ibrahimu mahali au urithi katika Ufalme ulioko juu mbinguni. Alimwahidia nchi aliyoiona na kuishi ndani yake.

### **Muhtasari**

1. Ibrahimu aliitwa na Mungu kuondoka Uru, aende kwenye nchi asiyojua.
2. Nchi hiyo ilikuwa ni nchi ya Israeli, na aliahidiwa kuwa ingekuwa yake milele.
3. Mungu alimwahidi Ibrahimu pia kupata mwana, na kwamba uzao wake ungeongezeka na kuwa taifa kubwa. Mwanawe huyo aliahidiwa kuwa mbaraka kwa mataifa yote.
4. Ibrahimu alimpata huyo mwana, Isaka, aliyezaliwa kwa muujiza wakati wazazi wake wakiwa wazee. Yesu Kristo naye ni mwana wa Ibrahimu, naye alizaliwa kwa muujiza kupitia kwa mwanamke aliyekuwa bikira.
5. Kama tunakuwa ‘Wa-Kristo’ kwa kumwamini na kubatizwa, tutakuwa tunahesabiwa kuwa wana wa Ibrahimu, na kuwa washiriki wa ahadi alizopewa.
6. Ahadi hizi zitatimia Yesu atakaporudi kuusimamisha Ufalme wa Mungu.

**Pendekezo:**

Mada hii inayohusu uzao wa Ibrahimu ni ngumu kidogo kueleweka kwa mara ya kwanza, lakini ni ya muhimu sana. Unaonaje ukiisoma tena kwa mara nyingine sasa!

**Kifungu cha kusoma:** Waebrania 11 (Zingatia hasa ms. 39, 40).

**Kujifunza kwa moyo:** Wagalatia 3:27 – 29.

<b>Jedwali la ahadi za Mungu kwa Ibrahimu</b>		
<b>Rejea katika Mwanzo</b>	<b>Mungu alichomuahidi Ibrahimu</b>	<b>Muhtasari</b>
12:2	Ibrahimu angekuwa taifa kubwa na Mungu angembariki.	Ibrahimu alikuwa Myahudi wa kwanza.
12:3	Katika Ibrahimu mataifa yote ya dunia yangebarikiwa.	Kupitia katika uzao wa Ibrahimu, tunaweza kupata mbaraka wa wokovu na sehemu katika Ufalme wa Mungu unaokuja duniani.
12:7	Nchi alimoishi Ibrahimu ingefanywa kuwa mali yake na uzao wake milele.	Hii ni nchi ya ISRAELI.
13:16	Wazaliwa wa Ibrahimu wangekuwa kama mavumbi ya nchi kwa wingi.	Ingawa kumekuwa na majaribio kadhaa ya kuwaangamiza Wayahudi, bado wapo, na ni wengi hata leo.
<b>Angalia pia Mwanzo 15:18, 17: 6-8, 22: 16 – 18</b>		

**MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA****WAYAHUDI KATIKA HISTORIA**

(Sehemu ya 1)

**SOMO:** Mwanzo 37**Mwanzo wa historia yao**

Habari za Wayahudi zinaanza hasa ni yule mtu mmoja aliyekuwa mtu wa imani sana, aliyetitwa Ibrahimu. Alipata mtoto wa kiume wakati wa uzee wake, aliyetitwa Isaka, na Isaka akawa na mwana aliyemwita Yakobo, aliyepewa jina la Israeli baadaye. Yakobo alipata wana kumi na wawili wa kiume, ambao ni mababa wa makabila kumi na mawili ya Israeli.

Mwana wa kiume wa pili kutoka mwisho alitwa Yusufu, na historia ya maisha yake tunayoipata kwenye Biblia ni ya kusisimua wakati wote tunapoisoma. Lakini ni zaidi ya kuwa historia; inatupa simulizi juu ya matukio muhimu kuhusiana na watu wa Biblia, Wayahudi. Ndani yake tunapata kielelezo cha ajabu cha vile mkono wa Mungu unavyoongoza masuala yanayohusu watu wake.

Tunaweza kukumbuka vile kaka zake Yusufu walivyomuza kuwa mtumwa kutokana na wivu, na vile baada ya kupatwa na majaribu mengi, Yusufu alivyopanda cheo kuwa mtawala wa Misri. Baada ya hapo, kutokana na njaa kali katika nchi ya Kanaani, baba yake na ndugu zake walihamia Misri kulikokuwa na chakula kwa wingi.

Kwa muda, Wayahudi (wanaoitwa pia 'Waisraeli' au 'Wana wa Israeli') walikuwa na raha kule Misri. Lakini baada ya Yusufu kufa, miaka ilivyopita, kwa kadri Wayahudi ilivyoongezeka kuwa wengi haraka, Wamisri walianza kuwahofia na kuwatesa kwa kuwafanya watumwa.

**Uhuru wa watumwa**

Pengine unaifahamu hadithi ya namna Mungu alivyowatoa watumwa wa Kiyahudi Misri, chini ya uongozi wa mtu aliyetitwa Musa, na kuwapitisha kwenye eneo lenye ukame na jangwa, mpaka kwenye mipaka ya nchi ya Israeli. Safari yao hiyo ndio wazo kuu la Kitabu cha Kutoka.

Katika msafara huo mrefu na wa hatari, Mungu aliwalisha na kuwakinga. Nabii Ezra akimsifu Mungu kwa hilo anasema: "Ukawapa na roho yako mwema ili kuwaelimisha, wala hukuwanyima mana vinywani mwao, tena ukawapa maji kwa ajili ya kiu yao. Naam, muda wa miaka arobaini uliwaruzuku jangwani, wasihitaji kitu; na nguo zao hazikuchakaa, wala miguu yao haikuvimba" (Nehemia 9:20,21).

**Mungu anatoa Sheria**

Baada ya kuivuka Bahari ya Shamu, walipokuwa wakiendelea na safari kuiendea nchi Mungu aliyowaahidia, waliufikia Mlima Sinai. Hapo kitu cha kipekee sana kilifanyika. Watu waliambiwa na Mungu wajikusanye chini ya mlima huo, na hapo Mungu alitoa tamko, kuwaambia:

"Ikiwa mtaitii sauti yangu kweli kweli, na kulishika agano langu, hapo ndipo mtakapokuwa tunu kwangu kuliko makabila yote ya watu"

(Kutoka 19:5).

Na watu waliitikia, wakisema: "Hayo yote aliyosema BWANA tutayatenda" (Kutoka 19:8).

Baada ya hapo Mungu alimpa Musa sheria zake, na Musa akawapa watu. Kwa hakika Sheria hizo zilikuwa ni za maana sana, ambazo hakuna taifa lingine lililowahi kuwa nazo, na kama Wayahudi wangepigatia ipasavyo, wangepigatia watu wenye raha kuliko watu wote katika dunia hii.

Kama ishara kuwa walikuwa ni watu wake maalumu, Mungu aliwaagiza wawe wakiitenga siku ya mwisho ya juma kwa kuifanya takatifu. Siku hiyo iliitwa Sabato; walitakiwa wapumzike siku hiyo na kuufikiria wema wa Mungu kwao.

Lakini hawakuzishika amri za Mungu. Hawakuweza kuzitii zote ilivyotakiwa. Ni jambo Mungu alijua lingetokea, hata hiyo aliliweka kuwalenga watambue na kujifunza kuwa, wasingeweza kujiokoa wenyewe. Ni hivyo hivyo na sisi leo; kwa sheria hakuna anayeweza kupata haki mbele ya Mungu. Walimkiuka Mungu mara nyingi, na hawakuifanya Sabato kuwa siku maalumu, kama walivyoagizwa.

Hatimaye waliifikia nchi ya Israeli na Mungu kuwa Mfalme wao. Aliwapa makuhani wa kuwafundisha njia zake, na waamuzi wa kuwatawala.

### **Wayahudi wataka mfalme**

Miaka karibu 400 ilipita. Wayahudi wakawa hawaridhiki, na wakataka wawe na mfalme kama mataifa yaliyowazunguka; mfalme wanayemwona. Kwa kuomba mfalme, walikuwa wakimkataa Mungu kuwa mfalme wao. Wakati Samweli akiwa mwamuzi wao, alimwambia Mungu vile walivyokuwa wakiomba mfalme, Mungu akasema:

“Hawakukataa wewe, bali wamenikataa mimi, ili nisiwe mfalme juu yao” (1 Samweli 8:7).

Mungu aliwapa walichokitaka. Unaweza kupenda kujisomea mwenyewe simulizi la kuisimua la kusimikwa kwa Sauli kuwa mfalme wa kwanza wa Israeli. Utalipata katika I Samweli 8 na 9.

### **Ufalme unagawanyika**

Sauli alifuatiwa na Mfalme Mkuu, mfalme Daudi, utakayesoma zaidi habari zake katika somo la mbele. Baada ya utawala mrefu wa miaka 40, Daudi alifariki, na mwanawe Sulemani akawa mfalme mahali pake.

Sulemani alitajirika sana; aliwatoza wananchi wake kodi kubwa. Hili liliwafanya wasiridhike naye. Sulemani alipokufa wananchi walikuja kwa mwanawe, Rehoboamu, kumwomba awape unafuu wa kodi. Utasoma katika I Wafalme 12, vile Rehoboamu alivyowasikiliza rafiki zake vijana, badala ya kupokea ushauri wa wazee wa hekima, waliokuwa washauri wa baba yake.

Walipokuja watu kumuuliza mfalme Rehoboamu kama amewakubalia ombi lao, Rehoboamu hakuwajibu kwa busara. Aliwajibu kama vile vijana walivyomshauri, kwa kuwaambia:

“Baba yangu alilifanya zito kongwa lenu, bali mimi nitaongeza kongwa lenu. Baba yangu aliwapiga kwa mijeledi, bali mimi nitawapigeni kwa ng’e” (1 Wafalme 12:14).

Haishangazi raia kumwasi mfalme kama huyo! Makabila 10 ya Israeli yalijitoa na kuanzisha ufalme wa kwao wenyewe, chini ya bwana mmoja aliyeitwa Yeroboamu. Ni Yuda tu (kabila lililokuwa la Rehoboamu), na kabila dogo la Benyamini, waliobakia katika uaminifu kwa Rehoboamu. Kuanzia wakati huo kwenda mbele, tuna historia mbili za falme mbili tofauti katika Biblia.

Kuna historia ya makabila 10 yanayotajwa mara nyingi kwa jina la ‘Israeli’ (au Ufalme wa Kaskazini), na historia ya makabila mawili yanayoitwa ‘Yuda’ (au Ufalme wa Kusini). Ufalme wa Israeli ulikuwa kaskazini mwa nchi, na Yuda kusini.


### **Ukaidi wa Wayahudi**

Katika Kitabu cha kwanza na cha pili cha Wafalme, tunasoma habari ya kusikitisha jinsi Wayahudi walivyomkiuka na kumsahau Mungu, kwa kuziacha njia zake. Mambo yalikuwa mabaya kiasi kwamba, hatimaye Mungu aliazimia kuwaadhibu watu wake, kulingana na tahadhari alizokuwa ametoa, kwa kuwafanya waondolewe kwenye nchi yao wakawe watumwa.

Utaweza kuona kutoka katika maneno kwenye 2 Nyakati 36, jinsi Mungu alivyokuwa amefanya kila aliloweza kuwarudisha watu kwenye njia zake, bila mafanikio. Kifungu kinasema:

“Naye BWANA, Mungu wa baba zao, akatuma kwao kwa mikono ya wajumbe wake, akiondoka mapema na kuwatuma, kwa sababu aliwahurumia watu wake na makao yake, lakini waliwadhihaki wajumbe wa Mungu na kuyadharau maneno yake na kuwacheka manabii wake, hata ilipozidi ghadhabu ya BWANA juu ya watu wake, hata kusiwe na kuponya” (2 Nyakati 36:15,16).

### Adhabu ilibidi ije!



Ukiukaji wa namna hiyo ilibidi utolewe adhabu. Ufalme wa Kaskazini ulitekwa kwanza. Mfalme wa Ashuru alikuja na kuipiga Israeli na kuwateka watu na kuwapeleka Ashuru, na hawakuwahi kuirudia nchi yao tena wakiwa kama taifa.

Baadaye Ufalme wa Yuda nao ulitekwa na mfalme wa Babeli, lakini Mungu aliahidi kuwa baada ya miaka 70 wangeirudia nchi yao. Wengi wao walifanya hivyo baada ya miaka hiyo 70, wakitiwa moyo na manabii wa Mungu, na wakalijenga upya hekalu la Mungu katika Yerusalemu. Vitabu vitatu vya mwisho vya Agano la Kale vya Hagai, Zekaria na Malaki, viliandikwa wakati huo.

### Kati ya Agano la Kale na Jipya

Baada ya manabii hao watatu (Hagai, Zekaria na Malaki), kulipita kipindi kirefu cha kama miaka 400, ambacho Wayahudi hawakupata ujumbe wowote wa moja kwa moja kutoka kwa Mungu. Mungu hakusema nao. Nabii Amosi alikuwa ametabiri juu ya kipindi hicho, miaka mingi nyuma:

“Angalia, siku zinakuja, asema Bwana MUNGU, ambazo nitaleta njaa katika nchi, si njaa ya kukosa chakula, wala kiu ya kukosa maji, bali ya kukosa kuyasikia maneno ya BWANA” (Amosi 8:11).

Kipindi hiki cha miaka 400 kinakuja kati ya kitabu cha mwisho cha Agano la Kale (Malaki), na kitabu cha kwanza cha Agano Jipya (Mathayo). Ndio maana, alipotokea Yohana Mbatizaji, kulikuwa na msisimko mkubwa sana kati ya watu. Baada ya mamia ya miaka ya ukimya, Mungu alikuwa anasema tena na watu wake.

### Myahudi wa muhimu kuliko wote

Yohana Mbatizaji alitumwa na Mungu kuiandaa njia ya mtu aliyekuwa mkubwa zaidi yake. Mungu alikuwa anataka kumtuma Mwanawe mwenyewe kuwaokoa watu wake. Na, kwa hiyo, katika nchi ya Israeli, miaka 2000 iliyopita, Bwana Yesu Kristo alizaliwa. Mara nyingine huwa tunasahau kuwa Yesu alikuwa Myahudi!

Unajua yaliyotokea kumhusu Yesu. Baada ya Wayahudi kumsikia na kuyaona matendo yake ya ajabu, walimkataa. Walimshawishi Pilato amsulubishe. Pilato hakuweza kuona kosa katika tuhuma zao. Hata hivyo, kwa kuwaitikia, aliwajibu kwa kusema: “Mimi sina hatia katika damu ya mtu huyu mwenye haki.” Wayahudi walimjibu na kusema: “Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu” (Mathayo 27:24,25).

Hakukuwa na hatia mbaya zaidi kuliko hii mbele ya Mungu; waliimwaga damu ya Mwana wa Mungu, isiyo na hatia. Hata hivyo, kutokana na mahubiri ya nguvu ya mitume, Mungu aliwapa tena fursa. Wayahudi walio wengi hawakujali fursa hiyo ya kurehemewa, na adhabu kali ilibidi ifuate. Ilikuwa ya kutisha sana.

### **Watu wasio na kwao**

Miaka kama 40 baada ya kufa kwa Yesu, majeshi ya Kirumi yalikuja na kuwapiga Wayahudi. Ulikuwa wakati wa mateso makali sana. Machungu ya vita hiyo yalikuwa kati ya mabaya kuliko yote katika Historia. Jiji la Yerusalemu lilitekwa na Warumi, na Wayahudi waliookoka walitawanywa katika mataifa yote ya dunia.

Mungu alikuwa amewaonya Wayahudi tangu zamani kwamba, hili lingetokea kama wangeziacha njia zake: “BWANA atakutawanya katika mataifa yote, tokea ncha hii ya dunia hata nchi hii ya dunia” (Kumb. La Torati 28:64).

Na kwa hiyo, kwa miaka kama 2000 iliyopita, Wayahudi walikuwa hawana nchi ambayo ni yao wenyewe. Na mbaya zaidi, wamepata mateso mengi ya kutisha sana. Laana mbaya sana za Kumb. la Torati 28 zimewashukia. Sehemu ya mateso haya yametokea katika miaka ya karibuni. Wengi wetu tutakuwa tunajua juu ya kambi za mateso alizoiweka Hitler, kiongozi wa Ujerumani, wakati wa vita kuu ya pili (1939 – 1945).

Zaidi ya Wayahudi milioni sita waliuwawa kikatili sana; ukatili ulioitetemesha dunia nzima. Soma tena Kumb. La Torati 28:64-67, na utayashangaa maneno hayo yaliyoandikwa na Musa zaidi ya miaka 3,000 iliyopita. Yamekuja kutokea hivyo-hivyo katika nyakati zetu hizi!

Ni simulizi la kuhuzunisha, lakini hatujafikia mwisho. Tunapaswa kujisikia vizuri bado katika kulisoma Neno la Mungu; tunaambiwa, hatimaye mambo yatakuwa mazuri.

### **Vipindi katika Historia (Miaka ni ya makadirio):**

1. Miaka 3500 iliyopita.	Mungu aliwatoa Wayahudi Misri, na kuwapa nchi ya Israeli waishi humo. Aliwafundisha njia zake. Badala ya wao kuwa kielelezo kwa mataifa mengine, Wayahudi walifuata uovu wa mataifa hayo.
2. Miaka 2500 iliyopita.	Mungu hatimaye aliwaadhibu kwa kuwatoa wawe mateka. Watu wa Yuda uliirudia nchi yao baada ya miaka 70, lakini bado waliendelea kumkiuka Mungu.
3. Miaka 2000 iliyopita	Baada ya kusulubiwa kwa Yesu Kristo, Wayahudi waling’olewa katika nchi. Kwa miaka kama 2000 wamekuwa hawana makao, tena wakibaguliwa na kuteswa.
4. Leo	Mungu anawarudisha tena watu wake katika nchi ya Israeli (Utasoma zaidi juu ya hili katika somo linalofuata).

**Vifungu vya kusoma:** Kumb. la Torati 28, 2 Nyakati 36:11 – 23.

**Jifunze kwa moyo:** Isaya 43:11,12

“Mimi, naam, mimi ni BWANA, zaidi yangu mimi hapana mwokozi. Nimetangaza habari, nimeokoa, nimeonyesha, na hapakuwa mungu mgeni kati yenu; kwa sababu hiyo ninyi ni mashahidi wangu, asema BWANA, nami ni Mungu”.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

### WAYAHUDI KATIKA HISTORIA

(Sehemu ya 2)

**SOMO:** Ezekieli 37

#### Bonde la mifupa-mikavu

Ezekieli alipewa maono ya ajabu. Yapo katika Ezekieli, Sura ya 37. Yalikuja kwa awamu tatu:

1. Ezekieli alioneshwa bonde lililojaa mifupa mikavu sana.
2. Ezekieli alitakiwa 'atoe unabii'; aiaturu mifupa, na alipofanya hivi, kukawa na mshindo mkubwa, mifupa ile ikasogeleana na kujiunga, ikawa ni sanamu tupu za mifupa ya watu. Alivyoendelea kuzitazama, kukawa na mishipa inatokea juu yake, kisha nyama na ngozi zikazifunika sanamu. Mifupa ikawa sasa ni mizoga ya watu waliokufa.
3. Mungu sasa akamwagiza Ezekieli atoe unabii kuutaka upepo uje ili miili ile ijazwe pumzi. Ezekieli alipofanya hivyo, pumzi iliingia, miili ikawa hai, na kuwa Jeshi Kubwa mno.



Ezekieli anaambiwa:

“Mwanadamu, mifupa hii ni nyumba yote ya Israeli, tazama, wao husema, mifupa yetu imekauka, matumaini yetu yametupotea, tumekatiliwa mbali kabisa” (Ezek. 37:11).

#### Awamu ya 1:

**Mifupa mikavu inamaanisha:** Israeli isiyo na matumaini, iliyotawanywa ulimwenguni kote na kuteswa.

Mungu anaendelea kusema katika msitari wa 12:

“Tazama, nitafufua makaburi yenu, na kuwapandisha kutoka katika makaburi yenu, enyi watu wangu, nami nitawaingizeni katika nchi ya Israeli”.

#### Awamu ya 2:

Mifupa kujiunga na kupewa miili **kunamaanisha**, Mungu kuwarudisha watu wake waliotawanyika katika nchi ya Israeli.

Mwishowe, kuhusu kuwapa uhai, Mungu anasema:

“Nami nitatia roho yangu ndani yenu, nanyi mtaishi, nami nitawawekeneni katika nchi yenu, nanyi mtajua ya kuwa mimi, BWANA, nimesema hayo na kuyatimiza” (ms. 14).



### Awamu ya 3:

#### **Miili isiyo na uhai kupewa pumzi ya uhai maana yake:**

Mungu atawapa watu wake Roho yake, watambue kwamba ni yeye anayetawala.

### Tuziangelie zaidi hizi awamu:

#### **Ya kwanza**

Hili lilishatokea. Waisraeli walitawanywa na walikuwa katika hali ya kukata tamaa, unabii wa Kumb. La Torati 28:65 – 67 ukiwa unatimia. Ulisema:

“Wala katika mataifa hayo hutapata raha iwayo yote, wala hutakuwa na kituo cha uwayo wa mguu wako, lakini BWANA atakupa huko moyo wa kutetema, na macho ya kuzimia, na roho ya kudhoofika; na uzima wako utakuwa na wasiwasi mbele yako; nawe utakuwa na woga usiku na mchana, wala hutaamini kamwe maisha yako. Asubuhi utasema, Laiti ingekuwa jioni! na jioni utasema, Laiti ingekuwa asubuhi! kwa kicho cha moyo wako (‘kwa hofu’ ya moyo wako) utakavyokucha (‘utakavyohofu’), na (kwa) kuona kwa macho yako utakavyoona”.

(Msitari huo wa mwisho wa 67, tafsiri ya Kiswahili ilikosewa sana!)

#### **Ya pili**

Ni hivi karibuni tu wana wa Israeli wamekuwa wakirudi katika nchi yao. Katika mwaka 1917 Azimio la Balfour lilisainiwa huko Uingereza, la ahadi ya kwamba Waingereza wangeifanya Palestina (inayoitwa sasa Israeli) iwe makao ya kitaifa kwa Wayahudi.

Hitler alipoingia madarakani Ujerumani alinua kuwaangamiza Wayahudi wote, na zaidi ya Wayahudi milioni 6 waliuawa katika mazingira ya kutisha sana. Kutokana na mateso yao, walijawa na tamaa kubwa ya kurudi Israeli na kuwa na nchi ya kwao wenyewe, mahali ambapo wangejisikia huru kutokana na mateso.

Katika mwaka 1948, baada ya mapambano makali, Israeli ilijitangaza yenyewe kuwa ni taifa. Kinyume na matarajio ya wengi, Waisraeli wameendelea kuwa taifa mpaka sasa. Imewezekanaje? Sababu ni kwamba, Mungu alisema wangukuwa taifa tena (kumbuka Ezekieli 37:12).

Naye Yeremia alitabiri hivi:

“Maana mimi ni pamoja nawe, asema BWANA, nikuokoe; maana nitawakomesha kabisa mataifa yote huko nilikokutawanya, bali sitakukomesha wewe kabisa.....” (Yer. 30:11)

“Aliyemtawanya Israeli atamkusanya na kumlinda, kama mchungaji alindavyo kundi lake. Kwa maana BWANA amemweka huru Yakobo, amemkomboa mkononi mwake aliyekuwa hodari kuliko yeye” (Yer. 31:10,11).

Awamu hii ya 2 imekuwa katika kutimia kwa sasa!

#### **Vipi ya tatu?**

Taifa la Israeli wanatambua kuwa Mungu ndiye anayetawala? Kwa bahati mbaya, sivyo. Wakati unakuja, hata hivyo, wakati ambao taifa la Israeli litamgeukia Mungu. Tunapewa sababu katika Zekaria 14:1-4. Wakati unakuja ambao mataifa yote yatajikusanya kinyume na Israeli. Kulingana na mambo yanayotokea duniani kwa sasa, hili haliwezi kuwa mbali.

Ni hapo hali ya mambo itakapokuwa ya kukatisha tamaa kabisa kwa Israeli, jambo la ajabu la kuisimua litakapotokea. Tunaambiwa:

“Hapo ndipo atakapotokea BWANA, naye atapigana na mataifa hayo, kama vile alivyopigana zamani siku ya vita” (Zekaria 14:3).

Msitari unaofuata unatuonesha Mungu atakavyowasaidia; atamtuma Yesu arudi! Tunaambiwa: “Na siku iyo miguu yake (Yesu) itasimama juu ya mlima wa Mizeituni.....”(ms. 4).

Hebu fikiria jinsi Wayahudi watakatavyojisikia, watakatavyotambua lililotokea; kumwona Yesu Kristo, waliyemsulubisha, amerudi sasa kutoka mbinguni, na kuwaokoa! Kwa vyovyote watamtambua na kumkubali. Nabii huyu Zekaria anatuambia:

“Nao (Wayahudi) watamtazama yeye ambaye walimchoma, nao watamwombolezea kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee” (Zek. 12:10).

Kwa hiyo Waisraeli ni lazima wabadilike. Watalazimika kuitambua dhambi yao waliyoifanya kama taifa katika kumuua Bwana Yesu, na watamkubali sasa awe kiongozi wao. Katika Ezekieli 37:23 inatajwa pia kwamba ‘watatakaswa’. Katika Ezekieli 36, ujumbe kama huo unatolewa:

Awamu ya 1	Israeli wanatawanywa na kuadhibiwa kwa uovu wao.	Ezekieli 36:16-20
Awamu ya 2	Mungu anawakusanya tena.	Ezekieli 36:21–24
Awamu ya 3	Israeli wanabadilishwa.	Ezekieli 36:25 – 28

### **Uanzishwaji wa Ufalme wa Mungu duniani tena**

Wayahudi watakapokuwa wametubu, Yesu atashika mamlaka katika Yerusalemu. Yesu atakapokuwa Mfalme, na Sheria ya Mungu itakapokuwa inaiongoza dunia, dunia itabadilika. Lakini wakati huo wa amani utafikiwaje?

Katika nyakati zote katika historia ya mwanadamu, mataifa yamekuwa yakienda kwa kuzifuata njia zake yenyewe. Yamekuwa yakijifanyia yanachotaka na kumpuuza Mungu; na ndivyo yanavyofanya hata sasa. Wakati Bwana Yesu Kristo atakapokuwa Mfalme katika Yerusalemu, atayataka mataifa yote yamche Mungu na kumtukua, kama tunavyosoma katika Ufunuo 14:7. Mataifa yale yatakayomkubali Bwana, yatabarikiwa sana katika Ufalme huo.

Lakini Bwana Yesu Kristo atakuwa pia na uwezo wa kuliadhibu taifa lolote linaloasi. Katika Zekaria 14 tunaambiwa kwamba, taifa lolote likikataa kwenda Yerusalemu kuabudu, halitapata mvua (ms.17,18). Na kama taifa kama Misri, ambalo kawaida hupata mvua ndogo sana, lisipotii, litapigwa pia na tauni.


Kwa hiyo itakuwa ni wakati wa amani na furaha kwa ulimwengu wote. Kuna vielelezo vingi vya kuisimua katika Biblia juu ya wakati huo. Kimojawapo kipo katika Isaya 11:6,9:

“Mbwa-mwitu atakaa pamoja na mwana-kondoo, na chui atalala pamoja na mwana-mbuzi, ndama na mwana-simba na kinono watakuwa pamoja, na mtoto mdogo atawaongoza..... Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu, maana dunia itajawa na kumjua BWANA, kama vile maji yanavyoifunika bahari”.


Mtume Paulo alipokuwa akiwaandikia Warumi (ambao ni watu wa kimataifa kama sisi), alitumia kielelezo cha mti wa Mzeituni ili kuonesha kuwa, watu wa kimataifa wanaweza kujiunga na hatma iliyoahidiwa kwa Wayahudi.

Soma hili kwa ajili yako mwenyewe katika Warumi 11 (na hasa msitari wa 13– 25). Angalia maonyo hayo yanayotolewa.


**MATAIFA NA WAYAHUDI KATIKA MPANGO WA MUNGU (Warumi 11).**




Mzeituni ukiwa unasimama badala ya Israeli.



Baadhi ya matawi yamekatwa. Matawi hayo yanawakilisha Waisraeli wasiomwamini Mungu. (ms. 17 – 20).



Matawi kutoka kwenye Mzeituni-pori (sisi) yanaweza kupachikwa. Matawi hayo ni waumini wa kimataifa wanaojiunga (ms. 17).



Baadhi ya matawi ya kiasili yanaweza kurudishiwa tena. Mungu anaweza kuwapachika tena Wayahudi wanaomgeukia tena na kumwamini (ms. 23).

**Vifungu vya kusoma:** Ezeieli 36-37, Zekaria 14, Warumi 11.

**Msitari wa kushika:** Zaburi 72:8

“Na awe na enzi toka bahari hata bahari, toka mto hata miisho ya dunia”.

**MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA****AHADI ZA MUNGU KWA DAUDI****SOMO:** 2 Samweli 7**Kijana mchungu-kondoo awa mfalme**

Utakuwa pengine umesikia juu ya Daudi, kijana aliyekuwa mchungaji wa kondoo, aliyemuua Goliati, mtu wa 'maraba mitatu' kwa kijiwe kimoja alichomtupia.

Daudi aliishi kama miaka 1000 kabla ya Yesu Kristo kuzaliwa. Alizaliwa katika eneo moja na Yesu, katika mji mdogo karibu na Yerusalemu uitwao Bethlehemu. Alikuwa mwana wa kiume wa mwisho wa Yese, aliyekuwa mmiliki wa hao kondoo.

Wakati Daudi alipokuwa bado mdogo, Mungu alimtuma nabii wake, Samweli, ampake mafuta ya kuwa mfalme juu ya Israeli. Lakini kwa wakati huo, mfalme Sauli, aliyekuwa mfalme wa kwanza wa Israeli, alikuwa akitawala. Sauli alimuonea sana wivu Daudi, na kwa nyakati mbalimbali alijaribu kumuua. Matokeo yake yalikuwa Daudi kumkimbia na kuwa mkimbizi.

Sauli hakuwa mfalme mzuri; hakumtii Mungu. Wakati ulifika akauawa katika pambano na Wafilisti. Hapo ndipo njia ilipofunguka kwa Daudi kuwa mfalme.

Baada ya majaribu na harakati nyingi, Daudi alijenga Ikulu yake katika Yerusalemu, na ndipo alipoishi na kutawala.

Daudi alipofikiria jinsi Mungu alivyombariki na juu ya Sanduku lake ambalo bado lilikuwa likikaa katika hema, alitaka kujenga Hekalu zuri katika Yerusalemu ambamo Sanduku hilo lingehifadhiwa ndani yake. Sanduku hilo lilikuwa sanduku ambamo ndani yake kuliwekwa kibao cha Amri-kumi za Mungu, na lilikuwa na kifuniko kilipowekwa juu yake 'kiti cha rehema'. Juu yake utukufu wa Mungu uling'aa.

Daudi alimwambia alichotaka kufanya Nathani, nabii wa Mungu. Nathani alimjibu Daudi kwa kumwambia aendelee, lakini usiku huo Mungu alisema na Nathani, na kumpa ujumbe maalum sana kwa Daudi.

**Ujumbe wa Mungu kwa Daudi**

Fungua tena 2 Samweli, Sura ya 7. Sehemu ya muhimu sana ya ujumbe huo wa Mungu kwa Daudi, ni katika msitari wa 12 mpaka wa 16. Hapa Mungu anamuahidi Daudi kupata mtoto wa kiume. Anasema juu ya 'mzao' huyo kuwa:

"Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa jina langu, nacho kiti cha enzi cha ufalme wake nitakifanya imara milele" (ms. 13).

Hili lilikuwa litokee baada ya Daudi kufa, kwa kuwa anaambiwa katika msitari wa 12 kuwa, ni hapo, "Siku zako zitakapotimia, ukalala na baba zako".

**Zaidi juu ya huyo Mwana wa Daudi**

Sasa Daudi alipata mwana aliyemwita Sulemani, aliyetawala baada yake katika Yerusalemu. Ahadi alizokuwa amepewa Daudi, kwa sehemu zilitimia katika Sulemani, lakini utimilifu wa ahadi hizo ulibidi usubiri ujio wa Bwana Yesu. Sulemani alifanywa mfalme wakati Daudi akiwa bado hai, na kwa vyovyote Sulemani hakutawala milele; alikufa.

Huyo mwana Daudi aliyekuwa ameahidiwa hasa, alikuwa awe mtu wa kipekee sana, kwa kuwa Mungu anasema juu yake kuwa:

"Mimi nitakuwa baba yake, naye atakuwa mwanangu" (2 Samweli 7:14).

Tugeukie Sura ya kwanza ya Luka. Hapa tunasoma juu ya malaika wa BWANA, aliyemtokea msichana mmoja, mmojawapo wa watu wa ukoo wa mfalme Daudi na kumwambia, atazaa mtoto wa kiume. Huyo alikuwa azaliwe, sio kwa njia ya kawaida ya baba wa kidunia, kama inavyokuwa kwa watoto wote. Alikuwa azaliwe kwa muujiza wa uweza wa Mungu. Mwanamke huyu aliyekuwa bado bikira, aliyelitwa Mariamu, aliambiwa:

“Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye-juu zitakufunika kama kivuli, kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu” (Luka 1:35).

Malaika alimwambia tena Mariamu:

“Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake. Atamiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme wake utakuwa hauna mwisho” (Luka 1:32,33).

Sasa tunaweza kuona jinsi ahadi Mungu aliyompa Daudi, ilivyotimia alipozaliwa Yesu Kristo:

1. Mungu alikuwa ndiye Baba yake.
2. Yesu amewekewa atawale Israeli milele.

### **Mfalme wa Wayahudi**

Yesu alizaliwa awe Mfalme. Mamajusi walipokuja kumsujudia Yesu, waliuliza, “Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi?” (Mathayo 2:2).

Yesu alipokamatwa na kupelekwa kwa Pilato ahukumiwe, Pilato alimuuliza: “Wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi?” Yesu alimjibu kwa kusema, “Wewe wasema” (Marko 15:2). Hii ni namna ya Kiyahudi ya kusema: “Ndiyo, kwa hakika ndiye”. Kama ambavyo tumekwisha kuona, Yesu atarudi katika dunia hii na kuwa Mfalme wa Wayahudi; na kutawala katika kiti cha enzi cha Daudi.

### **Mfalme wa dunia yote**

Yesu hatakuwa Mfalme wa Wayahudi tu atakaporudi. Atakuwa Mfalme wa dunia nzima. Mungu alisema hivi juu yake: “Ni neno dogo sana wewe kuwa mtumishi wangu, ili kuziinua kabila za Yakobo, na kuwarejesha watu wa Israeli waliohifadhiwa; zaidi ya hayo nitakutoa uwe nuru ya mataifa, upate kuwa wokovu wangu hata miisho ya dunia” (Isaya 49:6). ‘Mataifa’ maana yake ni, ‘Watu wasio Wayahudi’.

### **Daudi Je?**

Ingawa Daudi alitambua kuwa ahadi hiyo ya Mungu isingetimizwa kwa kipindi kirefu sana, alikuwa na shukrani sana kwa Mungu. Tunaweza kusoma maombi yake ya kushukuru katika 2 Samweli 7:18-29. Mungu alimwambia:

“Na nyumba yako, na ufalme wako, vitathibitishwa milele **mbele yako**” (2 Samweli 7:16). Maana yake ni **‘akiwepo’**.

‘Nyumba’ inaweza kuwa na maana ya jengo. Hekalu liliitwa, ‘Nyumba ya Mungu’. Lakini ‘nyumba’ inaweza kuwa na maana pia ya familia au ukoo, na hiki ndicho kinachomaanishwa katika ahadi hizi kwa Daudi.

Kwa hiyo Daudi mara nyingi aliifikiria hiyo ahadi, au agano, ambalo Mungu alikuwa amempa, na analiongelea katika Zaburi. Kwa mfano, katika Zaburi 89: 2-4 analikumbuka likisema:

“Maana nimesema, Fadhili zitajengwa milele, katika mbingu utathibitisha uaminifu wako. Nimefanya agano na mteule wangu, nimemuapia Daudi, mtumishi wangu. Wazao wako nitawafanya imara milele, nitakijenga kiti chako cha enzi hata milele”.

<b>AHADI ZA MUNGU KWA DAUDI (2 Samweli 7)</b>	
<b>Andiko</b>	<b>Muhtasari</b>
Ms. 12: “Siku zako zitakapotimia ukalala na baba zako, nitainua mzao wako nyuma yako, atakayetoka viunoni mwako, nami nitafanya imara ufalme wake”.	Maisha ya Daudi yalipokwisha, alikufa. Mungu alimwinua mmoja kati ya wazaliwa wake, na Mungu atausimamisha tena Ufalme wake.
Ms. 13: “Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa jina langu,	Huyo ‘mzao’ atamjengea Mungu nyumba. Sulemani alimjengea Mungu nyumba. Yesu Kristo anamjengea Mungu nyumba <b>hata sasa</b> (Soma Waefeso 2:19-22).
...nacho kiti cha enzi cha ufalme wake nitakifanya imara milele”.	Mungu atafanya Ufalme wa Yesu imara milele. Sulemani hakutawala milele, wala Ufalme wa Israeli haukudumu milele. Yesu ndiye atakayeutawala milele.
Ms. 14: “Mimi nitakuwa baba yake, naye atakuwa mwanangu;  akitenda maovu, nitamwadhibu...”	Mungu atakuwa ndiye baba kwa mzaliwa huyu wa Daudi, naye atakuwa Mwana wa Mungu. Yesu ni Mwana wa Mungu. Yesu hakutenda dhambi, hivyo Mungu hakulazimika kumwadhibu.
Ms. 16: “Na nyumba yako, na ufalme wake, vitathibitishwa milele mbele yako.  Nacho kiti chako kitafanywa imara milele”.	Nyumba ya Daudi na Ufalme wake vitasimamishwa, na Daudi atakuwa yupo hapo. Hili litatokea hapo Yesu atakaporudi. Daudi atafufuliwa kutoka kwa wafu na kuwa katika Ufalme huo. Yesu atatawala kutoka katika kiti cha enzi cha Daudi (Yerusalemu), na Ufalme wake utakuwa hauna mwisho.

### **Kitu cha kutazamiwa**

Paulo anatuambia kwenye Waebrania 11:39,40 kuwa:

“Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi, kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi”.

Sasa, Ibrahimu na Daudi na waaminifu wengine wengi, walikufa wakijua kuwa, katika siku ya kuja kwa Yesu Kristo, watafufuliwa tena na ‘kukamilishwa’. Watapewa uzima wa milele na wote wale walio wa Kristo. Lakini kama kifungu hicho kinavyoonesha, uzima wa milele hautakuwa kwa ajili ya watu hao waaminifu tu, unaweza ukawa wetu pia.

### **Msitari wa msingi**

Tumeona kwamba Yesu Kristo ni mzao wa Ibrahimu, na mzao wa Daudi. Msitari wa kwanza kabisa wa Agano Jipya, unaanza na:

“Kitabu cha ukoo wa Yesu Kristo, mwana wa Daudi, mwana wa Ibrahimu” (Mathayo 1:1).

Kwa hiyo tunaweza tu kulielewa Agano Jipya, kama tumelisoma na kulielewa Agano la Kale.

### **Muhtasari**

1. Mungu alimuahidia Daudi mwana.
2. Mwana huyo alikuwa ni Yesu, Mwana wa Mungu.
3. Amewekewa kuwa Mfalme; atawale katika Kiti cha Enzi cha Daudi milele.
4. Atakaporudi kutawala, watumishi waaminifu wote wa Mungu watapewa uzima usio na mwisho, na watashirikishwa katika Ufalme wake huo katika dunia.

**Vifungu vya Kusoma:** 2 Samweli 7, 1 Nyakati 17.

**Jifunze kwa moyo:** 1 Nyakati 17 : 11, 12

“Na itakuwa, siku zako zitakapotimia, uende na babazo, nitainua mzao wako nyuma yako, atakayekuwa wa wana wako, nami nitakifanya imara kiti cha enzi cha ufalme wake milele”.

## MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

### *Karatasi ya maswali: namba 4*

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa 'Kazi ya ziada' unaweza kulijibu swali kama ukipenda, au kuliacha kama unaona huliwezi. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

### **MASOMO: 12 – 15**

12. A. Mungu alimwambia nini Ibrahimu, alipokuwa akiishi Uru?  
B. Mungu alimwagiza Ibrahimu amfanyie nini Isaka?  
C. Neno 'uzao' lina maana gani (kama katika Mwanzo 13:15)?  
D. Ni nani aliyekuwa mzaliwa wa muhimu kuliko wote kwa Ibrahimu?  
E. Kwa kuwa Ibrahimu alimtumaini na kumtii Mungu, Mungu alimbariki. Kati ya mibaraka yake mingi, ni ipi miwili unayofikiri ni ya maana zaidi? Toa sababu.
- 13 A. Andika mistari michache juu ya wafuatao:  
a) Yusufu  
b) Musa  
c) Sauli
- B. a) Ni kwa nini Mungu aliwapeleka wana wa Israeli utumwani?  
b) Watu wa Yuda walichukuliwa utumwani wapi?  
c) Walikaa huko kwa muda gani?  
d) Walifanya nini waliporudi?
- 14 A. Ni mistari gani katika Zekaria inayoonesha kuwa:  
a) Mataifa yote yatakuja kupigana juu ya Yerusalemu.  
b) Bwana atapambana kwa ajili ya Israeli.  
c) Yesu Kristo atarudi katika mlima wa Mizeituni.  
d) Bwana atakuwa Mfalme juu ya dunia yote.  
e) Watu watakaopambana dhidi ya Yerusalemu watapigwa kwa tauni.  
f) Watu watakaobaki (kati ya yale mataifa yaliyokuja juu ya Yerusalemu) watakwenda Yerusalemu kumwabudu Mfalme.
- B. Kwa maneno yako mwenyewe, sema unabii wa mifupa-mikavu unachomaanisha (maelezo yasizidi mistari 10).

*Kazi ya ziada:*

- C. Toa maelezo juu ya Yerusalemu kwa:  
a) Nyakati za kale  
b) Sasa  
c) Wakati unaokuja  
(Somo la 9 na 14, na masomo yako ya Biblia yatakusaidia)



**MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA****BABA NA MWANA****SOMO:** Isaya 45

“Je! Wewe waweza kuuvumbua ukuu wa Mungu?” (Ayubu 11:7)

Hili swali liliulizwa maelfu ya miaka iliyopita. Jibu lake ni lile lile leo kama lilivyokuwa kwa siku hizo; kwa vyovyote hatuwezi! Hakuna kitu kabisa tunachoweza kujua kumhusu Muumbaji Mkuu wa vitu vyote, nje ya yale Yeye Mwenyewe anayotuambia katika Neno lake; katika Biblia. Hata hivyo hakuna tumaini la uzima wa milele tunaloweza kulipata, bila ya huko kumjua.

Njia pekee ya kuweza kumjua Mungu ni kwa kukisoma kitabu chake, Biblia, au kulisikiliza Neno lake, alilotupa. Mungu mwenyewe amesema:

“Mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu, asema BWANA. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu” (Isaya 55:8,9).

**Mungu ni Mmoja**

“Sikiliza, Ee Israeli, BWANA, Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja. Nawe mpende BWANA, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote” (Kumb. La Torati 6:4,5).

Musa aliyasema maneno haya kwa Waisraeli wakiwa nyikani. Ujumbe kwamba ‘Mungu ni mmoja’, umerudiwa-rudiwa mara nyingi katika Maandiko. Katika Isaya 45:5 tunaambiwa:

“Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine, zaidi yangu mimi hapana Mungu”.

Miaka zaidi ya elfu baada ya Musa, mtume Paulo anasema kitu hicho hicho:

“Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, mwanadamu Kristo Yesu” (1 Timotheo 2:5). Na tena, katika 1 Timotheo 6:15,16 Paulo anamuongelea Mungu kuwa ni:

“Yeye aliyehimidiwa, Mwenye uweza peke yake, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana; ambaye yeye peke yake hapatikani na mauti,  
amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hakuna mwanadamu awezaye kumwona. Heshima na uweza una yeye hata milele. Amina”.

**Huyu Mungu aliye Mtakatifu ni Mungu wa Upendo**

Kama Biblia ingetuambia tu juu ya uweza na utakatifu wa Mungu, kwa vyovyote tungemcha, lakini tungeona shida kumpenda. Lakini Mungu ametuonesha kuwa, yeye pia ni mwema na amejaa huruma. Mwandika Zaburi anatuambia kuwa:

“BWANA amejaa huruma na neema, haoni hasira upesi, ni mwingi wa fadhili... Kama vile baba wahurumiavyo watoto wake, ndivyo BWANA anavyowahurumia wamchao. Kwa maana, Yeye anatujua umbo letu, na kukumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi”

(Zaburi 103: 8,13,14).

Ni katika huruma na upendo wake, Mungu ametupa Bwana Yesu Kristo kuzichukua dhambi zetu.

## Mwana wa Mungu

Tangu mwanzo Mungu alikuwa amepanga kumtuma Mwanawe kutuokoa. Kuna utabiri mwingi kumhusu Yesu katika Agano la Kale. Katika Isaya 7:14, kwa mfano, tunaambiwa:

“Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye utamwita jina lake Imanueli”.

Maana ya Imanueli ni ‘Mungu pamoja nasi’. Mungu hapa anaahidi kumtuma Mwanawe mwenyewe. Angalia vifungu vingine hivi vinavyoonesha kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu:

<p>Wagalatia 4:4 “Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria”.</p>	<p>Marko 1:11 “Na sauti ikatoka mbinguni, Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu, nimependezwa nawe” (Mungu alisema hili katika ubatizo wa Yesu).</p>	<p>Yohana 20:31 “.....ili mpate kuamini ya kwamba, Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake”.</p>
---	---	---

## Yesu hakuwapo kabla

Mtoto anapozaliwa, ndipo maisha mapya yanapoanza. Kuzaliwa kwa Yesu Kristo hakukuwa na utofauti.

Kuna watu wanaofikiri kuwa, Bwana Yesu Kristo alikuwepo kabla hajazaliwa na Mariamu. Kwa sehemu mtu anaweza kusema hivyo, kama ni kwa kumaanisha kuwa Mungu alishapanga tokea mwanzo kuwa angepata Mwana.

Mungu anapopanga kitu, tunajua kwa uhakika kabisa kuwa kitatokea. Yesu Kristo ni msingi wa kusudi la Mungu; ni mhimili wa mpango wote mkubwa wa wokovu. Kwa hiyo, Mungu alipokuwa akiwaambia waaminifu wa kale katika Agano la Kale kuhusiana na mpango wake huo, aliwaambia juu ya Kristo.

Kwa namna hiyo hiyo Biblia inamwongelea Kristo kuwa ni: “Mwana-kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia” (Ufunuo 13:8). Hili halina maana kuwa Yesu alichinjwa kabla dunia haijaumbwa au wakati ikiumbwa. Tukio hili la kutisha la kuuwawa lilitokea mara moja tu kama miaka 2000 iliyopita, Yesu aliposulubiwa (Waebrania 9:25–28).

Kwa kuwa kifo cha Yesu ni cha msingi sana katika kusudi la Mungu, Mwenyezi Mungu amekiongelea kama tukio lililo la muhimu sana linalowagusa watu wa nyakati zote, tangu wakati wa Agano la Kale. Kwa hiyo, ni kifo cha Yesu ambacho kimeyabadili mambo yote, “tangu kuwekwa misingi ya dunia”.

Biblia inatumia lugha ya ‘kuwepo-kabla’ katika kumwelezea Bwana Yesu, lakini haina maana kuwa tayari alishakuwepo; akiishi kabla ya kuzaliwa kwake. Alikuwepo, ndiyo, lakini ni katika mawazo ya Mungu; katika mpango wake. Mungu alipanga kufanya Yesu azaliwe kwa wakati aliouweka, ‘katika utimilifu wa nyakati’ (Waebr. 9:26).

Ni pale Mariamu alipomzaa mtoto wake huyo wa kiume wa kwanza, ndipo Bwana Yesu alipoanza kuwepo; alipoanza kuishi. Ni kama inavyokuwa kwetu.

## Asili ya Yesu

Kwa kuwa Yesu alizaliwa na mwanamke, alikuwa na hulka kama ya kwetu. Katika Waebrania 2:17 tunaambiwa:

“Kwa hiyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote”.

Wakati wa uhai wake hapa duniani, alijaribiwa kwa namna nyingi, lakini hakuwahi kuanguka dhambini. Hebu vitazame vifungu hivi, vyote vikiwa vimechukuliwa kutoka katika kitabu kwa Waebrania, kuona kuwa Yesu alikuwa na hulka kama yetu, alipokuwa akiishi hapa duniani:

Waebrania 4:15

“Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu, bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi”.

Waebrania 2:14

“Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu ya mauti, yaani, Ibilisi”.

Waebrania 2:9

“Ila twamwona yeye aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika, yaani, Yesu, kwa sababu ya maumivu ya mauti, amevikwa taji ya utukufu na heshima, ili kwa neema ya Mungu aionje mauti kwa ajili ya kila mtu”.

Waebrania 5:7,8

“Yeye, siku hizo ya mwili wake, alimtolea yule, awezaye kumwokoza na kumtoa katika mauti, maombi na dua pamoja na kulia sana na machozi, akasikilizwa kwa jinsi alivyokuwa mcha Mungu, na, ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata”.

Kwa vyovyote, Yesu alikuwa hivi kabla ya kufa na kufufuka kwake tu. Baada ya kufufuka alipewa hulka tofauti ya utukufu na nguvu; hulka ya kutoweza kufa tena.

### **Wazo potofu**

Watu wengi wameyapuuzia mafundisho ya Biblia yanayomhusu Mungu, na kuja kuamini kitu wanachokiita, “Utatu Mtakatifu”. Wanasema kuwa Mungu anazo nafsi tatu: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, na zote ziko sawa. Hakuna ukweli juu ya dhana hii. Tutatafakari kuhusu Roho Mtakatifu mbeleni kidogo, kwenye Somo la 20.

Maneno ‘Utatu-Mtakatifu’ na ‘Mungu-Mwana’ hayapo kabisa katika Biblia yenyewe. Pale neno ‘Mungu-Mwana’ linapoonekana, ni makosa ya waliotafsiri tu, wakiwa wameongeza waliyoaminishwa na watu. Hili linathibitika hata tukilinganisha na tafsiri ya Kingereza.

Katika Injili ya Yohana, kwa mfano, tunaambiwa: “Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua” (Yoh.1:18). Katika Biblia ya Kingereza, tunasoma: “No one has seen God at any time. The only begotten Son, He has declared Him.” *Only begotten Son ni Mwana pekee, sio* Mungu Mwana. Na ndivyo ilivyo katika Kiyunani (kuna wakati tumekoseshwa na waliotafsiri!).

Tumekwishaona mafundisho ya moja kwa moja ya Biblia kuwa **Mungu ni mmoja**, na kwamba **Yesu ni Mwanawe**. Kama vile mwana-aliye-mwema anavyokuwa chini ya baba yake, ndivyo Yesu alivyokuwa chini ya Mungu.

Yesu hakuwahi kudai kuwa yuko sawa na Mungu, bali alimtegemea Baba yake kwa mambo yote na kumwomba. Alisema, “Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda” (Yohana 5:19).

Ni kweli kwamba Yesu aliwahi kusema: “Mimi na Baba tu umoja” (Yohana 10:30). Alikuwa na maana kuwa, yeye na Baba yake walikuwa wamoja kidhamira na kimalengo, na aliomba umoja huo uwepo pia kati Yao na wanaokuwa wafuasi (Yohana 17:21). Zaidi ya hapo, tunaambiwa:

“Basi, vitu vyote vikiisha kutiishwa chini yake (Yesu), ndipo Mwana mwenyewe naye atatiishwa chini yake yeye aliyemtiishia vitu vyote, ili kwamba Mungu awe yote katika wote” (1 Wakorintho 15:28).

Msitari huu unatuambia kuwa, hata baada ya utawala wa Yesu wa miaka 1000 katika dunia (ambao ni kipindi cha Ufalme wa Mungu), Yesu ataendelea kuwa chini ya Baba yake, na Mungu kuwa ‘yote katika wote’.

### Imani ya 'Utatu' ilitoka wapi?

Wakristo wa awali hawakuamini 'utatu'. Waliamini kile Biblia inachofundisha, kuwa: "Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, mwanadamu Kristo Yesu" (1 Tim 2:5).

### Sasa, mambo haya potofu ya 'Utatu' yalitoka wapi?

Ilikuwa imepita miaka zaidi ya 300 baada ya kuzaliwa kwa Yesu, 'Wakristo' walipoanza kuaminishwa katika 'utatu'. Wazo hilo halikuwa na msingi katika Biblia, badala yake lilitokana na imani za kale za Wayunani, ambao hawakuwa wakijua lolote kumhusu Mungu Mmoja Pekee Aliye Wa Kweli. Pole pole, kanisa lililichukua wazo hilo la 'Mungu mmoja katika nafsi tatu', na kuukana ukweli wa Biblia unaomhusu Mungu.

'Imani ya Mitume' iliyotungwa kama miaka 100 baada ya Kristo kupaa kwenda mbinguni, inaonesha imani waliyokuwa nayo Wakristo wa awali, Wakristo wa kwanza. Inasomeka hivi:

"Namwamini Mungu Baba, Mwenye uweza wote, Muumba wa mbingu na nchi. Namwamini Yesu Kristo, Mwana wake wa pekee, Bwana wetu. Aliyechukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, akazaliwa na mwanamwali Mariamu....." Hiki ndicho hasa Biblia inachofundisha!

Ukuu na uweza wa Mungu ni vitu ambavyo viko nje ya uwezo wetu wa kufikiri. Tunajikuta tukishindwa kuelewa hasa-hasa jinsi Mungu huyu wa milele, alivyoweza kupata mtoto na msichana huyo 'wa kimwili na damu', lakini yeye Mungu anatuambia ndivyo ilivyokuwa. Tunajua Neno lake ni kweli; wajibu wetu ni kulipokea hivyo kwa imani.

Kama tunahitaji kumpendeza Mungu, ni lazima tulipokee lile analotuambia bila kuongeza mawazo ya kibinadamu yasiyo ya Kimaandako; yasiyo kwenye Biblia.

#### Muhtasari

1. Kuna Mungu mmoja tu.
2. Mungu **sio** 'watatu katika mmoja'. Mafundisho ya Utatu Mtakatifu hayapo kwenye Biblia.
3. Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, aliyezaliwa na mwanamwali Mariamu. Yesu Kristo **sio** Mungu-mwana.
4. Yesu alikuwa ni mwanadamu, lakini kwa kuwa Mungu alikuwa ni Baba yake, alikuwa na utofauti wa muhimu na mwanadamu mwingine yeyote. Kwa kushinda dhambi amekuwa Mkuu juu ya wote.
5. Kuzaliwa kwa Yesu kulikuwa ni muujiza kwa kuwa, mama yake alikuwa bikira. Baba yake alikuwa ni Mwenyezi Mungu.

#### Vifungu vingine vya kupitia:

Yesu alianza kuishi alipozaliwa.	1 Petro 1:20, Waebrania 9:26
Yesu alikuwa ni mtu.	Matendo 2:22, Wafilipi 2:8, Waebrania 2: 9, 14 – 18
Mungu ni Mkuu kuliko Yesu	Waefeso 4: 6, 1 Wakorintho 11:3, Yohana 14: 28, Yohana 10: 29

**Vifungu vya kusoma:** Kumb. la Torati 6, Mathayo 1:18–25

**Jifunze kwa moyo:** 1 Timotheo 2:5

"Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja; mwanadamu Kristo Yesu".

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## MAISHA YA YESU

SOMO: Luka 2

“Malaika akamwambia, usiogope, Mariamu, kwa maana umepata neema kwa Mungu. Tazama, utachukua mimba na kuzaa mtoto mwanamume, na jina lake utamwita Yesu. Huyu atakuwa mkuu, ataiwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake. Atamiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme wake utakuwa hauna mwisho” (Luka 1:30 – 33).

Ni ujumbe wa ajabu kiasi gani huu, malaika aliomletea Mariamu! Lakini kuna moja lililomtatiza zaidi. Aliambiwa huyo mtoto atakayemwita Yesu atakuwa, ‘Mwana wa Aliye juu’. Mariamu alimuuliza malaika, “Litakuwaje neno hili?”

Malaika alimjibu kwamba, Mungu angetumia uweza wake kuwezesha mimba ya Mwanawe kutungwa. Kwa hiyo, hakuna mwanamume ambaye angehusika; ilikuwa Yesu awe mwana halisi wa Mungu.

Soma simulizi juu ya kuzaliwa kwa Yesu katika Mathayo 1 na 2, na katika Luka 2. Utaweza kuona ya kwamba, hakuna mahali katika Sura hizi panaposema Yesu alikuwa mbinguni kabla ya kuzaliwa kwake. Wazo kama hilo lingepingana na maelezo ya Kibiblia, kuhusiana na namna mama yake alivyoshika mimba na Yesu alivyozaliwa.

**Ubatizo wa Yesu.**

Biblia haisemi mengi kumhusu Yesu akiwa mtoto. Inaruka na tayari anakuwa kwenye ubatizo wake na Yohana Mbatizaji katika Mto Yordani. Ubatizo huo **haukuwa** wa kunyunyuzia vimaji kichwani au kuosha kichwa. Ulifanyika katika mto, na baada ya hapo **alipanda kutoka majini** (Marko 1:10).

Mbingu zilifunguka na Mungu akamshushia Yesu Roho yake ‘Takatifu’. Sauti ilitoka mbinguni ikisema: “Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye” (Mathayo 3:17).

Kwa kubatizwa, Yesu ametuonesha jinsi ubatizo ulivyo wa muhimu, na Mungu aliongezea kuthibitisha kupendezwa. Baada ya kubatizwa tunasoma kuwa, Yesu alikwenda nyikani, ambapo alijaribiwa na Ibilisi (Mathayo 4:1).

**Lilikuwa ni ‘dudu’ gani lililomjaribu?**

Kilichotokea hasa ni nini pale nyikani? Ibilisi ni nini? Hebu tuyachunguze kwa umakini majaribu mawili kati ya yale matatu yaliyompata:

“(Ibilisi) akampandisha juu, akamwonyesha milki zote za ulimwengu kwa dakika moja. Ibilisi akamwambia, nitakupa wewe enzi hii yote, na fahari yake, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa yeyote kama nipendavyo. Basi, wewe ukisujudu mbele yangu yote yatakuwa yako” (Luka 4-5-7).

Hakukuwa na mlima mrefu hapo mahali Yesu alipokuwa (ilikuwa nyikani), na hakuna ulipo popote katika ulimwengu huu, mlima ambao mtu akipandishwa, anaweza kuona falme zote za dunia. Kwa hiyo isingeweza kuwa kwamba Yesu kweli alipandishwa mahali pa namna hiyo.

Zaidi ya hapo, Biblia inasema kuwa dunia ni mali ya BWANA; iko mikononi mwa Mungu, **sio** Ibilisi. Inasema: “Aliye juu ndiye anayemiliki katika ufalme wa wanadamu, naye humpa amtakaye, awaye yote” (Danieli 4:32). Zaburi ya 24:1 inasema: “Nchi na vyote viijazavyo ni mali ya BWANA, dunia na wote wakaa ndani yake”.

Kwa hiyo inabidi tufikirie kwa makini maana iliyoko katika jaribu hili.

Sasa hebu tuangalie jaribu lingine lililomkabili:

“(Ibilisi) akamwongoza mpaka Yerusalemu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, jitupe chini kwa maana imeandikwa, atakuagizia malaika zake wakulinde, na ya kwamba mikononi mwao watakuchukua, usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe” (Luka 4:9-11).

Kwanza tujiulize kama kweli Bwana Yesu angeweza kulifuata hilo ‘dudu’ lililojaa uovu, lisiloonekana, kutoka hapo nyikani, kupanda naye njia yote mpaka Yerusalemu, na kisha kukubali kuwekwa juu kwenye kinara cha hekalu, ili tu ajibu, “Imenenwa, usimjaribu Bwana Mungu wako” (Luka 4:12). Kwa vyovyote, kama kungekuwa na dudu la namna hiyo, Yesu angelitambua mara moja, na kukataa kuwa na ushirika wowote nalo.

Kama hatuwezi kuelewa kwa namna majaribu haya yalivyotokea kiuhalisia, tutawezaje kuelewa yanachotufundisha?

Yesu alijijua kuwa alikuwa ni Mwana wa Mungu, na kwamba aliwekewa kuwa Mfalme juu ya falme zote za dunia. Katika jaribu la kwanza, aliweza kuzifikiria falme hizi na utukufu wake akilini mwake, alipokuwa hapo nyikani. Lakini pia alifahamu kutokana na Agano la Kale kuwa, alipaswa kupata mateso na kufa kwanza msalabani, kabla ya kuyapata mamlaka hayo ya Ufalme wa dunia na utukufu wake.

Kwa jaribu la pili, Yesu atakuwa alifikiri kujitupa chini kutoka kwenye kinara cha hekalu bila kuumia kungekuwa njia nzuri ya kujijengea umaarufu, na kuthibitisha ya kuwa alikuwa ni Mwana wa Mungu. Hili lingeirahisisha kazi ya kuhubiri Injili iliyokuwa mbele yake. Lakini, alitambua hiyo haikuwa namna Mungu alivyotaka.

Kwa hiyo, tunafikiri, majaribu haya yalikuwa ni fikra zilizomjea Yesu akilini akiwa nyikani. Alikuwa muda mfupi uliopita amejazwa Roho kutoka juu baada ya kubatizwa. Alikuwa sasa amepata nguvu sana zinazomvuta azijaribu, hata kama ni kwa kuyafanya mawe yawe chakula ili ale, kutokana na njaa aliyokuwa nayo.

Lakini Yesu alijua kuwa, uweza unaotoka kwa Mungu ni lazima utumike kwa namna inayofaa. Kuongelea ‘Ibilisi’ ni namna tu ya Ki-maandiko ya kusemea kwa kuficha, msukumo katika hulka zetu wanadamu unaotujia akilini mwetu sisi wote, kutuvuta tufanye yasiyokubalika. Kuutambua ni muhimu sana. Yesu alipatwa na majaribu haya kama na sisi yanavyotupata, lakini hakuwahi kujiachia ashindwe.

### **Yesu alikuwa na hulka gani?**

Baba yake Yesu alikuwa ni Mungu, lakini mama yake Mariamu alikuwa mwanadamu. Je, Yesu alikuwa wa kimbingu, au alikuwa mwanadamu kama sisi?

<b>Hulka ya kibinadamu (kama sisi)</b>	<b>Hulka ya kimbingu (kama Mungu)</b>
Tunazaliwa.	Mungu amekuwepo nyakati zote (Zaburi 90:2).
Tunaweza kujaribiwa na tunafanya dhambi.	Mungu hawezi kujaribiwa na hawezi kukosea.
Tunakufa.	Mungu hawezi kufa. Yeye ni wa milele.

Ingawa Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu na alikuwa na Roho yake, alikuwa bado ni mwanadamu. Kama tulivyoona katika somo letu lililopita, rejea zifuatazo zinaonesha hili wazi: Waebrania 2:9, 14- 18; 1 Timotheo 2:5; Matendo 2:22.

Hatuwezi kuelewa sana jinsi Yesu alivyokuwa na baba wa kimbingu na mama wa kidunia. Tunapaswa tu kupokea kile Biblia inachosema juu yake. Biblia inatambia pia jinsi Yesu alivyokuzwa (alivyo 'adhimishwa') na kupewa utukufu (Wafilipi 2:9-11). Ni lazima tulipokee hili nalo.

### **Huduma ya Yesu**

Baada ya ubatizo wake na majaribu katika nyika tunasoma kuwa, Yesu alisafiri katika miji yote na vijiji, akihubiri Habari Njema ya Ufalme wa Mungu, akiwa na wanafunzi wake kumi na wawili.

Sasa hebu tuyafikirie mafundisho yake, na miujiza aliyofanya. Tutatazama pia namna alivyoishi na jinsi alivyokikabili kifo chake:

#### **1. Mafundisho ya namna tunavyopaswa kuishi:**

Katika Mathayo, Sura ya 5, 6 na 7 yamejaa mafundisho ya hekima ya Yesu, aliyoyatoa katika hotuba yake maarufu inayojulikana kama, Hotuba ya Mlimani. Kitu cha kwanza anachokisema Yesu ni: "Heri walio maskini wa roho, maana ufalme wa mbinguni ni wao" (Mathayo 5:3).

Kwa kuwa hapo Yesu aliongelea Ufalme wa Mbinguni, ni wengi sana wanaofikiri Ufalme huo uko mbinguni. Lakini hebu uangalie msitari wa tano unachosema. Anasema: "Heri wenye upole, maana hao watairithi nchi."

Ufalme wa mbinguni- maana yake ni Ufalme wa 'kimbingu'. Hebu yaangalie maneno yaliyo katika Sala ya Bwana, katika Mathayo 6:10, Yesu anapowafundisha wanafunzi wake kuomba. Anawaambia waombee Ufalme wa Mungu uje, ili mapenzi ya Mungu: "Yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni". Kwa hiyo, Ufalme wa mbinguni utakuwa ni hapa hapa katika nchi, katika dunia.

Hapa kuna baadhi ya mambo mengine Yesu aliyofundisha kwenye Hotuba ya Mlimani. Anawaambia watu kuwa:

- ✚ Wawapende adui zao.
- ✚ Wasiwahukumu wengine.
- ✚ Kumtazama mwanamke kwa kumtamani (kwa nia ya ngono), ni kubaya sawasawa na kuzini.
- ✚ Waziachie taa zao ziwake (yaani, waoneshe imani yao katika maisha yao).
- ✚ Wanapotoa kitu au msaada, wafanye kwa siri (wasijitangaze).
- ✚ Wasihofie mambo ya maisha haya; wamtumainie Mungu kuwapatia mahitaji yao.
- ✚ Wautafute kwanza Ufalme wa Mungu.

Yesu aliwaonya wafuasi pia katika Mathayo 7:13–23, kuwa:

- ✚ Wasifuate-mkumbo: Ni wachache wangeiona njia iendayo uzimani.
- ✚ Kuna kujuta: Wengi wanaojihesabia haki wenyewe watahuzunika sana, baada ya kuona hawakupata nafasi katika Ufalme wa Mungu.

#### **2. Kufundisha kwa mifano:**

Katika Mathayo 13 kumejaa mifano. Utagundua iliyo mingi inavyohusu Ufalme. Mifano katika Luka 15 inatuonesha jinsi Mungu anavyotutaka tuikatae dunia, na kuifuata kweli yake.

#### **3. Mafundisho kwa unabii:**

Mathayo 24 ni unabii Yesu alioutoa, kwa kuwa wanafunzi wake walitaka kujua ni lini hekalu katika Yerusalemu lingebomolewa kulingana na Yesu alivyosema. Hili lilitokea katika mwaka wa 70 B.K. (Baada ya kuzaliwa Kristo). Walitaka pia wafahamu kungetokea ishara gani kuonesha kuwa Yesu anarudi na dunia imefikia mwisho wake.

Hili lilijadiliwa katika Somo la 8 (ni vizuri ulisome tena). Mafundisho ya Yesu yaliyo mengi yalikuwa juu ya Ufalme wa Mungu unaokuja.

## **Miujiza ya Yesu**

1. **Miujiza ya Uponyaji:** Injili zimejaa miujiza mingi ya kuponya aliyoifanya Yesu. Alikuwa akiwahurumia watu na alipenda kuwasaidia. Uweza wake ulikuwa mkubwa; aliweza hata kufufua waliokufa.
2. **Miujiza mingine:** Yesu aliyageuza maji kuwa divai, alitembea juu ya maji, alilisha maelfu ya watu n.k. Alitumia wakati wote uweza aliokuwa nao kusaidia, na kamwe haikuwa kuwavutia watu au kuringishia. Miujiza aliyoifanya ilikuwa ni ishara ya uweza aliokuwa nao na mamlaka, na ilitoa fursa kwa watu kujifunza kitu. Ilionesha wema na huruma aliyokuwa nayo.
3. **Yesu alivyoishi:** Mwana wa Mungu alizaliwa katika hori la kulia ng'ombe. Mara nyingi hakuwa na makao, aliweza hata kusema: "Mbweha wana pango, na ndege wa angani wana viota, lakini Mwana wa Adamu hana hana pa kujilaza kichwa chake" (Luka 9:58).

Kabla ya kufa, Yesu aliwaosha wanafunzi wake miguu yao. Hii ni kazi iliyokuwa ikifanywa kwa kawaida na watu wa chini sana; watumwa. Ingawa alikuwa Mwana wa Muumba Mkuu wa ulimwengu wote, Yesu hakuishi maisha ya kifahari. Hili linatufundisha kuwa wanyeyekevu, na kuwatumikia wengine.

Bwana Yesu alitumia muda wake mwingi katika maombi kwa Baba yake wa mbinguni. Kabla hajawachagua wanafunzi wake kumi na wawili, alikesha usiku mzima akiomba. Hakuomba kwenye hadhara kuonesha watu alivyokuwa akijua kuomba; aliwakosoa viongozi wa kidini kwa kufanya hivyo. Aliwakosoa kwa unafiki wao kwa kuwaambia hivyo. Kamwe hakujali kudharauliwa!

## **Maandalizi ya kifo**

Kuna siku Yesu aliwachukua watatu kati ya wanafunzi wake, akapanda nao mlimani. Alipokuwa akisali hapo 'sura ya uso wake ikageuka', Musa na Eliya wakaonekana wakiwa naye wakizungumzia habari za kufa kwake katika Yerusalemu. Maono haya ya Yesu akiwa katika hali ya ufukufu, yalikuwa ni picha yake ya mbele wakati wa Ufalme. Yatakuwa yalimpa nguvu kuutazamia huo Ufalme, wakati akikabiliana na mauti yake.

Alifahamu kutokana na unabii katika Agano la Kale kuwa, angekufa kifo cha kikatili. Zaburi ya 22, 69 na Isaya 53 ni sehemu za utabiri uliohusu kifo chake. Yesu alianza sasa kuwatahadharisha wanafunzi wake kuwa angeteswa na kufa, lakini aliwaambia pia kuwa angefufuka kutoka kwa wafu (Luka 9:22).

Viongozi wa kidini walikuwa wakati wote wakitaka kumnasa, na Yesu alijua walimchukia. Walijaribu kumuua kwa kumpiga mawe mara mbili, lakini 'saa yake ilikuwa haijaja ya kufa'.

"Ikawa, siku za kufa kwake zilipokuwa karibu kutimia, yeye aliukaza uso wake kwenda Yerusalemu".

Hakuwa na woga wa kufa. Alijua ilikuwa ndio njia pekee ya kuweza kuwasaidia wanadamu wadhambi. Alijua angeweza tu kuwasaidia kwa namna hiyo, kama yeye mwenyewe hakuwa na dhambi. Alipambana kila siku na dhambi, na akashinda. Ametuachia kielelezo cha ajabu. Anawaambia wafuasi wake kuwa hawana budi kumfuata:

"Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate" (Luka 9:23).

**Vifungu vya kusoma:** Mathayo 5, 6 na 7; Luka 9.

**Kujifunza kwa moyo:** Luka 1:32

"Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake".



**MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA****KIFO CHA YESU****SOMO:** Marko 14 na 15**Tatizo la Dhambi**

Ni dhahiri kuwa, dhambi ni janga kubwa kwa mwanadamu. Ni tatizo ambalo hata mtu anayeonekana mkweli sana, anashindwa kukabiliana nalo sawasawa. Hakuna mtu anayeweza kuishinda dhambi kwa jitihada zake mwenyewe. Biblia yote inahusu namna Mungu alivyotoa jawabu kwa tatizo hili.

Mungu alimtoa Mwanawe, Bwana Yesu Kristo, awe dhabihu inayokubalika kwa ajili ya dhambi ya mwanadamu, na Bwana Yesu alifanya kazi pamoja na Baba yake kufanikisha jambo hilo. Yesu alijitoa mwenyewe kwa utii kuwa hiyo dhabihu, kwa kuivunja nguvu ya dhambi kati ya watu. Hili limewezesha wale wanaomfuata, wa enzi zote, kujaribu kama yeye kupambana na dhambi kwa kufuata mfano wake.

Dhabihu ya Bwana Yesu imemwezesha Bwana Yesu Kristo mwenyewe kuyaepuka matokeo ya hukumu ya kifo iliyotolewa, iliyorithiwa kutoka kwa Adamu. Hili limewezesha wafuasi wa kweli wa Yesu kusamehewa dhambi zao, na hatimaye nao watapata uzima wa milele. Yesu alikuwa, katika yote mkamilifu; hakufanya dhambi yoyote.

**Utabiri juu ya mateso ya Bwana Yesu Kristo**

Tunaweza kusoma juu ya mateso aliyoyapata Bwana katika Injili zote. Lakini, tunapata picha iliyojaa zaidi tunaposoma pia vifungu vilivyotabiria mateso hayo.

Hebu fungua Zaburi ya 22. Zaburi hii inatuwezesha kuelewa jinsi Yesu alivyokuwa akijisikia, alipokuwa akiwambwa msalabani:

“Lakini mimi ni mdudu wala si mtu; laumu ya wanadamu na mzaha wa watu. Wote wanionao hunicheka sana, hunifyonya, watikisa vichwa vyao; husema, amemtegemea BWANA, na amponye; na amwokoe sasa, maana apendezwa naye” (Zab. 22:6-8).

Sio tu uchungu, bali pia aibu ya kusulubiwa ilimlema sana Yesu. Isome Zaburi hii kwa uangalifu na utaona pengine kuwa, maneno yake yanatusaidia, kuliko mengine yote, kuyaelewa hasa yaliyompata Bwana Yesu. Angalia tena msitari wa 15 na 16:

“Nguvu zangu zimekauka kama gae, ulimi wangu waambatana na taya zangu; unaniweka katika mavumbi ya mauti. Kwa maana mbwa wamenizunguka; kusanyiko la waovu wamenisonga, wamenizua (‘wamenipigilia’) mikono na miguu”.

**Yalivyofikia hapo**

Viongozi wa Kiyahudi walichukizwa sana na Yesu, makundi makubwa ya watu walipokuja kumsikiliza na kuwaleta wagonjwa wao waponye. Walikuwa wakimwonea wivu na kukasirika. Hawakutambua kuwa, miujiza aliyokuwa akiifanya ilikuwa uthibitisho kuwa, alikuwa Mwana wa Mungu. Wivu na chuki zao ziliwatia giza.

Walipanga mauaji; Yesu auawe. Walimtuhumu kwa kukufuru; tuhuma iliyokuwa ikihukumiwa kifo kulingana na amri za Mungu walizopewa. Kwa vyovyote madai yao yalikuwa ya uongo, lakini hawakujali hilo!

Kwa wakati huo Israeli ilikuwa chini ya utawala wa Kirumi, na ingawa viongozi wa Kiyahudi, makuhani na mafarisayo, walikuwa wamemhukumu Yesu kuuawa, hawakuwa na uwezo wa kutekeleza hilo bila kupata idhini ya mamlaka ya Kirumi.

Jina la mtawala wa Kirumi katika Israeli kwa wakati huo alikuwa akiitwa Pontio Pilato. Wayahudi walimleta Yesu kwa Pilato na kudai kuwa alipaswa kusulubiwa (kuuawa kwa kupigiliwa msalabani). Pilato alifahamu kuwa Yesu hakuwa na kosa, na kuwa Wayahudi walitaka auawe kwa kumuonea wivu tu.

Lakini Pilato aliogopa kusimama kinyume cha Wayahudi, wasije wakamchongea kwa Kaisari, Mfalme Mkuu wa Warumi, akaiipoteza kazi yake; alikuwa na makosa yake mengine. Kwa hiyo aliwakubalia ingawa kwa shingo upande, na kumtoa Yesu kwao ili asulubishwe. Kwa hakika hiki kilikuwa kifo cha mateso sana kilichowahi kubuniwa na watawala; na Pilato alijua Yesu hakuwa na hatia.

Warumi nao, kwa vyovyote, walipaswa kubeba lawama kwa yale yaliyompata Bwana Yesu.

### Ni kwa nini ilibidi Yesu ateseke kiasi hicho?

Tunapomfikiria Yesu akiwa ananing'inia msalabani na kukumbuka kuwa hakuwa na kosa lolote, tunajiuliza: "Kwa nini ilibidi limpate hili?" Tunajua alikuwa siku zote akifanya mambo yale yanayompendeza Mungu tu!

Kitu kimoja ni hakika: ilikuwa ni njia pekee ya kumwezesha mwanadamu aokolewe na dhambi zake. Yesu alimwomba Baba yake mara tatu, yasimpate yote: "Ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke" (Mathayo 26:39). Hata hivyo alikuwa makini kuongezea, kusema, "Walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe". Mungu angeweza kumwokoza Mwanawe na mateso yale, lakini ilikuwa haiwezekani; ilikuwa ni njia pekee.

### Kwa nini Yesu alilazimika kufa?

Adamu alikosa, kwa hiyo alikufa. Mauti yake yalikuwa ni adhabu. Tunaambiwa: "Mshahara wa dhambi ni mauti" (Warumi 6:23). Hii ni sheria ya Mungu isiyoweza kuvunjwa. Kwa hiyo:

Watu wote (kasoro Yesu) wanakufa kwa kuwa:

1. Wote tuna hulka ya kufa ya Adamu.
2. Wote tunapokosea, tunafanya dhambi.

Yesu alikufa kwa kuwa:

1. Alikuwa na hulka ya kufa ya Adamu. Lakini, **hakukosea**. Hakufanya dhambi. \*Sababu moja tu; hakuna ya 2.

Yesu alijaribiwa kama tunavyojaribiwa (na mara nyingine zaidi yetu sisi), hata hivyo hakukosea; hakuanguka dhambini. Katika Waebrania 4:15 tunaambiwa:

"(Yesu) alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi".

Kwa hiyo ilibidi Yesu afe kwa kuwa alikuwa na hulka ya kibinadamu, lakini **hakustahili kufa** kwa kuwa hakufanya dhambi. Kwa sababu hii Mungu aliweza kumfufua kutoka kwa wafu, bila kuikiuka kanuni yake aliyoweka, ya mauti kuwa mshahara wa dhambi.

Baada ya Yesu kufufuka, Mungu alimpa hulka mpya; hulka ya **kutokufa**, isiyotokana na dhambi ya Adamu. Ni hulka mpya ambayo pia haiwezi kujaribiwa na dhambi.

Tunaweza kusamehewa dhambi zetu tunapokuwa na ushirika na dhambi ya Yesu, kwa kuzikiri dhambi zetu, kubatizwa na kutubu. Yesu atakaporudi, tutaweza nasi kuyashinda mauti.

### Msalaba unatufundisha nini?

Kuwambwa msalabani kwa Bwana Yesu kulikuwa ni tukio la kutisha. Lilionesha uovu wa wanadamu ulivyo katika kumchukia na kumuua kikatili Mwana wa Mungu, aliyekuwa mkamilifu wa wema. Kitendo hicho kinaonesha wanadamu wanavyoweza kuwa wabaya, na vile wasivyoweza kamwe kujiokoa wenyewe.

Ni vizuri tutambue na sisi tu wadhambi, na kwamba tunahitaji sana kuokolewa. Tunafanya vizuri kutambua kuwa, Bwana Yesu alikuwa dhambi ya 'kukubalika'. Alikuwa kama mwana-kondoo asiye na mawaa, na

Mungu alimridhia kuwa sadaka hii iliyokuwa kamilifu; kuwa toleo kwa ajili ya wote wanaomwamini. Yesu ni: “Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu” (Yohana 1:29).

Somo lingine la muhimu ni hili: Msalaba wa Kristo unaonesha upeo wa upendo wa Mungu kwetu. Paulo anaweka hivi:

“Yeye asiyemwachia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye? (Warumi 8:32).

### **Wamoja na Mungu**

Mwanadamu alitenganishwa na Mungu na dhambi. Ukarabati wa utengano huo unaitwa katika Maandiko, “Upatanisho”. Hiki ndicho dhabihu ya Bwana Yesu ilichoweza kutufanyia. Imeweza kutuleta, hatimaye, katika u-moja na Mungu; kuwa na mahusiano safi na maelewano. Uhusiano huu mpya unakuja kwa kumhama Adamu, na kuja kwa Yesu kupata msamaha wa dhambi zetu. Daudi anasema katika Zaburi:

“Heri aliyesamehewa dhambi, na kusitiriwa makosa yake. Heri BWANA asiyemhesabia upotovu”  
(Zab. 32:1,2).

### **Tuna wajibu gani?**

Mungu amefanya kila aliloweza kwa ajili yetu. Ametupa Yesu awe sadaka; awe dhabihu. Yesu aliyatoa maisha yake kwa ajili yetu. Lakini, bila ya kuamini kikweli kile Mungu alichokifanya kwa ajili yetu, dhabihu ya Yesu haiwezi kuwa na maana yoyote.

“Tufanyeje basi?”, Baadhi ya Wayahudi walimuuliza mtume Petro swali hili, na jibu lake linatufaa hata sisi leo. Petro aliwaambia:

“Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi” (Matendo 2:38).

Katika kifungu kingine Petro anasema tena:

“Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe” (Matendo 3:19).

### **Neema ya Mungu na imani yetu**

Kwa hiyo tunakuja katika chimbuko lenyewe la Injili. Kwa upendo wake wote, Mungu amemtoa Yesu awe dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu. Huu upendo wa Mungu wa bure unaongelewa mara nyingi katika Agano Jipya ukiitwa: “Neema yake”. Katika Waefeso 1: 6–8 tunasoma juu ya hiyo **neema**:

“Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo Mpendwa (Yesu Kristo). Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake. Naye ametuzidishia hiyo katika hekima yote na ujuzi”.

Tunaweza kuikataa neema ya Mungu na upendo wake, tunaweza kuidharau na kuipuuza, lakini, kama tu-wajanja, hatutafanya hivyo. Ni zawadi ya maana sana hii tunayopewa ya upendo na uzima. Kama tuna akili nzuri, tutataka kuwa miongoni mwa wale Yesu anaowaambia katika Marko 16:16, akisema: “Aaminiye na kubatizwa ataokoka”.

### **Ubatizo ni mwanzo wa maisha mapya**

Sisi sote ni wana wa Adamu, na kama Adamu, tunapenda zaidi njia zetu wenyewe kuliko Njia ya Mungu. Lakini Yesu, alipoutoa uhai wake kuwa dhabihu ya dhambi, alitwezesha kuwa ‘wana wa Mungu’; kuwa sehemu ya familia ya Kristo. Mwenyewe alisema:

“Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuata”  
(Luka 9:23).

Ni lazima tubatizwe kulingana na agizo lake. Hili lina maana kuwa, badala ya kutembelea njia zetu za dhambi, ni sharti nasi **tuifie** dhambi, yaani, tufanye kila jitihada kuacha kutenda dhambi. Tunapaswa tutembelee na Kristo katika upya wa uzima, wakati wote tukijitahidi kuifuata njia ya Mungu badala ya yetu. Mtume Paulo anatuambia:

“Hao walio wa Kristo Yesu wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake. Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho” (Wagalatia 5:24,25).

#### **Muhtasari**

1. Watu wote wanastahili kufa kwa sababu wote ni wadhambi.
2. Mungu, kwa upendo wake kwa wanadamu, ameonsha namna ambavyo dhambi zinaweza kusamehewa.
3. Namna hiyo ni kupitia katika kifo cha Mwanawe wa pekee, Yesu, aliyeishi maisha ya kuishinda dhambi.
4. Ingawa Yesu aliishi maisha hayo kikamilifu, alikuwa na hulka yetu sisi wanadamu inayopaswa kufishwa.
5. Mungu alimfufua Yesu kutoka kwa wafu, kwa kuwa hakuwa na dhambi.
6. Kama tukikubali kuwa tu-wadhambi tunaostahili kufa, tukimjea Mungu kupitia kwa Yesu, atatusamehe dhambi zetu.
7. Kama tukizitambua dhambi zetu na kubatizwa, tunaweza kuwa wana wa Mungu; watu wenye tumaini la uzima wa milele.

**Vifungu vya kusoma:** 2 Wakorintho 5, 1 Petro 1

**Msitari wa kushika:** Warumi 5

“Mungu anaonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu”.


## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

### UFUFUO NA KUPAA KWA YESU KRISTO

**SOMO:** Yohana 20

Kwa huzuni wanawake walikwenda kwenye sehemu mwili wa Yesu ulipolazwa. Walibeba marashi kwa ajili ya kuupaka mwili wake. Hawakujua namna gani wangeliondoa jiwe kubwa lililowekwa mlangoni pa kaburi, lakini walijisikia kwenda kuupaka mwili wa Bwana wao. Walipolifikia kaburi karibu walikuta:

- Jiwe limeondolewa!
- Kaburi liko tupu!
- Malaika walikuwa hapo!



Wanaambiwa na malaika: “Kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu? Hayupo hapa, amefufuka” (Luka 24:5,6).

Wanawake hao walirudi na kuwaambia wanafunzi wa Yesu kuwa Yesu amefufuka, lakini hakuna hasa aliyewaamini. Petro na Yohana wanakwenda mbio kaburini kujionea wenyewe. Ni hakika wanakuta kaburi lipo wazi na sanda aliyovikwa Yesu imejiviringa pembeni.

Mariamu Magdalena, aliyekuwa mmojawao wanawake wale, anarudi kaburini na hapo analia. Alifikiri mtu ameuiba mwili wa Yesu, ingawa malaika walikuwa wamesema amefufuka katika wafu. Yesu anakuja na kusema naye, lakini Mariamu anafikiri ni mtunza-bustani (Yohana 20:14 – 18).

Kisha Yesu anasema, “Mariamu!” Anamtaja jina lake, na ghafla Mariamu anamtambua kuwa ni Yesu. Alikuwa kweli hai! Alikuwa amefufuka!

#### **Ni kweli Yesu alifufuka kutoka wafu?**

Wapo watu ambao hawaamini maelezo ya Biblia kuhusu kufufuka kwa Yesu. Zifuatazo ni baadhi ya sababu wanazotoa kwa kutokuamini kwao:

1. Wanasema: “Yesu hakufa msalabani; ilionekana tu kama amekufa. Alizinduka baadaye kutokana na ubaridi wa kwenye kaburi”.

**Lakini** Biblia inasema wazi kuwa, Yesu alikuwa amekufa msalabani (Yoh. 19:33). Katika Marko 15:42–45 tunasoma vile Pilato alivyotaka kuona kama Yesu alikuwa kweli amekufa. Alimtuma akida wa Kirumi kuthibitisha, na akida huyu alimletea habari kuwa ni kweli alikuwa amekufa. Akida hakuwa mtu wa kuamini, ila kuthibitisha kama alikuwa amekufa au yuko hai.

2. Wanasema: “wanafunzi waliuiba mwili”!

**Lakini**, hili haliwezi kuwa kweli. Kuhani-mkuu na wazee hawakutaka watu wajue kuwa kaburi lilikuwa tupu, na kwamba Yesu alikuwa hai tena. Waliwahonga watu waliokuwa wakililinda kaburi ili waseme wanafunzi wake wameuiba mwili. Soma Mathayo 28:11-15, na utaona uongo huu ulivyotungwa.

Hakuna kitu katika maelezo ya Biblia kinachodokeza kuwa wanafunzi wa Yesu waliuiba mwili. Wanafunzi hawakuamini kwanza kuwa Yesu alikuwa hai tena, mpaka walipomwona. Baada ya kufa kwake walikuwa

wameogopa na kuhuzunika sana, kama vile hawaamini kilichotokea. Tena hawakuwa katika hali ya kuweza kuwafanyia ujanja wakubwa wa Kiyahudi.

Baadaye, walipothibitisha kuwa Yesu amefufuka, walikuwa watu waliobadilika sana. Walihatarisha maisha yao wakihubiri kuhusu ufufuo huo, na wapo hata waliokufa kwa imani yao. Kama wangekuwa kweli wameuiba mwili na kufanya ujanja, wasingeweza kufanya mambo hayo.

3. Wanasema: “aliuacha mwili wake nyuma, na kurudi kama mzima au roho”. Lakini, Biblia inatuambia waziwazi katika Marko 16:6 kuwa, wale wanawake walikwenda kaburini mwili ulipolazwa, na malaika walisema nao pale. Kama kweli Yesu aliwatokea wanafunzi wake na kuwaonesha makovu katika mikono yake, miguu na mbavu, basi ni lazima awe amerudi kutoka kwa wafu, na kaburini alipokuwa amelazwa lazima paonekane patupu. Kwa vyovyote, viongozi wa Kiyahudi wangependa waoneshe kwamba alikuwa bado amekufa, lakini hawakuweza kwa kuwa alikuwa hai.

Imani ilihitajika ili kukubali kuwa Yesu alifufuka kutoka kwa wafu. Hata Tomaso, aliyekuwa mfuasi wa Yesu, mwanzoni hakuamini. Hakuwa ameshawishika kuamini mpaka alipomwona Yesu kwa macho yake. Yesu anamwambia: “Heri wale wasioona, wakasadiki” (Yoh. 20:29).

### **Wakati wa Ufalme wa Mungu ulikuwa umefika?**

Wanafunzi wa Yesu, hatimaye, walipohakikisha kuwa Yesu alikuwa hai tena, walitegemea kwamba angeusimamisha Ufalme wa Mungu moja kwa moja. Kwa siku 40 Bwana alikuwa nao, akiwafundisha juu ya Ufalme huo (Matendo 1:3). Walimuuliza:

“Je, Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme?” (Matendo 1:6).

### **Yesu aliwajibu:**

“Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe” (Matendo 1:7)

Kulikuwa na kazi ya kufanywa kabla Ufalme huo haujasimamishwa. Wanafunzi ilibidi waende ulimwenguni, wakiihubiri Injili ya huo Ufalme. Yote haya yalitokea miaka 2,000 iliyopita, lakini kazi hiyo ya kuhubiri bado inaendelea hata sasa.

### **Kupaa**

Wakati Yesu alipokuwa akiwazungumzia wanafunzi wake mambo haya katika Mlima wa Mizeituni, nje kidogo ya Yerusalemu, alinyakuliwa kutoka kwao kwenda mbinguni. Walipokuwa wakimtazama anavyopaa, malaika wawili waliwasemesha. Maneno ya hao malaika yanatuambia kwa uhakika kuwa, Yesu atarudi. Tunaambiwa:

“Walipokuwa wakikaza macho mbinguni, yeye alipokuwa akienda zake, tazama, watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe, wakasema, Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi hiyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni”

(Matendo 1:10,11).

Hebu ona jinsi msitari huu unavyokazia mambo. Hausemi tu kuwa, ‘Yesu atarudi’. Unasema, **“Huyu Yesu...”** na kama vile kuondoa mashaka yoyote wanayoweza kuwa nayo, anasema, **“aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni.....”**

Walimwona Yesu akienda kimwili juu (kumbuka, hakuwa roho).

Atakuwa ni Yesu huyo huyo, na **atarudi kwa namna hiyo hiyo kama alivyokwenda**. Ulikuwa ni ujumbe mzuri sana wa matumaini, malaika hao waliowapa hao wanafunzi. Atakuja tena kimwili, sio kwa kufa tena, bali

kutawala kama Mfalme juu ya dunia yote. Hapo ndipo atakapourudishia upya Ufalme wa Israeli (Matendo 1:6).

### Ufufuo wa Yesu, na Ufufuo wetu

Katika 1 Wakorintho 15, mtume Paulo anaongelea ufufuo wa Yesu Kristo. Anasema, kama Yesu hakufufuliwa kutoka kwa wafu, basi imani yetu ni bure, na dhambi zetu hazijasamehewa. Wale ambao wamekufa 'wameishia'; hakuna matumaini juu yao (1 Wakor 15:17-19). Ni picha mabaya ilioje!

**Lakini** anasema katika 1 Wakorintho 15:20 – 23 kuwa:

"Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala (waliokufa).	Kristo amefufuliwa katika wafu. Yeye ni wa kwanza; wengine watafuata.
Maana mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kiyama ya wafu (ufufuo) uliletwa na mtu.	Mauti ililetwa na Adamu, ufufuo kutoka kwa wafu umeweza kuja tu kwa njia ya Yesu.
Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa".	Kila mtu anakufa kwa kuwa kila mtu yuko 'katika Adamu'. Wale wote walio 'katika Kristo' (walio 'Wakristo'), watawekwa hai Kristo atakaporudi duniani.





Hili linamaanisha kuwa, kama tutakufa kabla Yesu hajarudi, sisi nasi tunaweza kufufuliwa kutoka kwa wafu. Lakini tutaweza tu kupewa nafasi katika Ufalme wa Mungu duniani kama tupo 'katika Kristo'. Tunaweza tu kuwa Wakristo kama tukibatizwa katika mauti yake (Tazama Wagalatia 3:27-29).

### Wafu wanafufuliwaje, na wanakuja na mwili gani?

Hili ni swali ambalo watu walikuwa wakijiuliza katika siku za Paulo (1 Wakorintho 15:35). Yesu alikuwa na mwili alipofufuka kutoka kwa wafu, kwa hiyo hao watakaofufuliwa kutoka kwa wafu atakaporudi, watakuwa na miili (hawatakuwa roho). Yesu anaishi sasa; amepewa mwili ambao hauwezi tena kufa.

Inakuwa wazi kama unavyoona unaposoma 1 Wakor. 15 kuwa, wale wanaopewa uzima usio na mwisho, watapeleka miili iliyobadilishwa.

Miili yetu ya sasa ni 'ya kufa'; inakufa. Tunapata maumivu, na kuna wakati tunaugua. Hao wanaopewa nafasi katika Ufalme wa Mungu, watakuwa na miili mipya, 'isiyokufa'. Watafanywa wasiwe 'wa kufa' tena, kama tunavyosoma katika 1 Wakor 15:50 – 57. Ni tumaini zuri la ajabu kiasi gani hili Mungu ametupa!

-  Tunaweza kusamehewa dhambi zetu kupitia kwa Bwana Yesu.
-  Tunaweza kufufuliwa kama alivyofanyiwa yeye.
-  Tunaweza kupewa miili isiyokufa.
-  Tunaweza kupata nafasi katika Ufalme wake duniani.

Ndio maana mtume Paulo anasema:

"Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo" (1 Wakor. 15:57).

Ni ujumbe wa maana sana wa wokovu. Yesu aliwaambia wanafunzi wake wauhubiri kwa watu wote. Sisi nasi tutahitaji kuifikisha kwa watu wengine.

### Muhtasari

1. Yesu alifufuka kutoka kwa wafu.
2. Hakuwa roho iliyofufuka; alikuwa na mwili wa nyama na mifupa.
3. Yesu yuko hai leo. Alipaa mbinguni alipo kwa sasa.
4. Atarudi katika dunia hii kwa namna ile ile alivyoondoka kwenda mbinguni.
5. Kama tumekuwa Wakristo, tunaweza kufufuliwa kwa wafu na kupewa miili isiyokufa, Bwana Yesu atakaporudi.

**Vifungu vya kusoma:** Matendo 1

Soma pia habari zinazohusu ufufuo katika Mathayo 28 na Luka 24.

**Msitari wa kushika:** Matendo 2:24

“...ambaye Mungu alimfufua (Yesu), akiufungua uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao”.



## MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

*Karatasi ya maswali: namba 5*

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa 'Kazi ya ziada' unaweza kulijibu swali kama ukipenda, au kuliacha kama unaona huliwezi. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

### MASOMO: 16- 19

16. A. Sahihi au Kosa? Katika semi zifuatazo, amua ni zipi zinasema ukweli na zipi zimekosewa:
- a) Mama wa Yesu alikuwa Mariamu.
  - b) Baba wa Yesu alikuwa Yusufu.
  - c) Yesu alikuwa mbinguni kabla ya kuzaliwa.
  - d) Mungu alijua tangu mwanzo kuwa angemtuma Yesu.
  - e) Yesu alikuwa na hulka ya kibinadamu (kama sisi) alipokuwa duniani.
  - f) Yesu anaitwa 'Mungu Mwana' katika Biblia.

Kazi ya ziada

B. Mpangilio wa sasa kulingana na **hadhi** ni huu:

Mungu – Yesu – malaika – mtu - wanyama.

Ni mpangilio upi uliokuwa kabla ya kifo cha Yesu? (Waebrania 2:9 inaweza kukusaidia)

17. A. Ni kwa namna gani Yesu alikuwa kama Mungu, Baba yake?  
B. Ni kwa namna gani Yesu alikuwa kama sisi?  
C. Kilichotokea ni nini wakati Yesu alipokuwa akijaribiwa nyikani?  
D. Tunaweza kujifunza nini kutokana na namna Yesu alivyoishi maisha yake?

Kazi za ziada

E. Yesu anasema nini katika Hotuba yake ya Mlimani juu ya:

- a) Talaka (Mathayo 5:32).
- b) Kuweka hazina (Mathayo 6:19-21).
- c) Kuhukumu wengine (Mathayo 7:1-5).
- d) Waalimu/Manabii wa uongo (Mathayo 7:15- 23).

F. Usume tena mfano wa Mpanzi (Mathayo 13: 1-8) na maelezo yake aliyotoa Yesu (Mathayo 13:18-23).

Kama mbegu inasimama badala ya Neno la Mungu, yafuatayo yanawakilisha nini:

- a) Njia
- b) Miamba
- c) Udongo mzuri.

Tunajifunza nini kutokana na mfano huu?

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## ROHO MTAKATIFU WA MUNGU

## SOMO: Marko 1

“Mungu akasema, iwe nuru, ikawa nuru” (Mwanzo 1:3). Inaonekana kama rahisi sana. Lakini hebu ifikirie hiyo nguvu kubwa ya kiutambuzi na kiuweza iliyohitajika, kabla hiyo nuru haijaweza kupatikana:

“Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi” (Mwanzo 1:1).

Fikiri tena juu ya kazi kubwa inayobidi ifanywe, mtu anapotaka kujenga nyumba. Fikiria jinsi inavyobidi kufanya maandalizi na kupanga; haja ya kupata mafundi wa namna mbalimbali, wote wakifanya kazi moja. Fikiri ni kiasi gani mtu analazimika kufikiri na kupanga, na ni nguvu au raslimali ngapi zinahitajika!

Tunaambiwa katika Zaburi:

“Kwa neno la BWANA mbingu zilifanyika, na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake.....Maana yeye alisema, ikawa, na yeye aliamuru, ikasimama” (Zab. 33: 6,9).

Katika Mwanzo 1:2 tunaoneshwa kuwa, ni Roho ya Mungu iliyotumika katika kuumba:

“Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji”.

**Pumzi ya Mungu na Roho ya Mungu**

Uweza wa Mungu ulitumika tena katika kuziongoza akili za watu walioandika Biblia. Biblia inajulikana kama, ni: “Andiko lenye pumzi ya Mungu”. Mungu aliwatumia watu walioandika, katika kuyaandika **maneno yake**. Kwa hiyo tunasoma katika 2 Petro 1:21 kuwa:

“Unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu, bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.”

‘Unabii’ hauna maana ya kutabiri tu; kusema yatakayotokea. Katika Biblia unabii una maana ya kusema anachosema Mungu; iwe ni juu ya mambo ya nyuma, ya wakati uliopo, au mambo yajayo.

Tazama: ni waandishi 30 walioandika maneno yaliyopo kwenye Biblia, kwa kipindi cha zaidi ya miaka 1500. Kama Mungu asingekuwa kwa ‘pumzi yake’ ameongoza uandishi huo, kwa vyovyote kungekuwa na mkorogano mkubwa wa mawazo na utata wa ubora.

Badala yake, Biblia inayaongelea mambo yake yaleyale inayosemea, kuanzia mwanzo hadi mwisho, tena katika mtiririko na uwiano mzuri wa ajabu.

Yafuatayo ni baadhi ya mambo tunayoambiwa kuhusu Roho ya Mungu:

1. Roho ya Mungu inaweza kuumba.	Kama ilivyo katika Mwanzo 1:2
2. Mungu, kwa Roho yake, anajua kila kitu.	Zaburi 139: 2-12
3. Mungu amefanya yote aliyounda kwa Roho yake.	Zaburi 104:29-30, Ayubu 26:13
4. Roho ya Mungu inawajia watu kuwawezesha kufanya mapenzi ya Mungu.	Waamuzi 6:34, 11:29, Wagalatia 5:16
5. Manabii walijua nini la kusema kwa njia ya Roho ya Mungu.	Mika 3:8, Zekaria 7:12, Nehemia 9:30, 2 Petro 1:21

### **Nini maana ya Roho Mtakatifu?**

Neno 'takatifu' lina maana ya 'kilichotengwa' kwa kusudi maalumu.

Kwa hiyo tunauzungumzia Uweza wa Mungu ulio Mkuu kama ni Roho iliyo ya kipekee sana; Roho Takatifu, kama mtume Petro anavyosema:

“Unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu, bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu” (2 Petro 1:21).

Katika Biblia, Roho Mtakatifu (au Roho Takatifu -'Holy Spirit'), ni uweza wa Mungu; uweza ambao katika huo Mungu anatimiza makusudi yake na mipango yake.

Neno 'Mtakatifu' lililotumiwa na waliotafsiri kwenye Kiswahili, sio sahihi. Linaleta kuhisi kama vile ni 'mtu' au 'nafsi', badala ya kitu (nguvu/uweza). Maana hiyo haiko kwenye lugha ya kiasili (Kiyunani, iliyotumika kuandika Agano Jipya), wala katika maneno 'Holy Spirit' kwenye Kingereza. (Tuelewe hivyo, ingawa tutaendelea kutumia neno 'Mtakatifu' zaidi kama lilivyoandikwa, kwa kuwa hatuwezi kubadili tafsiri iliyopo hapa)

### **Roho Mtakatifu na Bwana Yesu Kristo**

Ni Roho Mtakatifu aliyefanya Bwana Yesu azaliwe. Kwa hiyo tunaambiwa juu ya Yesu kwamba:

“Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi: Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu” (Mathayo 1:18).

Katika ubatizo wake katika Mto Yordani, Yesu alipewa Roho Mtakatifu bila kipimo (yaani, bila kuwekewa kiwango). Tunasoma katika Yohana 3:34 kuwa:

“Kwa kuwa yeye aliyetumwa na Mungu huyanena maneno ya Mungu; kwa sababu hamtoi Roho kwa kipimo” (yaani, .....kwa sababu hiyo, Mungu hampi Roho yake kwa kumpimia).

Kwa hiyo, Yesu Kristo alipewa uweza wote. Kwa watu wengine katika nyakati za Agano la Kale na Agano Jipya, Mungu aliwamegea tu kishemu cha uweza wake. Hakuna mtu mwingine aliyewahi kufaa kupewa uweza kama huo Mungu aliomba Yesu. Yesu alitumia uweza huo mkubwa katika kufanya miujiza, na ulimsaidia katika kazi yake ya kuhubiri.

Hebu angalia maneno haya kutoka katika Isaya 61:1,2:

“Roho ya Bwana Mungu i juu yangu, kwa sababu BWANA amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao..... kuwafaraji wote waliao”.

Hebu kisome hicho kifungu chote katika Biblia yako. Picha unayoipata ni picha ya Yesu akitumia Roho ya Mungu katika kuifanya kazi ya Mungu. Hakuitumia kujijenga au kujinufaisha, bali katika kuwafundisha na kuwasaidia wengine.

### **Wanafunzi wake waliahidiwa Roho Mtakatifu**

Yesu aliwaahidia wale wanafunzi wake kumi na wawili kuwa, nao pia wangepewa Roho Mtakatifu baada ya yeye kuondoka na kuwaacha kwenda zake mbinguni. Katika Yohana 14:25, 26 anawaambia:

“...Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia”.

Baada ya Bwana Yesu kuwaacha, wanafunzi hao wangehitaji msaada katika kuhubiri kwao, na katika kuwekea misingi kanisa la kwanza. Mungu pia angetumia Roho Mtakatifu katika kuwawezesha kuliandika Agano Jipya.

Utambue hapa ya kuwa, katika mistari hiyo hapo juu, Roho Mtakatifu angekuwa/ingekuwa hapo kuwafundisha na kuwafanya wakumbuke yote yale Yesu aliyosema na kufanya, katika maisha yake hapa duniani. Roho Mtakatifu anazungumziwa hapa kuwa ni 'Msaidizi' na kwingine anaitwa 'Mfariji'.

Yesu, mara kadhaa, anazungumzia Roho Mtakatifu kama vile ni mtu; hili linawachanganya wengi. Lakini ukiangalia vizuri, ni lugha tu ya picha. Hebu tufungue Zaburi ya 65, na kusoma msitari wa 13. Unasema:

“Na malisho yamevikwa kondoo, na mabonde yamepambwa nafaka, yanashangilia, naam, yanaimba”.

Sasa, tunaposoma hivi, tunapata picha nzuri sana ya mazao mengi ya nafaka yaliyoshonana kwenye bonde, lakini hatufikiri hata kidogo kuwa bonde kweli linaweza kushangilia na kuimba. Ni namna tu ya mwandika Zaburi ya kulisemea jambo; kuelezea shangwe. Bonde halina midomo! Ni jinsi tu kitu kinavyoweza kuelezewa kwa namna nyingine au kwa hamasa fulani.

Yesu anaposemea Roho Mtakatifu kama vile ni nafsi fulani inayofanya hili au lile, anatuonesha tu uhalisia wa hiyo Roho kimfano; huo uweza wa Mungu.

Mfano mwingine wa lugha kama hii upo katika Methali 3:13–19. Isome mistari hii na utagundua kuwa, mwandishi anaongelea 'hekima' kama vile ni mwanamke mrembo, mwenye maadili. Hii ni namna iliyo dhahiri zaidi ya kusema kuwa, hekima ya kweli inayotokana na kumjua Mungu, sio tu kwamba ni kitu kizuri sana (msichana-mrembo), bali pia ni kamilifu.

Maandiko yanatumia lugha kama hiyo kuihusu Roho ya Mungu, kuonesha vile uweza wake ulivyo mkamilifu na unayofanya yasiyoshindwa. Utaona mifano mingine ya matumizi ya namna hii ya lugha mbeleni.

### **Roho yawajea wanafunzi**

Tumeshaona kuwa Yesu aliwaahidia 'uweza' wanafunzi wake, kabla ya kupaa kwenda mbinguni. Aliwataka wasiondoke Yerusalemu: “bali waingoje ahadi ya Baba” (Matendo 1:4).

Aliwataka **wabatizwe**: “Katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache” (ms. 5).

Katika Matendo 2 tunasoma vile, walipokuwa wakisubiri pamoja, Roho Mtakatifu alivyowajea: “Kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi” (ms.2). Upepo huo uliitikisa nyumba walimokuwa wakikaa. Ndimi za moto zilionekana kwa kila mmoja wao, na kuanzia hapo, waliweza kufanya miujiza.

### **Jinsi hiyo Roho inavyotujea**

Huo uweza wa kipekee ulihitajika katika kuwaweka pamoja waumini wa kwanza (kanisa/eklesia), na hauhitajiki kwa sasa. Kuna mengi zaidi juu ya hili katika somo linalofuata. Kwa sasa, Mungu anaongea nasi kupitia katika Neno lake.

Tumeshaona ya kuwa hao walioandika Biblia, walifanya hivyo kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Ni vizuri kutambua hapa pia kwamba, maneno haya mawili, Roho Mtakatifu, hayapo katika Agano la Kale. Katika Agano la Kale maneno yaliyotumika ni 'Roho ya Mungu'. Roho ya Mungu iko katika Neno lake.

Yesu aliwahi kusema: “Maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima” (Yohana 6:63). Kwa hiyo, tunapolisoma Neno la Mungu, kwa namna fulani tunaipata Roho ya Mungu. Kulisoma Neno la Mungu kunaweza kuleta mabadiliko makubwa katika maisha yetu, na kunaweza kutusaidia kukua katika kumpendeza Mungu.

Hebu basi tulisome Neno la Mungu kwa bidii zaidi na kwa kuomba, tukiyakumbuka maneno ya Petro katika waraka wake wa kwanza, yanayosema: “Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa, yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpata kuukulia wokovu” (1 Petro 2:2).

**Tumejifunza nini juu ya Roho Mtakatifu?**

1. Roho Mtakatifu ni uweza wa Mungu.
2. Biblia iliandikwa kwa uweza wa Roho Mtakatifu.
3. Yesu alizaliwa kwa uweza wa Roho Mtakatifu.
4. Manabii wote wa Mungu walipewa kwa kipimo Roho yake, lakini kwa Yesu ilitolewa 'bila kipimo'.
5. Uweza maalumu ulitolewa wa Roho katika karne ya kwanza, baada ya hapo uliondolewa.
6. Kwa sasa Mungu anatuzungumzia kupitia katika Neno lake, Biblia, iliyoandikwa kwa uweza wa Roho Mtakatifu.

**Vifungu vya kusoma:** Matendo 10: 34–43, Yohana 14

**Jifunze kwa moyo:** Marko 16:15,16

“Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa”.

**MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA****KARAMA ZA ROHO MTAKATIFU****SOMO:** Matendo 8

Yesu aliwaahidi wanafunzi wake kuwa wangepewa Roho Mtakatifu. Aliwaambia:

“Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya, watahika nyoka, hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa, wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya” (Marko 16:17,18).

Wafuasi hao walikuwa wameahidiwa kupewa Roho Mtakatifu kwa uweza maalumu, ili kuwasaidia katika kazi yao. Walikuwa wameambiwa wasiondoke Yerusalemu, “Bali waingoje ahadi ya Baba” (Matendo 1:4). Kwa hiyo waliingoja kama walivyoamriwa.

Tumshaona jinsi siku moja, katika siku ya Pentekoste, walipokuwa wote pamoja, jambo la ajabu lilipotokea. Nyumba walimokuwamo, ilitikiswa na upepo wa nguvu uliokuwa ukivuma na kwenda kwa kasi, na: “Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka” (Matendo 2:4). Sasa, ni kwa nini wanafunzi walipewa karama maalumu ya kiroho? Tumeambiwa hapa walisema kwa lugha nyingine!

**Zilithibitisha kuwa ujumbe waliotoa ulitoka kwa Mungu**

Yesu alikuwa amesulubiwa, na Mungu alikuwa amemfufua kutoka kwa wafu. Alikuwa amepaa kwenda mbinguni, akikiacha kikundi hiki kidogo cha wanafunzi kumi na wawili (mitume) kwenda ulimwenguni mwote, kuihubiri, “Injili kwa kila kiumbe” (Marko 16:15). Ilikuwa ni kazi kubwa.

Je, watu wangewasikiliza? Mazingira yalikuwa magumu, na walikuwa watu wa kawaida tu wasio na umaarufu wowote. Kwa hakika isingekuwa rahisi watu kuamini habari ya mtu aliyerudishiwa uhai baada ya kufa kwa siku tatu. Agano Jipya lilikuwa bado halijaandikwa.

Kwa hiyo wanafunzi walipewa uweza wa kufanya miujiza na kuongea katika lugha zisizokuwa zao kama ishara ya kuwa, walilokuwa wakisema lilitoka kwa Mungu.

Katika siku hiyo ya Pentekoste, walitoka hapo na kuwahubiri Wayahudi katika lugha ambazo hawakuwahi kujifunza. Ni wazi wasingeweza kuziongea bila ya uweza walioupata kutoka kwa Mungu. Ndio maana watu waliowasikia, tunaambiwa:

“Wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana, Tazama, hawa wote wasemao (wanaohubiri) si Wagalilaya? Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyojaliwa nayo?” (Matendo 2:7,8).

Kulikuwa na watu wengi waliotoka katika mataifa mengine pale Yerusalemu siku ile, waliokuwa wamekuja kuidhimisha siku-kuu ya Pentekoste.

**Karama hizi za Roho zilisaidia kuliongoza kanisa**

Matokeo ya mahubiri yao ya siku hiyo ya Pentekoste ni kwamba, wanaume na wanawake wapatao 3,000 walijiunga na wanafunzi hao na kuwa Wakristo (Matendo 2:41). Kwa namna hii kanisa la Kikristo lilikuwa limeanza vizuri.

Lakini hebu fikiria vikwazo ambavyo wangevipata. Familia kubwa kama hiyo ya Wakristo ingehitaji mtu wa kuwaongoza, kuwafundisha na kutoa ushauri kuhusiana na mipango waliyokuwa wakipaswa kuifanya kwa ajili ya kuieneza Injili. Wasingejifunza kitu kutoka katika Agano Jipya, kwa kuwa lilikuwa bado halijaandikwa.

Kwa hiyo vipawa vya Roho vilitumwa, sio tu kwa ajili ya kuwahakikishia walio nje ukweli wa ujumbe wa mitume, bali pia kusaidia na kuwafundisha Wakristo hao wa kwanza, na kuyawekea taratibu makusanyiko ya awali yaliyokuwa yakianza.

### **Karama hizi zilikuwa ni nini?**

Tumeshaona kuwa mitume hao waliweza kuongea katika lugha za kigeni, lakini tuaambiwa pia kuwa, waliweza pia kuwaponya wagonjwa.

Katika 1 Wakorintho 12:4-22 mtume Paulo anaonesha jinsi waumini mbalimbali walivyopata karama mbalimbali, na namna kila moja ilivyokuwa itumike kwa ajili ya wengine. Baada ya hapo katika msitari wa 28 na wa 29 anatoa orodha ya hizo karama:

“Na Mungu ameweka wengine katika kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, na wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha”.

### **Karama za Mungu hazinunuliwi**

Mara baada ya wanafunzi kupokea karama za Roho Mtakatifu, walitoka kuanza kuhubiri. Mfuasi wa Yesu aliyetwa Filipo alishuka kwenda Samaria na kuanza kuwafundisha watu huko. Wengi waliomsikiliza waliyaamini maneno yake juu ya Yesu na Ufalme wa Mungu unaokuja, na wakabatizwa. Miongoni mwa wale waliobatizwa alikuwapo mtu aliyetwa ‘Simoni, mchawi’. Alikuwa mtenda miujiza aliyewashangaza wengi katika Samaria kwa miaka mingi, kwa ujanja wake.

Mitume waliokuwa katika Yerusalemu waliposikia juu ya watu wengi kujiunga katika Samaria, walimtuma Petro na Yohana kuongeza nguvu pale.

Petro na Yohana, wakiwa ni mitume, waliweza kuwapa wengine uweza wa Roho Mtakatifu, kwa kuwawekea mikono yao. Hiki ni kitu kilichokuwa kikiweza kufanywa na wale mitume wa kwanza tu.

Huyo Simoni, akiwa anatazama, aliona wanaume hao wawili wakiwawekea mikono yao wafuasi wapya na kuwafanya wapate Roho Mtakatifu. Alishangaa! Alianza kufikiri angeweza kutajirika na kuwa maarufu sana, kama angeweza naye kuwapa watu karama hii. Alitaka kuununua uweza huo kwa Petro. Hiki kilikuwa kitu kibaya sana kujaribu kufanya. Petro alimwambia:

“Huna fungu wala huna sehemu katika jambo hili, kwa kuwa moyo wako si mnyofu mbele za Mungu. Basi, tubia uovu wako huu, ukamwombe Bwana, ili kama yamkini, usamehewe fikra hii ya moyo wako. Kwa maana nakuona u katika uchungu kama nyongo, na tena u katika kifungo cha uovu” (Matendo 8:21-23).

Simoni aliogopa, na kumwomba Petro amwombe. Hatuambiwi kilichoendelea.

Habari hii inatuonesha wafuasi wa awali wakitumia uweza wa Roho Mtakatifu, katika kuwahubiri watu juu ya Yesu na Ufalme unaokuja.

Soma Matendo 8:15 – 25 na utafakari vizuri yafuatayo:

1. Msitari wa 18 unasema kuwa, ilikuwa ni kwa kuwekewa mikono **na mitume tu** ndipo walipopata Roho Mtakatifu.
2. Simoni hakupata karama ya Roho Mtakatifu alipobatizwa.
3. Mtume Petro na Yohana waliwapa waumini wapya waliobatizwa karama za Roho Mtakatifu, baada ya kuomba na kuwawekea mikono (hii ilikuwa ni namna ya kuwabariki).
4. Baada ya Simoni kupokea Roho Mtakatifu kwa namna hiyo, hakuweza yeye kuwapatia wengine; na hiki ndicho hasa alichokitaka.

Hili linatuonesha ya kwamba, ni **mitume tu** waliokuwa na uwezo wa kutoa karama za Roho Mtakatifu. Walipokufa hakuna karama tena zilizotolewa na zilitokomea na watu wa kizazi kile.

## Mwisho wa hizo karama

Tumekwishaona kuwa, katika enzi hizo za Wakristo wa kwanza hakukuwa na Agano Jipya; lilikuwa bado halijaandikwa. Tunafikiri hii ilikuwa ndio sababu ya Mungu kutoa hizo karama, kwa kuwa zilikuwa ni za muhimu sana.

Leo tunaweza kusoma wenyewe (au kusomewa) juu ya maisha ya Bwana Yesu, na tunaweza kuzisoma/kusomewa barua ambazo mitume waliwaandikia Wakristo wa wakati wao. Lakini mitume wao hawakuwa na Maandiko hayo. Mitume, manabii na waalimu wenye uweza huo maalumu kutoka kwa Mungu, walikuwa ni msaada wa lazima sana kwa makanisa ya kwanza.

Uandishi wa Agano Jipya ulipokamilika, hapakuwa na haja tena ya msaada wa kipekee kutoka kwa Mungu. Mambo yote ambayo Wakristo wangetaka kuyajua, yalikuwa yameandikwa kwa ajili yao katika Biblia. Na, kwa hiyo, karama hizo za kiroho ziliondolewa.

Mtume Paulo alisema hili lingetokea, akiwaandikia Wakorintho. Aliwaambia:

“Upendo haupungui neno (haushindwi) wakati wowote, bali ukiwapo unabii (yaani, karama ya kusema anachosema Mungu) utabatilika (utashindwa); zikiwapo lugha (yaani, karama ya kuweza kuongea lugha zingine bila kuzijifunza) zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika”

(1 Wakorintho 13:8).

Inaelekea karama hizi hazikuondolewa haraka wakati Agano Jipya lilipokamilika. Miaka ilivyopita wale Wakristo waliokuwa nazo walikufa, na Wakristo waliofuata hawakuzipewa; kwa hiyo hazipo.

## Kuna aliye na karama hizi leo?

Wapo watu wanaodai kuwa wana hizo karama za Roho. Na hasa wanadai wana uwezo wa kuongea ‘vilugha’ na kuponya wagonjwa. Tuwachukulieje hao wanaodai wanao uweza wa miujiza ya Roho ya Mungu kwa wakati huu?

1. Tujikumbushe mtume Paulo alichosema katika 1 Wakorintho 13 kuwa, wakati ungefika ambapo karama za kiroho zingeondolewa. Wakati huo ulikuja lini, kama sio muda mfupi baada ya Agano Jipya kukamilika? Haiwezi kuwa inasubiri ujio wa Ufalme, maana wakati huo karama hizo zitaongezwa kuliko ilivyowahi kutokea. Karama hizo zinaongelewa kuwa ni, “kipawa cha mbinguni...nguvu za zamani zijazo” (Waebrania 6:4,5). Wafuasi wa Kristo wa kwanza walipata ‘malimbuko’ tu ya karama hizi zitakazotolewa kwa wingi wakati wa Ufalme.
2. Tumeona kuwa karama za Roho Mtakatifu zilitolewa ili kulisaidia Kanisa la Kweli. Kanisa lenye kweli linaliamini na kulihubiri Neno la Mungu. Watu karibu wote (kama sio wote) wanaodai kuwa na uweza huo leo, wanahubiri mambo ambayo hayafundishwi katika Neno la Mungu. Kwa hiyo inatupasa tuyakatae madai yao.
3. Inatubidi tukiri kuwa, hatuvutiwi na wingi wa ile inayoitwa ‘miujiza’ wanayoifanya. Mara nyingi uponyaji wao umeonekana haukuwa lolote baada tu ya muda, na unafuu unaopatikana unaweza kuelezeka kisayansi. Watu wa mazingaumbwe na waganga-wa-kienyeji, au wachawi wanaweza mara nyingi nao kufanya hivyo hivyo. Hakuna aliyewahi kumfufua mfu!

Mungu kweli anaweza, na hata sasa anafanya kazi kupitia katika Roho yake leo, lakini **haruhusu watu watumie Roho yake**. Watu wanaoamini yale yote yaliyoandikwa katika Biblia, hawatadai kuwa wana karama za Roho. Wanatambua kuwa karama hizo ziliwekewa kupita baada ya Maandiko ya Agano Jipya kukamilika.

## Mungu bado anafanya kazi

Kwa sasa, hatuna uwezo wa kufanya miujiza na kuongea vilugha. Hata hivyo, Roho Mtakatifu wa Mungu bado anafanya kazi leo, kama kwa mfano, Mungu anapojibu maombi, na Mungu bado anaongea nasi kupitia



katika Neno lake. Tunapoisoma Biblia, tunakuwa tunafundishwa na Roho ya Mungu, kwa namna iliyo ya hakika sana.

Kama tunataka kumpendeza Mungu, basi hebu tuoneshe tunavyomshukuru kwa yale yote aliyotufanyia kwa kulisoma Neno lake, na kujifunza yote tunayoweza kutokana nalo. Neno linasema: “Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kuwaongoza, na kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema” (2 Timotheo 3:16,17).

#### **Muhtasari**

1. Karama za Roho Mtakatifu zilitolewa kwa Wakristo wa awali tu.
2. Zilikuwa zikidhi malengo matatu:
  - (a) Kukamilisha Agano Jipya.
  - (b) Kuwa ishara kwa wasioamini.
  - (c) Kusaidia katika kulijenga kanisa la kwanza.
3. Zilitolewa tu mpaka Maandiko ya Agano Jipya yalipokamilika, baada ya hapo ziliondolewa.
4. Hakuna mtu tangu hapo ameweza kufanya miujiza kwa uweza wa Roho Mtakatifu.
5. Hao wanaodai kufanya miujiza leo, wanaweza kuwa tu na uwezo fulani usio wa kawaida, kama Simoni katika Samaria.

**Vifungu vya kusoma:** 1 Wakorintho 13 na 14

**Jifunze kwa moyo:** 1 Wakorintho 13:8

“Upendo haupungui neno wakati wowote, bali ukiwapo unabii utabatilika, zikiwapo lugha, zitakoma, yakiwapo maarifa, yatabatilika”.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

### DHAMBIBI NA MATOKEO YAKE (SEHEMU YA 1)

**SOMO:** Mwanzo 2 na 3

Dunia iko katika hali mbaya: vita, njaa, magonjwa, vurugu, mauaji, mateso n.k. Lakini, Mungu aliiumba dunia ikiwa 'njema'. Ni mwanadamu aliyeichafua! Hulka ya mwanadamu ya uchoyo, ubinafsi, wivu na kutotii-mamlaka vimeiharibu jamii na dunia hii.

#### Yalianzia wapi 'kwenda mrama'?

Hapo mwanzo Mungu alimuumba mwanadamu wa kwanza, Adamu. Adamu aliumbwa kutokana na mavumbi ya nchi:

"Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya nchi, akampulizia puani pumzi ya uhai, mtu akawa nafsi hai" (Mwanzo 2:7).

Mungu aliweka bustani nzuri kwa ajili ya Adamu kuishi humo, na baada ya hapo akampatia mke aliyemwita Hawa. Adamu na Hawa hawakuonesha kama wangemtii Mungu au la mpaka walipojaribiwa. Mungu alikuwa amewapa amri moja ndogo:

"Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika" (Mwanzo 2:16,17).

#### Adamu na Hawa walikuwa na uchaguzi

Wangeweza kumtii Mungu, au kutomtii na kula tunda la mti uliokatazwa. Walikuwa huru kuchagua. Mungu hakuwa ametengeneza watu walio kama mashine; wasioweza kuchagua kama watii au wasitii. Mungu alitaka wawe watu wanaoweza kuichagua njia yake kwa sababu ya kumpenda na kumheshimu.

Nyoka alikuja na kuwadanganya. Nyoka aliwaambia kuwa wasingekufa kama wangekula tunda lililokatazwa, na kwamba badala yake wangekuwa kama Mungu, wakijua mema na mabaya. Adamu na Hawa walitaka kuerevuka; kufanana zaidi na malaika. Walichagua kulila hilo tunda, na kwa kufanya hivyo walifanya dhambi kwa kutomtii Mungu.

#### Adhabu

Mungu alikuwa amewaambia wangekufa kama wasingemtii. Kwa hiyo Adamu na Hawa walihukumiwa kifo, na kutimuliwa watoke katika bustani ya Edeni. Ingawa waliishi maisha marefu baada ya hapo, walibadilika na kuwa viumbe vinavyokufa. Walikuwa sasa wakichoka, wakiugua, wakizeeka na hatimaye kufa, kama ilivyo sasa kwako na kwangu.

#### Kifo ni nini?

Kifo kilikuwa ni adhabu kwa sababu ya dhambi. Mungu alikuwa amesema:

"U mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi" (Mwanzo 3:19).

Kwa hiyo mwili wa Adamu ulioza alipokufa na aliyarudia mavumbi, ambayo ndiyo yaliyokuwa yametumika kuufanya mwili wake. Mavumbi ni udongo. Mungu alimuumba Adamu kutokana na udongo wa nchi, na baada ya hapo alimpulizia pumzi ya uhai, kabla hajawa 'nafsi hai':

VUMBI + PUMZI YA UHAI = NAFSI HAI

Adamu alipokufa, ilikuwa ni:

NAFSI HAI – PUMZI YA UHAI = NAFSI ILIYOKUFA

Kwa hiyo tunaona kuwa:

### NAFSI HAI ukitoa PUMZI YA UHAI ni VUMBI (udongo)

Hakuna sehemu ya Adamu iliyokwenda kuishi mbinguni alipokuwa amekufa; kwa hakika hakuna! Mauti yake yalikuwa ni adhabu ya Mungu kwa ajili ya dhambi, na kifo maana yake ilikuwa ni mwisho wa kuishi; mwisho wa uhai wote. Kifo cha Adamu hakikuwa kiwe na utofauti wowote na chetu. Sisi wote tunafanya dhambi, kwa hiyo sote tunakufa:

“Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi” (Warumi 5:12).

Hili halina maana kwamba watu wote ni wauaji au wazinzi au waongo. Mawazo yasiyo ya wema, yenye ubaya: kiburi, choyo, hasira n.k (ambayo ni udhaifu wetu wote wa kila siku), yote ni dhambi machoni pa Mungu. Hakuna kati yetu atakayekwenda mbinguni tukifa.

### Hakuna chochote kinachoitwa ‘roho’ kisichokufa

Hakuna mahali ambapo Biblia inataja uwepo wa ‘roho’ isiyokufa. Hili lina maana ya kwamba, hakuna kitu kinachoendelea kuishi mtu anapokuwa amekufa. Hakuna cheche ya uhai ya kimbingu isiyozimika katika mwanadamu anapokufa.

### ‘Roho’ ni uhai: kiumbe hai, mtu, nafsi

Ifuatayo ni orodha ya baadhi ya vifungu vilivyopo katika Biblia, vinavyoonesha sehemu neno hili ‘roho’ linapotumika. Hebu uvitazame mwenyewe, uone kama utakubaliana na maoni yaliyotolewa:

REJEA	MAONI
Mwanzo 46:15	Wana wa Yakobo (wanaoishi) wanaitwa ‘nafsi’ ( <b>kwa Kingereza-souls</b> ); lenye maana ya ‘roho’.
Mwanzo 46:26	“Nafsi zote” (all souls) hapa kwa hakika inamaanisha “watu wote”.
Walawi 5:2	“Kama <u>mtu</u> akigusa kitu kilicho najisi ....” -neni ‘roho’ (soul) hapa ndilo lililotafsiriwa ‘mtu’.  “Kama <u>mtu</u> akifanya dhambi, na ....” (ms. 17): Neno ‘roho’ (soul) hapa ndilo lililotafsiriwa ‘mtu’.
Walawi 17:12	Maana ya roho ni <b>mtu</b> . Roho (souls) zinaweza kufanya dhambi, kwa maneno mengine <b>watu</b> wanaweza kufanya dhambi. “.....Hapana mtu mingoni mwenu aliye na ruhusa kula damu.....” (ms. 12).  Neno ‘roho’ (soul) hapa ndilo lililotafsiriwa ‘mtu’. Hapana <u>mtu</u> (‘roho’ yaani mtu) kati yao aliyekuwa akiruhusiwa kula damu.
Yoshua 10:28, 30,32, 35, 37	Neno <u>wote</u> katika mistari hiyo limekaa badala ya Roho: ‘ <u>roho</u> wote pia’ (All the souls).  ‘Roho wote’ (yaani, watu wote) waliangamizwa kabisa. (‘Roho’ wanaweza kuangamizwa; kuuwawa!)  Neno ‘wote’ tena ni neno ‘roho’. “Wao wakawapiga <u>wote</u> pia waliokuwamo....” (And they smote <u>all the souls</u> that were.....)

Yoshua 11:11	Waliwaua roho wote (watu wote); hakuna aliyebaki akipumua.
Matendo 27:37	“Na sisi tuliokuwa ndani ya merikebu tulipata <u>watu 276</u> ”. Neno ‘watu’ hapa ni neno ‘roho’. Roho 276 ni watu 276. (“And we were in all in the ship 276 <u>souls</u> ”) Roho hapa ni wazi ni hao abiria.

Kuna mifano mingi zaidi tungeweza kutoa kuonesha kuwa neno ‘roho’ maana yake ni mtu (au kiumbe hai). Waliotafsiri kwenye Kiswahili, kwa vyovyote walishakuwa na namna zao za kuamini, walichofanya tu ilikuwa kuweka vile walivyoona. Utata unaondoka kama tunaweza kulinganisha na Kingereza, ingawa nacho kina machapisho mengi-mengi.

Neno ‘Roho’ katika Kiebrania ni neno pia linalotumika kuhusiana na wanyama. Hili, bila shaka, linatusaidia kulielewa vizuri zaidi Kimaandiko. Kwenye Mwanzo 1:21, 24, 2:19 ni neno lililotafsiriwa ‘kiumbe hai’ kwenye Kiswahili. Kwenye Kingereza ni ‘living creature’. Yote haya yanathibitisha kile kinachosemwa katika Mhubiri:

“Kwa maana linalowatukia wanadamu linawatukia wanyama, jambo moja lawatukia; anavyokufa huyu ndivyo anavyokufa huyu, naam, wote wanayo pumzi moja; wala mwanadamu hana kitu cha kumpita mnyama; kwa maana yote ni ubatili. Wote huenda mahali pamoja, wote hutoka katika mavumbi, na hata mavumbini hurudi tena” (Mhu. 3:19, 20).

Hakuna utofauti wowote kati ya mtu na mnyama katika mauti. Mnyama hana sehemu inayokwenda mbinguni anapokufa, na mwanadamu ni hivyo hivyo. Wote wanakuwa ni miili isiyokuwa na uhai wanapochacha kupumua; inaoza, inakuwa udongo:

“Roho”: uhai, mtu, kiumbe hai

Vifungu hivi vinatuonesha kinachotokea tunapokufa:

Zaburi 146:4	“Pumzi yake hutoka, hukurudia udongo wake, siku hiyo mawazo yake yapotea”.
Mhubiri 9:5	“Wafu hawajui neno lolote.....”
Zaburi 6:5	“Mautini hapana kumbukumbu lako, katika kuzimu (kaburi) ni nani atakayekushukuru?”
Zaburi 39:13	“Uniachilie nikunjuke uso, kabla sijaondoka nisiwepo tena”.
Zaburi 115:17	“Sio wafu wamsifuo BWANA, wala wowote washukao kwenye kimya” (kaburini).

Vifungu hivi vyote vinaonesha kuwa, watu waliokufa hawana utambuzi wowote; hawawezi kufikiri.

Mfalme Hezekia alipoambiwa kuwa alikuwa afe, alisononeka sana. Alitaka aendelee kuishi kwa kuwa alijua kwenye mauti hakukuwa na kitu. Alimwomba Mungu aishi, ili aweze kuendelea kumsifu:

“Kwa kuwa kuzimu hakuwezi kukusifu; mauti haiwezi kukuadhimisha; wale washukao shimoni hawawezi kuitarajia kweli yako”

(Isaya 38:18).

Badala yake, anamwambia Mungu: “Aliye hai, naam, aliye hai, ndiye atakayekusifu, kama mimi leo” (ms.19).

**Je, mfalme Daudi?** Tunaambiwa wazi mfalme Daudi hakwenda mbinguni, ingawa anaitwa mtu aliyekuwa na moyo uliompandeza sana Mungu (Matendo 2:34, 13:22)

Watu wote tupo kwenye hukumu ya kifo kwa sababu ya dhambi. Hakuna anayeendelea kuishi kwa namna yoyote nyingine baada ya kufa.

Kama hatulielewi hili vizuri, hatuwezi kamwe kutambua jinsi ambavyo Bwana Yesu alivyoteseka na kufa ili kutuweka huru na dhambi, na matokeo yake.

Kama tungekuwa na ‘roho zisizokufa’, kusingekuwa na haja ya Yesu kutufia. Biblia inatuambia, hakuna tumaini la uzima kama sio katika Kristo.

#### **Muhtasari**

1. Mungu alimuumba Adamu kutokana na mavumbi ya nchi.
2. Alimfanya aweze kuishi kwa kumpulizia pumzi ya uhai katika pua zake.
3. Mungu alimpa Adamu amri. Alimwambia kwamba kama akiivunja amri yake, adhabu yake itakuwa kifo.
4. Adamu na Hawa hawakumtii Mungu; waliivunja amri yake. Matokeo yake wakawa viumbe vinavyokufa.
5. Watu wote wanatokana na Adamu, na wanairithi hulka yake ya dhambi. Watu wote wanakosa na wanakufa.
6. Neno ‘roho’ linamaanisha uhai au kuwa hai, na kwa kawaida linatumika kwa mtu.
7. Msemo ‘roho isiyokufa’ haupo kwenye Biblia.
8. Kifo ni adhabu na matokeo ya dhambi (sio ‘Mungu kumpenda anayekufa zaidi’!).
9. Hakuna sehemu ndani yetu au kitu kinachoendelea kuishi tunapokufa.

**Kifungu cha kusoma:** Mhubiri 9

**Msitari wa kushika:** Zaburi 146:4

“(Mtu anapokuwa akifa)Pumzi yake hutoka, huurudia udongo wake, siku hiyo mawazo yake yapotea”.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## DHAMBI NA MATOKEO YAKE (SEHEMU YA 2)

**SOMO:** Mhubiri 3

**Baada ya kifo – nini?**

Kuna nadharia nyingi zinazotofautiana juu ya nini kinatokea tunapokufa. Ni watu wachache wanaopenda kufikiri wanapokufa inakuwa ndio mwisho wao. Hapa kuna baadhi ya nadharia walizonazo:

- Wapo wanaofikiri wanageuka na kuwa wanyama (huu unaitwa ‘umwilisho’).
- Wapo wanaofikiri kuna kitu ndani yao kinachoendelea kuishi mahali fulani.
- Wapo wanaofikiri hakuna tumaini kabisa la namna yoyote ya uhai baada ya kifo.
- Na wengine wanaamini kutakuwa na siku ya ufufuo wa wafu, ikifuatiwa na hukumu, na uzima wa milele kwa waaminifu.

**Biblia inasemaje?**

Kama tulivyokwishaona, kifo ni adhabu hutokana na dhambi. Kuwa katika hali ya kufa ni kuwa katika hali ya kutotambua chochote; kutokuwa na mawazo ya namna yoyote. Kwa hiyo, mauti ni mwisho kabisa wa uzima na hakuna kinachoendelea kuishi. Andiko linasema:

*“Waliohai wanajua ya kwamba watakufa, lakini wafu hawajui neno lolote, wala hawana ijara tena, maana kumbukumbu lao limesahauliwa. Mapenzi yao na machukio yao, na husuda yao imepotea yote pamoja, wala hawana sehemu tena katika jambo lolote lililofanyika chini ya jua” (Mhubiri 9:5,6).*

Je, hili lina maana kuwa hakuna tumaini lolote juu yetu? Hakuna tumaini mbele ya kaburi?

**Ahadi ya ufufuo na uzima wa milele.**

Kusingekuwa na tumaini lolote kama Mungu asingemtuma Yesu Kristo. Yesu mwenyewe alisema: “Msiposadiki ya kwamba mimi ndiye, mtakufa katika dhambi zenu” (Yohana 8:24).

Lakini kwa sababu ya kile Yesu alichofanya katika maisha yake yasiyo na dhambi na kwa kufa kwake, tunaweza kuwa na tumaini la uzima baada ya kufa. Neno linasema:

*“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye”*  
(Yohana 3:16,17).

Tunaweza kusamehewa dhambi zetu kupitia kwa Yesu. Yesu alisemewa na Yohana Mbatizaji kuwa ni: “Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu” (Yohana 1:29). Tunakufa kwa sababu ya dhambi. Kama dhambi zetu zinasamehewa kabisa, hatuwezi kubakia tumekufa. Tunakuwa kama ilivyokuwa kwa Yesu.

Jisomee mwenyewe Yohana 6:39,40,44. Tunajua ya kwamba Yesu anaongelea hapa kufufuliwa kwa wafu mara tatu, ‘siku ya mwisho’. Hasa katika msitari wa 40 anasema: “Mapenzi yake baba yangu ni haya, ya kwamba kila amtazamaye Mwana na kumwamini yeye, awe na uzima wa milele, nami nitamfufua siku ya mwisho”.

Ufufuo wa wafu unaongelewa pia katika Yohana 5:28,29. Yesu anasema:

*“Msistaajabie maneno hayo, kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka, wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu”.*

Nabii Danieli naye alilisemea hili akionesha kuwa, ni sehemu tu ya wale watakaofufuliwa watakaopewa uzima wa milele: “Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele” (Danieli 12:2).

Kwa hiyo, kutakuwa na hukumu. Tunaambiwa kuwa, wale watakaokuwa hai wakati wa kurudi Yesu, watahusika pia na hiyo hukumu. Yesu atawahukumu: “Walio hai na waliokufa, kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake’ (2 Tim. 4:1).

Hao watu watakaonekana wanafaa, watapewa nafasi katika Ufalme wa Mungu utakaoanzishwa hapa duniani. Yesu atawaambia:

*“Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu” (Mathayo 25:34).*

Hawa watu waliokuwa waaminifu watapewa uzima wa milele; maisha yaliyo makamilifu na yasiyo ya dhambi. Tunasoma katika Luka 20:35,36 kuwa, watakuwa kama malaika:

*“Wale wahesabiwao kuwa wamestahili kuupata ulimwengu ule, na kule kufufuka katika wafu, hawaoni wala hawaolewi, wala hawawezi kufa tena, kwa sababu huwa sawasawa na malaika, nao ni wana wa Mungu, kama vile walivyo wana wa ufufuo”.*

Tumaini la Mkristo lipo katika ufufuo wa kimwili kutoka kwa wafu, na nafasi katika Ufalme wa Mungu katika dunia hii atakaporudi Yesu.

### **Wadhambi wanakwenda motoni?**

Je, kuna hasa sehemu ya kutisha inayoitwa ‘kuzimu’ watu waovu wanapokwenda kuteswa baada ya kufa? Tumeshona kuwa, mtu anapokufa, uhai wake unakuwa umefikia mwisho moja kwa moja! Hawezi tena kufikiri au kuhisi chochote. Kwa hiyo ‘kuzimu’ ni nini, na ni wapi?

Neno ‘kuzimu’ ni neno lenye maana ya ‘mahali palipofichwa’ au ‘mahali palipofunikwa’. Ni neno linalotumika katika Biblia kumaanisha mahali palipofichika au palipofunikwa kwa ajili ya wafu; ni kaburi.

Maana ya ‘kuzimu’ ni ‘KABURI’

Katika Agano la Kale, neno la Kiebrania lililotafsiriwa ‘kuzimu’ ni ‘sheol’. Limetumika katika vifungu vifuatavyo:

Katika Zaburi 49:15 mwandika Zaburi anasema: “Mungu atanikomboa nafsi yangu, atanitoa mkononi mwa kuzimu”.

Katika Zaburi 55:15 mwandika Zaburi anasema: “Mauti na iwapate kwa ghafla, na washuke kuzimu wangali hai”.

Neno hili ‘kuzimu’ ni neno ‘sheol’; halina maana nyingine. Sio mahali pa ajabu-ajabu, pasipoeleweka.

Katika Agano Jipya, neno lililotafsiriwa ‘kuzimu’ ni ‘hades’ katika Kiyunani.

Katika 1 Wakorintho 15:55, mtume Paulo anasema: “Ku wapi, Ewe mauti, kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti, uchungu wako?”

Katika Ufunuo 1:18 Yesu anasema: “.....Ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu”.

Neno ‘mauti’ na neno ‘kuzimu’, yote ni neno ‘hades’ katika lugha ya Kiyunani; maana yake ni moja (Kiyunani ndiyo lugha ya asili iliyotumika kuandika Agano Jipya lote; lugha zingine zote ni tafsiri).

Hili linatuonesha kuwa, katika Agano la Kale na Agano Jipya, neno 'kuzimu' lingeweza kutafsiriwa 'kaburi' moja kwa moja.

Maana ya kuzimu ni 'KABURI'

Kwa hiyo, kuzimu sio mahali pa kutisha pa mateso kwa ajili ya wadhambi wanapokuwa wamekufa.

### **Yesu alirudi kutoka kuzimu**

Baada ya Yesu kufufuka kutoka kwa wafu na kupaa mbinguni, Petro aliwahubiri watu waliokusanyika Yerusalemu kwa ajili ya sikukuu ya Pentekoste. Aliwaambia kuwa, mfalme Daudi alikuwa amemtabiria Yesu kufufuliwa kutoka kwa wafu. Unabii huu unapatikana kwenye Zaburi ya 16, na Petro anauongelea katika Matendo 2:27 akisema:

*"Kwa maana hutaiacha roho yangu katika kuzimu, wala hutamtoa Mtakatifu wako aone uharibifu".*

Petro anasema kuwa, Daudi alikuwa akimtabiria Yesu Kristo:

*"Yeye mwenyewe (Daudi) akitangulia kuyaona haya, alitaja habari za kufufuka kwake Kristo, ya kwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuona uharibifu" (ms.31).*

Roho yake Kristo (yaani, Kristo mwenyewe) hakuachwa kuzimu (yaani, kaburini) kwa kuwa Mungu alimfufua siku ya tatu. Mtakatifu wa Mungu hakuona uharibifu (yaani, hakuishia mautini).

Katika Ufunuo 1 Yesu anazungumzia ufufuo wake mwenyewe, na pia ahadi yake ya kuwafufua wafuasi wake waaminifu, anaposema:

*"Nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu" (Ufun. 1:18).*

Wafuasi wa Yesu waliokwisha kufa, wamefungiwa katika makaburi (au kuzimu). Yesu anao ufunguo (anao 'uweza') wa kuyafungua makaburi hayo wakati akirudi, na kuwafufua waliokufa na kulazwa humo.

### **Kuzimu ('hades')**

Mara nyingine 'kuzimu' kunafikiwa kuwa ni mahali pa giza au ukungu mnene, zinapokaa roho za watu waliokufa. Tunajua hili haliwezi kuwa kweli kwa kuwa Biblia inatuambia: *"Wafu hawajui neno lolote"* (Mhubiri 9:5).

***Hakuna mtu aliyekufa anayejua kitu; anayepata raha au maumivu, kwa kuwa hakuna wanachotambua.***  
'Kuzimu' tumeshaona, ni "kaburi" tu.

### **Vipi juu ya moto wa kuzimu; wa milele?**

Yesu anasema mara tatu katika Marko 9 juu ya 'moto usiozimika'. Anasema:

*"Ni afadhali kuingia katika uzima u kigutu, kuliko kuwa na mikono miwili, na kwenda zako Jehanum, kwenye moto usiozimika"*

*(Marko 9:43).*

Sasa Yesu hapa alimaanisha nini?

Neno 'Jehanum' katika msitari huo ni neno 'Gehenna' katika Kiyunani, linalotokana na neno 'Ghi-Hinnom' katika Kiebrania. Ghi-Hinnom lilikuwa ni jina la bonde lililokuwa nje kidogo ya jiji la Yerusalemu. Ni mahali ambapo miaka mingi nyuma wafalme wa Israeli waliteketezea watoto wao kwa moto, wakitambikia miungu ya kigeni. Ni bonde linaloitwa, 'Bonde la wana wa Hinomu' katika 2 Wafalme 23:10.



Katika kipindi cha Yesu, bonde hilo (Jehanum) lilikuwa ni mahali mizoga ya wanyama na takataka za Yerusalemu zilipoteketezwa. Moto ulikuwa ukiwaka hapo wakati wote; lilikuwa ni 'dampo' la jiji. Palikuwa mahali pa kitu kuteketezwa moja kwa moja; kisionekane tena.

Yesu alipolitumia neno 'Jehanum' watu walielewa alikuwa akisemea mahali hapo, ikiwa ni ishara ya kuharibiwa au kuteketea moja kwa moja; kuangamia. Yesu hakuwa akisemea watu kuteseka kwenye adhabu isiyo na mwisho ya moto. Mungu wa upendo hawezi kufanya hivyo; asingeiweka adhabu ya namna hiyo. Wangejuta tu kwa adhabu na kuangamia kwa kufa; wasiwepo tena.

#### **Muhtasari**

1. Biblia inafundisha kuwa kifo ni mwisho wa uhai wote.
2. Haitoi ahadi ya kwenda mbinguni.
3. Inaahidi kuwa Yesu atarudi na kuwafufua wafu.
4. Wakati huo, atawapa wafuasi wake waaminifu uzima usio na mwisho.
5. 'Kuzimu' ni kaburi; mahali ambapo waliokufa wanazikwa.
6. 'Jehanum' ni bonde lililokuwa nje ya jiji la Yerusalemu (**'Ghi' bonde-la-ukoo-wa 'Hinnom'**), mahali zilipochomewa taka. Limetumiwa katika Biblia kama ishara ya 'kuteketeza'.

**Kifungu cha kusoma:** Yohana 11:1 – 45

**Mistari ya kushika:** 1 Wakorintho 15: 22,23:

*"Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika katika Kristo wote watahuishwa. Lakini kila mmoja mahali pake; limbuko ni Kristo, baadaye walio wake Kristo, atakapokuja".*

## MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

*Karatasi ya maswali: namba 6*

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa 'Kazi ya ziada' unaweza kulijibu swali kama ukipenda, au kuliacha kama unaona huliwezi. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

### MASOMO: 21- 23

- 20 A. Nakili na ukikamilishe kifungu hiki (utahitaji maneno zaidi ya moja kwa baadhi ya majibu).

Roho Mtakatifu ni ..... wa Mungu. Mungu ..... mbingu na nchi kwa kutumia ..... yake. Maneno ya kwenye Biblia ni maneno yake. Aliitumia ..... yake kuwaambia walioandika nini waandike, kwa hiyo Biblia inaelezewa kuwa ni 'Neno lenye ..... ya Mungu'.

Yesu alizaliwa kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Ni uweza wa Mungu uliomfanya ..... ashike mimba ya Yesu, na Yesu alipewa huo uweza, ambao ni Roho ya Mungu, wakati ..... Aliitumia uweza huo .....

Roho Mtakatifu anaitwa pia 'Mfariji' au 'Msaidizi'. Ni uweza uliotolewa kuwasaidia ..... kwa njia ya kuwakumbusha mambo Yesu aliyowaambia. Tunasoma juu ya nguvu hiyo akiwashukia wanafunzi wa Yesu katika Matendo, Sura ya ..... Baada ya Bwana Yesu..... nguvu hiyo iliondolewa.

- B. Zawadi (au karama) za Roho Mtakatifu zilitolewa kwa ajili gani?  
C. Zilitolewa zidumu kwa muda gani?

- 21.A. Kati yake zilizokuwa za maana zaidi ni zipi?

- B. Ni zawadi ( au karama) ipi iliyo ya muhimu kuliko zote? (1Wakor. 13)  
C. Ni watu gani waliokuwa na uwezo wa kuwapa watu wengine zawadi (au karama ) hizo?  
D. Je! Zipo hata leo?

22. A. Biblia inatuambia juu ya jinsi Adamu alivyoubwa?

- B. Hawa aliumbwaje?  
C. Ni nyoka aliyewafanya Adamu na Hawa wale tunda la mti uliokatazwa?  
D. Adhabu ya Adamu kwa kumkiuka Mungu ilikuwa ni nini?  
E. Ni kwa nini watu wote wanakufa?

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## KWA NEEMA MMEOKOLEWA

SOMO: Warumi 5

## NEEMA

Katika Biblia **neema ya Mungu** maana yake ni wema wa upendo wa Mungu kwa wanadamu. Ni kitu asichokistahili mtu, na ni zawadi ya bure kabisa inayotoka kwake. Neema hiyo inaeleweka vizuri zaidi katika kumtoa Bwana Yesu kwa ajili ya kutuokoa.

(Utahitaji kulikumbuka hili vizuri unavyojifunza somo hili)

**Ni kufa au kupona**

Sisi wote tunaelewa vizuri sana kuwa, maisha yetu yatakatizwa hivi karibuni au baadaye kidogo kifo kikija. Mungu alimtuma Mwanawe, Bwana Yesu Kristo, duniani, ili kuifungua njia ya uzima. Hii njia ya wokovu kutokana na mauti ndio 'moyo' wenyewe wa Injili ya Kikristo.

Dhambi zetu zinatutenganisha na Mungu, ambaye ndiye aliye chanzo cha uhai wote. Yesu alikuja kumrejesha mwanadamu kwa Mungu, kwa kuionesha njia ya uzima. Mtu anaweza akaijua Biblia yake vizuri sana kutoka Mwanzo mpaka Ufunuo, anaweza akawa na ufahamu mkubwa wa mambo Biblia inayofundisha, lakini hili haliwezi kumwokoa. Kama mtu hajielewa na kuipokea dhabihu Yesu aliyoitoka kwa ajili yake kwa moyo wa ukweli, hawezi kuwa na tumaini la uzima.

**Mawazo potofu**

Watu wengi wanafikiri kuwa, mambo mazuri wanayofanya na mambo mabaya wanayofanya yanalinganishwa, kuona vile walivyo mbele ya Mungu. Wanafikiri kuwa, kama mema wanayofanya ni mengi kuliko mabaya, wana **haki** ya kupata upendeleo wa Mungu. Hili sio kweli hata kidogo!

Wengi wanaodai kuwa ni Wakristo, wanaotambua kuwa Mungu amelipa kitu cha thamani kubwa kuwezesha wokovu wao kupatikana, wanajisikia wanastahili kuupata mbaraka huu kwa mambo wanayofanya.

Ni rahisi sana kwetu kufikiri tunastahili kuzipata zawadi za Mungu, lakini, zawadi sio haki, na haziwezi kuwa. Ni mishahara tu inayofanyiwa kazi. Paulo anatuambia:

“Mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama (zawadi) ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu” (Warumi 6:23).

Mungu amefanya mengi sana kwa ajili yetu. Tunahitaji kuonesha shukrani zetu kwa kumpendeza, kwa hiyo tunafikiri kuwa mambo tunayofanya yanaweza 'kuilipia' mibaraka ya Mungu.

Ni mojawapo ya mafundisho makuu kabisa katika Maandiko kuwa, msamaha wa dhambi na uzima wa milele katika Ufalme wa Mungu ni **karama** ya Mungu; ni vitu tu vya ukarimu wake. Haviwezi kuwa haki; havilipiwi.

**Maandiko yanafundisha kuwa:**

- Sisi wote tu-wadhambi na tupo katika hukumu ya kifo.
- Hatuwezi kujiokoa wenyewe (inatupasa tuwe na unyenyekevu wa kulikubali hili).
- Mungu ametoa njia ya wokovu kupitia kwa Bwana Yesu Kristo.
- Njia hii ipo kwa ajili yetu kama tukiiamini Injili, inayopatikana katika Neno la Mungu, Biblia.

**Kumwamini Mungu**

Yasome maneno haya kwa umakini:

**Waefeso 2: 4-9**

“Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu, alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema. Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu; ili katika zamani (nyakati) zinazokuja audhihirishe wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu. Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa (kitu cha kupewa; zawadi) cha Mungu, wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu”.

- Mungu anatupenda sana, ingawa tu wadhambi. Ametupa uhai wa kuwa pamoja na Kristo.
- Wokovu huu ni kitu cha kupewa; ni zawadi.
- Ametupa wokovu huu katika Yesu, ili katika wakati unaokuja aweze kutubariki hata zaidi na uzima katika Ufalme wake.
- Wokovu huu ni tuzo itokayo kwa Mungu. Inabidi tumwamini. Hakuna tunachoweza kufanya kuupata, kwa hivyo hakuna kuringa.

Sasa hebu soma Warumi 3:20-28 kwa makini. Utaona kuwa ujumbe ni huo huo. Hakuna kitu ambacho Wayahudi wangeweza kufanya kwa kuishika Sheria, na hakuna tunaloweza kufanya katika maisha yetu, kutuwezesha tuonekane watu wa haki mbele ya Mungu. Sisi wote ni wadhambi. Lakini, kwa neema yake Mungu, anawahesabia haki wale wanaomwamini Bwana Yesu.

Ni Mungu peke yake na Bwana Yesu walio ‘wa Hak’i. Hata hivyo, kama tukiamini kuwa Yesu alitufia, na kuikubali dhabihu aliyoitoa kwa ajili yetu, Mungu atatusamehe dhambi zetu, na kutuhasabia nasi Haki. Ona tena mtume Paulo anavyourudia ukweli huu wa muhimu kwamba ‘yote ni ya Mungu’, na kwamba hakuna mtu anayeweza kuringa kwamba ameokoka:

“Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na tuwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo mnasimama ndani yake; na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu” (Warumi 5: 1, 2).

Mistari hii inatuambia wazi namna alivyo mfuasi wa kweli wa Bwana Yesu. Mtu wa namna hiyo ana amani na Mungu kwa kuwa, ameletwa katika ushirika tena na Mungu kupitia katika dhabihu ya Yesu. Amekubalika kwa Mungu, na ni raia mtarajiwa wa Ufalme wa Mungu.

Kilichomleta katika uhusiano huo ni imani yake kwa Mungu. Kwa sababu ya mambo haya, anaweza kuwasiliana na Mungu; anaweza kumkaribia kwa njia ya maombi. Mfuasi wa namna hiyo **ameifikia neema**.

**Tunaweza kujali tunavyoishi?**

Kwa hiyo tumeona jinsi mtu anavyoweza kumkaribia Mungu, na kuweza kukubalika kwa neema yake. Mtu aliyefikia hapo amekuwa ‘sawa’ na Mungu.

Lakini hatujasemea chochote kuhusu anavyopaswa kuishi. Tunaweza kuwa huru tena kujifurahisha na kujifanyia tunavyotaka? Mtume Paulo alifikiri watu wangeweza bado kufikiri hivyo; tumesoma juu ya neema ya Mungu kwenye Sura ya 5 ya waraka wake kwa Warumi. Sasa hebu angalia msitari wa kwanza wa Sura ya 6. Unauliza: “Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi?”

Analijibu swali hilo mwenyewe katika msitari wa pili, akisema: “Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?”

Endelea kusoma hadi msitari wa 14, na hasa uzingatie kinachosemwa katika msitari wa 11 na 12:

“Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu. Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake”.

Kama kweli tunamwamini Bwana Yesu Kristo, tutaishi kama vile tunamwamini. Tutajitahidi sana kufanya anayosema; ndipo tutakapokuwa kikweli wafuasi wake.

Kwa upande mwingine, mtu ambaye hafanyi jitihada yoyote kuyafanya mapenzi ya Mungu na kumtii, hawezi kuwa mfuasi wa kweli. Kama angekuwa ameamini kikweli, angetii. Hana imani iliyo na udhati, na hivyo **hajaifikia** hiyo neema ya Mungu.

Mtume Yakobo anatuambia: “Imani isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake” (Yakobo 2:17). Imani ambayo haimfanyi mtu ajitahidi kuifuata namna ya kuishi ya Mkristo na kuishinda dhambi ndani yake, sio imani lolote.

### **Kuanza maisha mapya katika Kristo**

Tunawezaje kuonesha kutambua kwetu kile Mungu alichokifanya kwa ajili yetu, na nia yetu ya kuishi kulingana na amri zake? Tayari tumeshasoma Warumi 6, msitari wa kwanza na wa pili. Hebu tuiangalie mistari miwili inayofuata:

“Hamfahamu ya kuwa sisi zote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima” (War. 6:3, 4).

Yesu alikufa na kufufuka kwa ajili yetu. Tunajishirikisha na dhabihu yake kwa kuzikwa, sio katika kaburi kama ilivyokuwa kwake yeye, bali katika maji. Huu ndio Ubatizo wa Kikristo. Mtu anapoibuka kwenye maji, amekuwa ‘mtu mpya’ katika Kristo, na anakuwa tayari kuishi maisha mapya. Anakuwa mfuasi wa kweli wa Bwana Yesu na anajitambua kuwa yupo ‘katika Kristo’; ni Mkristo.

**Ufuasi:** Ubatizo ni mwanzo mpya, na dhambi zetu za nyuma zinasamehewa tunapobatizwa. Hata hivyo, hata tukijitahidi kiasi gani, tutakuwa bado tunaendelea kufanya baadhi ya mambo kimakosa na kufikiri isivyofaa.

Lakini kumbuka: Mkristo ambaye amebatizwa, anaweza kumkaribia Mungu kupitia kwa Kristo. Anaweza kukiri kushindwa kwake, na kuonesha kusikitishwa na dhambi yake. Na Mungu atamsamehe kwa ajili ya Kristo.

Kwa hiyo, kamwe tusikate tamaa. Tukiwa na upendo wa Baba kutusaidia, hatimaye tutaufikia Ufalme wa Mungu utakapokuja. Yesu alisema: “Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme” (Luka 12:32). Anayo shauku ya kutuingiza katika Ufalme wake.

### **Umuhimu wa imani**

IMANI ni kumtumaini MUNGU

Mwandishi kwa Waebrania anatuambia katika Waebrania 11:6 kuwa: “Pasipo imani haiwezekani kumpendeza (Mungu)”. Kuwa na imani ni kumtumaini Mungu kabisa; kuweka maisha yetu mikononi mwake, kama mtoto mdogo anavyomtegemea baba yake na kumheshimu.

Kama tuna imani ya kumtumaini hivyo, tumeweza kuifikia neema ya Mungu. Lakini hatuwezi kuamini kitu kama hatukijui vizuri; na hatuwezi kuliadini Neno la Mungu mpaka tunapokuwa tumeyaelewa mafundisho yake. Hii ndiyo sababu ya sisi kuisitiza sana haja ya kuelewa kile Biblia inachofundisha. Jisomee mwenyewe Warumi 10:13-17. Msitari huo wa mwisho unasema: “Imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo”. Hili ni la muhimu sana!

### **Wafuasi enzi za Agano la Kale**

Kama kuamini katika Yesu ni kitu cha lazima kwa wokovu wetu, itakuwa vipi kwa watumishi wa Mungu wakati wa Agano la Kale? Watawezaje kuokolewa wakati waliishi kabla Kristo hajaja?

Ni muhimu kutambua kuwa, wale walioishi katika nyakati za Agano la Kale, walifahamu kumhusu Kristo. Hawakumfahamu kwa jina la 'Yesu', ila walimjua kama 'Mwana wa Mungu aliyeahidiwa'; Masihi; Mwana-kondoo wa Mungu.

Waaminifu wa kale walitambua kutokana na Neno la Mungu kuwa, watu wote wanahitaji kuokolewa. Waliambiwa kuwa Mungu angelifanikisha hili kwa kifo cha 'mtu mkamilifu', ambaye angekubali kuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi. Angeutoa uhai wake kwa ajili ya wokovu kwa wanadamu wote.

Ibrahimu alikuwa mmojawapo wa 'wakuu' katika Agano la Kale. Tunaambiwa katika Wagalatia 3:8 ya kuwa: "Andiko....lilimhubiri Ibrahimu habari njema zamani, kusema, katika wewe mataifa yote watabarikiwa".

Na tunasoma juu ya Yesu akiwaambia Wayahudi: "Ibrahimu, baba yenu, alishangilia kwa vile atakavyoiona siku yangu; naye akaiona, akafurahi" (Yoh. 8:56).

Kwa hiyo, Ibrahimu na wafuasi wengine wengi wa Agano la Kale waliamini katika Kristo, kama ambavyo imekuwa kwetu, ingawa hawakuwa na fursa hii kubwa tuliyo nayo, ya kuweza kuzisoma habari za Injili zinazotuambia juu ya maisha na kazi za Bwana Yesu alipokuja.

Kwa kuwa Maagano yote mawili yanatuambia habari za **neema ya Mungu** inayofanya kazi kwa ajili ya wokovu wetu, tunahitaji kujifunza Biblia yote, na sio Agano Jipya tu.

#### **Muhtasari**

1. Hakuna mtu anayeweza kujiokoa mwenyewe; hakuna mtu anayeweza kuokolewa bila ya unyenyekevu.
2. Ni neema ya Mungu inayoleta wokovu; ni neema hii inayotupa Habari Njema za kazi za Yesu na mpango wa Ufalme wa Mungu.
3. Inatubidi tuwe na imani ndipo tunapoweza kuipata neema ya Mungu.
4. Kama tuna imani, tutajaribu kuishi kulingana na maagizo ya Mungu.
5. Imani ya kweli itajionesha kwa namna mtu anavyoishi katika maisha yake; itathibitisha kuwa ufuasi wake ni wa kweli!

**Vifungu vya kusoma:** Zaburi 32, Warumi 4

Usome tena Wagalatia 3; Tito 3:4-6 na 2:11-13

**Jifunze kwa moyo:** Warumi 5: 1, 2.

"Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na tuwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo. Ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikilia neema hii ambayo tunasimama ndani yake; na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu".

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## UFUFUO KUTOKA KWA WAFU

SOMO: 1 Wakorintho 15

Neno 'Ufufuo' maana yake ni kuwa hai tena

Lazima lilikuwa ni tukio zuri sana la ajabu kuliko yote katika historia ya dunia, Yesu alipotoka kwenye kaburi lake, baada ya kuwa mfu kwa siku tatu. Wanafunzi wake walipomwona, hawakuweza kuyaamini macho yao. Walifikiri walichokiona kilikuwa roho, lakini Yesu aliwaambia:

“Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone. Kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo”.

Na baada ya kusema hayo aliwaonesha mikono yake na miguu yake. Basi walipokuwa hawajaamini kwa furaha, huku wakistaajabu, aliwaambia: “Mna chakula chochote hapa? Wakampa kipande cha samaki wa kuokwa. Akakitwaa, akala mbele yao” (Luka 24:39-43).

Wakawa, hatimaye, wameamini ya kuwa alikuwa amepata uzima tena. Mungu alikuwa amemfufua kutoka kwa wafu, na kumpa uzima wa milele. Tunasoma juu ya Yesu mwenyewe, akisema: “Tazama, ni hai hata milele na milele” (Ufunuo 1:18).

**Yesu atawafufua wafuasi wake**

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuwa, nao pia watafufuliwa kutoka kwa wafu. Hebu uangalie tena msitari huo tuliounukulu sasa hivi. Yesu alisema, yeye ni, ‘Aliye hai’, na alikuwa amekufa. Anaendelea kusema: “Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu (kaburi)”.

Sasa, kama unao ufunguo wa mlango fulani, ina maana ya kuwa unaweza kuufungua huo mlango. Yesu anao ufunguo wa mauti. Hii ni namna ya kusema kuwa, anao uwezo wa kuyafungua makaburi, na kuwaweka huru wale waliozikwa humo. Mamlaka hiyo amepewa na Mungu. Hebu tusome Injili ya Yohana, Sura ya 5: 20-29. Ona hasa analosema Yesu katika msitari wa 21:

“Maana kama Baba awafufuavyo wafu na kuwahuisha, vivyo hivyo na Mwana awahuisha wale awatakao”.

‘Kuhuisha’ ni kufufua; ni kumpa mtu uhai tena. Mungu amempa Yesu jukumu na uweza wa kuwarudishia tena watu waliokufa uhai.

**Ibrahimi aliahidiwa ufufuo**

Kama tulivyokwisha kujifunza katika Somo la 12, Mungu alifanya Maagano makubwa sana na Ibrahimu. Kati ya hayo, mojawapo lilikuwa: “Nchi hii yote uionayo, nitakupa wewe na uzao wako hata milele” (Mwanzo 13:15).

Hata hivyo tunajua Ibrahimu alikufa bila ya ahadi hiyo kutimizwa. Ilikuwa ni lazima Ibrahimu afufuliwe kutoka kwa wafu ndipo Mungu aweze kulitimiza Agano hili naye. Bwana Yesu Kristo alitumia hoja hii kuuthibitisha ufufuo wa wafu. Unaweza kulisoma hili katika Mathayo 22:31,32.

Yesu tena aliwaambia Wayahudi wa wakati huo kuwa, wangemwona Ibrahimu, Isaka na Yakobo katika Ufalme wa Mungu, na wao wenyewe wakitupwa nje (Luka 13:28).

**Tumaini walilokuwa nalo waaminifu wote**

Watu wa Mungu wa nyakati zote walikufa wakiitazamia siku ambayo wangepufuliwa na kuyarudia maisha. Paulo anatuambia juu ya baadhi ya watu hao, kuwa: “Wakafa katika imani, wasijazipokea (‘kabla hawajazipokea’) zile ahadi, bali wakazona tokea mbali” (Waebrania 11:13).

Mbele zaidi anawasemea tena watu hao, ambao walikuwa wamelala mautini katika imani kuwa: “Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi” (Waebr. 11:39, 40).

Tunaona katika msitari huu kuwa, zawadi ya uzima usio na mwisho itatolewa kwa pamoja kwa watu wanaomwabudu Mungu katika kweli.

Wakristo wa awali waliutazamia wakati huo. Mmoja wao alipokufa, walimwongelea kama ‘aliyelala usingizi’ kwa kuwa, kama ambavyo watu wanaamka baada ya kulala, ndivyo ambavyo wafuasi wa Yesu watakavyoamshwa kutoka katika usingizi wao wa mauti.

Katika Sura ya 15 ya Wakorintho wa kwanza, uliyokwisha isoma, Paulo anawaambia wafuasi kuwa, Yesu aliwatokea ‘ndugu’ zaidi ya 500 baada ya kufufuka kwake, na kuwa: “Katika hao wengi wanaishi hata sasa, ila baadhi yao wamelala” (ms. 6). Wakati huo Paulo akisema hivyo, baadhi ya ndugu Yesu aliwatokea walikuwa bado wapo.

Tumaini hili la ufufuo na uzima wa milele linawaleta pamoja wafuasi wa kweli wa Kristo tangu siku hizo hata sasa.

### **Yesu na ufufuo**

Yesu alikuwa na marafiki watatu, Lazaro na dada zake, Martha na Mariamu, waliokuwa wakiishi Bethania, kijiji kidogo nje kidogo ya Yerusalemu. Hao walielewa juu ya ufufuo. Siku moja Lazaro alipomwa dada zake walimuagizia Yesu, lakini mpaka alipokuja Lazaro alikuwa amekwisha kufa. Martha alipomwona Yesu, alimwambia: “Bwana, kama ungalikuwapo hapa, ndugu yangu hangalikufa” (Yohana 11:21).

Yesu anamwambia, “Ndugu yako atafufuka” (ms. 23.) Sasa hebu tuangalie kwa makini jibu analotoa Martha: “Najua ya kuwa atafufuka katika **ufufuo siku ya mwisho**” (ms. 24).

Kwa hakika, Martha alijua kuwa kulikuwa na siku ya ufufuo mbeleni. Yesu anamwambia: “Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima” (ms. 25). Sasa, ili kuwaonesha wote waliokuwa pale kuwa alikuwa na **uweza wa kuwafufua waliokufa**, Yesu anamwita Lazaro atoke kaburini; naye anaamka na kutoka!

Tofauti na Yesu, Lazaro hakupewa uzima wa milele alipofufuka. Ilikuwa afe tena, lakini, kama Martha alivyosema, atafufuka tena katika ufufuo siku ya mwisho. Hili ni jambo Yesu alilowafundisha marafiki zake hao, na walimwelewa na kumwamini.

### **Kitu bora zaidi kuliko maisha yalivyo sasa**

Maisha yamejaa matatizo kwetu sisi wote. Walio wengi kati yetu wanajua mtu anavyojisikia akiumwa; tunakuwa na hofu ya mambo mengi. Kifo kinaweza kuwachukua tunaowapenda muda wowote. Tunajua pia kuwa, uzee lazima uje kwa wakati wake, na maumivu yake na uchungu. Ni kweli tunataka kuishi milele katika dunia hii yenye shida?

Maisha ambayo Yesu aliwaahidi wafuasi wake akirudi, ni kitu kilicho tofauti sana na maisha yetu ya sasa na kashkashi zake nyingi. Katika maneno matamu ya Ufunuo 7:16,17 tunaambiwa juu ya wale watakaoupata uzima huo, kuwa:

“Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote. Kwa maana, aliye katikati ya kiti cha enzi atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao”.

Hawatakuwa tena na miili yenye udhaifu inayoharibika, bali watakuwa washiriki wa maisha ya kiroho ya Mungu mwenyewe. Katika Marko 12:25 Yesu anasema:

“Watakapofufuka katika wafu, hawaoi wala hawaolewi, bali huwa kama malaika walioko mbinguni”.



Wale watakaopewa uzima wa milele na Yesu katika kurudi kwake, watayafurahia maisha ya afya njema na nguvu zisizo na mipaka, na kuwa huru na matatizo ya sasa.

### **Ufufuo utakuwa lini?**

Ni miaka zaidi ya 2000 imepita tangu Yesu afufuliwe kutoka kwa wafu. Atawafufua lini wale ambao wamekufa katika imani? Mtume Paulo anatumia hili swali, akisema:

“Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa. Lakini kila mmoja mahali pake; limbuko ni Kristo; baadaye walio wake Kristo, atakapokuja”

(1 Wakorintho 15:22, 23).

Tumekwisha kuona tayari ya kuwa, Yesu Kristo anarudi kuusimamisha Ufalme wa Mungu na kuitawala dunia yote. Atakapokuja kulifanya hili, atawafufua wafu. Baada ya hapo wale waliokuwa waaminifu watapewa uzima wa milele, na wataifurahia fursa ya maana ajabu ya kumsaidia Yesu kuitawala dunia. Tunasoma katika Ufunuo 5:9,10 maneno ya wimbo wanaouimba siku hiyo:

“Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi”.

### **Wapo watakaokuwa hai wakati Yesu akirudi**

Nini kitawatokea wale walio hai wakati Yesu anarudi? Katika 1 Wathesalonike 4:14-17 Paulo anatumia kidogo juu ya hili. Anasema:

“Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani, na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele”.

Hebu yatazame maneno: “Tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani”.

Unaweza ukafikiri anasemea habari ya kwenda mbinguni hapa. Lakini yachunguze tena. Paulo haongelei juu ya kumlaki Bwana mbinguni; anasema ‘hewani’. Kwa hiyo baada ya ufufuo wa wafu na kukusanywa pamoja na wafuasi walio hai wakati huo wa kurudi kwa Yesu, wale wote wanaohusika watachukuliwa kimuujiza kumtumikia Bwana Yesu katika kazi yake ya kuitawala dunia.

La muhimu kwa wafuasi wote wa Yesu ni kwamba, katika siku hiyo ‘watakuwa pamoja na Bwana milele’, yaani katika Ufalme wake katika dunia.

### **Huwezi kuwa pande zote**

Watu wengi (pengine karibu wote) wanaoamini juu ya uzima baada ya kifo, wanaamini kuwa watu wanakwenda mbinguni wanapokufa. Mwili wa mtu ambaye amekufa unalazwa katika kaburi, lakini, wanasema, mtu anayo roho ambayo inaendelea kuishi. Mtu akifa, hiyo roho inatoka na kwenda mbinguni kuwa na Mungu.

Biblia, kwa upande wake, inasema waziwazi kuwa, Bwana Yesu atarudi katika dunia na kuwafufua waliokufa. Sasa, **mawazo haya yote mawili hayawezi kuwa sahihi.**

Kusema kuwa roho ambayo imeshakuwa na Mungu mbinguni inarudi kuungana na mwili, alafu mtu analetwa hukumuni, ni upuuzi. Biblia haisemei chochote juu ya mtu yeyote kwenda mbinguni. Inachosema ni kwamba, muumini huyo aliyekufa atalala kaburini akiwa hajitambui na hatambui lolote, mpaka Bwana Yesu atakapomfufua kutoka kwa wafu, katika ujio wake.

## **Kristo atakapokuja**

Wote walioisikia Injili wataletwa mbele ya Bwana Yesu Kristo. Wafu watafufuliwa, na walio hai watakusanywa pamoja nao. Kabla hajawapa baadhi yao uzima wa milele, ni lazima kutakuwa na hukumu. Utasikia mengi juu ya hukumu katika somo litakalofuata.

Hebu usome tena 1 Wakorintho 15:51-58. Hapa mtume Paulo anauongelea huo wakati Wakristo waaminifu watakapopewa zawadi hiyo kuu ya uzima usio na mwisho; au kama anavyoita Paulo, 'kutokuharibika'. Kwa kadri tunavyoutazamia huo wakati, mtume huyu anatutaka tuimarike, tusitikisike na tuzidi sana kuzitenda kazi za Bwana siku zote, tukijua ya kwamba taabu yetu 'siyo bure katika Bwana' (1 Wakor.15:58).

### **Muhtasari**

1. Mungu amempa Yesu uweza wa kufufua wafu.
2. Yesu atalifanya hili atakaporudi tena duniani kuusimamisha Ufalme wake.
3. Kwa wakati huo, atawakusanya wale walio 'katika Kristo' wanaoishi wakati wa kurudi kwake na waliokufa.
4. Wale ambao wameishi kiuaminifu, atawapa uzima wa milele, na wataishi na kuitawala naye dunia.

**Vifungu vya kusoma:** 1 Wathesalonike 4, Waebrania 11, Yohana 11, Mathayo 22:23-33.

**Mistari ya kushika:** Yohana 5:28, 29

"Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu ('ufufuo wa kukataliwa')".

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## HUKUMU

**SOMO:** Mathayo 25

**Ni lazima kumtii Mungu**

Mfalme Daudi alipokuwa amekikalia ‘kiti chake cha enzi’ katika jiji lake la Yerusalemu, aliazimia kulirudisha Sanduku la Agano la Mungu kutoka Kiriath-Yearimu, lilipokuwa limekaa kwa muda. Mkokoteni ulitegeshwa wa kukokotwa kwa mnyama. Yote yalipokuwa yametengemaa, makuhani wa Mungu walitembea kando-kando la hilo sanduku lilivyokuwa likivutwa.

Lilipokuwa likienda, wale ng’ombe walikwazwa na kitu, na bwana mmoja aliyekuwa akiitwa Uza alinyosha mkono kulizua sanduku kwa kuwa lilitetereka. Tunaambiwa, haraka tukio la kutisha lilitokea: Mungu alimpiga Uza: “Kwa kosa lake, hata akafa pale pale” (2 Samwel 6:7).

Ni kwa nini adhabu kwa Uza ilikuwa kali kiasi hicho, wakati alichofanya kilikuwa ni kulishikilia tu Sanduku la Mungu, tena kwa nia njema? Mungu alikuwa amesema wazi katika Kitabu cha Hesabu kuwa, Sanduku lake lilikuwa ni la kubebwa tu na makuhani mabegani mwao. Kwa hiyo Uza alikuwa ama hakuijua amri hiyo ya Mungu, ama hakuchagua kuitii. Kwa sababu hiyo, alikuwa na hatia mbele ya Mungu.

Habari hii inatufundisha kuwa, Mungu ni Mtakatifu na Mkuu sana. Anataka watu wanaomtumikia wamtii.

**Watu wanaoupuuza upendo wa Mungu**

Yesu aliwahi kutoa hadithi ya mfalme aliyefanya karamu ya harusi kwa ajili ya mwanawe. Maandalizi yalipokamilika aliwatuma wafanyakazi wake kuwakaribisha walioalikwa, lakini walikataa kwenda.



Waalikwa walipendelea zaidi kuendelea na shughuli zao za kila siku, kuliko kuitikia wito wa mfalme wao wa kuhudhuria sherehe yake. Kwa sababu hiyo, mfalme alikasirika, na akawatuma watumishi wake kwenda kuwaangamiza hao watu waliodharau mwaliko wake (Mathayo 22:1-7).

Mungu ni Mfalme Mkuu sana na ameandaa karamu kwa ajili ya Mwanawe, Yesu. Kama kwa neema yake anawakaribisha watu kuifurahia raha ya Ufalme wake katika dunia, na mtu anasema, kwa makusudi: “Sihitaji hilo Mungu analoniitia, na sitamtii,” basi kutakuwa na siku ya hukumu, na mtu huyo ataangamizwa. Katika Wagalatia 6:7 tunaambiwa: “Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi, kwa kuwa, chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna”.

**Ufufuo na hukumu**

Biblia inatufundisha kuwa, kutakuwa na siku ya hukumu baada ya ufufuo. Mungu ana upendo; lakini pia ni mkweli na wa haki. Kama tunavyoambiwa katika Kutoka 34:7, yeye siye: “Mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe”.

Hawezi kutoa uzima wa milele kwa watu ambao wamepuuza upendo wake; ambao, wakiwa wanajua kuwa Yesu aliwafia, hawafanyi jitihada yoyote kumtumikia na kumtii. Kwa hiyo, Paulo anatuambia:

-  “Sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu” (Warumi 14:10).
-  “Imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya” (2 Wakorintho 5:10).

**Lazima uje wakati wa kujibu**

Yesu aliwahi kuwaambia wanafunzi wake: “Ninyi mwaniita, Mwalimu, na, Bwana; nanyi mwanena vema, maana ndivyo nilivyo” (Yohana 13:13). Katika wakati wa Agano Jipya, kama mtu alikuwa amemnunua mtu

(mtumwa), alikuwa akimiliki jumla. Mtumwa alikuwa hawezi tena kujipendeza mwenyewe. Jukumu lake lilikuwa moja tu katika maisha yake; kumfurahisha bwana wake.

Sasa Yesu ametununia kwa damu yake, alipoutoa uhai wake msalabani, uwe dhabihu kwa ajili ya dhambi. Kwa hiyo Paulo anatuambia:

“Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu” (1 Wakorintho 6:19, 20).

Maana ya hili ni kwamba, tunawajibika kwa Bwana Yesu kwa namna tunavyoyaishi maisha yetu. Atakapokuja tena, atawapa zawadi ya uzima wa milele waliokuwa waaminifu, na atawaadhibu wale walioibeza njia yake.

### **Ukweli katika mfano**

Ili kuwafundisha wafuasi wake juu ya wajibu wao kwake, Yesu alitoa mfano tunaouona katika Mathayo 25:14-30. Usome, tafadhali, kwa manufaa yako. Ona hasa kinachosemwa kwenye msitari wa 21, kuhusu zawadi itakayotolewa kwa mtumishi atakayeonekana mwaminifu: “Ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako”.

Mtu ambaye hakutii hawezi kutegemea kupata tuzo kama hiyo, kwa kuwa amekuwa mtumwa asiyefaa. Adhabu yake inakuwa kali na amri inatoka:

“Mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno” (ms. 30).

### **Mhukumu wa haki**

Yesu atakaporudi, atawafufua wafu na kuwakusanya wale kati ya wanafunzi wake watakaokuwa wakiishi wakati huo. Itakuwa ni wakati wa hukumu. Baada ya mchujo, wale watakaokuwa wamekubaliwa, watapewa uzima wa milele, na Yesu atawaambia:

“Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu” (Mathayo 25:34).

Yesu mwenyewe ndiye atakayekuwa ‘mhukumu’ (angalia Yohana 5:28-30). Atahukumu kwa hekima Mungu aliyompa. Katika Isaya, tunaambiwa:

“Wala hatahukumu kwa kuyafuata ayaonayo kwa macho yake, wala hataonya kwa kuyafuata ayasikiayo kwa masikio yake; bali kwa haki atawahukumu maskini, naye atawaonya wanyenyekevu wa dunia kwa adili” (Isaya 11:3, 4).

Watu wanaweza tu kuhukumu kwa yale wanaoyaona na wanaoyasikia, lakini Bwana Yesu, kwa kuijua mioyo ya watu ilivyo, hatafanya makosa katika kuhukumu kwake.

### **Nani watakuwa katika Kiti cha Hukumu?**

Wale wote Bwana anaowahesabia kuwajibika kwake, waliosikia wito wa Mungu wa uzima, na kujua kuwa walipaswa kuitikia, watakusanywa mbele ya Kiti cha Hukumu cha Kristo.

Lakini hawatakuwa ni hao tu. Kutakuwa na watu; wanaume kwa wanawake, walioishi kabla ya Yesu kuzaliwa, na wengine baada ya hapo. Wote wataitwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo kujibu juu ya lile walilofanya kuhusiana na ujumbe wa Injili. Injili ni ‘lulu’ ya thamani kubwa. Wale wasiokuwa waaminifu watakuwa katika kiti cha hukumu pamoja na wale waliojaribu kuishi kwa kufuata mfano wa maisha makamilifu ya Bwana Yesu Kristo. Katika Waebrania tunaonywa:

“Kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi; bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao” (Waebrania 10:26, 27).

Yesu mwenyewe anatuambia: “Mtu yeyote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele ya Baba yangu aliye mbinguni” (Mathayo 10:33).

Watu ambao hawakuwahi kumfahamu Mungu wa kweli, na mpango wake wa wokovu, hawatafufuliwa kwa ajili ya hukumu. Unaweza ukawa unaikumbuka mistari ya Zaburi 49 inayosema juu ya mtu kama huyo, kwamba:

“Atakwenda kwenye kizazi cha baba zake; hawataona nuru hata milele. Mwanadamu mwenye heshima, iwapo hana akili, amefanana na wanyama wapoteao” (Zab. 49:19, 20).

Utakuwa umetambua pia ya kuwa, wazo la kwenda mbinguni tunapokufa ni tofauti kabisa na ukweli. Halitokani na ukweli unaofundishwa kwenye Biblia.

### **Shangwe kwa wanaokubalika**

Wale watakaokubaliwa katika hukumu, watapewa uzima usio na mwisho. Miili yao haitapatwa na uchungu tena au kuchoka, au udhaifu mwingine wowote ule wa kibinadamu. Akili zao nazo hazitavutwa tena kuwaza mawazo mabaya. Utakuwa wakati wa shangwe sana kwa waaminifu.

Katika Biblia, wakati wa kurudi Kristo unazungumziwa kama vile ni Sherehe ya Harusi. Katika Ufunuo tunaambiwa: “Heri walioalikwa karamu ya harusi ya Mwana-kondoo” (Ufunuo 19:9).

Wakati Yesu alipokuwa na wanafunzi wake, wakila mlo wa mwisho wa pamoja kabla ya mauti yake, aliwaambia:

“Nami nawawekea ninyi ufalme, kama vile Baba yangu alivyoniwekea mimi; mpate kula na kunywa mezani pangu katika ufalme wangu; na kuketi katika viti vya enzi, huku mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli” (Luka 22:29,30).

Ufalme utakapokuja, mitume wa Yesu watakuwa watawala juu ya Israeli, nchi itakayokuwa wakati huo **taifa-muhimu** juu ya mataifa yote duniani. Kila mfuasi atakayekubalika kwa Yesu, atakuwa na sehemu katika hiyo kazi ya kuiongoza dunia. Kwa hiyo tunasoma katika Ufunuo 5 msitari wa 9 na 10 juu ya wafuasi waaminifu wanaoimba wimbo, wakisema:

“Ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi”.

### **Kitakachowapata wale watakaokataliwa ni nini?**


Tumekwishaona kuwa, wote wanaoletwa mbele ya Kiti cha Hukumu cha Kristo watagawanywa kwenye makundi mawili. Kristo atawakubali baadhi yao na kuwakataa wengine, na kuwapa uzima wa milele wale aliowakubali. Lakini kitawatokea nini wale watakaonekana hawafai? Adhabu yao itakuwa nini?

Hatuufahamu undani wote, ila kuna mambo ambayo ni ya uhakika. Kwanza, watajigundua walivyokuwa wajinga. Wataona walivyopata fursa iliyokuwa nzuri ajabu ya mibaraka ya Mungu na kuidharau. Hili litawaumiza sana mioyo. Yesu anasema juu ya watu hao:

“Kutakuwa na kilio na kusaga meno, mtakapomwona Ibrahimu na Isaka na Yakobo na manabii wote katika ufalme wa Mungu, nanyi wenyewe mmetupwa nje” (Luka 13:28).

Mwisho wataangamizwa kabisa. Yesu aliifaninisha hukumu na mavuno ambapo, mbegu njema inatenganishwa na magugu yasiyo na kazi; yasiyofaa. Nafaka inahifadhiwa kiuangalifu ghalani, lakini magugu yanachomwa moto (Mathayo 13:36-43). Paulo alifundisha kitu hicho waziwazi, akisema:

“Wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake...(atawalipiza) kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake” (2 Wathesalonike 1:7-9).



Kuna vifungu kadhaa katika Biblia vinavyoelekea kutuonya tusijiamini sana juu ya hukumu. Yapo pia Maandiko yanayoonekana kututia moyo tuwe na matumaini kabisa. Sio kwamba kuna kujipinga. La kutambua tu ni kwamba, hatuwezi kujiamini sana wenyewe; wote tu-wadhaifu. Hata hivyo, tunaweza kuutumainia kabisa uweza wa kuokoa wa Mungu wetu. Tunaambiwa:

“Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?”

(Warumi 8:32).

Ingawa tunaweza kuanza kwa kuogopa juu ya Mungu, tutaweza pole pole kujifunza kumpenda na kumtumainia kabisa. Yohana anasema:

“Katika hili pendo limekamilishwa kwetu, ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu....katika pendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu” (1 Yohana 4:17,18).

#### **Muhtasari**

1. Kutakuwa na ‘siku ya hukumu’.
2. Itakuja baada ya ufufuo.
3. Wote ambao wamejua na kuelewa kweli kumhusu Mungu wataletwa hukumuni.
4. Watu watakaoshinda katika ‘kiti cha hukumu’ watapewa uzima wa milele.
5. Watu watakaokuwa wamekataliwa watajuta sana na wataangamizwa.

**Kifungu cha kusoma:** 2 Wakorintho 5

**Msitari wa kushika:** 2 Wakorintho 5:10

“Imetupasa sisi wote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya”.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## UZIMA WA MILELE

SOMO: Yohana 3

Utakuwa umekwishaona katika mafundisho haya ya Biblia ya kwamba, mwanadamu wa kwanza, Adamu, aliumbwa kwa Mungu kuutengeneza mwili kwa udongo, na kisha kuupulizia pumzi ya uhai. Lakini, Adamu na Hawa walikosa, na hivyo walibadilika na kuwa viumbe vinavyokufa.

Watu wote, wanaume kwa wanawake, hatimaye wanakufa, kwa kuwa wote wanakosa; ni wadhambi. Ni kitu kisichokubalika mbele ya Mungu, kwa wadhambi kuishi milele. Haiwezekani!

Kuna mtu mmoja tu ambaye amewezeshwa kutokufa tena, naye ni Bwana Yesu Kristo. Aliweza kuishinda nguvu ya mauti kwa kuishi maisha yasiyo ya dhambi. Hii ndiyo sababu ya Mungu kumfufua kutoka mautini na kumpa uzima usio na mwisho. Mungu mwenyewe hawezi kufa; yeye ni wa, "Tangu milele, na sasa, na hata milele" (Yuda 25). Ukimwacha Mungu, ni Bwana Yesu Kristo na malaika, ndio tu kwa sasa 'wasiopatikana na mauti' (1 Timotheo 6: 15, 16).

Jambo jema sana kuihusu Injili ni kwamba, kwa kuliadini kusudi la Mungu na kazi za wokovu za Yesu, inawezekana ni **sisi** kuwa na tumaini la uzima wa milele. Paulo anasema, neema ya Mungu:

"Sasa inadhihirishwa kwa kufunuliwa kwake Mwokozi wetu Kristo Yesu, aliyebatilisha mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile Injili" (2 Timotheo 1:9,10).

## Hatuwezi kulipwa uzima wa milele

"Mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama (zawadi) ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu" (Warumi 6:23).

Kama tulivyokwisha kuona, uzima wa milele ni zawadi ya Mungu. Hakuna mtu kati yetu, hata awe mwema kiasi gani, anayeweza kuistahili.

Kama wadhambi, la maana zaidi tunaloweza kulitegemea na kujifurahisha kwalo katika maisha haya, ni baadhi ya mambo mazuri tunayoweza kuyapata kwenye Sayari yetu hii, mpaka tunapofikia miaka 70 au 80. Ni wachache wanaovuka hapo, na wanapovuka wanadhoofika.

Hebu angalia ulinganisho ufuatao kwenye Zaburi ya 90:

HULKA YA MUNGU YA MILELE (Zab. 90:2)	HULKA YA MWANADAMU (Zab. 9:10)
"Kabla haijazaliwa milima, wala hujaiumba dunia, na tangu milele hata milele, ndiwe Mungu".	"Siku za miaka yetu ni miaka sabini, na ikiwa tuna nguvu miaka themanini; na kiburi chake ni taabu na ubatili; maana chapita upesi tukatokomea mara".

Kwa hiyo tutakwenda kaburini na kuishia; hatutakuwepo tena, kama hatukuwa na tumaini la Biblia la uzima wa milele uliopo katika Yesu Kristo. Wahusika wote wakuu katika Biblia waliokuwa na imani, walioziadini ahadi za Mungu; walikuwa na tumaini hili la uzima. Waliutazamia wakati ulio bora zaidi wa kuja mbeleni.

Ona kinachosemwa kumhusu Ibrahimu, Sara, Isaka, Yakobo, Daudi na wengi wengineo:

"Hawa wote wakafa katika imani wasijazipokea ('kabla hawajazipokea') zile ahadi, bali wakazona tokea mbali na kuzishangilia, na kukiri kwamba walikuwa wageni na wasafiri juu ya nchi" (Waebrania 11:13).

Paulo na Yohana, kama ilivyokuwa kwa mitume wengine, waliutazamia uzima wa milele. Walitumaini katika:

“Tumaini la uzima wa milele, ambao Mungu asiyeweza kusema uongo aliuahidi tangu milele”  
(Tito 1:2).

“Na hii ndiyo ahadi aliyotuahidia, yaani, uzima wa milele” (1 Yohana 2:25).

### **Uzima wa milele sio kwa kila mtu**

Kama ingekuwa ni moja kwa moja kila mtu anaweza kupata uzima wa milele, kusingekuwa na haja ya kujitahidi kuzitii amri za Mungu. Ahadi ya uzima usio na mwisho imetolewa kwa wale tu wanaotaka kuuitikia upendo wa Mungu. Kama ukisoma Warumi 2:6,7 utaona kuwa tuna uchaguzi. Mungu atawapa uzima wa daima wale tu ambao:

“Kwa saburi katika kutenda mema, wanatafuta utukufu na heshima na kutokuharibika”.

Kama hatuutafuti, kwa vyovyote hakuna tumaini la kuupata mbeleni.

### **Maisha ya milele na Uzima wa milele**

Utakuwa umegundua kuwa, baadhi ya vifungu tulivyovinukulu vinaongelea kutokuharibika kuwa ni uzima wa milele. ‘Uzima wa milele’ ni uzima wa kuwa kwa namna Mungu alivyo. Kama tukiishi maisha ya kumcha Mungu, kwa neema yake, atatazawadia uzima huo usio na mwisho.

KUWA NA UZIMA WA MILELE NI KUISHI MILELE KATIKA HAKI KWA UHUSIANO MWEMA NA MUNGU.

### **Ni lini uzima huo wa milele utatolewa?**

Utatolewa na Yesu Kristo kwa waaminifu baada ya kuwafufua waliokufa. Nabii Danieli aliutazamia wakati huo, akisema:

“Wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele” (Dan. 12.2).

Hili litakuwa wakati Yesu atakaporudi na kuwaita wale ‘waliolala’ katika mavumbi ya nchi. Danieli anawaita ‘walalao’ kwa kuwa, Bwana atawaamsha watoke kutoka makaburini walipo.

Katika Yohana, tunasoma: “Saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima” (Yohana 5:28, 29).

Katika Somo la 25 na 26 tulijadili kufufuliwa kwa wafu na hukumu itakayofuata. Wale watakaokuwa wamemfuata Yesu kiuaminifu, watakuwa wale wanaoitwa ‘Watakatifu’; watu wanaopewa kutawala na Mfalme Yesu katika utawala wake wa miaka 1000 kutokea Yerusalemu.

Watu hawa, wanaume kwa wanawake, watapeleka uzima wa milele, sio tu kwa kuwa itakuwa ni neema ya tuzo yao kutoka kwa Mungu kwa uaminifu wao katika kizazi hiki, bali pia kwa kuwa itakuwa ni lazima kuwe na watawala walio wakamilifu, wenye afya bora, wasiokufa, katika Ufalme wa Mungu.

### **Kwa nini ni hivyo?**

Katika mifumo yetu ya kiutawala kwa sasa, watawala na wakubwa wengine, kwa nadra wanakuwa watu wa kweli na wa haki. Kwa wale wanaojitahidi, bado hawawi na hekima ya kutosha kujua la kufanya, kuondoa uovu ulio katika maeneo yao na katika dunia. Mara nyingi hawawi pia na raslimali au uwezo wa kuyafanya mambo mazuri ambayo wangependa kuyafanya. Na hata aliye bora kabisa, anapokwenda vizuri na kufanya yaliyo mema kwa ajili ya wengine, anazeeka au kuugua na kufa.

Wale watakaopata uzima wa milele hawatabadilika au kudhoofika, na kwa kuwa wamekuwa wateule wa Mungu, watakuwa na maarifa na hekima na haki.



## MTAKATIFU NI MUUMINI WA KWELI

Neno 'takatifu' lina maana ya 'kilichotengwa' au 'safi'. Waumini wa kweli hawawi kama watu wa kidunia; wanamcha Mungu.

### **Watakatifu wasiokufa wataonekana je?**

Wengi wanajiuliza jinsi watakatifu watakwavyokuwa, watakapokuwa wamepewa uzima wa milele. Wataweza kutambulika? Watakula na kulala? Ingawa hatuujui undani wote, Biblia inatupa maelezo kadhaa juu ya hili.

Tunafahamu kuwa Ibrahimu, Isaka, Yakobo na manabii watakuwa wakitambulika wakati wa Ufalme (Luka 13:28).

Tunao mfano wa Yesu mwenyewe. Alitambuliwa wazi na wanawake fulani, na mitume, baada ya kufufuliwa kwake. Alikula chakula na wanafunzi wake. Mwili wake bado ulikuwa na makovu ya mateso ya kikatili aliyoyapata msalabani, na wanafunzi wake waliruhusiwa kumgusa.

Ni kweli kulikuwa na wakati walikuwa wamejiuliza kama alikuwa ni mtu ama 'roho', alipowatokea kiajabu-ajabu mbele yao. Lakini aliwaambia:

“Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina **mwili na mifupa** kama mnavyoniona mimi kuwa nayo (Luka 24:39).

Ni wazi kuwa Yesu akiwa amepata uzima wa milele, alikuwa bado ni mwili wa nyama na mifupa. Neno 'mwili' katika msitari huo, kwenye Biblia ya Kingereza ni 'flesh' lenye maana ya 'nyama'.

Andiko halisemi kuwa alikuwa na mwili na damu (kama tulivyo sisi) kwa kuwa, kulingana na Maandiko: “Uhai wa mwili u katika hiyo **damu**” (Walawi 17:11). Kwa maneno mengine, maisha ya kawaida yanawezeshwa kuwepo na damu, lakini sasa Yesu alikuwa akiishi kwa roho ya Mungu; sio damu.

Yesu atakapowapa watu uzima wa milele, miili yao ya kibinadamu itakuwa miili ya kiroho: “Hupandwa mwili wa asili; hufufuliwa mwili wa roho” (1 Wakorintho 15:44). Ni, “Sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa” (ms. 53).

Miili yao mipya itakuwa sasa ikiishi kwa roho ya Mungu, badala ya kuishi kwa damu inayokufa. Hakutakuwa na uchungu tena, wala kuugua, wala udhaifu wa kimwili au kiakili. Hakutakuwa na maumivu ya aina yeyote. Neno linasema:

“Naye (Mungu) atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita” (Ufunuo 21:4).

### **Maajabu ya uzima wa milele**

Kwa hakika itakuwa ni hali nzuri ya ajabu sana ya kuweza kuishi. Katika hali hiyo, tutaweza kufurahia kikamilifu vitu vyote vizuri Mungu atupavyo.

Kutakuwa na mibaraka ya afya njema, nguvu, chakula bora, amani na usalama, na kujua zaidi kuyahusu mambo ya Mungu. Hakutakuwa tena na mapambano dhidi ya dhambi kwa 'wenye haki'.

Utakumbuka ya kwamba kwa kipindi kifupi katika karne ya kwanza, mitume walipewa karama (zawadi) za Roho Mtakatifu. Wapo walioweza kuihubiri Injili kwa lugha za kigeni, na wengine waliweza kuponya magonjwa ya kimwili na kiakili. Haya yalikuwa ni 'malimbuko' tu (mavuno ya kwanza) ya karama hizo, watakazokuwa nazo watakatifu katika Ufalme wa Mungu. Tumepewa kuona kidokezo hicho cha ajabu cha nyakati hizo zinazokuja mbeleni.

Uzima huo sio tu wa miaka hiyo 1000 ya Ufalme, bali ni wa milele. Pengine hili ni gumu sana kwetu kulielewa, kwa sababu ni tofauti mno na maisha ya sasa tunayoishi. Wapo ambao wameshawishika hata

kufikiri kuwa maisha yasiyo na mwisho yatakuwa kitu cha kuchosha. Lakini, kamwe Mungu hawezi kuahidia watu wake kitu ambacho hakina mvuto. Andiko linasema:

“Maana tangu zamani za kale watu hawakusikia, wala kufahamu kwa masikio, wala jicho halikuona Mungu, ila wewe, atendaye mambo kwa ajili yake amngojoye” (Isaya 64:4).

Tafsiri hapa ya Kiswahili ameleta shida kupata kinachosemwa. Kwa usahihi zaidi (tukilinganisha na Biblia yoyote ya Kingereza) ingekuwa: “Maana tangu zamani za kale watu hawakusikia kwa masikio yao, wala jicho halikuona, ila wewe, Mungu, mambo unayotenda kwa ajili ya yeye akungojeaye”.

Hatuwezi kuyaelewa maajabu ya wakati huo, wakati shughuli kubwa na tukufu ya utawala wa Yesu Kristo wa miaka elfu moja itakapokamilika. Baada ya hapo mambo yatakuwa mazuri hata zaidi. Tunaambiwa, Mungu atakuwa: “Yote katika wote” (1 Wakorintho 15:28). Uhusiano kati ya Mungu na vitu alivyounda utakuwa mkamilifu; umetengemaa. Hivi ndivyo Mungu alivyopanga tangu mwanzo.

Hii ndiyo ahadi ya uzima wa milele.

#### **Muhtasari**

1. Mungu, Yesu na malaika ndio pekee walio na ‘kutokuharibika’ kwa sasa.
2. Baada ya hukumu walio ‘wa haki’, watakatifu, watapewa nao uzima wa milele; watapewa kutokuharibika.
3. Watakaowezeshwa kutokuharibika watakuwa wamepewa miili ya kiroho.

**Vifungu vya kusoma:** Danieli 12: 1-3, 1 Wakorintho 15:50-57

**Kujifunza kwa moyo:** Yohana 3:16

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele”.

## MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

*Karatasi ya maswali: namba 7*

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa 'Kazi ya ziada' unaweza kulijibu swali kama ukipenda, au kuliacha kama unaona huliwezi. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

### MASOMO: 24 – 27

24 A. Eleza jinsi tunavyoweza kuokolewa.

B. Eleza kwa maneno yako maana ya 'neema' au 'rehema'.

Kazi ya ziada

C. Nini maana ya: 'Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi?' (Warumi 6:1).

25. A. Ni namna ipi sahihi ya kumwelezea muumini wa kweli ambaye ndio amefariki?

- a) Amekufa.
- b) Amekwenda mbinguni.
- c) Amelala usingizi.

- B. a) Toa sababu zinazoonesha kuwa Yesu hakuwa 'roho' alipofufuka kutoka kwa wafu.  
b) Kazi ya ziada: Unaweza kutoa vifungu vingine ukiacha Luka 24, kulithibitisha jibu lako katika (a)? Kama 'ndio' vitaje.  
c) Je? Waumini watakuwa na 'miili' watakapofufuka kutoka kwa wafu?  
d) Kazi ya ziada: Unaweza kutoa msitari wa rejea kuthibitisha jibu lako katika (c)?
- C. a) Katika Yohana, Sura ya 11, Mariamu alisemaje mara tu alipomwona Yesu?  
b) Lazaro alitokaje kaburini?  
c) Katika Yohana 12:10-11 tunaambiwa kuwahasu makuhani wakuu?

Kazi ya ziada

- D. Mistari gani katika Yohana 5 inayosema kuwa:  
a) Mungu ametoa mamlaka yote ya kuhukumu kwa Mwanawe?  
b) Wakati unakuja ambao wote walio makaburini wataisikia sauti ya Yesu?  
c) Kama tunayasikia maneno ya Yesu na kumuamini, tunaweza kupita mauti na kuwa na uzima?

26. A. Yaweke matukio haya katika mpangilio sahihi:  
UFUFUO / KURUDI YESU/ KUUSIMAMISHA UFALME / HUKUMU

- B. a) Hebu andika Mathayo 25:31 – 32.  
b) Mwana wa Adamu katika msitari wa 31 ni nani?  
c) Msitari wa 34 unasema zawadi kwa 'wenye haki' ilikuwa ni nini?  
d) Ni nini ambacho wenye haki walifanya, ambacho wasio na haki hawakufanya?
- C. Ni watu gani ambao hawatahukumiwa?

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## MALAIKA

**SOMO:** Waebrania 1

Malaika ni wajumbe wa Mungu. Wanaweza kuingia 'uwepo' Mtakatifu wa Mungu, kwa hiyo ni sharti wawe viumbe wasio na dhambi. Hatuambiwi malaika wako wangapi, ila tunajua hesabu yao ni kubwa kwa kusoma Waebrania 12:22, na Mathayo 26:53.

**Malaika wanafanya nini?**

- ✚ Wanatoa ujumbe
- ✚ Wanaongoza
- ✚ Wanafanya ulinzi na kuokoa
- ✚ Wanaangamiza

Tutaviangalia vipengere hivi kimoja-kimoja:

**1. MIFANO YA MALAIKA WAKITOA UJUMBE**

MAREJEO	MAELEZO
Mwanzo 18	Ibrahimi aliambiwa kuwa, yeye na Sara wangepata mtoto wa kiume. Malaika hao wanaelezwa kuwa ni 'watu'; hawakuwa tofauti ni watu wa kawaida. Mara nyingine malaika wanaweza kuonekana tofauti sana, hasa wanapokuwa wanaonesha utukufu wa Mungu.
Mwanzo 19:1-5	Hapa wawili kati ya malaika hao wanakwenda kumtembelea Lutu na kumtahadharisha kuwa, Mungu alikuwa na mpango wa kuiangamiza Sodoma na watu wa Sodoma. Malaika hao walikuwa ni 'watu'.
Mwanzo 22:11, 15	Malaika aliita kutoka mbinguni kumzuia Ibrahimi asimchinje mwanawe, Isaka. Baada ya hapo malaika walimbariki Ibrahimi kwa imani na utii wake.
Kutoka 3:2	Musa alikuwa ameambiwa kuwa, Mungu angemtuma Misri kuwaokoa wana wa Israeli kutoka kwenye utumwa wao. Malaika aliyempa huo ujumbe alikuwa katika moto kwenye kichaka kinachoungua.
Waamuzi 6:11-24	Malaika anamwambia Gideoni kuwa, Mungu angemsaidia kuwapiga maadui wa Israeli. Huyu malaika alipotea kwenye moto Gideoni aliowasha.
Luka 1:11 – 19	Zakaria anaambiwa na malaika kuwa, yeye na Elisabeti wangepata mtoto wa kiume, ambaye ni Yohana Mbatizaji.
Luka 1:26	Malaika Gabrieli anamwambia Mariamu kuwa, angekuwa mama wa Yesu.
Matendo 8:26	Filipo anaagizwa kukutana na mtu wa Kushi. Aliweza baada ya hapo kumfundisha juu ya Yesu na kumbatiza. (Kwenye msitari wa 29 malaika anaitwa 'roho')

**2. MIFANO YA MALAIKA WAKIONGOZA WATU**

- (i) Ibrahimi alimtaka mtumishi wake amtafutie mke mwanawe, Isaka, lakini alikuwa awe mwanamke wa kumfaa! Ibrahimi anamwambia mfanyakazi wake huyo kuwa, malaika angemsaidia (Mwanzo 24:7); na kweli alimwongoza.
- (ii) Musa alipowaongoza wana wa Israeli kutoka Misri, nguzo ya wingu ilikwenda pamoja nao. Iliwalinda na kuwaonesha njia. Tunaambiwa kuwa malaika wa Mungu alikuwa pamoja nao katika hiyo nguzo ya wingu (Kutoka 14:19 na Kutoka 23:20, 21).

Ni muhimu kutambua hapa kuwa, ingawa malaika wa Mungu alikuwa na wana wa Israeli wakati wote walipokuwa nyikani, hata hivyo walimwasi Mungu. Malaika hakuwazuia wasiasi.

### 3. MIFANO YA MALAIKA WAKIWALINDA NA KUWAOKOA WATU WA MUNGU

- (i) Marafiki watatu wa Danieli waliokolewa kwenye tanuru la moto na malaika (Dan. 3:28).
- (ii) Danieli mwenyewe aliokolewa kwenye handaki lenye simba. Malaika 'aliyafumba makanwa ya simba' (Dan. 6:22).
- (iii) Malaika alifungua milango ya gereza kwa ajili ya mitume kutoka (Matendo 5:19), na katika Matendo 12 alimfungulia Petro (ms. 7).

### 4. MIFANO YA MALAIKA WAKIANGAMIZA

- (i) Mji wa Yerusalemu ulipozungukwa na majeshi ya Ashuru wakati wa mfalme Hezekia, Hezekia alimlilia Mungu apate msaada. Malaika aliwaangamiza Waashuru wote waliokuwa wakimdharau Mungu wa Israeli (2 Wafalme 19:35).
- (ii) Mfalme Herode, wakati za Agano Jipya, aliuwawa na malaika sababu ya kiburi chake (Matendo 12:23).

#### **Malaika hawatendi dhambi**


Katika nyakati za Kutoka, malaika walisababisha uharibifu ulioletwa na tauni. Akielezea hili, mwandika-Zaburi anasema kuwa, Mungu:

“Akawapelekea ukali wa hasira yake (Wamisri), ghadhabu, na uchungu, na taabu, kundi la malaika waletao mabaya” (Zab. 78:49).

Malaika wenyewe hawakuwa waovu, lakini walitumwa na Mungu kuwafanyia mambo tunaoyaona kuwa mabaya (lakini yalikuwa kwa vyovyote ni ya lazima). Hakuna malaika wanaofanya dhambi. Lakini vipi juu ya 2 Petro 2:4 ambapo tunaambiwa: “Ikiwa Mungu hakuwaachilia malaika waliokosa.....”

Neno hapa lililotafsiriwa 'malaika' linaweza pia kutafsiriwa 'wajumbe'; linaweza kumaanisha wajumbe wa kimbingu (malaika) au wajumbe wa kidunia (watu waliobeba ujumbe). Neno la kiasili lililotumiwa katika Biblia ('aggelos' katika Kiyunani), halitambulishi kama wajumbe hao walikuwa wa 'kimbingu' au wa 'kidunia'. Watu waliotafsiri mara nyingine walikosea!

Tunafikiri kuwa, 2 Petro 2:4 inaweza kuwa inaongelea kilichoandikwa katika Hesabu 16.



### **Malaika wanaonekanaje?**

Kwa kawaida, malaika huwa wanafanya kazi zao bila ya kuonekana na watu. Wakati Elisha na mtumishi wake, Gehazi, walipokuwa wakiwindwa na mfalme wa Shamu (Syria), Elisha alijua Mungu angemsaidia lakini mtumishi wake aliogopa sana. Elisha alimwomba Mungu amfumbue mtumishi wake macho. Gehazi alipofumbuliwa ndipo alipoona kuwa:

“... kile kilima kilikuwa kimejaa farasi na magari ya moto yaliyomzunguka Elisha pande zote”

(2 Wafalme 6:17).

Jeshi la malaika wa Mungu lilikuwa hapo kuwalinda!

Tumeshaona kuwa malaika waliomtokea Ibrahimu na Lutu walifanana na watu, na kwa hiyo, kwa vyovyote isingewezekana wakawa na mabawa. Lakini tumeshaona pia kwamba, malaika waliweza kuwa katika moto na katika wingu, kama ilivyokuwa katika kichaka kilichokuwa kikiungua, na katika nguzo ya wingu kule nyikani.

Kwa hiyo malaika hawana muonekano wa namna moja, na wanaweza pia kutoweka tu kiajabu-ajabu, kama ilivyokuwa kwa yule aliyemtembelea Gideoni.

### **Yesu na malaika**

Malaika waliwaambia Yusufu, Mariamu na wachungaji wa makondeni kuhusu kuzaliwa kwa Yesu. Waliendelea kumwongoza Yusufu kwa kumwambia kumchukua kitoto Yesu kwenda chini Misri, na walimwambia pia lini warudi baada ya hali kuwa shwari.

Zaburi ya 91:11 ilitabiria malaika kumsaidia Yesu. Katika Mathayo 4:11 tunasoma kuwa, baada ya majaribu ya Yesu ya nyikani, walikuja malaika ‘wakamtumikia’. Kutumikia ni ‘kuhudumu’, kwa hiyo inaelekea malaika walimhudumia Yesu kwa kumletea chakula, baada ya kufunga kwake kwa muda mrefu.

Katika bustani ya Gethsemane, Yesu alipojua kusulubiwa kwake kumefika, aliomba aweze kufanya lile Mungu alitakalo. Malaika alimtokea, “Akamtia nguvu” (Luka 22:43). Angeweza kuukwepa msalaba; kukwepa kukamatwa, na kumwomba Mungu atume majeshi kumi na mawili ya malaika kumwoko. Lakini alijua ilimpasa afe kwa ajili yetu. Ilikuwa ndio njia ya pekee ya sisi kuweza kusaidiwa kuondokana na tatizo letu sugu la dhambi.

Tungeweza kutegemea Mungu amfanye Mwanawe awe kama malaika, lakini haikuwa hivyo; alikuwa mtu. Ni katika kuwa katika hali yetu wanadamu, ndivyo ambavyo angeweza kujaribiwa; kuvutwa na dhambi. Aliteseka na hatimaye kufa. Malaika hawawezi kufa (Luka 20:36).

Katika Waebrania 2:9 tunaambiwa kuwa, Yesu, alifanywa mdogo punde kuliko malaika, ‘Kwa sababu ya maumivu ya mauti’. Tunaambiwa tena: “Hatwai asili ya malaika, ila atwaa asili ya mzao wa Ibrahimu” (ms. 16).

Alipofufuka kutoka kwa wafu, malaika walikuwapo. Hebu fikiriri walivyofurahi! Akiwa ameishinda dhambi na mauti, Yesu alipewa hadhi ya juu zaidi ya malaika. Hana tena hulka ya kiasili ya binadamu wengine:

“(Yesu) akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu; amefanyika bora kupita malaika...” (Waebr. 1:3,4).

Heshima ya kukaa katika mkono wa kuume wa Mungu ni ya Bwana Yesu Kristo peke yake. Hakuna malaika aliyewahi kupewa fursa ya namna hiyo (Waebr. 1:13). Katika Sura hiyo malaika wanaelezewa kuwa ni: “Pepo na watumishi wake kwa miali ya moto” (ms. 7). Anasema malaika: “Wote si roho watumikao wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu?” (ms. 14). Neno ‘wote’ hapo ni la muhimu. Hakuna malaika anayeweza kumwasi Mungu.

Malaika wanafanya kazi kwa ajili ya wale watakaourithi wokovu. Tuliona katika kisa cha Towashi wa Kikushi (Matendo 8:27-39) jinsi malaika alivyomuweka towashi huyo katika mazingira yaliyomwezesha kujifunza ukweli wa Injili, na kubatizwa. Tuliona mitume wakiwa wanasaidiwa watoke gerezani. Lakini malaika hawamsaidii kila mtu! Wanatumika kwa ajili ya **wale tu** watakaourithi wokovu (Waebr. 1:14).

### **Kazi ya malaika leo**

Ingawa hatuwaoni, malaika wanaweza kutusaidia hata leo, lakini ni kama tunaishi kwa kujaribu kumpendeza Mungu. Zaburi ya 34:7 inasema kuwa, malaika wa Mungu wapo kuwazungukia '**wamchao na kuwaokoa**'. Wanaweza kutusaidia, lakini haina maana kwamba waumini hawatapatwa na wakati mgumu.

Shida katika maisha zipo ili kutufundisha mambo fulani-fulani, na kutuweka karibu na Mungu. Wala malaika hawatawazuia waumini wasifanye dhambi. Kumbuka, malaika hakuwazuia wana wa Israeli kuasi wakiwa nyikani!

### **Kazi ya baadaye ya malaika**

Bwana Yesu Kristo hivi karibuni atarudi hapa duniani, lakini hakuna anayejua ni lini. Hata malaika wa Mungu mbinguni hawajui (Marko 13:32). Atakapokuwa anarudi, malaika wataongozana naye. Katika 2 Wathesalonike 1:7,8 tunaambiwa, Bwana Yesu atafunuliwa kutoka mbinguni:

“Pamoja na malaika wa uweza wake katika mwali wa moto, huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu”.

Malaika watahusika katika kuwakusanya watu kwa hukumu. Katika wakati huo, waumini wa kweli watafanywa wawe kama malaika. Hawataoa au kuolewa tena, au kuweza kufanya dhambi, au kufa (Mathayo 22:30, Luka 20:36). Ndio maana kunakuwa na shangwe mbinguni (kati ya malaika), kila mdhambi mmoja anapotubu!

### **Muhtasari**

1. Malaika ni wajumbe. Wanaweza pia kuongoza, kulinda, kuokoa au kuangamiza.
2. Wanawasaidia wale ambao ni waumini wa kweli, lakini hawamzuii mtu asitende dhambi.
3. Kwa kawaida hawaonekani. Kwa nyakati walipoonekana, walionekana kuwa katika hali tofauti-tofauti.
4. Malaika hawawezi kuasi; hawawezi kufanya dhambi. Hawaoi na kamwe hawafi. Katika Ufalme, waumini watakuwa hivyo.
5. Kwa mara ya kwanza, Yesu alikuwa, kihadhi, mdogo kuliko malaika. Baada ya ufufuo wake aliwekwa juu yao.
6. Malaika wataambatana na Yesu atakaporudi hapa duniani.

**Vifungu vya kusoma:** Tafadhali zipitie tena rejea zilizoko kwenye somo hili. Zisome zote na utapata ufahamu juu ya malaika na kazi wanazofanya kwa niaba ya Mungu.

**Msitari wa kushika:** Waebrania 1:14

“Je! Hao wote si roho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu?”

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## IBILISI, MAPEPO, SHETANI

**SOMO:** Mathayo 8:14-34

## IBILISI NA PEPO

Kuna maneno mawili ya Kiyunani yaliyotafsiriwa ‘Ibilisi’ katika Biblia zetu, na kwa kuwa yanamaanisha vitu tofauti, tutahitaji hasa kujua kila neno lina maana gani. Maneno hayo ni:

Daimon – lenye maana ya ‘roho mbaya au roho mwovu’

Diabolos – lenye maana ya ‘msingizaji au mchongezi’

Totalichunguza neno Ibilisi (diabolos) katika somo litakalofuata. Neno ‘daimon’ linatumiwa katika Kiyunani tunapoambiwa, Yesu: ‘akawatoa pepo’. Yesu aliponya magonjwa yote watu waliyokuwa wakiugua. Aliwapa vipofu kuona, aliwezesha viziwi kusikia, aliwafanya na walemavu wa miguu kutembea. Yesu aliwaponya pia watu wengi waliokuwa na magonjwa ya kiakili; kichaa na matatizo kama ya kifafa.

Katika siku hizo, kama ugonjwa ulikuwa mgumu kueleweka, watu walisema kuwa mgonjwa huyo ‘alikuwa na pepo’ au ‘ameshikwa na pepo’. Soma kwa makini Mathayo 8:16,17. Tunaambiwa hapa kwamba:

“...wakamletea (Yesu) wengi wenye pepo; akawatoa pepo kwa neno lake, akawaponya wote waliokuwa hawawezi (‘wagonjwa’)”.

Yesu akawaambia, Isaya alikuwa ametabiria jambo hilo, aliposema:

“Mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, na kuyachukua magonjwa yetu” (Isaya 53:4).

Hili linatufundisha kuwa:

“Kushikwa au kuwa na pepo” **ni sawa na kuwa na** ‘udhaifu au magonjwa mbalimbali’. Yesu aliwaondolea udhaifu na magonjwa hayo.

**Sanamu (miungu ya wongo) iliyokuwa ‘pepo’**

Katika sehemu zingine kwenye Biblia ambapo neno ‘daimon’ lilitumika, mara nyingi lilikuwa likiongelea ibada za miungu ya uwongo. Tuangalie Zaburi ya 106.

Zaburi hii inatuambia juu ya makosa mengi Waisraeli waliyokuwa wakiyafanya na vile, pamoja na hayo, Mungu alivyoendelea kuwabariki. Soma msitari wa 36-38 mwandika-Zaburi anaposema juu ya wana wa Israeli kuwa:

“Wakazitumikia sanamu zao, nazo zikawa mtego kwao. Naam, walitoa wana wao na binti zao kuwa dhabihu kwa mashetani”.

Neno ‘**mashetani**’, hapa ni neno ‘**daimon**’ katika Kiyunani, lililotafsiriwa pia ‘**pepo**’, kwenye Kiswahili. Katika msitari wa 37 shutuma dhidi yao zimerudiwa, lakini hapa tunaambiwa kuwa: “Waliwatoa wana wao na binti zao kuwa dhabihu kwa mashetani”. Ni wazi basi kuwa, ‘mashetani’ wanaotajwa hapa, walikuwa ni sanamu; miungu ya uwongo ya mataifa yaliyokuwa yakiizunguka Israeli.

Kuna matumizi ya neno hili katika Agano Jipya yanayoleta maana hiyo hiyo katika 1 Wakorintho 10:20. Mtume Paulo anawaambia Wakorintho ya kwamba, vitu vile watu wa kimataifa: “Wavitaovyo sadaka, wavitoa kwa mashetani, wala si kwa Mungu”.



Kama ukirudi nyuma kwenye msitari wa 19 utaona kuwa, hayo ‘mashetani’ yalikuwa, ‘sio’ kitu. Yalikuwa sanamu; miungu isiyokuwa ya kweli ya watu wa kimataifa, wasiomjua Mungu.

Wakristo wamepewa kumwabudu Mungu mmoja tu aliye wa kweli; miungu mingine yote ni sanamu, hapa ikiitwa ‘mashetani’. Vitu visivyoyote na uhai watu wanaviabudu bure; kwa Myahudi wa kweli huo uliitwa *umataifa* au *ukafiri*.

**Angalizo:** Neno lenye maana ya ‘roho mbaya au roho mwovu’ (daimon) kwa kawaida limetafsiriwa ‘pepo’, lakini lisichanganywe na neno ‘Ibilisi’. Sehemu zingine, neno, ‘mashetani’ limetumika badala ya pepo.

## **SHETANI**

Neno ‘shetani’ katika Agano la Kale lina maana ya ‘adui’ au ‘anayepinga’. Mfano wa jinsi lilivyotumika upo katika 1 Wafalme 11:14 ambapo tunasoma, kuwa: “Ndipo BWANA akamwondokeshea Sulemani adui, Hadadi Mwedomi”. Na mbele kidogo kwenye 1 Wafalme 11:23-25 tunaambiwa: “Tena, Mungu akamwondokeshea adui mwingine, Rezoni mwana wa Eliada.....Naye akawa adui wa Israeli siku zote za Sulemani”.

Sulemani alianza ufalme wake vizuri akimpenda sana Mungu, lakini baadaye alinasa katika kuabudu sanamu. Matokeo yake, Mungu alimwondokeshea maadui ili asipate amani. Neno hilo ‘adui’ ni neno hilo hilo lililotafsiriwa ‘shetani’ sehemu zingine.

Mfalme Hadadi na mfalme Rezoni walimsumbua Sulemani na Israeli (‘waliwapinga’); na sababu ni kwamba, Sulemani na Israeli walikuwa wamemkiuka Mungu; walikuwa wakifanya dhambi. Hadadi na Rezoni walikuwa ‘shetani’ kwa Sulemani na Israeli.

Lakini, katika Biblia ‘shetani’ sio mara zote anakuwa adui mbaya. Katika Hesabu tunaambiwa juu ya nabii aliyekuwa akiitwa Balaamu, aliyekuwa akienda safari ambayo Mungu hakuwa akitaka aende. Maandiko yanasema:

“Hasira ya Mungu ikawaka kwa sababu (Balaamu) alikwenda; malaika wa BWANA akajiweka njiani, ili kumpinga” (Hes. 22:22).

Neno ‘kumpinga’ hapa pia ni neno ‘shetani’ (‘kuwa shetani’), katika Kiebrania. Biblia ya Kingereza inasema *‘The angel of the LORD stood in the way for an adversary against him’*. Hapa ‘shetani’ alikuwa ni malaika mwaminifu wa Mungu anayefanya mpenzi ya Mungu, aliyetumwa kumzuia Balaamu njiani asiende kuwalaani wana wa Israeli.

Ni wazi neno hilo haliwezi kumaanisha kiumbe mwovu, au malaika mwovu. Hakuna malaika anayeweza kuwa mwovu. Shetani ni adui, mpinzani; mtu anayepinga. Anaweza kuwa mwema au mbaya.

MAANA YA SHETANI NI ADUI AU MPINZANI; MTU ANAYEZUIA
---

Wakati Petro alipojaribu kumzuia Yesu asiendee njia ambayo Mungu alimtaka aiendee; njia ya msalaba, Petro alikuwa ‘adui’. Yesu alimwambia Petro:

“Nenda nyuma yangu, Shetani, u kikwazo kwangu”. Sababu ni kwamba, Petro alikuwa akitaka kumgeuza Yesu asiufuate mpango wa

Mungu. Yesu anamwambia, “Huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu” (Mathayo 16:23).

Kwa hiyo, Petro alikuwa ‘shetani’; alikuwa hapa akimpinga Yesu; akipingana na kusudi la Mungu. Unaweza kuona, hata katika Agano Jipya maana ni ile ile. Adui mkubwa kuliko wote wa mtu ni hulka yake mwenyewe ya dhambi. Mara nyingi inakuwa katika kumpinga Mungu.

Neno ‘shetani’ linaweza kutumiwa kwa hiyo hulka. Hili linaweza kuonekana tena vizuri kwa kulinganisha Matendo 5 msitari wa 3 na wa 4.

Ms.3: “Petro akasema, Anania, kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu na kuzuia kwa siri sehemu ya kiwanja?”

Ms.4: “...Ilikuwaje hata ukaliweka neno hili moyoni mwako? Hukumwambia uongo mwanadamu, bali Mungu”.

Ni mawazo yaliyokuwa potofu ya Anania yaliyomfanya afanye vile. Neno ‘shetani’ limetumiwa katika msitari wa 3 kuiwakilisha hulka ya dhambi aliyokuwa nayo Anania, iliyokuwa ikiyapinga nafsini mwake maadili ya kiroho; mambo ya Mungu.

### **Lusifa alikuwa ni nani?**

Watu wanaoamini juu ya uwepo wa ‘dudu’ ova linaloitwa ‘shetani’ lisiloonekana, wanapenda kuthibitisha kuamini kwao kwa kunukulu mara nyingi Isaya 14:12-16. Mistari hiyo inasema:

“Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa uliyewaanguka mataifa....”

Maneno, ‘nyota ya alfajiri’ katika Biblia ya Kingereza ni ‘Lucifer’ (Lusifa). Kwa hakika, kama ukikisoma kifungu hicho chote (Isaya 14), utaona kuwa, Lusifa alikuwa ni mfalme wa Babeli, ‘mwenye kuonea’ (anayeelezewa kwenye msitari wa 4). Ulikuwa ni unabii wa kuanguka kwa ufalme wa Babeli; kitu kilichotokea miaka kama 500 kabla ya kuzaliwa kwa Yesu.

Kwa namna hiyo hiyo, Ezekieli 28:14-16 mara nyingine inasemewa kusemea uwepo wa ‘dudu’ hilo:

“Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; nami nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu...Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako”.

Ni wazi kuwa ujumbe huu ulikuwa ni kwa ajili ya mfalme wa Tiro, kama msitari wa 12 unavyosema. Hauhusiani na uwepo wa ‘dudu’ lolote hai ova lisiloonekana.

### **Ni nini kilichotokea katika Bustani ya Edeni?**

Unakumbuka ni nini kilichotokea katika Bustani ya Edeni? Mungu alipomwita Adamu kutoka mahali alipojificha na kumuuliza kama alikuwa amekula kutoka katika mti wa ujuzi wa mema na mabaya, Adamu alijibu: “Huyo mwanamke **uliyenipa** awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala” (Mwanzo 3:12).

Ukilitafakari jibu hilo utaona kwamba, Adamu alikuwa ni kama anamwambia Mungu kosa halikuwa lake; ni la Mungu. Yeye ndiye aliyempa huyo mwanamke, na mwanamke ndiye wa kulaumiwa kwa kumpa hilo tunda. Lakini, kosa lilikuwa ni **la kwake** mwenyewe.

Kisha Mungu akamuuliza mwanamke alichofanya ni nini, na mwanamke akajibu: “Nyoka alinidanganya, nikala”. Kwa maneno mengine, alimtupia lawama nyoka; lilikuwa ni kosa la nyoka, sio lake.

Adamu na Hawa walikuwa na shauku ya kutupia lawama kwingine, badala ya kubeba lawama wenyewe kwa makosa yao. Sisi wote tumekuwa hivyo! Hatupendi kuwajibishwa kwa mawazo na matendo yetu mabaya wenyewe; hatupendi kukubali kosa. Pengine ndio maana watu wengi wanapenda kuamini kuwa, kuna ‘dudu’ hilo lisiloonekana linaloitwa ‘shetani’ linalowadanganya watu wamwasi Mungu.

Mungu alimruhusu nyoka kuongea; hili sio ajabu sana. Ni kama alivyomruhusu punda wa Balaamu kuongea katika Hesabu 22:28. Anao uhuru wa kutumia alivyoviumba kutimiza malengo yake.

Adamu alipaswa kujidhibiti na kumkataa nyoka, lakini Mungu aliwaacha Adamu na Hawa wajaribiwe, na wakaanguka. Nyoka hakuwafanya walile lile tunda; alichofanya tu ilikuwa kuwajaribu. Adamu na Hawa hawakumtii Mungu; walijiamulia tu wenyewe kufanya walichotaka.

#### **Muhtasari**

1. 'Pepo' katika Biblia ni magonjwa yaliyofikiwa kusababishwa na roho wabaya/wachafu. Yesu alipoyaponya ilihesabiwa 'ametoa pepo'.
2. Neno 'mashetani' au 'mapepo' ni tofauti na neno Ibilisi (tutakalolijadili katika somo lijalo).
3. 'Shetani' maana yake ni adui/mtu anayepinga. 'Adui' huyo anaweza kuwa wa kheri au wa shari.
4. Neno Lusifa katika Isaya 14 kwenye Biblia ya Kingereza linamwongelea mfalme wa Babeli, sio 'dudu' hai lisiloonekana.

**Vifungu vya kusoma:** Mathayo 16:21-28, Hesabu 22

**Mistari ya kujifunza:** Mathayo 8:16, 17

"Hata kulipokuwa jioni, wakamletea wengi wenye pepo; akawatoa pepo kwa neno lake, akawaponya wote waliokuwa hawawezi, ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, Mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, na kuyachukua magonjwa yetu".

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## IBILISI NA DHAMBI

**SOMO:** Waebrania 2: 9 - 18

Ni kweli Biblia inamwongelea Ibilisi. Ibilisi ni nini au ni nani? Neno la Kiyunani ni 'diabolos'. Hebu tuone kama Biblia inaweza kutupa jibu yenyewe.

Katika 1 Yohana 3:8 tunapewa sababu ya Mungu kumtuma Yesu; ni, "Ili azivunje kazi za Ibilisi." Alidhihirishwa kusudi anayofanya Ibilisi yasiwe yakishinda. Katika Waebrania 2:14 tunaambiwa pia kuwa, Yesu alikuja amharibu Ibilisi na kazi zake.

Waebrania 2:14	Maana
"Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu ya mauti yaani Ibilisi".	Waumini wana damu na mwili (ni binadamu); na Yesu alikuwa kama wao. Yesu alikufa ili aweze kumwagamiza yeye aliye chanzo cha kifo ambaye ni Ibilisi (yaani dhambi).

Huu msitari unachosema ni kwamba, Yesu alizaliwa kama anavyozaliwa mtu yeyote; na hili ni ili aweze kumwagamiza Ibilisi, kwa kufa msalabani.

Tujiulize: kama Ibilisi angekuwa kiumbe kisicho cha kawaida kwa namna yoyote, Yesu angewezaje kwa kufa kwake kukiangamiza? Na kama kimeangamizwa hakiko basi!

Tunajua ya kuwa dhambi ndiyo iletayo mauti; **mshahara wa dhambi ni mauti**. Kwa hiyo, Ibilisi ambaye Yesu alimwagamiza katika Waebrania 2:14 alikuwa hasa ni nguvu ya dhambi, iliyokuwa ndani yake. Nguvu hiyo iko ndani yetu sisi wote. Kumbuka: Yesu aliirithi hulka ya dhambi kupitia kwa mama yake, Mariamu. Katika Waebrania 9:26 tunaambiwa kuwa:

"Katika utimilifu wa nyakati, (Yesu) amefunuliwa, azitangue dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake".

YESU ALIMSHINDA IBILISI = YESU ALIISHINDA DHAMBI NAFSINI MWAKE

Yesu aliishi maisha makamilifu; hakuitii dhambi. Tunaambiwa: "Alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi" (Waebr. 4:15). Sisi tunajaribiwa, tunaanguka. Yesu alijaribiwa lakini kamwe hakushindwa; hakuanguka. Aliweza kuishinda dhambi kwa namna hii, kwa kuwa alikuwa Mwana wa Mungu.

Alipambana na dhambi maisha yake yote, na hatimaye msalabani aliibomoa kabisa dhambi kwa kuishinda ile hulka iliyomfanya ajaribiwe. Kwa sababu hiyo, Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, na kumpa 'mwili wa utukufu', usiojaribika kwa dhambi na usiokufa.

#### Kwa hiyo Ibilisi ni nini?

Ibilisi na dhambi ni kitu kile-kile. Yote ambayo Biblia inasema juu ya Ibilisi, inasema pia juu ya dhambi:

- Ibilisi ana uadui na Mungu ...ndivyo ilivyo dhambi
- Ibilisi anamjaribu mtu ...ndivyo ilivyo dhambi
- Ibilisi ni mdanganyifu...ndivyo ilivyo dhambi
- Ibilisi ana nguvu ya mauti...na dhambi inayo
- Ibilisi aliangamizwa kwa kifo cha Kristo...ndivyo ilivyokuwa dhambi.

Kwa kulinganisha hivi tunaona kwamba, Ibilisi na dhambi ni kitu kimoja. Kwa hiyo dhambi inatoka wapi? Biblia ina jibu kwa swali hili, pia. Dhambi inatoka katika mioyo yetu wenyewe. Yesu aliwahi kusema:

“Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wivi, uuaji, uzinzi, tamaa mbaya, ukorofi, hila, ufidadi, kijicho, matukano, kiburi, upumbavu. Haya yote yaliyo maovu yatoka ndani, nayo yamtia mtu unajisi” (Marko 7:21-23).

Mambo haya mabaya hayapo tu katika mioyo ya watu wabaya. Hata watu wanaoonekana wema kabisa, wana uovu mioyoni mwao. Mtume Paulo akiwa ni mtu mwema kama alivyokuwa, aliona kwa kawaida vigumu kufanya yaliyo sahihi, na rahisi kufanya yasiyo sawa. Anasema katika Warumi 7:18 kuwa, ndani ya mwili wake, ‘halikai neno jema’.

Yakobo anatupa ujumbe huo-huo. Ni kutoka ‘ndani’ yetu, na sio kutoka nje tunapopata majaribu ya dhambi. Anasema:

“Kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Halafu, ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti” (Yak. 1:14, 15).

**Angalizo:** Ingawa kifungu hiki kutoka katika Yakobo kinaongelea majaribu, hakitaji Ibilisi kabisa. Kila mtu anajaribiwa na mawazo yake mwenyewe mabaya, yakimvuta na kumdanganya.

IBILISI NI MSUKUMO WA DHAMBI ULIO NDANI YA HULKA YA MWANADAMU
---

### **Ibilisi aliyemjaribu Yesu**

Tulikwisha kuona katika Somo la 17 kuwa, yule mjaribu wa Yesu asingeweza kuwa Ibilisi anayeishi. Dunia ni mali ya Mungu na vyote vijazavyo (Zaburi 24:1). Yeye ndiye anayeidhibiti, na hakuna kiumbe kisichoonekana ambacho kingeweza kumpa Yesu, “Enzi hii yote na fahari yake” (Luka 4:6).

Zaidi ya hayo, tunajua Yesu asingelifuata ‘dudu’ la namna hiyo akijua kuwa ni ovu, kwenda nalo Yerusalemu au popote kwingine!

Kama tulivyoona, ‘Ibilisi’ katika majaribu hayo yalikuwa ni mawazo mabaya yaliyokuwa yakimjea Yesu, na tamaa iliyokuwa ikimvuta kumtaka akwepe machungu na mateso ya msalabani.

### **Ni kwa nini ‘Ibilisi’?**

Ni kwa nini Biblia mara nyingi inalitumia neno ‘Ibilisi’ badala tu ya kusema ‘dhambi’. Na kwa nini inamwongelea Ibilisi kama vile inasemea mtu asiyeonekana mwenye mamlaka makubwa? Kwa hakika, ni ili tuweze kutambua jinsi dhambi ilivyo na nguvu na inavyodanganya.

Tunahitaji kulielewa hili vizuri kabla hatujaweza kutambua hasa jinsi wote tunavyohitaji kuokolewa na dhambi. Tunapokuwa tumetambua haja hii, tunaweza kuanza kuelewa lile Bwana Yesu alilofanya kwa ajili yetu katika ushindi wake juu ya dhambi.

### **Muumba mmoja mwenye uweza wote**

Mungu ni Mkuu juu ya vitu vyote. Angeweza kweli kupingwa na kiumbe kiovu, kiwe ibilisi au shetani? Tunajua isingewezekana.

Lakini wazo la uwepo wa mamlaka iliyo kubwa ya uovu inayopingana na Mungu, limekuwa likishikiliwa na mataifa tangu enzi za kale. Waajemi wa zamani waliamini juu ya uwepo wa mamlaka mbili kuu, moja ikiwa ni Mungu na ya pili ikiwa ni ya shetani. Ya kwanza ilihesabiwa kuendana na uwepo wa nuru na wema, na ya pili, giza na uovu.

Mungu aliwatoa Israeli Misri ili awatenge na kuwafundisha, waweze kuwa watu wake, la kwanza akiwaambia: “Mimi ni BWANA, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri...Usiwe na miungu mingine ila mimi” (Kutoka 20:2,3.) Kwa kusahihisha imani potofu zilizoingia, Mungu alituma ujumbe kwa watu wake kupitia kwa nabii wake Isaya, akisema:

“Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine; zaidi yangu mimi hapana Mungu. Nitakufunga mshipi ijapokuwa hukunijua; ili wapate kujua toka maawio ya jua, na toka magharibi, ya kuwa hapana mwingine zaidi ya mimi; mimi ni BWANA, wala hapana mwingine. Mimi naiumba nuru, na kulihuluku giza; mimi nafanya suluhu, na kuhuluku ubaya; **Mimi ni BWANA, niyatendaye hayo yote**” (Isaya 45:5-7).

(Neno ‘ubaya’ hapa tusilichanganye na ‘dhambi’. Lina maana ya matatizo, kama ambavyo Mungu anavyowaletea wadhambi wasioyati mapenzi yake).

Kwa hiyo Mungu ‘angewafunga Wayahudi mshipi’, ili mataifa mengine waweze kumjua Mungu pekee aliye wa kweli, asiye na ‘mpinzani’, aliye chanzo cha yote. Kuna mamlaka iliyo kuu, na ni moja tu juu ya mbingu yote; inayoyapanga mambo yote. Mamlaka hii ni ya Muumba mmoja tu, aliye Mkuu sana, anayeyashikilia mambo yote kwa Neno la uweza wake. ‘Nguvu ya dhambi’ (ibilisi), iliyoko katika moyo na maisha ya mwanadamu, ndio upinzani pekee anaoupata Mungu.

### **Dhambi ni tatizo kubwa**

“Toka mbinguni BWANA aliwachungulia wanadamu, aone kama yuko mtu mwenye akili, amtafutaye Mungu. Wote wamepotoka, wameoza wote pamoja, hakuna atendaye mema, la! Hata mmoja” (Zaburi 14:2,3).

Hivi ndivyo mwandika–Zaburi anavyoweka. Katika Warumi 3:23 Paulo anatuambia kitu hicho-hicho, anaposema:

“Wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu”. Maneno hayo hayavutii kusoma. Hakuna kati yetu anayependa kuambiwa, ‘umekosa!’

Kila tunapokuwa tumekosea, tunajaribu kuweka visingizio, au kumlaumu mtu mwingine. Hatupendi kukubaliana na ukweli kuwa tuna hulka ya uovu. Lakini, bila kufanya hivyo hatuwezi kuanza kuelewa lile Mungu alilotufanyia katika kumtuma Yesu Kristo, na hatuwezi kuuitikia upendo wake.

Si wengi wanaotulia na kufikiri jinsi Mungu alivyoyakusudia wayaishi maisha yao, na wachache wanaojaribu kufanya hivyo, haraka wanajikuta katika mgogoro mkubwa. Nabii Yerima akiusemea moyo wa mwanadamu ulivyo, anasema ni: “Mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha” (Yer. 17:9).

Kila mtu ambaye kikweli anajaribu kuishi maisha mazuri; ya kiuaminifu, mbele ya Mungu, atasikitishwa na hili. Paulo anaelezea vizuri tatizo linalomjea katika Waraka wake kwa Warumi, anaposema:

“Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani ndani ya mwili wangu, halikai neno jema; kwa kuwa kutaka nataka, bali kutenda lililo jema sipati. Kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi; bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo” (War. 7:18,19).

### **Sasa tunapaswa tufanye nini?**

Kama tumetambua dhambi ilivyo ndani yetu, ni lazima tujitahidi kushindana nayo na kuiepuka. Hiyo ndio maana ya **kutubu**; kugeukia upande wa pili na kwenda mbele.

Hili ni jambo ambalo hatuwezi kulifanya bila ya msaada wa Mungu na mafundisho ya Neno lake. Kupitia katika mauti ya Yesu, tunaweza kumkaribia Mungu na kupata msamaha wa dhambi tunaposhindwa, na kuwa na tumaini la uzima.

Toba inaanza tunapotambua jinsi tulivyo wadhambi na dhambi ilivyo na nguvu. Toba inakuja tunapoitambua dhambi yetu na ubaya ulio ndani yetu (hili ni la muhimu sana).
---

Tunapotubu kwa utambuzi, tunakuwa wafuasi wa Bwana Yesu, tukimfuata na kuiendea njia yake. Yesu aliishi maisha yaliyo makamilifu. Kuwa ‘wafuasi wake’ maana yake ni kujitahidi kwa uwezo wetu wote kuiepuka dhambi; kujaribu kuishi alivyoishi. Paulo anasema:

“Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?” (Warumi 6: 1, 2).

Hatuwezi kuendelea na namna yetu ya maisha tuliyoizoea. Mbele zaidi katika Sura hiyo ya Warumi 6, mtume Paulo anasema:

“Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake; wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki” (ms. 12-13).

### **Itatubidi tuendelee kupambana na dhambi siku zote**

Kitu kimoja ni cha uhakika: hatutaweza kuvishinda vita hivi katika maisha haya. Hatutakaa tufikie wakati ambao tutaweza kusema, “Mapambano dhidi ya dhambi yamekwisha, na tumeshinda”.

Kama isingekuwa ni kwa msamaha wa Mungu ulio katika Kristo, uliopo kwa ajili yetu katika maisha yetu ya kila siku, tungeona mapambano yetu kuwa kitu kisichowezekana. Lakini, siku moja vita hii itakwisha!

Bwana Yesu atakaporudi duniani kuusimamisha Ufalme wa Mungu, wale watakaokuwa wamekuwa wafuasi wake waaminifu watabadilishwa; watafanywa wawe kama malaika. Watapewa uzima wa milele, kama ulivyojifunza katika Somo la 19, 25 na 27.

Lakini haitakuwa hivyo tu. Hulka yao itabadilishwa kiroho, dhambi haitakuwa tena na nguvu ndani yao. Hawatakuwa tena wakitamani kufanya mambo yasiyo sawa au kufikiri mambo mabaya. Vita itakuwa imekwisha, na dhambi itakuwa imeshindwa milele katika kufikiri kwa mfuasi. Tunasoma juu ya hili katika 1 Wakorintho 15:51-57.

#### **Muhtasari**

1. ‘Ibilisi’ ni neno la Kibiblia linalosimama badala ya nguvu ya dhambi katika hulka ya mwanadamu.
2. Yesu aliishinda nguvu hiyo ndani yake; ndio maana inasemwa kuwa alimshinda Shetani au Ibilisi.
3. Dhambi ni uovu, na haikubaliki kwa Mungu. Watu wote wanafanya dhambi au wamefanya dhambi (kasoro Yesu tu).
4. Ni lazima tutubu. Hili linamaanisha kusikitishwa kiukweli na dhambi zetu, na kukubali kwamba tumekosa.
5. Ni lazima tutubu na kuamini kuwa Mungu atatusamehe, hata kama tumekosea baada ya kuwa wafuasi.

**Vifungu vya kusoma:** Yakobo 1:12-27, Warumi 6, Warumi 7:14-25

**Mistari ya kushika:** Yakobo 1:14, 15

“Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti”.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## UBATIZO

**SOMO:** Yohana 3

Baada ya kufufuka na kutoka kaburini, na muda mfupi kabla ya kupaa kwenda mbinguni, Bwana Yesu Kristo alisema ifuatavyo kwa mitume wake:

“Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini, atahukumiwa” (Marko 16:15, 16).

Mambo mawili yako wazi sana katika maneno haya:

1. Kabla mtu yeyote hajaweza kuamini na kubatizwa, ni sharti aijue ile Injili aliyoifundisha Yesu, na kuelewa Habari Njema ya Ufalme wa Mungu.
2. Hakuna ambaye anaweza kujifurahisha mwenyewe kuhusu Ubatizo. Ubatizo sio kitu ambacho tunaweza kukifanya kama tukijisikia; ni cha lazima! Kama mtu hakuamini na kubatizwa, huyo yuko katika hukumu ya kifo; hana tumaini la uzima ujao.

Kutubu kunaanza kabla ya kubatizwa, mtu anapoisikia (au kuisoma) Injili na kuelewa. Injili inaibadilisha namna yake ya kufikiri na kuanza kuacha kufikiri kikawaida. Anaanza kufikiri kwa namna ya Mungu; kwa namna Mungu anavyotaka.

Ubatizo ni namna aliyoichagua Mungu kwa ajili yetu kuanza maisha mpya. Tunapomgeukia, tunaitii amri yake kwamba tubatizwe, dhambi zetu zinasamehewa, na tunaanza maisha mapya mbele yake.

### Yesu alitupa kielelezo

Yesu hakuwahi kufanya lolote baya. Hakuwa na haja ya kubatizwa ili dhambi zake ziweze kusamehewa, kwa kuwa hakutenda dhambi. Hata hivyo, katika Mathayo 3:13-17 unaweza kusoma vile Yesu alivyoshuka katika mto Yordani, na kubatizwa mtoni humo na binamu yake, Yohana.

Yohana alitambua kuwa Yesu hakuwa na kosa, na akasema hakuwa akistahili kumbatiza. Ilikuwa ni kweli tupu, lakini Yesu alimwambia: “Kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote” (Mathayo 3:15).

Kwa kubatizwa, Yesu ametupa kielelezo cha kufuata.

### Ubatizo unamaanisha nini?

Uligundua katika hicho kifungu cha Mathayo kuwa, Yesu alibatizwa ndani ya mto Yordani, na baada ya hapo, “**Akapanda kutoka majini?**”

Kuwafanya watoto kuwa Wakristo kwa kuwanyunyizia vimaji au kuwaosha vichwa hakupo kabisa katika Biblia.

Tunafundishwa waziwazi kuwa, kuamini ni lazima kuje kabla ya kubatizwa. Mtoto mdogo anawezaje kuamini, kabla hajawa mkubwa wa kutosha kuelewa?

Wayunani (Wagiriki) walitumia neno linalotafsiriwa ‘kubatiza’ katika Kiswahili, walipokuwa wakiweka nguo rangi. Kitambaa (au nguo) ‘kilibatizwa’ kwa kutumbukizwa chote kwenye maji. Hakuna kipande katika nguo hiyo kilichoachwa nje, ili rangi ikolee.

Biblia inapoongelea Ubatizo inamaanisha kutumbukizwa mzima-mzima katika maji. Kuna maana yake nzuri kwa kitendo hiki cha kuzikwa mzima ndani ya maji na baada ya hapo kuibuka, kama tutakavyoona baadaye.



### **“Tubuni mkabatizwe”**

Kama tulivyokwishaona, huu ulikuwa ndio ujumbe wa Yohana Mbatizaji. Injili inawataka watu wabadili fikra zao na maisha yao, na wamgeukie Mungu. Hii ndio Biblia inayoita ‘toba’.

Petro aliutoa ujumbe huo kwa Wayahudi waliomsulubisha Yesu, katika siku ya Pentekoste baada ya Yesu kupaa. Walikuwa wameifuata njia potofu; hawakuwa wamemtambua Yesu wa Nazareti kuwa alikuwa Mwana wa Mungu.

Walipogundua kosa walilofanya, waliwauliza mitume: “Tutendeje, ndugu zetu?” Tunaambiwa: “Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu” (Matendo 2:38).

### **Ubatizo wa mtume Paulo**

Mtume Paulo ni mfano mzuri wa kuelezea jinsi ambavyo toba inavyomfikisha mtu katika Ubatizo. Paulo alikuwa akiendelea katika njia mbaya; alikuwa akiwatesa waliokuwa wafuasi wa Yesu. Hakuamini ya kuwa Yesu alikuwa kikweli ni Mwana wa Mungu.

Paulo alipokuwa akisafiri kwenda Dameski kuwakamata na kuwatesa Wakristo huko, Bwana Yesu alimtokea na kusema naye. Paulo alipomwona, alijifikiria tena. Alimtambua sasa Yesu alikuwa ni nani.

Paulo alipokuwa ametambua alivyokosea, aliyatoa maisha yake yote kumfuata Yesu. Yesu alimtuma mfuasi wake mmoja aliyetitwa Anania kwa Paulo, na Anania alimsaidia aweze kuona tena, na kumwagiza abatizwe (Matendo 9:17,18). Kwa hiyo Paulo alipouamini ukweli aliomhusu Yesu, alisikitika kwa mabaya aliyofanya, na kuanza maisha mapya kwa kubatizwa.

Kuna maelezo mengi katika Matendo ya Mitume, ya watu walioamini na kuigeukia njia ya Mungu na wote walibatizwa.

### **Habari ya towashi wa Kikushi**

Hebu isome hii katika Matendo 8:26-40. Huyu towashi alikuwa ni mtu wa heshima; mtu mkubwa. Alikuwa amekwenda Yerusalemu kumwabudu Mungu. Alipokuwa ameondoka kurudi nyumbani, alikuwa akisoma kutoka katika Isaya 53, ambapo mateso na kifo cha Masihi kinaongelewa. Hakuelewa anachosoma; kifungu kilikuwa kikisema:

“Aliongozwa kwenda machinjoni kama kondoo, na kama vile mwana-kondoo alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya. Vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake. Katika kujidhili kwake hukumu yake iliondolewa. Ni nani atakayeeleza kizazi chake? Kwa maana uzima wake umeondolewa katika nchi”

(Matendo 8:32,33).

Ghafla alijewa na mfuasi aliyekuwa akiitwa Filipo, ambaye Mungu alikuwa amemtuma kumsaidia. Filipo alimuuliza kama alikuwa akielewa alichokuwa akikisoma, na towashi alimjibu, “Nitawezaje kuelewa, mtu asiponiongoza?”

Filipo alianza kumfafanulia kifungu hicho, na kumhubiria habari za Yesu. Mara walipofika kwenye maji, towashi alimwambia, “Tazama, maji haya; ni nini kinachonizuia nisibatizwe?”

Hebu liangalie jibu la Filipo kwa umakini. Alimwambia: “Ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana”.

Baada ya hapo, tunaambiwa, **wakatelemka wote wawili majini**; kwa hiyo lisingeweza kuwa jambo la kunyunyizia vimaji. Hapo Filipo akambatiza huyo towashi. Baada ya hapo tunaambiwa, walipopanda kutoka majini, Filipo alitoweka, na Mkushi huyo akaendelea zake akifurahi. Alikuwa ameigundua Njia ya Uzima.

### **Habari ya akida wa Kirumi**

Hebu isome habari hii katika Matendo 10. Akida Kornelio alikuwa, “Mtu mtauwa, mchaji wa Mungu, yeye na nyumba yake yote, naye alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi, na kumwomba Mungu daima” (ms.1,2).

Unaweza kufikiri hakukuwa na chochote zaidi cha yeye kufanya kwa jinsi alivyokuwa mwema; lakini kilikuwapo. Mungu alimtuma malaika kwa Kornelio, na malaika akamwambia Kornelio amwagizie mtume Petro aje, ambaye, “Atakuambia (Kornelio) yakupasayo kutenda”.

Sasa Petro, akiwa ni Myahudi, asingeweza kamwe kuingia katika nyumba ya mtu wa kimataifa (asiye Myahudi). Lakini Mungu alikuwa amesema naye kwa njia ya maono, na kumwambia aende na watu waliotumwa na Kornelio kwake. Ni Wayahudi tu waliokuwa wameitwa kwa habari ya Injili, mpaka wakati huo.

Petro alipofika nyumbani kwa Kornelio, alimkuta akida huyo akimngojea na familia yake na marafiki. Alimkaribisha Petro na kumwambia juu ya malaika aliyemtembelea, na kumwambia:

“Basi sasa sisi sote tupo hapa mbele za Mungu, tupate kuyasikiliza maneno yote uliyomriwa na Bwana”  
(ms. 33).

Petro aliwaambia watu waliokuwa hapo juu ya Yesu; maisha yake, kifo na ufufuko wake. Kabla hajamaliza kusema, karama ya Roho Mtakatifu iliyokuwa imetolewa kwa waumini wa Kiyahudi tu, iliwashukia wale waliokuwa pale wakisikiliza. Hakukuwa na shaka sasa kuwa, Mungu alikuwa amewakubali. Kwa hiyo hatua ya muhimu ya lazima ilifuata. Petro alisema:

“Ni nani awezaye kuzuia maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi? Akaamuru wabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo” (ms. 47, 48).

**Somo linaeleweka:** Hata wanaoishi kwa imani; watu wanaomcha Mungu, wanaweza tu kuwa na sehemu katika ushirika na Kikristo kwa kubatizwa. Ujumbe ni kwamba:

- Ni lazima kwanza watu waupate ujumbe wa Injili.
- Wauamini kwa mioyo yao yote.
- Ni lazima waondokane na kufikiri wanavyojifikiria, na watake kuifuata namna ya Mungu.
- Ni lazima baada ya hapo wabatizwe.
- Kwa kufanya hivyo wanaanza maisha mapya katika Kristo.

## Maana ya Ubatizo

“Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima” (Warumi 6:4).

Bwana Yesu alisulubiwa na mwili wake ulilazwa kaburini. Baada ya siku tatu, Mungu alimfufua.

Tukielewa kuwa Bwana Yesu aliteseka na kufa kwa ajili yetu, kama tuna hekima, tutasema kama Wayahudi walivyosema katika siku ile ya Pentekoste, “Tutendeje?” Jibu ni lile lile hata leo: “Tubuni, mkabatizwe”.

**Maana halisi ya kubatizwa:** Kama mwili wa Yesu ulivyolazwa katika kaburi, katika Ubatizo mwili wako unazikwa kwenye maji. Tunakuwa tumezikwa ‘pamoja naye’. Kwa kufanya hivi tunaonesha kukiri kwamba tunastahili kufa kwa sababu ya dhambi zetu, na ni ishara ya kufa na Kristo. Na kama alivyofufuka na kutoka kaburini, nasi tunaibuka katika maji. Huku ni kuzaliwa upya, na kuanza namna ya maisha mapya.

## Kuzaliwa upya

Myahudi mmoja aliyekuwa akiitwa Nikodemo, siku moja alikuja kwa Yesu usiku kumuuliza kuhusu mambo anayofundisha. Yesu alimwambia, “Ni lazima uzaliwe tena”. Nikodemo alifikiri hili haliwezekani, na ni kweli ni hivyo, kama ukiyachukua maneno ya Yesu bila kuelewa maana aliyokuwa nayo.

Yesu alikuwa akisemea kuzaliwa upya kunakotokea katika kubatizwa. Alimwambia Nikodemo: “Amini, amini, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu” (Yohana 3:5).

Kumbuka maneno tuliyoanza nayo: “Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa”. Watu wote ni wadhambi, na dhambi inatupeleka kwenye mauti. Kifo ni mwisho wa uhai, na hakuna lolote la kutazamia mbele ya hapo. Hakuna tumaini mpaka tunapokuwa tumezaliwa upya kwa njia ya Ubatizo.

### **Maisha mapya**

Kuamua kubatizwa ni uamuzi wa maana kuliko uamuzi wowote mwingine mtu yeyote anaoweza kuufanya. Sio kitu cha kuchukulia juu-juu tu.

**Kabla ya kubatizwa:** Ni lazima tuelewe na kuyaamini mafundisho ya kweli ya Biblia.

**Baada ya kubatizwa:** Ni lazima tupambane na dhambi, na kujitahidi kutii maagizo ya Mungu na kumtumikia.

Tunaweza tu kufanya hili kama tunalisoma Neno la Mungu. Itatubidi tuache kufanya mambo ambayo tunajua yataamchukiza Mungu. Hili litakuwa na maana ya kutumia muda mdogo zaidi na watu wasiomjali Mungu, hata kama walikuwa marafiki wa karibu, kwa kuwa wanaweza kutuvuta mbali na Mungu. Itakuwa ni jitihada za kila siku, lakini itakuletea zawadi nono sana. Bwana Yesu alisema:

“Kila mtu aliyearcha nyumba, au ndugu wa kiume au wa kike, au baba, au mama, au watoto, au mashamba, kwa ajili ya jina langu, atapokea mara mia, na kuurithi uzima wa milele” (Mathayo 19:29).

### **Muhtasari**

1. Mungu ametuamuru tubatizwe.
2. Ubatizo ni kuzamishwa (kuzikwa) kwenye maji.
3. Ni ishara ya kufa na Kristo, na kuibuka katika maji ni mwanzo wa maisha mapya.
4. Tunapobatizwa tunaanza maisha mapya ‘katika Kristo’ (Warumi 6:3,4).

**Vifungu vya kusoma:** Soma tena masimulizi katika Matendo 8, 9 na 10. Soma pia Warumi 6.

**Mistari wa kushika:** Warumi 6:3,4.

“Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima”.

## MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

*Karatasi ya maswali: namba 8*

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa 'Kazi ya ziada' unaweza kulijibu swali kama ukipenda, au kuliacha kama unaona huliwezi. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

### MASOMO: 28 – 31

28. A. Vifungu vifuatavyo vinatuambia nini juu ya malaika?

- a) Mathayo 26:53
- b) Matendo 12:5–10
- c) Waebrania 1:7
- d) Luka 1:19

B. Ni sahihi au si sahihi?

- a) Malaika wanaweza wakawepo mbele ya Mungu.
- b) Malaika kuna wakati wanaonekana kama watu.
- c) Wapo malaika wanaofanya dhambi/ wanaokosea.
- d) Malaika kamwe hawaoi.
- e) Malaika hawawezi kuongea.
- f) Malaika hawafi.
- g) Malaika wanawaepusha waumini wasitende dhambi.

29. A. Watu katika vifungu vifuatavyo wanaelezwa kuwa wana 'pepo'.

- a) Mathayo 9:32 – 34
- b) Mathayo 12: 22 – 45
- c) Mathayo 17:14 – 27

Kutokana na maendeleo ya kisayansi ya sasa kuhusiana na tiba, tusingewaelezea kwa namna hiyo. Tugesema wana matatizo gani?

B. Kwa nini Yesu alimwita Petro 'Shetani'?

C. Wapo watu wanaofikiri shetani ni malaika aliyetupwa kutoka juu kutokana na uovu wake. Unalifikiriaje wazo hilo?

D. Ni uongo gani ambao nyoka alimwambia Hawa katika Mwanzo 3?

30. A. Ibilisi ni nini?

B. Yesu aliziharibuje kazi za Ibilisi?

C. Iandike Mathayo 15:19. Msitari huo unatufundisha nini juu yetu wenyewe?

D. Ni kwa nini tunahitaji kutubu?

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## NDOA YA KIKRISTO

SOMO: 1 Wakorintho 7

Ndoa ni makubaliano ya mwanamume mmoja na mwanamke mmoja kuishi pamoja. Haitoshi tu kuwa na 'kaya' moja. Watu hao wawili ni lazima wajioneshe hadharani kuwa wanakuwa mume na mke, kwa hiyo makubaliano yao yanafanywa mbele ya mashahidi. Lakini, ndoa na Kikristo si hivyo tu.

Kwa ndoa ya Kikristo, ahadi wanazotoa wanaoana mbele ya wanaoshuhudia, zinafanywa pia mbele ya Mungu, na zinakuwa za kudumu. Mungu anachukizwa na kuachana (Malaki 2:16). Kama inawezekana, ni vizuri kuisajili hiyo ndoa Serikalini, muweze kupata na cheti cha ndoa.

Mpango wa Mungu ni kwamba mume mmoja na mke mmoja waishi pamoja wakati wote

- ✚ Mungu alipomuumba mwanamke awe 'msaidizi wa kufanana' na mume (Mwanzo 2:18), alitaka wasaidiane kwa kila mmoja kumjali mwenzake kwa kila hali: kiroho, kimwili na kifikra.
- ✚ Mungu aliposema ya kuwa wawe 'mwili mmoja' (Mwanzo 2:24), alionesha kuwa walipaswa wawe wamoja, mmoja kwa mwingine: waaminifu, wanaoelekeana, wakweli na wanaotegemeana wakati wote.
- ✚ Mungu alipowabariki Adamu na Hawa na kuwaagiza wazae na kuongezeka (Mwanzo 1:28) alikuwa akionesha kuwa, ndoa iliyo imara inatoa fursa nzuri ya watoto kukulia ndani yake.

Hata hivyo, sio kila mtu analazimika kuo au kuolewa. Yesu Kristo hakuo, na pia, kwa kadri tunavyojua, na mtume Paulo naye, ingawa alisema angeweza kuwa na mke kama angetaka. Ukweli ni kwamba, baadhi ya watu wameumbwa kwa namna ambayo wanapendelea kubakia wenyewe, wakati wengine wanapenda kuwa katika ushirika na msaada wa mwenzake; wa mume au mke.

Paulo aliwashauri waumini waliokuwa katika Korintho akiwaandikia kuwa, waoe (au kuolewa) tu kama walikuwa hasa na haja ya kufanya hivyo. Wapo watu ambao wanaweza kumtumikia Mungu vizuri zaidi wasipooa au kuolewa ( 1 Wakor. 7:32-35), wakati wengine wanahitaji wenza (ms. 2-9). Yote yanategemea tulivyo kila mmoja kimwili na kimawazo.

Ndoa ni mpango aliouweka Mungu. Sio njia rahisi ya kumpata mtumishi wa ndani bure, au kumpata mwanamume wa kukutunza. Kuna kanuni muhimu za kujua na za kuzingatia kama ndoa hiyo itakuwa ni ya kupendeza mbele ya Mungu.

Tutazipitia kuanzia mvulana anapofikiria kumpata mke, au msichana anapoamua kutaka kuolewa. Kuna somo la ziada litashughulikia mazingira tofauti yanayoweza kujitokeza, kutokana na mila za ndoa za kijadi na tofauti zingine za kimienendo.

**Ngono kabla ya ndoa**

Kitu cha kwanza kuelewa ni kwamba, kujamiiana ni kitu alichokiweka Mungu, lakini hapendi tendo hilo lifanyike nje ya ndoa.

Biblia inalaani matumizi mabaya ya ngono. Kufanya mapenzi kabla ya ndoa na nje ya ndoa, umalaya, ufiraji na ubakaji, ni vitendo vinavyoshutumiwa vibaya sana. Sehemu pekee iliyo sahihi na muafaka ya ngono ni kwa walioana.

**Biblia inasema:** "Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazini, wala wafiraji, wala walawiti...." (1 Wakorintho 6:9,10).

Kama huko nyuma tulikuwa tumefanya mambo hayo ya kijinga, ni lazima sasa tuache, tutubie dhambi hizo, na kumwomba Mungu atusamehe. Kwa kubatizwa kwetu katika jina liokoalo la Yesu, tunaweza kupata mwanzo mpya wa maisha unaompendeza Mungu.

Mapenzi ndani ya ndoa ni tuzo inayotoka kwa Mungu. Ni mbaraka uliowekwa kusudi, pamoja na mengine, wapatikane watoto ndani ya upendo na uangalizi wa baba na mama. Hakuna amri inayosema Wakristo wanapaswa kupata watoto wengi iwezekanavyo; baadhi ya makanisa yanakazia hili tu ili kuongeza idadi ya wafuasi wao.

Wazazi watapaswa kuifikiria hali ya familia yao kabla ya kuamua wapate watoto wangapi. Kama ilivyo kwa mambo mengine katika familia, mume na mke inawabidi wajaadili jambo hili na kufikia makubaliano juu ya ukubwa wa familia wanayoitaka. Lakini kufanya mapenzi ni njia pia aliyoitoa Mungu, ya mume na mke kuoneshana upendo walio nao mmoja kwa mwingine, kwa namna iliyo ya kipekee sana (1 Wakorintho 7:3-5).

### **Kutafuta mume au mke**

Wakati mfuasi wa Kristo anapotaka kuo au kuolewa, atataka amfahamu huyo anayemtaka ni mtu wa namna gani. Biblia inatoa amri iliyo wazi ambayo watu wanapaswa kuitii.

Muumini ni sharti aoe (au aolewe na) muumini
--

Kama wawili wanawajibika kuishi pamoja katika ushirika wa kiroho, ni lazima imani yao iwe moja. Mtume Petro anawaita: ‘warithi pamoja na neema ya uzima’ (1 Petro 3:7).

Ni lazima wawe na uelewa wa pamoja wa kile Biblia inachofundisha. Muumini anayeo (au kuolewa na) asiyeamini, atapata ugumu na migogoro katika ndoa yake. Kwa maneno mtume Paulo aliyopewa na Mungu kuonya, anasema:

“Msifungwiwe, nira pamoja na wasioamini” (2 Wakorintho 6:14). Nira ni kitu kinachounganisha pamoja; ni mfano wa ndoa.

Na kuhusiana na wajane, anasema:

“Mwanamke hufungwa maadamu mumewe yu hai, lakini ikiwa mumewe amefariki, yu huru kuolewa na mtu yeyote amtakaye, **katika Bwana tu**” (1 Wakor. 7:39).

### **Maisha ya pamoja**

Mwanamume Mkristo anayejali, na mwanamke Mkristo anayejituma, ni mbaraka mkubwa kwao wenyewe, na kwa wale wanaomwabudu Mungu pamoja nao. Mume ni lazima ajitahidi kuufuata mfano wa Bwana Yesu Kristo, aliyekuwa kielelezo cha hali ya juu sana cha upendo wa kuwajali wote wale aliowakuta katika maisha.

Mtume Paulo alipokuwa akiwaandikia Waefeso alieleza kuwa, wanaume wanapaswa kuwa na mwenendo katika familia, kama ule Yesu aliokuwa nao kwa wafuasi wake:

“Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe; kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa; naye ni mwokozi wa mwili....Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake” (Waef. 5:23 – 25).

Kuwa kiongozi wa familia hakuna maana ya kuwa mume anaruhusiwa kujiweka juu ya kila mtu hapo, akitegemea kila kitu kifanywe kulingana na amri zake, na kusikilizwa wakati wote. Hivyo sivyo Yesu alivyowaongoza wanafunzi wake. Yeye alikuwa miongoni mwao kama ‘atumikaye’ (Luka 22:27). Aliyachukulia mahitaji ya wengine kama vile yalikuwa ya muhimu kuliko ya kwake mwenyewe.

Hili lina maana ya kuongoza kwa 'kuwa mfano'. Mume ana jukumu la kuelekeza na kudhibiti, kusimamia vipengere vyote vinavyohusu maisha ya familia, na kuyaongea mambo na wanafamilia wake kunapokuwa na maamuzi muhimu ya kufanywa.

Muhimu kuliko yote, mume ataiongoza familia yake katika kuabudu na kuifundisha, katika maombi ya familia na usomaji wa Biblia wa kila siku. Kumhusu Ibrahimu, Mungu alimsifu akisema hivi:

"Nimemjua ya kwamba ataamuru wanawe, na nyumba yake baada yake waishike njia ya BWANA, wafanye haki na hukumu" (Mwanzo 18:19).

Kwa hiyo mume ni lazima ajichukulie kuwa ni mkuu juu ya familia yake, anayewajibika juu ya maisha yao mbele ya Mungu, na aichukulie nyumba yake kama ni 'kanisa dogo' (na kweli, kama hakuna waumini wengine katika mazingira hayo, hiyo ndio fursa pekee atakayokuwa nayo ya kuweza kumwabudu Mungu akiwa na wengine).

Anapaswa kuishirikisha familia yake katika ibada na kuiongoza katika Njia za Mungu; ingawa ni wale tu waliobatizwa watakaoshiriki naye mkate na divai.

Katika baadhi ya nchi, mifumo wa maisha ya kazi, kimila, iko katika namna ambayo wanawake ('wake') katika familia ndio wanaofanya kazi ngumu karibu zote. Ndoa ya Kikristo ni ushirika, na mume anayependa kuzishika amri za Mungu, atapenda kushiriki katika kazi zote ngumu katika maisha, na mke wake, na familia.

Atapenda, "Kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu" (1 Petro 3:7), na kumpenda kama anavyojipenda mwenyewe (Waefeso 5:28). Namna hii ya ushirika wa kiroho unaofanya kazi, utakuwa kitu cha furaha kwa familia yote. Kufanya kazi kwa pamoja na kushirikiana katika majukumu, kutakuwa pia ni njia nzuri sana ya kuwaonesha majirani jinsi Ukristo wa kweli ulivyo.

### **Mke Mkristo**

Mpaka sasa tumeangalia wajibu na majukumu ya mwanamume ('mume') Mkristo, lakini anaweza tu kuyafanya mambo hayo kwa mafanikio kama ana mke aliye tayari kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Kunaweza kusiwe na wanawake/wasichana wanaoamini wanaoishi karibu, kwa hiyo anayetaka 'kuwa mume' atalazimika kumtafuta 'mwenza' mwenye kupenda kujifunza Injili ya kweli, aliye tayari kuipokea njia ya wokovu inayofundishwa katika Biblia, kwa kuamini na kubatizwa. Baadhi ya wasomaji wa masomo haya watakuwa wameshaoa (au kuolewa na) wenza ambao hawajifunzi nao mafundisho haya; hili ni jambo tutakaloliangalia katika somo linalokuja.

Lakini mtu anayetafuta mchumba wa kuoja atakuwa ameelewa haja ya kupata mwenza mwenye mwamko wa mambo ya kiroho, mwanamke atakayeweza kushirikiana naye katika mambo yote ya maisha yake katika Kristo. Ni hivyo hivyo pia kwa mwanamke au msichana Mkristo anayetaka kuolewa.

Hawa aliumbwa awe msaidizi wa kumfaa Adamu, na huu ni mpango ambao wanawake walioolewa wote wanapaswa kuufuata. Kuna picha nzuri ya ajabu inayomhusu 'mke mwema' katika Methali 31. Anasemewa kuwa ni mke ambaye moyo wa mumewe humwamini, na ambaye, "Humtendea (mumewe) mema, wala si mabaya, siku zote za maisha yake" (Meth. 31:11,12). Anakuwa mchapa-kazi kwa ajili yake mwenyewe na familia yake, na mkarimu na mwelewa, na muhimu zaidi, ni "Mwanamke amchaye BWANA" (ms. 30).

Wanawake wengi waaminifu katika Maandiko waliishi kwa namna hiyo. Waliwatia moyo na kuwasaidia waume zao, huku wakiwaachia wawaongoze. Sara alikuwa miongoni mwao, na alijinyenyekeza kwa Ibrahimu, kiasi kwamba alimchukulia kuwa ni 'Bwana' wake, kwa kumtii katika mambo yote (1 Petro 3: 1-6). Mume naye asiitumie vibaya heshima hiyo. Katika familia ya Kikristo, yeye na mke wake ni: "Warithi pamoja wa neema ya uzima" (ms. 7).

Mtume Paulo alimuagiza Tito na wazee wa kike:

“Wawatie wanawake vijana akili (‘wawafundishe’), wawapende waume zao, na kuwapenda watoto wao, na kuwa wenye kiasi, kuwa safi, kufanya kazi nyumbani mwao, kuwa wema, kuwatii waume zao wenyewe; ili neno la Mungu lisitukanwe” (Tito 2:4, 5).

Inawezekana kuwa ajabu kuwataka wanawake wawapende waume zao, lakini hili sio jambo ambalo wanandoa wote wanafanikiwa. Wapo wanaoishi pamoja kwa kujinufaisha tu wenyewe na kupata watoto, lakini mara nyingi si hasa kama wanapendana, na wala hawafanikishi kuwalea watoto wao vyema.

Lakini, maisha katika familia ya Kikristo yanamshirikisha Mungu. Kwa ajili hiyo, wakina-mama wana jukumu la kutekeleza katika kuonesha upendo kwa familia nzima; mguso-wa-upole ambao ni wao tu wanaoweza kuutoa, katika kuelekeza kwa ukaribu na kuwafundisha watoto, na hasa wanapokuwa wadogo. Andiko linasema, mzazi ana wajibu wa kumlea: “Mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee” (Methali 22:6).

Hili ni adili la Ki-Mungu: Wanandoa wanaoamini, wanaishiriki mibaraka waliyopewa na Mungu, huku wakiilea familia yao kukua katika kuijua kweli ya Mungu. Kwa namna hiyo, watoto wao na wao wenyewe, wote watakuwa mbaraka kwa wote watakaokutana nao. Katika maisha yao ya pamoja na ya furaha katika Kristo, wengine wataona mbaraka mkubwa wanaoufurahia, na hivyo Mungu atatumizwa katika mambo yao yote.

#### **Muhtasari**

1. Ndoa imewekwa na Mungu, na ni kitu kizuri na cha haki.
2. Wapo watu wanaoridhika kubaki wenyewe, na hili pia ni zuri na la haki. Kuka hivyo kunaweza kumwongezea mtu fursa ya kumtumikia zaidi Mungu.
3. Kufanya mapenzi ni mbaraka wa Mungu, lakini ni ruhusa tu kwa mume na mke.
4. Ngono nje (au kabla) ya ndoa ni dhambi; ni lazima iepukwe.
5. Ndoa inaruhusiwa tu kufanywa na mtu aliye wa imani yako; muumini aliyebatizwa.
6. Waume wanapaswa kuwatunza wake zao na watoto wao, na kuongoza familia zao katika mambo yote, na hasa katika ibada kwa Mungu, kusoma Biblia na kuomba.
7. Wanawake (‘wake’) ni lazima wawatii waume zao na kuziongoza familia zao katika Njia za Mungu.

**Vifungu vya kusoma:** Waefeso 5, Methali 31:10-31, Timotheo 3, Wakolosai 3:12-25.

**Mistari wa kushika:** Mathayo 19:5,6

“Kwa sababu hiyo mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe”.



## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## MATATIZO KATIKA NDOA

SOMO: Mathayo 19

Mpango wa Mungu kwa ndoa ya Kikristo ni kwa waumini wawili, wa kike na wa kiume, kuishi pamoja kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Lakini, kwa sababu ya mazingira yanayojitokeza, imekuwa sio rahisi wakati wote kulifikia lengo hilo. Matatizo yanatokea, na somo hili litayatazama baadhi; yaliyozoeleka sana. Tunakushauri uwasiliane na mkufunzi wako, kuweza kupata msaada zaidi wa kibinafsi juu ya haya na shida zingine.

**Ndoa na Asiyeamini**

Muumini ni lazima aoe au aolewe na aliye muumini (2 Wakorintho 6:14). Lakini ni vipi kuwahusu wale ambao wanakuwa wamekwishaoa au kuolewa wakati wanapokuja kulielewa kusudi la Mungu? Watengane, au waendeleo kuishi na wenza wao wasioamini?

Hili lilikuwa ni tatizo la kawaida katika karne ya kwanza. Kwa kadri Injili ilivyohubiriwa na watu kuja kuisikia na kuiamini, walibatizwa katika Jina liokoalo la Yesu. Lakini, mara nyingi familia zao zilibakia katika kutokuamini na kulitokea migawanyiko ndani ya familia. Linapotokea hili inakuwaje; waumini wanajitenga na kutawanyika, au wanaendelea kukaa hapo na kusuluhisha migogoro yao?

Ushauri wa Agano Jipya unaonesha jinsi maisha ya ndoa yalivyo ya muhimu mbele ya Mungu. Tunapooa au kuolewa, tunakuwa na wajibu juu ya wengine. Ni kosa kuwaacha hao; badala yake ni wajibu kujitahidi kuifanya ndoa iendeleo, na kuyaweka mambo tunayoamini katika matendo ndani ya familia.

Kwa hiyo, Biblia inatuambia tuendeleo na maisha pamoja na wenza wetu kama tunaweza, na kwa mwenendo wetu wa Kikristo tunaweza kuwaonesha waume zetu au wake zetu vile upendo wa Mungu ulivyo, katika Kristo Yesu. Maandiko yanasema:

“Ninyi wake, watiini waume zenu kusudi, ikiwa wako wasioamini Neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake zao, pasipo lile Neno; wakiutazama mwenendo wenu safi, na wa hofu (wa kumcha Mungu)” (1 Petro 3:1,2).

“Mwanamke, ambaye ana mume asiyeamini, na mume huyo anakubali kukaa naye, asimwache mumewe. Kwa maana yule mume asiyeamini hutakaswa katika mkewe; na yule mke asiyeamini hutakaswa katika mumewe. Kama isingekuwa hivyo, watoto wenu wangekuwa si safi; bali sasa ni watakatifu. Lakini yule asiyeamini akiondoka, na aondoke” (1 Wakorintho 7:13-15).

**Maandiko yanatufundisha kuwa, kila linalowezezana lifanywe kuwafanya waliooana waendeleo na maisha ya pamoja.**

Mungu atachukuliaje? Tunajifunza kuwa, Mungu atachukulia ndoa ile iliyofanywa kabla yeyote kati yao hajaufahamu ukweli wa Kibiblia, kuwa ni mahusiano matakatifu, na watoto hatawachukulia vibaya. Changamoto ni jinsi ya kujaribu kuueneza ukweli wa Kikristo ndani ya familia, kwa aliyeamini kuwa kielelezo cha mwenendo mwema kibinafsi.

Kama matatizo ndani ya ndoa yanajitokeza, ni muhimu yakabiliwe kiusahihi kwa kukumbuka kuwa, kuna wajibu katika mazingira yoyote yale, kuifanya ndoa iendeleo. Hili lina maana ya kukubali jambo, hata kama haliridhishi sana. Hivi ndivyo Yesu alivyofanya alipokufa ili tuweze kupata tumaini la wokovu.

Biblia inalinganisha ndoa na uhusiano uliopo kati ya Kristo na kanisa (Wakristo), kwa hiyo mfano wake unaweza kutupa nguvu matatizo yanapozuka. Talaka inaonekana haraka kama suluhu mambo yanapokuwa magumu, lakini ni lazima kukumbuka kabla ya kuchukua hatua kama hiyo kuwa, Mungu anasema:

"Mimi nakuchukua kuachana" (Malaki 2:16)

### **Ndoa kati ya Waumini**

Mungu alipanga ndoa iwe ni mahusiano ya kudumu maisha yote. Ahadi katika kuoana hazifanywi ili zivunjwe; ni ahadi za kudumu kwa maisha yote kwa wanandoa. Mmojawao katika ndoa anapokufa, mwenzake aliyebaki anakuwa huru kuo au kuolewa tena (Warumi 7:2,3).

Kanuni ya kipekee iliyo tofauti inakuja tu pale mmojawao anapokuwa sio mwaminifu kwa mambo ya ngono. Kuna wakati Bwana Yesu aliulizwa alikuwa akifikiri nini kuhusu ndugu zake Wayahudi walivyokuwa wakitoa talaka (pengine kirahisi). Waliomuuliza walitaka kujua kama Yesu alifikiri ndoa iliyofutwa, ilikuwa imefutwa hivyo-hivyo mbele ya Mungu au inakuwaje.

Bwana Yesu aliwarejesha wasikilizaji wake kwenye ndoa ya kwanza kabisa, kwenye Kitabu cha Mwanzo, Sura ya pili na kuwakumbusha kinachosemwa, kuwa: "Aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe" (Mathayo 19:6). Tunaona hapa ya kuwa, Mungu anachukulia ndoa kama kitu **kilichoungwa**. Alipoendelea kuulizwa, Yesu alisema:

"Kila mtu atakayemwacha mkewe, isipokuwa ni kwa sababu ya uasherati, akaoa mwingine, azini; naye amwoaye yule aliyeachwa azini"

(ms. 9).

Ndoa ya waumini wa Kikristo, kwa hiyo, ni ya kudumu maisha yote. Kama mmojawao anakuwa mzinzi; anafanya mapenzi na mtu mwingine, ndoa yao inahatarika. Lakini ni muhimu bado kujaribu kuifanya iendeleo.

Nabii Hosea alikuwa na mke asiyekuwa mwaminifu, lakini alijitahidi sana kumrudisha amrudie. Tunapaswa kukumbuka kuwa, ni lazima tuwe tayari kusamehe baya alilofanya mweza wetu kinyume na sisi, kama tunataka Mungu naye atusamehe tunapofanya mabaya kinyume chake.

Kama mwenzake asiye mwaminifu hawezi kurudi, na hatimaye kunakuwa na kuachana, lazima hatua zichukuliwe kuhakikisha athari zake zinakuwa ndogo kwa wengine kwenye familia hiyo. Kama mwanandoa anafariki, na aliyebaki anaona inawezekana na inafaa kuishi mwenyewe, ni vizuri zaidi asioe au kuolewa tena.

### **Matala**

Wanaume wengi, hasa katika nchi za Kiislamu na kwa mila za Kiafrika, wanaweza kuwa ni wake wengi, wanapoupokea ujumbe wa Injili ya Kikristo. Wafanye nini: wajitenge na wake zao au waendeleo nao? Ndoa za wake wengi (matala), zilikuwepo pia enzi za kale kwenye Biblia.

Mfalme Daudi alikuwa na wake kadhaa. Mfalme Sulemani alikuwa na mamia ya wanawake na mahawara. Lakini mpango wa Mungu umekuwa wakati wote ukitambulika: Mungu alikusudia mume mmoja kwa mke mmoja waishi pamoja kama mume na mke.

Wakati wote mambo mengine yanapofanyika, mara nyingi yamesababisha zaidi matatizo na kuleta huzuni. Yesu aliweka wazi kuwa, ipo sasa njia ya namna moja tu inayokubalika ya kuishi pamoja, kwa kusema:

"Kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa mwili mmoja" (Mathayo 19:5).

Kwa hiyo, hakuna anayeweza kuchukua zaidi ya mke mmoja baada ya kuwa amebatizwa katika Kristo. Je, wale ambao wanao tayari wake kadhaa, inakuwaje? Ushauri wetu ni kuwa, yeyote ambaye anao wake zaidi

ya mmoja, aendelee nao; atambue kuwa bado anawajibika kwao wote. Aendelee kuwa mume mwema kwao, na baba wa watu wake wote wanaomtegemea.

Wakristo hawaachi au kukwepa majukumu yao wanapobatizwa; wanajikuta wakiwajibika hata zaidi kwa wategemezi wao. Hata hivyo, Ushirika wetu wa kueneza Injili wa Kikristadelfia (CBM) unashauri kuwa, kwa kuwa matala hayaendani sawasawa na maadili ya Kikristo, ndugu aliyeko kwenye matala hastahili kuwa ‘mzee-kiongozi’ kwenye kusanyiko la Kikristadelfia.

### Harusi

Matatizo yanaweza kutokea kama inafikiriwa kuwa sherehe kubwa ya harusi ni ya lazima, wakati vijana wenyewe ni wadogo; hawajawa na kitu. Hii ndio sababu katika nchi kadhaa watu wanaishi pamoja nje ya ndoa, wakitegemea kufunga ndoa watakapopata uwezo, lakini mara nyingi hawaufikii. Kwa wakati huo wote watoto wao wanawazaa nje ya ndoa, katika mfumo usioeleweka, na matatizo yapozuka inakuwa balaa. Muumini afanye nini?

“Muumini anapaswa kuoa au kuolewa kabla hajaanza kuishi na mwenzake. Kufanya mapenzi kabla ya ndoa ni dhambi. Biblia inasema: “Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinz Mungu atawahukumia adhabu” (Waebrania 13:4).

Kitu kinachohitajika tu ni kisherehe kidogo katika kumshirikisha Mungu, familia na marafiki, washuhudie kwamba watu wawili hao wameoana. Kama inawezekana, mwende mkaisajili ndoa hiyo Bomani (Serikalini), na kupata vyeti vya ndoa. Hakuna haja ya kuwa na vitu vya gharama kuhusiana na vyakula vinavyoliwa au mavazi, na haijalishi ni wapi sherehe inapofanyika.

Popote palipo na nafasi ya kutosha kuingiza hao watu wanaokuja kushuhudia, panatosha. Epuka kwenda Kanisani kuoana na mtu ambaye hayaelewi mafundisho ya kweli ya Biblia. Ahadi zinazotolewa mbele ya mashahidi, zinamaanisha kwamba wanandoa hao wataishi pamoja mbele ya Mungu kwa maisha yao yote. Usihusishe jambo hili la Kikristo na kanuni za ndoa zenye misingi yake katika upagani. Mkristo anapaswa kuachana na mambo ya kipagani.

Kunakuwa mara nyingine na matatizo kuhusiana na mahari kuwa kubwa, na inaweza kuchukua muda kwa kijana wa kiume kuweka pesa, mpaka zitoshe kwa ajili ya msichana aliyemchagua. Kama anamwoa msichana anayetoka katika familia ya Kikristo, hawapaswi kwa vyovyote kumtoza mahari ya juu, badala yake watapenda wawatie moyo wanandoa hao wanaoana, waweze kuanza maisha yao ya pamoja bila ya matatizo mengi.

Lakini kama mahari ni kubwa, hakuna la kufanya isipokuwa ni kwa mvulana anayeo kusubiri mpaka atakapokuwa na mahari inayotakiwa. Kwa wakati huo, yeye na mwenzake wanapaswa wabakie wasafi, wakijichunga na kuusubiria wakati watakapoweza kuoana.

### Kutafuta mume au mke mzuri!

Tatizo lililo gumu kuliko yote linaweza likawa kumpata mume au mke wa Kikristo anayefaa, na hasa kama wako waumini wachache tu wanaoishi katika mazingira husika. Kitu cha kwanza kukumbuka ni kwamba, ni hali ya kiroho ya huyo unayemtaka kuwa naye iliyo ya muhimu zaidi; zaidi kuliko anavyoonekana kimaumbile au mali aliyonayo. Mungu huutazama moyo, na sio sura ya nje, na sisi ndivyo tunavyopaswa kutazama (1 Samweli 16:7).

Ni lazima tuoe au kuolewa na mwenzetu wa imani moja; muumini aliyebatizwa.

Uchaguzi wa mume au mke unapaswa ufanywe kuwa jambo la maombi ya dhati. Ibrahimu alipata usumbufu mkubwa kwa ajili ya kumpatia Isaka mke anayemfaa, na tunaweza, kwa kuwa waangalifu, tukalazimika kufanya kama alivyofanya Ibrahimu; kwenda mbali.

**Mbaraka kutoka kwa Mungu**

Ndoa ya Kikristo sio kitu cha matatizo tu yanayongojea kutatuliwa, ingawa katika somo hili tumejadili matatizo kawaida yanayojitokeza. Kuoana, kwa upande mwingine, ni mbaraka mkubwa unaotoka kwa Mungu, wa kufurahiwa kwa pamoja.

Maisha ya kifamilia, kama watu wanayaelewa na kuyaishi inavyotakiwa, yana mazuri mengi na yanaweza kufanikisha mengi. Kwa sababu hiyo, ujio wa pili wa Yesu, anapokuja kuusimamisha Ufalme wa Mungu duniani, unafananihwa katika Maandiko na kuanza kwa maisha ya ndoa ya Kikristo. Andiko linasema:

“Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa harusi ya Mwana-kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari” (Ufunuo 19:7).

#### **Muhtasari**

1. Kusudi la ndoa ni kuwaweka pamoja mwanamume anayeamini na mwanamke anayeamini, waishi pamoja kwa maisha yao yote. Kama bado, tafuta ‘mwenzu’ anayeamini!
2. Kama tumekwishaoa au kuolewa wakati tunapompokea Kristo, ni lazima tubakie na wenzu wetu na kujaribu kuwaonesha Njia ya Mungu.
3. Ahadi tunazopeana wakati wa kufunga ndoa sio kitu cha mzaha; ni lazima ziheshimiwe. Kama baada ya jitihada kubwa bado ndoa inakwama, ushauri ni lazima utafutwe kwa wazee kwenye eklesia au kwa wakufunzi.
4. Kwa wale wanaoaa, mume mmoja kwa mke mmoja ndivyo inavyotakiwa. Endapo mwanamume ameshakuwa na zaidi ya mke mmoja wakati anapokata shauri, basi ni lazima abakie katika uaminifu kwa kuendelea kuwa mume wa wake zake wote. Asiongeze mke mwingine.
5. Oa au olewa kisheria mbele ya Mungu; mbele ya mashahidi, hata kama unachoweza kumudu ni kasherehe kadogo tu.

**Vifungu vya kusoma:** Mwanzo 24, Mathayo 5:31,32, Zaburi 128, 1 Timotheo 2

**Msitari wa kushika:** Waebrania 13:4

“Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzizi Mungu atawahukumia adhabu”.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

### WAJIBU WETU KWA TAIFA

**SOMO:** 1 Petro 2

**Angalizo:** Taifa ni nchi tunayoishi ndani yake (ambayo ndani yake kuna viongozi wake, sheria na taratibu zake).

Kwa nyakati zote katika historia, Mungu amekuwa akijiandalia watu ambao wanaelewa makusudi yake, na ambao watakuwa washiriki wa mibaraka ya Ufalme wake na kuufurahia Uzima wa Milele. Kwa nyakati za nyuma katika Agano la Kale, watu hao walikuwa wakiishi kama taifa moja ambalo ni Taifa la Israeli, na Mungu alikuwa ndiye Mfalme wao.

Kwa wakati huo hapakuwa na tatizo kati ya taifa na wananchi wake, kwa kuwa wote walikuwa wakihesabiwa kuwa ni waumini. Mambo yalibadilika, na sasa tunahitaji kutafakari wajibu wa Mkristo kwa nchi yake, na hasa kuhusiana na mambo ya kisiasa na migogoro ya kivita.

### Watu wa Mungu

Mungu bado anaendelea kujiandalia watu, na sasa ni kutoka katika mataifa yote. Ni watu watakaokuwa wa muhimu sana, kwa ajili ya mpango wake wa kuweka Ufalme wake katika dunia nzima. Mtume Yohana aliona kwa njia ya maono umati huo, na anauelezea kuwa, ulikuwa ni:

“Mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi na mbele ya Mwanakondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao, wakilia kwa sauti kuu wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwanakondoo” (Ufunuo 7:9,10).

Watu hao watakusanywa pamoja, wakati wa kurudi kwa Bwana Yesu Kristo duniani, kuanzisha ‘taifa’ jipya; taifa lake Mungu mwenyewe, na watatawala pamoja na Mfalme Yesu kwa miaka 1000 ya Ufalme huo katika dunia (Ufunuo 5:9, 10; 20:4).

Ufalme wa Mungu uliwahi kuwepo miaka mingi zamani, wakati wafalme walipotawala wakikikalia Kiti cha Enzi katika Yerusalemu na kutawala juu ya Israeli. Hili litatokea tena hapo Mfalme Yesu atakaporudi (Matendo 1:6; Luka 1:32, 33).

### Ufalme wa Mungu (nyakati za kale)

Miaka 3,500 iliyopita katika Mlima Sinai, Mungu aliwakusanya wana wa Israeli, waliokuwa ndio wametoroka tu kutoka Misri, na kufanya agano nao (Kutoka 19:1-8). Agano ni makubaliano. Walikuwa waishike Sheria aliyowapa kupitia kwa Musa, baada ya hapo wangeirithi nchi ya Kanaani; ambayo ni nchi ya Israeli leo.

Sheria za Mungu zilikuwa ndizo Sheria za kuliongoza taifa hilo. Baadaye, Mungu aliteua wafalme kwa ajili ya watu wake. Jeshi la mfalme, lilikuwa ni jeshi la Mungu, na vita vyake vilikuwa ni vita vya Mungu. Mfalme alikuwa hapo kwa ajili ya kufanya Mungu aliyomuamuru.

Baadaye haya yote yalibadilika. Wafalme waliisahau Sheria ya Mungu na kufuata mifano mibaya ya mataifa yaliyowazunguka, na hatimaye, Mungu aliamua kuusitisha Ufalme wake huo katika dunia. Kwa kuanzia, taifa la Ashuru lilibeba mateka makabila ya kaskazini ya Israeli (Ufalme wa Israeli), na baadaye Babeli iliuchukua mateka Ufalme wa kusini; Ufalme wa Yuda.

Watu hao walivyosambaa walikuwa wakimbizi wasio na kwao. Walijikuta wakiishi katika nchi zilizoabudu miungu wengine, ambayo sheria zao mara nyingi zilikuwa zikipingana na hizo za Mungu mmoja aliye wa kweli; Mungu wa Waisraeli.

Jinsi walivyoishi katika mazingira hayo, kuna umuhimu mkubwa kwetu kuelewa. Sababu ni kuwa, wale wanaokuwa watu wa Mungu kwa sasa, wanaweza nao kukabiliwa na changamoto za namna ya kuishi katika nchi walimo, zilizo na sheria ngumu na mambo yanayofanywa.

### **Kumtii Mungu au mwanadamu?**

Uzoefu wa Danieli na marafiki zake unatupa kielelezo kizuri cha namna ya kuishi katika mataifa tunamoishi kwa sasa. Walikuwa wamebebwa mateka na mfalme Nebukadreza wa Babeli alipoivamia Yuda na kuishinda Yerusalemu, kama miaka 600 Kabla ya Kristo. Kuanzia mwanzo wa maisha yao katika nchi ya kigeni, walionesha kutaka kumweka Mungu mbele katika maisha yao. Hebu tuone mifano ifuatayo:

<b>TATIZO</b>	<b>KILE DANIELI NA/AU RAFIKI ZAKE WALICHOFANYA</b>	<b>KILICHOTOKEA MWISHONI</b>
Danieli na rafiki zake walipewa chakula ambacho iliwezekana kilikuwa kimetolewa sadaka kwa sanamu (nyama iliyotambikiwa). Hawakukubali kuila, ingawa walijua hili lingemuudhi mfalme na maafisa wake.	Hawakuila ile nyama, badala yake waliomba wapewe mboga za majani.	Mungu aliwatunza na wakaonekana kuwa na afya bora kuliko wale wengine waliokula nyama (Dan. 1:15-17).
Nebukadreza aliwaamuru watu wote wawe wakiinama na kuisujudia sanamu aliyoisimamisha.	Marafiki watatu wa Danieli waligoma kuabudu kitu kingine chochote, ila Mungu tu.	Walitupwa ndani ya tanuru la moto, lakini Mungu aliwaokoa na hawakudhurika.
Maadui wa Danieli walitaka kumwangamiza, kwa kumshawishi mfalme mpya, mfalme Dario, apige marufuku maombi yote, mpaka yanapokuwa yameelekezwa kwake.	Danieli aliendelea kufanya alivyokuwa akifanya. Alimwomba Mungu madirisha yake yakiwa wazi.	Danieli alitupwa katika tundu la simba, lakini Mungu alimwokoia na hakudhurika.

### **Hii mifano inatufundisha:**

- ✚ Kumweka Mungu mbele katika maisha yetu.
- ✚ Kushikamana na imani yetu na kamwe tusirubuniwe.
- ✚ Kwamba Mungu peke yake ndiye wa kuabudiwa.

Lakini Danieli na marafiki zake hawakuwa watu wanaojitafutia matatizo. Hawakuwa wakitafuta fursa za kuzivunja sheria zinapoendana na Sheria za Mungu. Walikuwa watu watiifu sana kwa sheria, na walionekana bora kabisa kati ya watumishi wa mfalme na hata wakawa maafisa wakubwa kabisa serikalini, wakisimamia kazi za mfalme.

Huu ni mfano wa muhimu sana, kwa wote wale wanaomfuata Bwana Yesu Kristo. Pale sheria za nchi zinapoendana na Sheria ya Mungu, nasi tunapaswa tuwe watu tunaositii sheria za nchi. Sheria nyingi za nchi mara nyingi zinakuwa zinakwenda sawa tu na Sheria za Mungu. Mfano: usiibe, usiue, usiseme uongo, waheshimu wakubwa n.k. Kama Danieli, ni wazi nasi tutaonekana hakuna kosa kulingana na tunayofanya (Danieli 6:4, 5).

Wakristo ni lazima wazitii sheria za nchi zao, mpaka pale sheria hizo zinapokwenda kinyume na Sheria za Mungu.

### **Ufalme wa Mungu: katika siku za Yesu**

Kwa miaka kama 2000, watu wa Mungu wameishi katika nchi zilizo na sheria na mawazo yake zenyewe. Ilikuwa hivyo hivyo kwa Bwana Yesu mwenyewe; aliishi Israeli kwa wakati ambao taifa lake lilikuwa nchi ya utawala wa Kirumi, na ni kwa sheria zao aliteswa na kufa.

Lakini kamwe hakuwa mchochezi wa kisiasa, ingawa wengi kati ya Wayahudi wenzake walifikiri angekuwa. Hakujaribu kuiondoa mamlaka ya Kiyahudi iliyokuwa ikitawala, iliyokuwa ikitumia vibaya nafasi yake katika maongozi ya hekalu na katika mambo mengine. Na hakutaka kuwapindua Warumi.

Akiwa ameulizwa wakati fulani vile alivyokuwa akiiona mamlaka ya Kirumi, Yesu alionesha jinsi sarafu ya Kirumi ilivyokuwa na picha ya Kaisari; aliyekuwa Mfalme Mkuu wa Warumi. Kwa kuitumia hiyo sarafu, aliweka kanuni ya muhimu sana, akisema:

“Mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na Mungu yaliyo ya Mungu” (Mathayo 22:21).

Hili lina maana kuwa, ni lazima tulipe kodi zetu kama sheria inavyotaka. Paulo naye analiweka hili wazi katika Warumi 13:7.

Tunatakiwa pia tufanye kila kitu tunachoamriwa, mradi hakipingani na matakwa ya Sheria ya Mungu. Kuna kutofautisha kwa muhimu hapa, na ni utofauti uliooneshwa kwanza na Bwana Yesu mwenyewe. Mara zote alimpa Mungu yaliyo ya Mungu, na sisi tunapaswa kufanya hivyo.

Watawala wa Kiyahudi walijaribu kumzuia Yesu asifundishe na kuponya, lakini Yesu hakuacha. Hata wakati ilipokuwa dhahiri kuwa anawaudhi na maisha yake kuwa hatarini, aliendelea na kazi yake ya wokovu. Sababu ni kuwa, Yesu alijua hiyo ilikuwa ni Kazi ya Mungu, na hilo lilikuwa ni kipau-mbele cha kwanza.

Wakati, hatimaye, Yesu aliposimama mbele ya Pontio Pilato, hali akiwa na fursa ya kuweza kusuluhisha tatizo lake na kujiokoa, aliweka hoja ya msingi wazi. Kwanza alimweleza huyo mtawala wa Kirumi pale kuwa, ingawa yeye, Yesu, alikuwa ni Mfalme, Ufalme wake ulikuwa bado haujaja. Alisema:

“Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi. Lakini ufalme wangu sio wa hapa” (Yohana 18:36).

Ni wazi kabisa Yesu alikuwa akifundisha kuwa, ungefika wakati ambao Ufalme wake ungesimikwa katika ulimwengu huu. Huu ndio wakati tunaoungoja, atakapoitawala dunia kwa mamlaka kutoka Yerusalemu. Wakati huo ulikuwa bado haujafika, na mpaka sasa bado.

Lakini hoja ya pili ya Yesu kwa Pilato ilikuwa kwamba, Mungu alikuwa bado akidhibiti mambo. Nyuma ya matukio yale yaliyokuwa yakitokea, Mungu alikuwa akiyaelekeza mambo kufanya mapenzi yake yatimie. Alimwambia mtawala huyo wa Kirumi: “Wewe hungekuwa na mamlaka yoyote juu yangu, kama usingepewa kutoka juu” (Yohana 19:11).

Mfano huo wa kiuaminifu wa Bwana Yesu ulifuatwa na mitume. Nao pia walikuwa wakweli; raia waliozitia sheria za nchi. Kamwe hawakujihusisha na mambo ya kisiasa. Walijiweka mbali na taasisi za kitaifa, jeshi la Kirumi, na mamlaka zilizoshughulikia utoaji wa haki. Walikuwa wamejitoa kwa kazi ya Bwana.

Kulipotokea migogoro kati yao na mamlaka za Kiyahudi au za Kirumi, walifanya nini? Walichofanya ni kumweka Mungu mbele na kutii mwongozo wake. Kwa hiyo, mitume walipoamriwa waache kumhubiri Yesu na Habari Njema ya wokovu, walichosema ni: “Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu” (Matendo 5:29).

### **Ufalme wa Mungu: kwa sasa**

Mfundisho haya na mifano ni msaada mkubwa sana kwetu katika kuamua tuishi kwa namna gani, tukiwa ni raia wa nchi zetu, zinazotutaka tufanye mambo yake kadhaa magumu. Kama wafuasi wa Bwana Yesu, kuna mambo kadhaa tunayopaswa tujitenge nayo kabisa, na ajira fulani-fulani tunazopaswa kuziepuka.

Tunapaswa kuepusha au kupunguza migongano ambayo inaweza kutupata katika kuitekeleza Sheria ya Mungu na hizo zilizoundwa na watu.

Mungu anawahesabu waumini-wa-kweli kuwa ni sehemu ya watu wake. Unaposoma 1 Petro 2 utagundua kuwa, lugha mwanzoni aliyoitumia Mungu kwa Israeli katika Kutoka 19, imekuwa lugha sasa ambayo Mungu anaitumia akiwazungumzia waumini wa Kikristo; wanaoitwa sasa: “Mzao mteule, ukuhani wa kifalme, **taifa takatifu**, watu wa milki ya Mungu” (1 Petro 2:9).

Ni jukumu lao kuishi katika njia ambayo inamtukuza Mungu. Unaona hapa ya kuwa, wamekuwa ‘**taifa**’ kwa namna yao iliyo tofauti; ingawa tunajua wametawanyika kati ya mataifa mengi wanamoishi.

### **Kujitenga na dunia**

Waumini ambao kwa sasa wamekuwa sehemu ya taifa la Mungu; sehemu ya Ufalme wake, wanamngojea Mfalme wao kurudi katika Yerusalemu. Katika kuja kwake, atawaita pamoja waumini hao kutoa huduma na kufanya kazi pamoja naye. Kwa sababu hiyo, ni sharti wasifanye kitu ambacho kitautibua uhusiano wao na Mungu mpaka Kristo atakapokuja. Mungu ni lazima awe wa kwanza katika mambo yote wanayofanya.

Hata hivyo, ingawa Mungu yuko kazini nyuma ya matukio yanayotokea ili kukamilisha mpango wake, haiwi wazi wakati wote inavyokuwa, na watu na mataifa Mungu atakavyoyatumia.

Kwa hiyo basi, ni kosa kujihusisha na mifumo ya serikali za kiwanadamu, katika siasa zake za kimitaa au kitaifa. Watu wa Mungu ni watu wa mpango wake Mungu, na tayari wana Mfalme wao ambaye ni Bwana Yesu Kristo. Ni makosa kujaribu kutumia mifumo ya kisiasa ya watu, kujaribu kuifanya dunia iwe mahali pazuri zaidi pa kuishi. Mungu atalifanya hilo Yesu atakaporudi. Kwa hiyo Mkristo wa kweli atajitenga; atajiepusha na siasa. Hataichangamkia na hatapiga kura.

Kwa namna hiyo hiyo, ni lazima kujiweka mbali na mazingira ambayo hayafai kwa mfuasi wa Kristo; kama kufanya kazi ya kutengeneza silaha za hatari, bunduki au milipuko. Kufanya kiapo cha uti kwa taifa au kwa mtawala wa kidunia nako ni lazima kuepukwe. Kama tulivyoona, Mkristo atakuwa mtii kwa sheria za nchi lakini kama kutakuwa na utata, achaguzi wake hatimaye atakuwa kushikamana na Yesu.

Kujiunga na jeshi la Polisi au jeshi la Ulinzi sio kitu kizuri pia; ni kazi za kutumia nguvu na kuua. Wale ambao tayari wamekuwa maaskari kabla hawajaja kulielewa hili, watahitaji kumwomba Mungu juu ya jambo hili na kuomba ushauri kutoka kwa wakufunzi wao. Mungu anaweza kumfungulia mtu njia nyingine katika shida zake zote.

Ni vizuri ieleweke vizuri kuwa, kujitenga na siasa za vyama na kazi mbaya hakuna maana ya kuwa, siasa na kazi zingine za taifa husika ni mbaya. Ni kanuni tu inayowahusu wanaotaka kumfuata Kristo, na ni jambo linalowahusu waumini wengine kila mahali. Wapo sasa chini ya “Sheria ya Kristo” (1 Wakor. 9:21), na ni lazima wajitahidi kuishi inavyotakiwa. Mtume Paulo alisema juu ya muindo yote ya kidunia:

“Tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana, msiguse kitu kilicho kichafu, nami nitawakaribisha”  
(2 Wakor. 6:17).

Kujitenga kwetu na mambo ya serikali za kibinadamu ni sehemu ya kuitwa kwetu tutoke katika dunia, ili tuweze kikweli kuwa watu wa Mungu.

### **Muhtasari**

1. Ni lazima tuzitii Sheria za Mungu.
2. Ni lazima tuzitii sheria za nchi zetu mpaka zinapokuwa zimegongana na Sheria ya Mungu.
3. Ni lazima tuepuke kazi yoyote, au kujihusisha na shughuli yoyote inayoweza kutuweka katika mgongano na Sheria ya Mungu.

**Mistari ya kusoma:** Danieli 3 na 4; Warumi 13; Mathayo 22:15-22



**Mistari ya kushika: 1 Petro 2:9-11**

“Ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu; ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu, mliokuwa hamkupata rehema, bali sasa mmepata rehema. Wapenzi, nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili zipinganazo na roho”.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## MAOMBI

**SOMO:** Zaburi 107

Kuweza kumwomba Mungu wa mbinguni ni fursa tuliyonayo ya maana na ya kipekee sana. Ni fursa ambayo yeye Mungu ameitoa kwa kila mtu aliye mnyenyekevu, na ambaye anatambua kuwa yeye Mungu ndiye aliyekifanya kila kitu kilichopo duniani. Kuomba/kusali kunaweza kukaonekana kuwa ni kitu kigumu. Sababu ni kwamba, kuna mtengano mkubwa sana uliopo kati ya Muumba aliye mbinguni na vitu alivyoviumba vilivyoko katika dunia.

Hata hivyo Mungu ameweka wazi wakati wote kuwa, yupo tayari kukaribiwa na watu ili waseme Naye, kama wana uelewa ulio sahihi mioyoni mwao, na kama wako tayari kulikubali Neno lake:

“BWANA asema hivi, Mbingu ni kiti changu cha enzi, na dunia ni mahali pa kuweka miguu yangu....lakini mtu huyu ndiye nitakayemwangalia, mtu aliye mnyonge, mwenye roho iliyopondeka atetemekaye asikiapo neno langu” (Isaya 66:1, 2).

Kwa hiyo tuna ahadi ya kwamba, Mungu atatuitikia kama tukimjea kwa unyenyekevu wa kweli.

Tunaweza tukafikiri kuwa sio rahisi kusema moja kwa moja na Mungu. Na kweli, katika nyakati za Agano la Kale, watu mara nyingi waliogopa sana walipokuwa wanajisikia wapo katika ‘uwepo’ na Mwenye-Enzi yote. Wana wa Israeli, kwa mfano, walipotoka Misri, utukufu wa Mungu uliposhuka katika Mlima Sinai, kila mmoja wao, akiwepo Musa, walitetemeka na watu kusimama mbali (Kutoka 19:17-20 na 20:18-21).

Mungu alikuwa akiwakaribia watu wake; taifa lake, lakini utisho wa Ukuu waliouona uliwafanya wajione hawawezi kuwa na ukaribu na Utakatifu wa uwepo wake. Pengine hata sisi tungejisikia hivyo hivyo. Waliogopa kiasi cha kumwomba Musa awe mtu wao ‘wa-kati’ kati yao na Mungu; kiunganishi chao; mpatanishi. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa kwamba, baada ya hapo Mungu aliwasiliana na Israeli kupitia kwa mtu-wa-kati.

Hema la Kukutania lilipojengwa kuwa mahali pa kuabudia nyikani, Utukufu wa Mungu uling’aa juu ya Sanduku la Agano katika sehemu takatifu zaidi ya Patakatifu (Patakatifu pa Patakatifu). Hakuna mtu aliyekuwa akiruhusiwa kuingia hapo penye ‘uwepo wa Mungu’, zaidi ya Kuhani Mkuu, mara moja kwa mwaka, katika Siku ya Upatanisho. Katika siku hiyo Kuhani Mkuu alizikiri mbele ya Mungu dhambi zote za taifa la Israeli, na kwa vizazi vingi huu ukawa ndio mfumo wa Upatanisho kwa Wayahudi wote.

Walikuwa ni watu wa kumkaribia Mungu, lakini kwa namna aliyoiweka, na hili lilikuwa ni jambo lililowekwa kuwaongoza kwenye ‘kazi za Yesu’, ambaye ni ‘Mpatanishi’ kwa ajili ya wafuasi wake. Alipopaa mbinguni, aliwekwa awe ‘Kuhani Mkuu aliye mwaminifu’ kwa ajili ya wanaomfuata wote, wawe Wayahudi au wasiwe, mradi wamebatizwa ‘katika Kristo’.

### Mtu wa kawaida anaweza kuongea na Mungu

Swali: Hakukuwa na njia nyingine ya kumjea Mungu ila kwa kupita kwa kuhani wa Kiyahudi au kwa kutoa sadaka? Ni vipi basi kwa:

- ✚ Watu walioishi kabla hakujiwa na taifa la Israeli?
- ✚ Watu ambao hawakuwa Wayahudi?
- ✚ Watu ambao walitaka tu kumwomba Mungu msaada?
- ✚ Wayahudi baadaye walipokuwa wakiishi katika nchi za kigeni?

Je, hawakuwa wakiweza kusema na Mungu moja kwa moja? Tunajua kutokana na kusoma kwetu Biblia zetu na mifano mingi sana ya maombi kwa Mungu wa mbinguni kuwa, Mungu wakati wote huwa anayasikia maombi ya watu.

Kwa mfano, tulisoma katika Mwanzo 24 kumhusu mfanyakazi wa Ibrahimu aliyeomba afanikiwe kwenye safari yake ya kumpatia Isaka, mwana wa Ibrahimu, mke. Tunaona namna mtumishi huyo alivyomshukuru Mungu maombi yake yalipojibiwa. Tunaweza kusoma pia katika Ayubu 42 jinsi Ayubu alivyoomba kwa ajili ya marafiki zake, hapo Mungu alipomponya kutoka katika ugonjwa wake wa kutisha.

Hana, mama yake Samweli alimwomba Mungu kwa sababu alikuwa tasa (1 Samweli 1 na 2), na Danieli, akiwa mateka Babeli, na madirisha katika chumba chake yakiwa yamefunguliwa kuielekea Yerusalemu ilipo, alipiga magoti mara tatu kila siku: “Akasali, akashukuru mbele za Mungu wake, kama alivyokuwa akifanya tokea hapo” (Dan. 6:10).

Tena, tunayo dua ya mfalme Sulemani akimwomba Mungu ili ayasikie maombi ya **wageni**, akisema:

“Hata na mgeni naye, asiyekuwa mmoja wa watu wako Israeli, atakapokuja kutoka nchi iliyo mbali sana kwa ajili ya jina lako, (maana watasikia habari za jina lako kuu, na za mkono wako ulio hodari, na za mkono wako ulionyoshwa); atakapokuja na kuomba kuielekea nyumba hii; basi, usikie huko mbinguni makao yako, ukatende kwa kadri ya yote atakayokuomba mgeni huyo; ili watu wote wa dunia wapate kulijua jina lako, na kukucha wewe....” (1 Wafalme 8:41-43).

Vipi juu ya watu hao wote, wanaomwitia Mungu wanapokuwa katika shida? Atawasikia hata kama mara nyingine wanakuwa wamemsahau? Jibu ni ‘ndio’, kama ni wakweli na wanyenyekevu, na wana moyo wa toba. Hebu tuiangalie mifano tuliopewa kwenye Zaburi ya 107:

- ✚ Wenye njaa na kiu wanalishwa (ms. 5,6).
- ✚ Wale wanaomuasi Mungu, lakini baadaye wakatubu, wanaponywa na shida zao (ms. 13).
- ✚ Mungu anawasikia wale ambao ‘wameyakaribia malango ya mauti’ (ms. 18).
- ✚ Mungu anawasikia wale ambao wako katika hatari ya kuzama majini (ms. 28).

Fundisho hili limejumlishwa kwenye msitari wa 6: “Wakamlilia BWANA katika dhiki zao, akawaponya na shida zao”.

### **Tutaongeeje na Mungu?**

Katika Agano Jipya wakati wa huduma ya Yesu, Bwana Yesu anatuambia juu ya ‘mtoza ushuru’ na ‘mdhambi’; watu ambao walidharauliwa na Wayahudi wengi. Mdhambi alisimama mbali, wala hakuthubutu kuinua macho yake, bali alijipiga-piga kifua chake na kuomba, “Ee Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi” (Luka 18:13).

Yesu anasema, mtu kama huyo alisikiwa na Mungu kwa maana alijinyenyekeza, tofauti na mafarisayo, ambao walijiona ‘wa maana’ sana kwa jitihada zao wenyewe za kuishi maisha mazuri.

Kwa hiyo tunaona ya kwamba, Mungu amewawekea watu wakweli, popote pale walipo, fursa ya kumkaribia kwa njia ya sala. Ni hivyo ilivyo hata wakati huu, na tunaweza kujifunza mengi sana kutoka katika mifano hii ya Kibiblia. Mtu yeyote yule, awe mwanamume au mwanamke, anayemtafuta Mungu na kujifunza Neno lake, kwa vyovyote ataona **haja** ya kumwomba.

Mungu anavijali viumbe vyake vyote na atasikia kila ombi lililo la kweli. Mtu anayemtafuta Mungu atapenda kumsifu na kumwabudu kwa dhiti; kumshukuru kwa mibaraka yake ya uzima na hasa kwa mbaraka wa Neno lake kwake, Biblia.

Anapokuwa amejifunza juu ya dhambi, atatamani kuzikiri dhambi zake kwa Mungu, na Mungu atamsikia. Lakini kuna jambo moja la kutambua. Mungu atasamehe tu dhambi kwa njia aliyoiweka; nayo ni kwa kupitia katika dhabihu ya Bwana Yesu Kristo, na hili linahitaji muumini awe amebatizwa kwanza.

Akida wa Kirumi, Kornelio, alikuwa akifanya maombi yaliyokuwa yakifaa sana. Tunaambiwa, alikuwa: “Mtu mtauwa, mchaji wa Mungu yeye na nyumba yake yote, naye alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi, na kumwomba Mungu daima” (Matendo 10:1).

Maombi ya Kornelio yalisikiwa, na Mungu akamtuma mtume Petro kumkamilisha kimafundisho, na baada ya hapo kumbatiza katika Jina liokoalo la Bwana Yesu (utakisoma hiki kifungu chote mbeleni).

Ombi la muhimu kuliko yote kwa ajili ya mtu anayejifunza kumhusu Mungu, pengine ni lile linalopatikana katika Kitabu cha Zaburi, Zaburi ya 119:

“Unifumbue macho yangu, niyatazame maajabu yatokayo katika sheria yako” (ms.18).

Tunapaswa wote kumwomba Mungu abariki kusoma kwetu na kujifunza kwetu Neno lake.

### **Mungu atajibu?**

Kwa lolote tunalotaka, tunapaswa kulileta kwa Mungu kwa njia ya maombi:

- ✚ Lakini, atajibu?
- ✚ Anajali wakati wote?
- ✚ Anaweza wakati wote kufanya linaloombwa?

Haya ni maswali ya kufaa, na yana majibu ya hakika kwenye Biblia.

Kusali sio fursa kwa ajili yetu kumwekea Mungu mahitaji yetu yote, ili atupe vitu vyote tunavyopenda kuwa navyo. Kuomba ni sehemu tu ya ibada yetu. Kunatupa nafasi ya kuyafikiria kwanza mambo mbele ya Mungu anayetupenda, na anayetutakia kilicho bora zaidi. Mtume Paulo anasema:

“Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu”

(Wafilipi 4:6).

Tunapaswa kuomba kwa imani, lakini ni lazima kuomba kulingana na mapenzi ya Mungu, ili mapenzi yake yatimie. Hili lina maana ya kusoma Biblia ili kuyajua mapenzi yake yalivyo, na kusudi lake, na sio kuomba kwa ajili ya vitu tulivyoambiwa hatuwezi kuvipata. Tukumbuke pia kwamba, Mungu mara nyingine anajibu maombi kwa kututaka tusubiri, mara nyingine kwa muda mrefu.

Ibrahimu aliomba, lakini ilimbidi asuburi kwa miaka mingi kumpata mwana, ambaye Mungu alikuwa amemwahidi kumpa. Mara nyingine Mungu anatumia kwa kukataa; kwa kuacha kutupa kile tunachomuomba. Yeye anajua lililo bora zaidi kwetu, kuliko tunavyojua wenyewe linalotufaa. Lakini kamwe haachi kutujali na kutupenda. Kwa wenye-haki, wakati wote, “Masikio yake hukielekea kilio chao” (Zab. 34:15).

### **Kujifunza kusali**

Tunajifunza kusali kwa namna ile ile tunavyojifunza kuongea; kwa kuanza kujifunza kwa wengine, na kujaribu baada ya hapo kufanya kama wao. Kwa hiyo inafaa twende kwenye Biblia kwa ajili ya mifano. Biblia imejaa maombi. Kwenye Zaburi, kwa mfano, kuna maombi kama 150 tofauti-tofauti tunayoweza kujifunza vitu ndani yake. Kuna mengi pia ya kujifunza katika maombi ya manabii na Yesu na wanafunzi wake.

Kama tukiyasoma Maandiko kila siku, tutajenga mwelekeo wa kiakili unaoweza kumpendeza Mungu. Tutajengeka kwa namna tunavyofikiri, na tutajengeka kwa namna tunavyosema na Mungu. Tunaweza pia kuwafanya wengine wawe kama sisi katika kuomba kwetu: kwa mfano katika kumshukuru Mungu kabla ya kula, au kwa kupiga magoti pembeni mwa kitanda kabla hatujalala.

Tunaweza kuomba wakati wowote ule, mara nyingi kwa kadri tunavyopenda: tukiwa nyumbani au safarini au kazini au shambani. Yesu alikuwa akipenda kuondoka kidogo peke yake asubuhi-subuhi, kwenda mahali palipotulia, kuomba.

Lakini tunaweza pia kuomba katika mkasa wowote, kama ambavyo tunavyoweza kumshukuru Mungu kwa mambo ambayo yamekwenda vizuri na kwa mibaraka yetu yote. Watu wengi wa-imani wanaona vizuri kuwa na muda maalumu wa maombi ya kibinafsi, mara nyingi asubuhi na jioni. Hili ni jambo jema, lakini kamwe tusipuuze fursa yoyote kungea na Bwana.

### **Maombi ya muumini aliyebatizwa**

Tulitaja awali katika somo hili kuwa, kuna jambo la kipekee kuhusu maombi kwa wale waliobatizwa katika Kristo. Kama vile ambavyo Kuhani Mkuu alivyokuwa mpatanishi kwa ajili ya Waisraeli, ndivyo ambavyo Yesu Kristo alivyo Mpatanishi kwa ajili ya wafuasi wake wote wa kweli. Uhusiano wa kipekee na Mungu kupitia kwa Mwanawe unaokuwepo, ni kitu kwa ajili yako kilichowekwa ukitazame kwa furaha kama, kwa neema ya Mungu, umebatizwa.

Ina maana kuwa, unapozikiri dhambi zako kwa Mungu kwa Jina la Yesu, Mungu **anakusamehe** dhambi zako, na hili lina maana ya kwamba hatazikumbuka tena.

<b>Yesu Kristo ni Mpatanishi kwa waumini waliobatizwa</b>
---

Dhambi za Waisraeli hazikuondolewa walipokuwa wakitoa sadaka za wanyama. Mshahara wa dhambi ni mauti. Wanyama hawakuwa na akili kuhusiana na dhambi, na wasingeweza kuifia dhambi; kutoa damu yao wenyewe. Imeandikwa katika Waebrania 10:4 kuwa: “Haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi”.

Lakini Yesu alikuwa ndiye sadaka kamilifu kwa kuwa, kwa damu yake mwenyewe alijitoka bila ya dhambi (Waebr. 9:12). Kwa hiyo, wale wanaobatizwa katika Yesu wana:

“Kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu”, ambaye, “Alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi”

(Waebr. 4:14, 15).

<b>Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu kwa ajili ya waumini waliobatizwa</b>
---

Ubatizo wa kweli wa Kikristo ni wa muhimu sana. Una matokeo ya kuziosha dhambi zetu (Matendo 22:16) na tunapokuwa tumebatizwa, ndipo tunapoweza kumkaribia Mungu kupitia kwa Yesu Kristo, tukijua ya kuwa: “Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote” (1 Yoh. 1:9). Ndipo tutakapoweza kutumia maombi Bwana Yesu aliyowafundisha wanafunzi wake, akisema:

“Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe siku kwa siku riziki yetu. **Utusamehe dhambi zetu**; kwa kuwa sisi nasi tunamsamehe kila tumwiaye. Na usitutie majaribuni, lakini tuokoe na yule mwovu” (Luka 11:2-4).

Haya yatakuwa ni maombi ya maana sana kufanya kwa kuwa, mwenye kheri ni yule: “Aliyesamehewa dhambi, na kusitiriwa makosa yake” (Zaburi 32:1).

**Muhtasari**

1. Ni lazima kumkaribia Mungu kwa namna aliyoiweka.
2. Mungu atayasikia maombi ya wote walio wanyenyekevu na wakweli.
3. Tunapaswa kutoa shukrani na sifa, kuzikiri dhambi zetu na kumwomba Mungu atuongoze na kutubariki.
4. Ni wajibu wetu kujifunza kuomba kwa ajili ya vitu sahihi na kwa namna iliyo sahihi.
5. Kuomba ni fursa tuliyo pewa ya bahati sana na ni mbaraka mkubwa. Ni lazima tuombe mara kwa mara.
6. Baada ya kubatizwa tunaweza kuomba kupitia kwa Bwana Yesu Kristo kwa ajili ya kusamehewa dhambi zetu. Ndipo Mungu atakapokuwa Baba yetu, na kuwa Mungu wetu.

**Vifungu vya kusoma:** Matendo 10; Zaburi 51, 102; Luka 18:1-14.

**Kujifunza kwa moyo:** Wafilipi 4:6

“Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu” .

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

### KUTEMBEA KATIKA NJIA MPYA YA UZIMA

**SOMO:** Warumi 6

#### **Mwanzo mpya**

Tunapobatizwa, tunaanza maisha mapya. Tunakuwa, “tulizikwa pamoja naye (Kristo) katika mauti yake”, wakati tulipotumbukizwa katika maji ya Ubatizo. Maisha tuliyoishi mpaka wakati huo yanakuwa yamefikia mwisho wake; yanakuwa yamepita. Inakuwa:

“Kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima” (Warumi 6:4).

Mabadiliko ya namna hiyo yanawezekana tu kwa neema ya Mungu. Tukiwa wana wa Baba yetu wa mbinguni, tunaweza sasa kumjea kupitia kwa Yesu. Tutashindwa kumpendeza mara nyingi kwa kadri tunavyojaribu, lakini tunapoomba msamaha, atatusikia kwa ajili ya Yesu. Andiko linasema:

“Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji” (Waebr. 4:16).

#### **Kujilisha Neno la Mungu**

Mtoto anahitaji kula, na anafanya hili lijulikane kwa njia moja ya uhakika; analia! Anahitaji kukua. Chakula ni cha muhimu ili aweze kukua. Na wale ambao wamezaliwa kuyaingia maisha mapya kwa kubatizwa, wanaweza tu kukua katika Kristo, kama maisha mapya yanalishwa na kutunzwa kwa Neno la Mungu. Mtume Petro anasema:

“Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu” (1 Petro 2:2).

Mungu ametupa Biblia ili iwe kitabu chetu cha kutuongoza. Itatusaidia kutufanya tuishi kwa namna anavyotaka, na kukua kuwa ‘mtu mpya’ katika Kristo kwa Neno lake, kwa kuwa:

“Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema” (2 Tim. 3:16, 17).

#### **Kuutazamia Ufalme**

Mtume Petro anatuambia kwamba, Mungu, “Hapendi mtu yeyote apotee” (2 Petro 3:9), na katika Yohana 3:16 tunasoma ya kwamba, Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee, Yesu, kusudi: “Kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele”.

Mungu anapenda atupe uzima wa milele katika Ufalme wake. Na kwa hiyo, anatuandaa sasa kwa ajili ya maisha hayo. Amemtoa Yesu kutusaidia, na kupitia kwa Yesu tunaweza kumkaribia Mungu kwa njia ya maombi.

#### **Msaada kutoka kwa Yesu**

Bwana Yesu aliwahi kusema: “Msiogope, enye kundi dogo, kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme” (Luka 12:32).

Kuna wakati Yesu alimtolea Mungu maombi kwa ajili ya wale wanaomwamini, wa nyakati zote. Unaweza kuyasoma haya katika Yohana 17. Angalia maneno yaliyopo katika msitari wa 24:

“Baba, hao ulionipa nataka wawe pamoja nami popote nilipo, wapate na kuutazama utukufu wangu ulionipa”.

Kwa hiyo, Yesu naye anatutaka tuwe katika Ufalme wake. Kwa hiyo atatusaidia njiani; kamwe hatatuacha tuhangaika peke yetu. Yesu sio tu Mwokozi ambaye kupitia kwake dhambi zetu zinasamehewa, bali pia ni Kiongozi wetu katika maisha haya. Atakuwa mshirika katika maisha yetu na changamoto zake, katika furaha na majonzi, na kutusaidia kutuingiza kuishi naye katika Ufalme wa Mungu.

Mtume Petro, mtu aliyemfahamu Yesu vizuri alipokuwa duniani, aliwaasa wanaomwamini wamfuate Yesu, huku wakimtwika fadhaa zao zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yao (1 Petro 5:7).

### **Kuwa sehemu ya familia moja kidunia**

“Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke, maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu” (Wagalatia 3:27, 28).

Haijalishi wewe ni nani, au upo wapi. Kama umekuwa Mkristadelfia kwa kubatiziwa Kristo, Wakristadelfia wengine wote ni ndugu zako; ni kaka na dada zako. Kumbuka, jina Kristadelfia lina maana ya ‘undugu katika Kristo’. Ni furaha kubwa sana kuwa sehemu ya familia hii, iliyosambaa katika sehemu zote za dunia.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake kabla ya kufa, na bado anasema hivyo na sisi leo: “Amri yangu ndiyo hii, mpendane, kama nilivyowapenda ninyi” (Yoh. 15:12).

Alitupenda sana, kiasi kwamba alikufa kwa ajili yetu. Aliutoa uhai wake kwa ajili yetu, kwa hiyo: “Imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu” (1 Yoh. 3:16).

Tunajua tunavyopaswa kufanyiana, lakini, kiuhalisia, ni vigumu sana. Hulka yetu ya awali inachukua muda mrefu kufa! Baadhi yetu wana hasira za haraka-haraka, wengine ni vigeu-geu na wepesi kulipuka n.k. Sisi wote tuna kasoro zetu.

Haya ni mambo, hata hivyo, tunayopaswa kuyapiga vita, na kujaribu kuwaonesha ndugu zetu katika Kristo upendo ule ambao Yesu ametuonesha. Kuna picha ya upendo huo katika 1 Wakorintho 13, ambapo tunaambiwa kuwa:

“Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake, hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote” (1 Wakor. 13:4-7).

### **Kumpenda jirani yetu**

Mwanasheria mmoja aliwahi kuja kwa Yesu na alimuuliza, ni ipi iliyokuwa amri kubwa kuliko zote. Yesu alimjibu:

“Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, mpende jirani yako kama nafsi yako” (Mathayo 2:37-39).

Hebu isome hadithi ambayo Yesu aliitoa kuhusiana na ‘jirani mwema’ katika Luka 10:30-37. Kama mtu yeyote ana shida, tunapaswa kumsaidia. Hatupaswi tusite na kujiuliza kama tunampenda au hatumpendi, au kama ni kweli anastahili kupata msaada wetu au hastahili.

Kitu cha muhimu kuliko vyote tunachoweza kuwafanyia wengine, ni kuwapasha Habari Njema ya Ufalme wa Mungu, ambayo sisi wenyewe tumekuja kuiamini. Kama ambavyo Mungu ametutaka tuzishike Njia Zake na kuwa washiriki wa shangwe ya Ufalme wake unaokuja, nasi ni lazima tutamani kuwavuta na wengine, wawe na ushirika katika mambo haya.



### **Kuomba na kuabudu**

Tunapobatizwa katika Kristo, tunakuwa wana wa Mungu, na tunaweza kumkaribia kwa maombi tukimwabudu na kumwomba atusaidie katika maisha yetu. Lakini ni wajibu tususahau Ukuu wake ulivyo, ingawa utukufu na Ukuu wake huo ni vitu vilivyo nje ya upeo wetu wa kuelewa vizuri. Katika Isaya 57:15 tunasoma kuwa:

“Aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye jina lake ni Mtakatifu, asema hivi: Nakaa mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu, tena pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua mioyo yao waliotubu”.

Yakobo anatuambia kuwa: “Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekevu” (Yakobo 4:6). Hata Bwana Yesu, Mwana wa Mungu, alijisemea mwenyewe kuwa alikuwa ni: “Mpole na mnyenyekevu wa moyo” (Mathayo 11:29).

Tunapomjea Mungu kwa njia ya maombi, tunahitaji kuukumbuka ujumbe kwa Waebrania unaosema: “Tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho” (Waebr. 12:28). Kama tunamjea kwa moyo huu, hakika hawezi kukosa kutosikia.

### **Heri wenye upole**

Katika ulimwengu huu, tunaambiwa wakati wote tupigania haki zetu. Wale wanaopambana kwa manufaa yao wenyewe kibinafsi, watu wanawahusudu. Swala la muhimu katika mawazo ya kila mmoja yamekuwa: ‘Nifanye nini niweze kujikwamua; niweze kupiga hatua?’

Hii sio namna ya Mkristo. Paulo anasema kwa watakatifu wa Filipi na kwetu kuwa, tuwe wanyenyekevu, na: “Kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake” (Wafilipi 2:3). Hiki ni kitu kigumu kufanya; sisi wote tunapenda kufikiri kuwa tuko bora zaidi kuliko wengine. Lakini tunaambiwa: “Tumikianeni kwa upendo” (Wagalatia 5:13).

Katika hili, kama ilivyo kwa mambo yote, Yesu ni kielelezo kwetu. Muda mfupi kabla hajafa, alipokuwa akila na wanafunzi wake, aliacha kula akajifunga taalo:

“Kisha akatia maji katika bakuli, akaanza kuwatawadha wanafunzi miguu, na kuifuta kwa kile kitambaa alichojifunga” (Yohana 13:4, 5).

Kumwosha miguu mtu mwingine ilikuwa ni kazi ya mtumwa, na ndicho Yesu alichofanya. Baada ya hapo aliwaambia wanafunzi wake: “Nimewapa kielelezo, ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo” (ms. 15).

Aliwahudumia wanafunzi wake kwa upendo na unyenyekevu, na sisi ni lazima tuhudumiane. Hivyo ndivyo tutakavyoweza kuwa watu wa namna Mungu anayoitaka katika Ufalme wake. Andiko linasema, “Heri wenye upole, maana hao watairithi nchi” (Mathayo 5:5).

### **Kumkumbuka Yesu**

Tunapobatizwa, tunaanza kuipita njia nyembamba iliyonyoka inayotuongoza kwenye Ufalme wa Mungu. Lakini bado sisi ni wanadamu sana, na tunaweza kirahisi kusahau lile Yesu alilolifanya kwa ajili yetu alipotufia msalabani.

Yesu alijua jinsi ambavyo kirahisi wanafunzi wake wangeweza kusahau, kwa hiyo aliwaagiza wafanye kitu kujikumbusha. Hebu fungua Injili ya Luka, na usome Sura ya 22:14-20. Hili lilitokea katika kile chakula cha mwisho, tunachokiita Chakula cha Bwana, tulichokwisha kiongelea, alipowaosha wanafunzi wake miguu yao.

Hebu ona jinsi mkate na divai vilivyokuwa ni kwa ajili ya kuwakumbusha wafuasi wake, jinsi Yesu alivyoutoa uhai wake kwa ajili yao. Aliwaambia: “Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu”.

Sasa tusome 1 Wakorintho 11:23-28. Wakristo wa awali walikutana katika siku ya kwanza ya kila juma, kumkumbuka Yesu kwa namna aliyoamuru.

Wafuasi wa kweli wa Bwana Yesu wanakutana pamoja, kama wafuasi hao wa kwanza walivyofanya. Kwa kawaida Jumapili ni siku iliyo nzuri zaidi kwa mikutano hiyo, nayo ni siku ya kwanza ya juma. Wanapokutana wanamwabudu Mungu pamoja na kumega mkate na kula, na kunywa divai kidogo, katika kukumbuka vile Yesu alivyoutoa mwili na damu yake kwa ajili ya wokovu wao.

Kwa kadri tunavyokomaa katika Kristo, kumkumbuka Yesu kwa namna hii kutakuwa kitu cha muhimu zaidi na zaidi kwetu, kinachotusaidia kutambua kuwa yupo nasi wakati wote.

#### **KWENDA KATIKA NJIA YA UZIMA KUNAMAANISHA**

... Kujilisha kwa kulisoma Neno la Mungu kila siku:

“Kufafanisha (‘kujifunza’) maneno yako (Mungu) kwatia nuru, na kumfahamisha (‘kumwelimisha’) mjinga” (Zaburi 119:130).

... Kumwomba Mungu na kumsifu wakati wote:

“Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu” (Wafilipi 4:6).

... Kuwapenda ndugu zetu:

“Wapenzi, na mpendane; kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu, na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu” (1 Yoh. 4:7).

... Kuwafikiria wengine, na kuwasaidia kila tunapoweza:

“Basi yoyote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo” (Mathayo 7:12).

... Kuacha kushiriki katika mambo ya kidunia; mambo ya dunia hii:

“Tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana. Msiguse kitu kilicho kichafu, nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wakike, asema Bwana Mwenyezi” (2 Wakor. 6:17, 18).

... Juu ya yote, kumpenda Mungu kuliko vitu vyote:

“Nawe mpende BWANA, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa nguvu zako zote” (Kumb. La Torati 6:5).

**Vifungu vya kusoma:** 1 Wakorintho 13; Luka 10:30 – 37; Luka 22:14-20; 1 Wakorintho 11:23-28.

**Msitari wa kushika:** 2 Wakorintho 5:17

“Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita, tazama! Yamekuwa mapya”.

## MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

*Karatasi ya maswali: namba 9*

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa 'Kazi ya ziada' unaweza kulijibu swali kama ukipenda, au kuliacha kama unaona huliwezi. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

### MASOMO: 32 – 36

32/33 A. Ndio au Hapana?

- a) Ni lazima Wakristo wote waoe au kuolewa?
- b) Muumini anaweza kuoa au kuolewa na asiyeamini?
- c) Kama tumefanya zinaa, tunaweza kusamehewa na kubatizwa?
- d) Kama mtu ameamua kuoa au kuolewa na mtu, anaweza kufanya naye mapenzi kabla ya kuoana.
- e) Ndoa kati ya waumini ni lazima idumu maisha yote?
- f) Ni lazima waliooana wawe na watoto?
- g) Mungu anachukizwa na wanaotengana?
- h) Kama mtu anayeamini ameoana na asiyeamini, ni vizuri zaidi kubakia katika ndoa kuliko kutengana na asiyeamini?
- i) Talaka inaweza kuruhusiwa kati ya Wakristo?
- j) Muumini ambaye amefanya uzinzi ni lazima aachike?
- k) Ni ruhusa muumini kuoa mke wa pili?
- l) Ndoa kati ya wawili wanaoamini inaweza kuvunjwa kwa kuwa wameacha kupendana?
- m) Mtu yuko huru kuoa au kuolewa na mtu mwingine kama mwenzake amefariki?

32/33 B. Vifungu vifuatavyo vinatufundisha nini?

- a) 2 Wakorintho 6:14
- b) Kazi ya ziada: Mathayo 5:31, 32.
- c) Wakolosai 3:12 – 25
- d) Waefeso 5:23 – 25
- e) 1 Timotheo 2:9- 15

34. A. Pendekeza aina za kazi ambazo waumini wanapaswa kuzikwepa.  
B. Ni kwa nini waumini wa kweli hawapaswi kupiga kura au kujishirikisha na mambo ya kisiasa?  
C. Yesu alikuwa na maana gani katika Yohana 18:36?

Kazi ya ziada

Andika orodha ya baadhi ya vitu tunavyojifunza katika 1 Petro 2:11-17.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## USOMAJI WA BIBLIA WA KILA SIKU

**Somo:** Zaburi 119: 89-112

Biblia ni kama kisima kirefu sana cha maji safi; kisima ambacho kamwe huwezi kukifikia chini kwa jinsi kilivyo kirefu. Hutaweza kamwe kufikia wakati utakapoweza kujisikia umeijua yote kabisa; huhitaji kulisoma tena Neno la Mungu. Hebu ona jinsi baadhi ya watu walivyolipokea Neno la Mungu.

WAYUNANI WA BEROYA

PAULO ALIVYOWAANDIKIA  
WATHESALONIKE

“...walilipokea lile neno kwa uelekevu kwa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo. Basi watu wengi miongoni mwao wakaamini” (Matendo 17:11,12).

“Mlipopata lile neno la ujumbe la Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadamu, bali kama neno la Mungu; na ndivyo lilivyo kweli kweli”  
(1 Wathesalonike 2:13).

Kwa hakika ni muhimu sana **tukisome** kitabu hiki kwa uangalifu! Mungu anaongea **nasi** katika Biblia! Inatupa tumaini la uzima kupitia kwenye Injili.

### Biblia na Yesu

Yesu, kwa vyovyote, alikuwa na Agano la Kale tu. Lakini utashangaa alivyolijua. Kwa kila tatizo na ugumu alioupata, aliendea Neno la Mungu moja kwa moja kwa ajili ya jibu. Hebu ione mifano hii:

1. Wakati mafarisayo walipomuuliza kama ilikuwa sahihi kwa mtu kumpa talaka mkewe, Yesu alirudi moja kwa moja kwenye simulizi la Adamu na Hawa kwenye Mwanzo. Aliwaambia: “Tangu mwanzo wa kuumbwa ulimwengu, (Mungu) aliwafanya mume na mke”. Unaweza kulisoma jibu lote katika Marko 10:5-12.
2. Yesu alipokuwa peke yake nyikani, majaribu yalimjea yakimtaka aifuata njia iliyokuwa rahisi zaidi kwake, badala ya kuifuata Njia ya Mungu. Aliyashinda mawazo hayo mabaya kwa kuyajibu kwa maneno kutoka kwenye Kitabu cha Kumbukumbu la Torati, mara zote akisema: “Imeandikwa...”
3. Maaskari walipokuja kumkamata Yesu, Yesu alijua kuwa kingefuatia kifo chake. Alikwenda bila kubisha kwa kuwa, alisema: “Haya yamekuwa ili maandiko yapate kutimia” (Marko 14:49). Maandiko yalikuwa yamezungumzia mauti yake. Kwa maisha yake yote, Yesu alikuwa akitimiza yaliyoandikwa juu yake katika Agano la Kale.

### Kukua katika kumjua Yesu

Petro anatusihi tukue: “Katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo” (2 Petro 3:18). Tunaweza tu kumjua Yesu kwa kusoma juu yake; na Injili zote nne zinatupa maelezo ya mambo Yesu aliyofanya na maneno aliyosema, na kwa namna gani aliutoa uhai wake wa ajili yetu.

Vitabu vingine katika Agano Jipya vinatusaidia kuelewa zaidi juu ya yale Yesu aliyofanya kwa ajili yetu katika kufa msalabani, na jinsi inavyotupasa kuishi maisha mapya katika Kristo.

Lakini haiwezekani kuyaelewa mambo haya bila kulisoma Agano la Kale nalo. Msitari wa kwanza kabisa wa Agano Jipya (Mathayo 1:1) unamsema: “Yesu Kristo, mwana wa Daudi, mwana wa Ibrahimu”. Ni lazima turudi nyuma kwenye Agano la Kale ndipo tunapoweza kuelewa Ibrahimu na Daudi walikuwa ni watu gani, na ni kwa nini Yesu anaitwa ‘mwana’ wao.

Yesu alilisoma Agano la Kale, ni wajibu wetu nasi kulisoma

### **Inatupasa kusoma kila siku**

Mtume Paulo anatuambia jinsi ilivyo muhimu kuyasoma Maandiko Matakatiifu katika maisha yetu. Anasema:

“Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema” (2 Timotheo 3:16, 17).

Mwenyezi Mungu anatupatia chakula ambacho miili yetu anakihitaji siku kwa siku. Yesu aliwakumbusha wanafunzi wake hili alipowaambia:

“Waangalieni ndege wa angani ya kwamba hawapandi wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani, na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi je! Si bora kupita hao? (Mathayo 6:26)

Kwa namna hiyo hiyo, uzima wetu mpya ulio katika Kristo utaendelea na utakua kama ukilishwa, na chakula unachokihitaji ni Neno la Mungu.

Ingekuwa hatari kama tungekaa bila ya chakula kwa juma zima, na kujaribu kujifidia kwa kula chakula chote cha juma kwa siku moja. Kwa jinsi hiyo, tunatakiwa kuzilisha akili zetu kwa Neno la Mungu kila siku. Kama tukifanya hivyo, litajenga uelewa wetu wa Njia za Mungu, na tutakua katika neema na ufahamu.

### **Kuyasoma Maandiko yote**

Sehemu kadhaa za Biblia kama Zaburi na masimulizi katika Injili, zinasomeka kiurahisi. Lakini kuna sehemu zinazoelezea habari mbaya za uovu na vita, ambazo hatupendelei kuzisoma. Vifungu vingine vina orodha ndefu za majina ya watu au maeneo, na tunaweza hata kujiuliza ni kwa nini vimewekwa humo. Lakini, kama tulivyosoma katika 2 Tim. 3:16, kila Andiko ‘lafaa.....’ Hakuna sehemu ya Maandiko isiyo na manufaa. Watu wote wana mahitaji, hulka, mazingira na mazoea yanayotofautiana, na Maandiko yapo kuwaridhisha wote.

Kuanzia msitari wa kwanza wa Mwanzo mpaka msitari wa mwisho wa Ufunuo, Biblia yote ni ‘Andiko’ lenye pumzi ya Mungu. Ni kitabu chote kabisa. Kama tungekuwa ni kujichagulia, tungenesoma tu vifungu vile vinavyotupendeza. Kamwe tusingeyajua mafundisho mengine ya umuhimu mkubwa kwenye Biblia, kama yale yanayohusu uovu mkubwa ulio ndani ya mwanadamu, na Utakatifu wa hali ya juu alionao Mungu, na unyenyekevu na utii anaoutaka kutoka kwetu.

### **Unahitajika mpango**

Ili tuweze kuisoma Biblia yote, tunahitaji kuwa na mpango wa namna tunavyoisoma. Umekuwa ukiutumia mpango wako wa kujisomea Biblia uitwao ‘Bible Planner’? Kama bado, wakati umefika wa kuanza sasa kuweza kuisoma Biblia yako kwa namna inayovutia, na umewekewa mihtasari katika kijitabu hicho kukusaidia kuyaelewa mambo unayosoma.

Sasa, utakapokuwa umemaliza kuisoma Biblia kwa kuutumia mpango huu, nini kitafuata? Jibu ni kwamba, utakuwa umekuwa tayari kuendelea na usomaji wako wa Biblia wa kila siku kwa kutumia kijitabu kingine (au karatasi), chenye majedwali ya siku na miezi, na masomo ya kila siku. Hicho kinaitwa Mshirika wa Biblia (The Bible Companion). Kiambatisho hiki kitakufanya ulisome Agano la Kale lote mara moja, na Agano Jipya mara mbili kila mwaka. Utajiona unakua hasa katika kuijua Biblia yako.

Kumbuka pia kwamba, Wakristadelfia duniani pote wanaisoma Biblia kila siku kwa kumtumia ‘mshirika’ huyu. Wote wanataka kukua katika kulielewa Neno la Mungu, kwa hiyo hauko peke yako katika kusoma kwako.

## **VIDOKEZO MUHIMU.**

### **Namna ya kusoma**

Ni wazo zuri unapokaa chini kuanza usomaji wako wa Biblia wa kila siku, kusoma Sura za siku hiyo moja kwa moja kwanza, kuona kinachozungumziwa. Baada ya kumaliza kusoma, fumba macho yako na ujiulize, ‘hivi

nimesoma nini?’ Kuna wakati utakumbuka ulichosoma kirahisi, kuna wakati utaona shida kukumbuka. Kama ni hivyo, utahitaji kuvisoma tena vifungu hivyo.

Kumbuka: kila neno katika Maandiko ni la muhimu (kama hakukuwa na makosa kwa waliotafsiri kwenye Kiswahili).

### **Misaada mingine kwa kusoma Biblia**

Kama Biblia yako haina nafasi ya pembeni iliyoandikwa mistari au haina ramani, au imechapishwa kwa namna tofauti, usijali; bado ulilonalo ni Neno la Mungu. Lakini kwa wale walio na vitu kama hivyo vya kuwasaidia katika Biblia zao, vidokezo vifuatavyo vitawasaidia kuvitumia:

#### **a) Rejea za pembeni/chini**

Baadhi ya Biblia zina rejea za mistari pembeni au chini; nazo zitaweza kuwa msaada. Utaona kiherufi kidogo au namba ya neno, na hiyo herufi au namba inaweza kuonekana kwa pembeni au chini ya ukurasa huo. Ukiifuatilia itakuonesha kwa msitari huo kwenye Sura hiyo, Sura na mistari mingine inayosema kitu kinachofanana na hicho ulichosoma. Hili litakusaidia kuelewa zaidi msitari uliuousoma.

#### **b) Sura na mistari**

Tofauti na vitabu vingine vyote, Biblia imegawanywa katika Mistari na Sura. Mgawanyo huu ulifanywa mamia ya miaka baada ya Biblia kukamilika. Kwa vyovyote huu ni msaada mkubwa kutuongoza kupata tunapopataka, tena kwa haraka.

Lakini sio wakati wote unatusaidia sana. Mara nyingine mgao huo unaikata hadithi vipande viwili, kama lilivyo simulizi la Mathayo 16 na 17, la ‘kugeuzwa sura’ mlima. Msitari wa mwisho katika Sura ya 16 unasema: “Pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika Ufalme wake”.

Yesu anaongelea hapa maono ya Ufalme waliyopewa watatu kati ya wanafunzi wake: Petro, Yakobo na Yohana. Sura ya 17, inaanza na: “Na baada ya siku sita, Yesu akawatwaa Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye, akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani”. Kwa hiyo unapoanza kusoma Mathayo 17, inakubidi kuangalia nyuma kwenye msitari wa mwisho ya Sura ya 16 kwanza.

Ni wazo zuri, hata hivyo, wakati wote, kuangalia kinachosemewa kwa Sura unayoisoma, kwa kuona kwanza ni nini kilichotokea nyuma, kwa kuitafakari mistari ya karibu.

#### **c) Tumia ramani zilizopo**

Baadhi ya Biblia zina ramani kwa mbele au nyuma. Unaposoma juu ya tukio lililotokea mahali fulani, patafute katika ramani. Kama ukifanya hivyo kila mara kunapotajwa mji, mto, mlima au ziwa, utajikuta unaifahamu nchi ya Israeli vizuri zaidi unavyoendelea. Unaweza kuelewa hadithi hiyo vizuri zaidi pia.

Kwa mfano, utakaposoma Luka 2 (katika Hatua ya 1, Siku ya 3) katika mpango wako wa kwanza wa kujisomea Biblia (Bible Planner), utaiona miji ya Nazareti, Bethlehemu na Yerusalemu yote inavyokuja kwenye simulizi hilo. Sasa hebu itazame ramani na utaona kwamba, ilikuwa ni safari iliyokuwa ndefu kutoka Nazareti mpaka Bethlehemu, lakini Bethlehemu na Yerusalemu hapakuwa mbali. Unapata picha na kuelewa zaidi.

### **Soma Biblia yako kwa maombi**

Wakati wote unapokaa chini kuisoma Biblia yako, mwombe Mungu akusaidie katika kuelewa Neno lake. Kuna msitari katika Zaburi ya 119 ambao ni ombi. Unasema: “Unifumbue macho yangu, niyatazame maajabu yatokayo katika Sheria yako” (Zab. 119:18).

Tunahitaji msaada wa Mungu kuweza kuelewa, na yeye wakati wote yupo tayari kuutoa. Kwa hiyo, usisahau kuuomba!

### **Kusikia na kufanya**

Mungu atatufundisha kwa Neno lake, lakini kusoma hakutoshi. Yakobo anatuambia, tuwe: “Watendaji wa neno, wala sio wasikilizaji tu” (Yak. 1:22). Yesu anawaongelea wengine waliokuwa wakimwita “Bwana, Bwana”, lakini hawakuwa wakifanya yale aliyowaamuru wafanye. Soma mwenyewe katika Mathayo 25:31-46.

Sasa fungua Mathayo 7 na uisome habari katika msitari wa 24 mpaka wa 29, juu ya watu wawili ambao wote walijenga nyumba zinazofanana. Mtu anayeyasikia maneno ya Yesu, na **kufanya anayosema**, anafananishwa na mtu yule mwenye busara aliyejenga nyumba yake katika mwamba.






### **Ijee Biblia kwa unyenyekevu wa moyo**

Mwenyezi Mungu amesema:

“Lakini mtu huyu ndiye nitakayemwangalia, mtu aliye mnyonge, mwenye roho iliyopondeka, atetemekaye alisikiapo neno langu” (Isaya 66:2).

#### **Muhsatari**

Isome Biblia yako:

-  kila siku. Hakikisha kusoma kwako kunavifikia vitabu vyote vya Biblia.
-  kwa moyo uliofunguka, ukiwa unairuhusu ikufundishe.
-  kwa umakini; ufikirie kila msitari na hakikisha unauuelewa.
-  kwa kuomba. Mwombe Mungu akusaidie uweze kuelewa kile unachosoma.
-  kwa kunyenyekea; ukiwa unataka kujua vile Mungu anavyokutaka uishi.

**Vifungu vya kusoma:** Zaburi 19, Zaburi 119:1-40, Marko 8:34-38.

**Mistari ya kushika:** Zaburi 119: 33, 34

“Ee BWANA, unifundishe njia ya amri zako, nami nitaishika hata mwisho. Unifahamishe nami nitaishika sheria yako. Naam, nitaitii kwa moyo wangu wote”.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## USHIRIKA NA WALIO WA IMANI MOJA

**SOMO:** 1 Wakorintho 3

Mungu alipomuumba mtu, alikifikia kilele cha kazi yake ya uumbaji. Mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu (Mwanzo 1:27). Aliumbwa hivyo ili aweze kuwa kama Mungu; mwenye utashi uliojengeka wa kutambua lililo jema na baya.

Lakini kulikuwa, hata hivyo, na moja lililopungua; Adamu alikuwa peke yake. Kwa huruma na rehema ya Mungu, alitambua kuwa Adamu alihitaji mshirika. Kwa hiyo Mungu alimuambia mwanamke, akisema: “Si vema huyo mtu awe peke yake” (Mwanzo 2:18).

**Ushirika ni nini?**

Adamu na Hawa waliumbwa kila mmoja kwa ajili ya mwenzake, na walitakiwa wasaidiane (Mwanzo 2:18). Hawa alipoletwa kwa Adamu, Adamu alisema: “Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu” (Mwanzo 2:23). Na mwandishi, akiandika alilosema Mungu anaongeza kuwa, mume na mke wanapaswa, kwa sababu hiyo, kuambatana pamoja; kushikamana, kuwa kitu kimoja (Mwanzo 2:24).

Huu ulikuwa ndio ushirika; kushirikiana katika yote yale Mungu aliyowapa; kufurahiana mmoja kwa mwingine, na kuitambua kwa shukrani mibaraka yote ya Mungu katika maisha yao. Wakati Bwana Mungu alipokuwa akija bustanini kukiwa kumepoa, mtu na mkewe na Mungu walikuwa katika ushirika mzuri, mkamilifu, wa kupendeza. Lakini hili halikudumu.

Dhambi ilipoingia ulimwenguni, ushirika huo ulivunjika. Mungu ni Mtakatifu; hawezi kuikubali dhambi, na wadhambi hawawezi kukaa mbele yake; hawawezi kukaa katika ‘uwepo’ wa Utakatifu wake. Kulikuwa na mtengano uliotokea mara tu Sheria ya Mungu ilipovunjwa (soma Mwanzo 3 tena).

Mungu alipokuja akitembea bustanini siku hiyo ‘wakati wa jua kupunga’, Adamu na Hawa wakijijua kuwa wamekuwa uchi, walijificha; ushirika wao na Mungu ulikuwa umevunjika (Mwanzo 3:7,8).

Hili liliyaathiri pia mahusiano yao ya kibinadamu; Adamu alimlaumu Hawa kwa lile lililotokea. Uhusiano wao wa karibu na Mungu ulikuwa umefikia mwisho. Walikuwa sasa wakiweza tu kuukaribia ‘uwepo wake’ kwa njia aliyoiweka. Walilazimika kuiacha hiyo bustani, na maisha yakaanza kuwa magumu.

Ushirika na Mungu unabakia katika mpito huo huo, hata kama mazingira ya sisi kuutafuta yamekuwa tofauti sana. Tunapokuwa na ushirika na wenzetu, ina maana kuwa tunaweza kuishiriki mibaraka ya Mungu na wengine wanaoamini tunayoamini, na kuutumainia wokovu ule ule.

Ushirika huo unaweza ukawepo hata kati ya watu ambao hawajawahi kukutana, kwa kuandikiana au kupigiana simu. Ushirika unaweza kufanya kazi, mradi wanakuwa na imani moja katika Kristo.

Duniani pote watu wanakuwa na ushirika mmoja, wanapokuwa ndani ya familia ya Mungu. Ndivyo ilivyokuwa kwa Wayahudi. Ushirika sio sawa na kuelewana tu na mtu; ni uhusiano wa kiroho unaojengeka kwa kuamini mambo yanayofanana juu ya Mungu.

Ushirika ni umoja. Ushirika wa Kibiblia una maana ya kuwa na imani moja na matumaini, katika kuabudu.

**Roho na Kweli**

Katika mojawapo ya safari zake katika Israeli, Yesu alipitia Samaria, sehemu ya nchi walipokuwapo watu waliokuwa wakichukiwa na Wayahudi. Yesu hakuwa na dharau kama wao, na alipopumzika kando ya kisima, aliongea na mwanamke mmoja wa Kisamaria.



Haraka mwanamke huyo aligundua ya kuwa, Yesu hakuwa Myahudi wa kawaida. Alipomuuliza Yesu ni sehemu ipi kati ya maeneo matakatifu ya kukumbukwa, aliyofikiri ni ya muhimu zaidi: Mlima Gezirimu-karibu na walipokuwa wakiongelea, au eneo Yerusalemu ilipo, Yesu alimpa jibu ambalo kwa vyovyote lilimshangaza.

Yesu alimwambia, haupo mlima uliokuwa wa maana zaidi, na kuongeza: “Saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba **katika roho na kweli**, kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu” (Yohana 4:23).

Miaka kama 40 baada ya mazungumzo hayo, Yerusalemu na Mlima Gezirimu hayakuwa tena maeneo ya ibada. Majeshi ya Kirumi yalikuwa yameivamia nchi ya Israeli katika mwaka 70 (Baada ya Kristo), na kuyateketeza maeneo yake ya kidini. Wale Wayahudi waliopona katika shambulizi hilo, na ambao hawakutoroka, walichukuliwa mateka na kuuzwa kama watumwa.

Kwa hiyo, kama dini yao ilitegemea uwepo wa mahekalu na maeneo matakatifu, iliwabidi wayaache. Yesu alisema kuwa, ibada ya kweli isingehusiana kwa lolote na majengo au sehemu za ibada, ila na udhati katika kuamini, na katika kweli. Maneno ‘Roho na Kweli’ katika msitari huo hapo juu ni ya muhimu sana.

Kuna watu leo wanaodai kuwa wanaongozwa na roho, lakini unapongea nao, haraka unatambua ya kuwa hawajui Biblia inachosema. Watakuwa pengine wanaamini juu ya kwenda mbinguni baada ya kufa, wakati Biblia inachofundisha ni kuwa, tumaini la kweli la Mkristo la kuanzishwa Ufalme wa Mungu katika dunia.

Utakuta wanaamini pia kuwa Yesu Kristo ni sehemu iliyo katika Mungu aliye na nafsi tatu, wakati Biblia inafundisha kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, aliyezaliwa na bikira Mariamu kwa muujiza wa Mungu; kwa roho yake. Watu wanaodai kuwa wana ‘roho’ na hawajui ukweli ulio katika Biblia, lazima wamekosea.

Kutokana na hili, wanaomwabudu Mungu kwa dhati; kwa Roho na Kweli, hawatavutiwa na makanisa makubwa au sehemu za kuabudia, au idadi kubwa ya washirika, au kuvuma kwokwote kwa dhehebu. Kanisa la kweli halihusiani na majengo, ila ni watu; na haijalishi ni wangapi.

Cha muhimu zaidi kwao kinakuwa ni kile walichoamini, na namna wanavyomwabudu Mungu. Ni muhimu kuwa na moyo sahihi kiibada, lakini ni muhimu sana kuamini mambo yaliyo sahihi, na kufanya yaliyo sahihi mbele ya Mungu.

### **‘Jitenge’**

Agano Jipya linawaamuru wafuasi wa Yesu kujitenga na dunia. Hili halina maana ya kuiacha dunia; kitu ambacho hakiwezekani. Kinachosemewa ni kuishi kwa namna iliyo tofauti na ‘udunia’, kwa kuzifuata Njia za Mungu. Ibrahimu aliishi pamoja na Wakanaani, lakini alijitenga nao; hakuishi walivyokuwa wakiishi. Anaelezewa kuwa alikuwa ‘mgeni na msafiri juu ya nchi’ (Waebrania 11:13).

Imani na matumaini yake yalikuwa ni kwa Mungu na ahadi zake. Bwana Yesu aliwaombea wafuasi wake Mungu awatenge na maovu ya duniani, na kusema:

“Wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu. Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli. Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma hao ulimwenguni”

(Yohana 17:16 – 18).

Yesu Kristo na mitume wake waliichukulia dunia kama mahali pa udhalimu na uovu (1 Yohana 2:16). Imejaa watu wasio na haja na mambo ya Mungu, na wanaoifanya hali iwawie ngumu Wakristo wa kweli, wanaotaka kutii mambo Mungu anayoamuru. Tutambue hapa ya kwamba, hili linawahusu hata watu tunaowaona ‘wa dini’ sana. Wote wanaoupinga ukweli unaomhusu Mungu, wanaweza kuwapotosha waumini katika Njia ya Mungu.

### **Makao ya Mungu**

Wakristadelfia mara nyingi wanaulizwa, “Lipo wapi kanisa lenu?” Watu wanategemea kuona jengo zuri linaloweza kuwavutia na kuwafanya waamini kuwa, ‘hili ni kanisa kweli la Mungu’. Ni vigumu kwa watu hao

kutambua kuwa, Mungu anataka watu na sio majengo. Lakini hivi ndivyo hali ilivyokuwa hata katika siku za Yesu na za mitume.

Kulikuwa na majengo mazuri wakati huo ambamo baadhi yao walikwenda humo kuabudu, na hasa Hekalu lililokuwa katika Yerusalemu, lililochukua miaka 40 kujengwa na kurembwa. Lakini Yesu alisema Hekalu hilo lilikuwa ni pango la wezi na wanyang'anyi, na aliwataka wafuasi wake wamfuata, waachane na makuhani.

Yesu hakuwahi kujenga jengo la kanisa au kuwataka wafuasi wake wajenge. Chakula chake cha mwisho kabla hajasulubiwa alikila na wanafunzi wake kwenye nyumba ya mtu, katika 'chumba cha juu' katika Yerusalemu, na ndipo hapo mitume walipokwenda kuabudia kwa muda baada ya Yesu kufa na kufufuka (Matendo 1:13 na 12:12).

Ibada za mitume wakati wa kanisa la awali, zilifanyikia majumbani (Wakolosai 4:15) au kwenye vyumba vya kupanga (Matendo 28:23-31). Walitambua ukweli kwamba, wao ndio waliokuwa 'mahali' anapokaa Mungu; walikuwa ndio 'hekalu' lake. Naye Mungu alikuwa akitaka aishi ndani yao, na pamoja nao, kila siku ya maisha yao. Ni hivyo hata leo!

Mtume Paulo atakuwa alikuwa akizungumzia jengo, wakati alipowaambia waumini wa Korintho kwamba, kazi yake katika Korintho, alipokaa miezi 18, ilikuwa na matokeo ya kuwekea msingi jengo (1 Wakor. 3:10). Alichokuwa akimaanisha ni kuwa, alikuwa ameweka msingi wa Yesu Kristo, kwa kuwafundisha ukweli kama ulivyo kumhusu Mwana wa Mungu, aliyekufa kwa ajili yao na kufufuliwa na Mungu kwa uzima wa milele. Aliwaambia sasa walikuwa wakipaswa kujenga juu ya msingi huo, kwa namna walivyokuwa wakiishi na kuamini (1 Wakor. 3:12-15). Baada ya hapo aliongeza:

"Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?" (ms. 16). Paulo analizungumzia hili tena katika Waefeso 2:19-22.

### **Kumega Mkate**

Mkate na divai vinatukumbusha juu ya mwili na damu ya Yesu, vilivyotolewa msalabani kwa ajili ya ondoleo la dhambi zetu. Hakuna la kushangaza au la kutisha juu ya vitu hivi. Mkate haubadiliki kuwa nyama (kuwa mwili) wa Bwana Yesu, na divai haiwi damu, kama watu wengine wanavyoamini kimakosa.

Ni vitu vilivyokusudiwa tu kuwakumbusha wanaoamini, juu ya kazi kubwa aliyoifanya Yesu kwa ajili yao, na ni waumini waliobatizwa tu wanaoshiriki katika kumkumbuka kwa namna hii. Yesu alisema hivi kwa wanafunzi wake: "Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu" (Luka 22:19).

Kumega-Mkate huku ndipo chimbuko la ushirika wa Kikristo lilipo. Waumini wanafanya kila jitihada kuweza kukutana kila juma (pale wanapoweza), kumkumbuka Bwana wao na wokovu wake mkuu. Wanahitaji kukutana mara kwa mara kuweza kukua pamoja katika upendo na katika kweli. Andiko linasema:

"Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia" (Waebr. 10:24, 25).

### **Kuabudu pamoja au kipekee**

Kwa namna walivyofanya waumini katika karne ya kwanza, ndivyo Wakristadelfia wanavyofuata. Kila juma kama kuna waumini kadhaa wanaokaa katika eneo moja, wanakutana pamoja mahali ili kumwabudu Mungu. Kwa kawaida inakuwa Jumapili. Wanaita kusanyiko lao 'Eklesia', neno la Kiyunani lenye maana ya 'Kusanyiko', lililotafsiriwa 'Kanisa' katika Kiswahili. Kibiblia, kanisa ni watu, sio mahali na sio jengo.

Wanakutana kwa kujengana katika Neno la Mungu, Biblia, na kuweka mipango ya kuihubiri Injili kwa wasio-washirika. Kila juma wanakutana kwa ajili ya kumkumbuka Bwana Yesu kwa namna alivyoagiza, kwa kushiriki mkate na divai katika huduma wanayoita, 'Kumega-Mkate'.

Kama ilivyokuwa kwa waumini katika karne ya kwanza, nao hawana wachungaji au mapadri au makuhani kwa ajili ya kuongoza ibada, kwa kuwa Bwana Yesu ndiye Kuhani Mkuu wao. Waumini wa kiume wanashirikiana katika kuongoza huduma. Mmoja anayesimamia anapanga nyimbo za kuimbwa, masomo yatakayosomwa na atakayewalisha wenzake Neno. Huyo anakuwa ametaarifiwa mapema (au anakuwa ni huyo huyo anayeongoza). Anaongoza pia maombi, na anawakaribisha wengine kusaidia katika mambo haya.

Masomo ya Biblia yanayosomwa yanakuwa yanatoka kwenye kalenda yetu ya usomaji wetu wa Biblia wa kila siku (Bible Companion), yanayoangukia siku hiyo. Mawazo ya hao waliopo hapo yanapokuwa yamewekwa sawa kwa mahubiri hayo katika kumkumbuka Bwana Yesu, waumini wote wanashiriki mkate na divai, kama Yesu alivyofanya kwenye chakula kile rasmi, katika chumba kile cha juu zamani.

Kama hakuna waumini wengine katika eneo muumini alipo, ni lazima mambo hayo bado yafanyike kwa kadri hali inavyoruhusu. Wajibu wa kuwafundisha watoto na wengine juu ya Injili, utakuwa jukumu la kila siku la mtu (au familia), na siku za Jumapili Bwana Yesu ni lazima akumbukwe katika mkate na divai katika 'umegaji mkate' wa kibinafsi au kifamilia.

Kama mtu yupo katika upweke kabisa, bado atakuwa ameshirikiana na Wakristadelfia wengine popote pale walipo, ambao nao watakuwa wakifanya kitu hicho hicho siku hiyo duniani pote. Mungu anaweza kupenda kuita wapatikane waumini wengine katika eneo alipo, na kuwezesha kuanza kwa Eklesia nyingine ya watu wanaomwabudu kwa hapo.

#### **Muhtasari**

1. Ushirika wa Kikristo au wa Kibiblia una maana ya kuabudu pamoja kwa wale wanaoamini na kuyatumainia mambo yanayofanana, yaliyo sahihi Kimaandiko.
2. Ushirika wa Kibiblia una maana ya kujitenga na wale ambao hawaamini mambo yaliyo sahihi Kimaandiko.
3. Kwa kuwa sio vizuri mwanamume au mwanamke awe peke yake, ni vyema unapoamini utafute ushirika na waumini wenzako mara kwa mara kwa kadri inavyowezekana.
4. Ni lazima kuutafuta ushirika na Mungu na Bwana Yesu wakati wote kwa njia ya maombi, na kwa kuisoma Biblia na kuitafakari.
5. Tunamkaribia Mungu, na Bwana Yesu, na waumini wenzetu, tunaposhiriki mkate na divai katika Kumega kwetu Mkate.
6. Tutakuwa na ushirika ulio mkamilifu na Mungu katika Ufalme wake duniani.

**Vifungu vya kusoma:** 1 Yohana 1, Warumi 14-15:7, 1 Wakorintho 10

**Kuweka moyoni:** 2 Wakorintho 6:16

“Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, ya kwamba, Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu”.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## UWEZO YA ULIMI

SOMO: Yakobo 1

**Kiti cha Hukumu**

Yesu Kristo atakaporudi kuusimamisha Ufalme wa Mungu, kila mtu aliyejua na kuelewa ujumbe wa Injili, ataitwa kumpokea na atahukumiwa naye. Wale ambao wamekuwa waaminifu kwake katika maisha yao watapelele nafasi katika Ufalme huo, na wale ambao hawakuwa, watakatajiwa na Bwana na kuondolewa wafe.

Kigezo cha hukumu hiyo kitakuwa, ni kwa kiasi gani tumeufanyia kazi ujumbe wa Injili katika maisha yetu (Warumi 2:16). Katika hili, Yesu atakuwa hasa akiangalia ni kwa namna gani tumeutumia ulimi wetu. Anasema:

“Basi, nawaambia, kila neno lisilo maana watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu. Kwa kuwa, kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa”  
(Mathayo 12: 36, 37).

Yesu hatasikiliza ni nini watu wanasema juu yetu. Pamoja na mambo mengine, atatuhukumu kwa yale tuliyosema juu ya watu wengine; juu ya vile tulivyotumia ulimi tuliopewa. Kama maneno yetu ni ya ‘bure’; kama hatujali tunachosema kwa hiyo tunasema kwa kuwasononesha wengine, itatupasa kujibu kwa ajili yao kwa Yesu.

**Maneno yaliyo bora**

Kuna fundisho lingine katika maneno hayo ya Yesu, ambalo ni lazima tulifikiri. Wazo la maneno ya ‘bure’ ni maneno ya kizembe; maneno yasiyo na maana. Yesu alilitumia neno kama hilo katika mfano, wakati alipoongea juu ya wafanyakazi waliokaa bure, ‘wasiokuwa na kazi’, waliokuwa wamesimama sokoni (Mathayo 20:3).

Inatupasa tuwe macho juu ya yale tunayosema kwa wenzetu, kwa kutumia maneno yanayosaidia kuwajenga wengine. Tutumie ndimi zetu kwa namna ambayo inasaidia katika kuzifanya kazi za Bwana. Kuna njia nyingi za kufanya hili:

1. Tutumie ndimi zetu katika kuabudu pamoja na ndugu zetu, tukimsifu na kumshukuru Mungu (Wakolosai 3:15-17).
2. Tutumie pia kuongea maneno ya faraja na amani, kuleta utulivu kulipo na hasira au ghadhabu (Methali 15:1, Mathayo 5:9).
3. Tuongee au kutuma ujumbe, kuwasaidia wengine kimawazo na kuwatuliza walio kwenye shida (2 Wakorintho 1:1-11).
4. Tuwalishe wenye njaa kiroho kwa Neno la Mungu: “Midomo ya mwenye haki hulisha watu wengi; bali wapumbavu hufa kwa kuwa hawana ufahamu” (Methali 10:21).

Kuna mifano mingi katika Biblia ya wanaume na wanawake waliobadilisha namna zao za kufikiri na kuzungumza walipoamini Injili. Mtume Paulo anasema: “Maneno yenu yawe na neema siku zote”. Katika maongezi yetu yote tunapaswa kutambua kitu cha ajabu kabisa Mungu alichotufanyia; kutuokoa kwa neema yake.

Pengine mfano mzuri unaofahamika sana ni wa Petro. Yesu alipokamatwa, Petro aliapa akikana kwamba hakuwahi kumjua. Lakini tunaona jinsi ambavyo, miaka kadhaa baadaye alivyoandika maneno matamu juu ya namna tunavyopaswa kutumia ndimi zetu katika 1 Petro 3:8-16. Anahitimisha kifungu hicho kwa kusema:

“Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu. Nanyi mwe na dhamiri njema, ili katika neno lile mnalosingiziwa, watahayarishwe wale wautukanao mwenendo wenu mwema katika Kristo” (ms. 15, 16).

Huu ni mfano mzuri kwetu kuufuata!

### **Nguvu ya Ulimi**

Katika Waraka wake kwa Warumi, mtume Paulo anasema:

“Itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana”  
(War. 12:1).

Ni dhahiri kutokana na nyaraka alizoandika Paulo kuwa, maneno haya yalikuwa na maana ya dhati na ya kimatendo kwake. Alipobalizwa alibadilika na kuwa ‘mtumwa wa Mungu’ (War. 6:22), na kutambua kuwa, alipaswa kumtii Bwana wake mpya katika mambo yote. Katika kila kitu alichofanya na alichosema, Paulo alijaribu kumtii Mungu.

Huu ni mfano tunaajaribu kuufuata katika maisha yetu, tunapokuwa wafuasi waliobatizwa wa Bwana Yesu Kristo. Kama Paulo, tunaona ni kitu kigumu sana kumpendeza Mungu; tunajikuta mara nyingi tukimkiuka, lakini tunamtaka atusamehe kwa njia ya Yesu.

Biblia inatufundisha kuwa, ulimi una nafasi ya muhimu sana katika mapambano yetu na hulka yetu ya kibinadamu. Kile tunachosema na vile tunavyokisema inaweza kuwaonesha watu, zaidi kuliko yale yote tunayofanya, kama tu wafuasi wa kweli wa Kristo au siyo. Tunaambiwa:

“Mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake hutoa yaliyo mema, na mtu mwovu katika hazina mbovu ya moyo wake hutoa yaliyo maovu. Kwa kuwa mtu, kinywa chake hunena yale yaujazayo moyo wake”  
(Luka 6:45).

Hata tujitahidi kwa kiasi gani kuuficha ukweli huu, maneno yetu yatawaambia watu kile hasa kilichopo moyoni mwetu; mambo hasa tunayoamini.

Yakobo (ambaye inaaminika alikuwa mdogo wake Bwana Yesu), aliandika maneno mazito sana yanayohusu ulimi. Tafadhali uyasome katika Yakobo 3 kabla ya kuendelea mbele na somo hili. Tunaweza kuhitimisha Yakobo anayotufundisha kihivi:

1. Tusipende sana kufundisha wengine (yaani, kwa kutumia ndimi zetu kuwaambia wengine kitu cha kufanya); badala yake tuwe vielelezo. Mungu atayahukumu maneno ya wale wanaofanya hivyo (ms. 1).
2. Ingawa ulimi ni kiungo kidogo sana katika miili yetu, unaongoza mwelekeo wa maisha yetu yote (ms. 3-5).
3. Kile tunachosema kinaweza kikaleta shida kubwa sana. Ni kama kuwasha moto (kwa cheche tu), ukalipuka na kushindikana.

Kama tukimuudhi mtu kwa maneno tuliyosema, anaweza akatujibu vibaya, na maneno makali zaidi na zaidi yakaendelea, watu wakashindwa namna ya kuyatuliza (ms. 5-6).

Yakobo anasema hili ni jambo la hatari sana; ni kama kuwashwa, ‘moto na jehnum’. Yesu ni mtu mwingine pekee katika Biblia (ukimwacha Yakobo), aliyelitumia neno ‘jehnum’. Tunafahamu kuwa Jehnum lilikuwa ni ‘dampo’ la takataka nje kidogo ya jiji la Yerusalemu, mahali ambapo Wayahudi walitupia takataka zao kuteketezwa. Moto huo haukuwa ukizimika, na Yakobo anatumia kuwa, hasira na migogoro tunayoweza kuisababisha kwa maneno yetu ‘ya bure’; maneno ya kizembe, ni kama moto huo usiozimika.

4. Hakuna anayeweza kuudhibiti ulimi; umejaa sumu (ms. 8). Haya ni maneno yanayofanana na yale anayosema mwandishi wa Zaburi: “Watu wasio haki wamejitenga tangu kuzaliwa kwao, tangu tumboni wamepotea, wakisema uongo. Sumu yao, mfano wake ni sumu ya nyoka, mfano wao ni fira kiziwi azibaye sikio lake, asiyesikia sauti ya waganga, ijapo wanafanya uganga kwa ustadi” (Zab. 58:3-5).

Kama muumo wa nyoka unavyokuwa wa sumu na unavyoweza kuua, ndivyo ambavyo maneno ya mtu mwovu unavyoweza kusababisha madhara makubwa kiroho na hata kimwili.

5. Tusitumie ndimi zetu kumwabudu Mungu na kumsifu, na tena kwa kuwalaani wengine (ms. 9).
6. Ndimi zetu zinaonesha kilichopo mioyoni mwetu. Tunaporinga au kusema maneno yanayouma kwa wengine, tunakuwa tunasema ‘uongo juu ya kweli’ (ms. 14, 15).
7. Ni wajibu wetu kuongea maneno yanayoonesha hekima ya Mungu na hulka yake katika maisha yetu, na wakati wote tupende kufanya suluhu; kuleta amani (ms. 17, 15).

### **Ghadhabu**

Ni wakati tunapokuwa na hasira na mtu, tunapojisikia kusema maneno yanayouma. Tunaweza kuwa tumeudhiwa na kitu kilichosemwa juu yetu, na tunataka kumrudishia maudhi. Mfalme Daudi alikuwa mtu aliyelielewa hili vizuri. Alikuwa ameudhiwa mara nyingi katika maisha yake na mambo watu waovu waliyokuwa wakisema juu yake. Kwa hekima kubwa alisema uzeeni:

“Usikasirike kwa sababu ya watenda mabaya, usiwahusudu wafanyao ubatili. Maana kama majani watakatika mara, kama miche mibichi watanyauka. Umtumaini Bwana ukatende mema, ukae katika nchi, upendezwe na uaminifu. Nawe utajifurahisha kwa Bwana, naye atakupa haja za moyo wako. Umkabidhi BWANA njia yako, pia umtumaini, naye atafanya. Ataitokeza haki yako kama nuru, na hukumu yako kama adhuhuri. Ukae kimya mbele za BWANA, nawe umngojee kwa saburi; usimkasirikie yeye afanikiwaye katika njia yake, wala mtu afanyaye hila. Ukomesha hasira, uache ghadhabu, usikasirike, mwisho wake ni kutenda mabaya. Maana watenda mabaya wataharibiwa, bali wamngojeao BWANA ndio watakorithi nchi. Maana bado kitambo kidogo asiye haki hatakuwapo, utapaangalia mahali pake wala hatakuwepo. Bali wenye upole watairithi nchi, watajifurahisha na wingi wa amani” (Zaburi 37:1-11).

Ni ushauri wa maana sana uliopo katika maneno haya. Ni sharti tumtumaini Mungu, na sio kujali sana watu wengine wanayosema. Wale ambao ni wapole wa wenye kupenda amani watairithi nchi, lakini watu waovu watatoweshwa milele. Tumwachie Mungu mwenyewe kuhukumu, ni yeye anayeyajua mambo yote; tusiwalaani wengine kwa yale tunayosema juu yao.

Paulo anaongezea kitu katika ushauri huu:

“Muwe na hasira, ila msitende dhambi; jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka...Neno lolote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia. Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi. Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya. Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi” (Waefeso 4:26, 29-32).

Kama tunavyomuomba Mungu kwamba aweze kutusamehe dhambi zetu, na kwamba asiweke hasira juu yetu kwa sababu ya yale tunayofanya, nasi inatupasa tuwasamehe wengine kila siku kwa ajili ya yale wanayosema au wanayotufanyia. Kila siku kabla hatujalala, tunapaswa tuisafishe mioyo yetu na chuki yoyote tuliyoipata juu ya wengine. Inatubidi pia tujifunze kuwaomba msamaha wale tunaoweza kuwa tumewaudhi.

### **Umbea**

‘Umbea’ ni wakati tunaposema maneno ya ‘bure’; maneno mabaya juu ya watu nyuma ya migongo yao. Inaweza ikawa kitu cha ukweli au kitu cha uongo. Umbea ni dhambi na inafaa tuuepuke kabisa. Tusiwaongee

watu wengine kwa ndimi zetu, na haitupasi kusikiliza umbea juu ya wengine. Biblia iko wazi kwenye ujumbe wake juu ya hili. Inasema:

“Mtu mshupavu huondokeshwa fitina; na mchongezi huwafarakanisha rafiki” (Methali 16:28).

“Walijawa na udhalimu wa kila namna, uovu na tamaa na ubaya; wamejawa na husuda na uuaji, na fitina, na hadaa; watu wa nia mbaya, wenye kusengenya, wenye kusingizia, wenye kumchukia Mungu, wenye jeuri, wenye kutakabari, wenye majivuno, wenye kutunga mabaya, wasiowatii wazazi wao, wasio na ufahamu, wenye kuvunja maagano, wasiopenda jamaa zao, wasio na rehema, ambao wakijua sana hukumu ya haki ya Mungu, ya kwamba wayatendao hayo wamestahili mauti, wanatenda hayo; wala si hivyo tu, bali wanakubaliana nao wayatendao” (Warumi 1:29-32).

“Bali wajane walio vijana ukatae kuwaandika hao maana, wakizidiwa na tamaa kinyume cha Kristo, wataka kuolewa; nao wana hukumu ya kuwa wameiacha imani yao ya kwanza. Tena, pamoja na hayo, hujifunza kuwa wavivu, wakizunguka-zunguka nyumba kwa nyumba; wala si wavivu tu, lakini ni wachongezi na wadadisi, wakinena maneno yasiyowapasa. Basi napenda wajane ambao si wazee, waolewe, wazae watoto, watawale na madaraka ya nyumbani; ili wasimpe adui nafasi ya kulaumu” (1 Timotheo 5:11-14).

Kwa bahati mbaya, tunaona habari zinazowahusu watu wengine kama zinavutia, na hasa kama zina taarifa za kuchochewa, au zinakuwa na uovyo fulani. Wakati wote tunapohadithiwa kitu, inatupasa tumsimamishe na kumwambia anayesimulia kuwa, hatuvutiwi! Kuna maswali mawili ya msingi tunayopaswa kujiuliza kuhusu umbea:

1. Tungeweza kusema (au kusimuliwa) jambo hilo kama Bwana Yesu Kristo angekuwa hapo?
2. Tungeweza kusimulia jambo hilo kama mtu tunayemsema angekuwa yupo na anasikia?

### **Kufuru**

Matumizi mabaya, yaliyo mabaya sana ya ndimi zetu, ni wakati tunaposema mambo kinyume cha BWANA, Mungu mwenyewe, au kinyume na Mwanawe. Katika Amri 10, Mungu alisema:

“Usilitaje bure Jina la BWANA, Mungu wako; maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia, mtu alitajaye jina lake bure”

(Kumb. La Tor. 5:11).

Agano Jipya nalo linasema wazi kitu hicho hicho:

“Lakini sasa yawekeni mbali nanyi haya yote: hasira, na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu” (Wakolosai 3:8).

Neno lililotafsiriwa ‘matukano’ lilipaswa kutafsiriwa ‘kufuru’, maana ndivyo linavyoamaanisha. Ni neno ‘blasphemy’ kwa lugha ya Kingereza, katika Biblia ya Kingereza (KJV).

Tunapaswa kuliheshimu sana Jina la Bwana Mungu na la Mwanawe katika maisha yetu. Tusiyatumie kwa namna isiyo ya heshima. Tusiyatumie kimazoea, au kama sehemu ya lugha-mbaya, au kwa kuapa. Maana ya ‘**kukufuru**’ ni ‘**kuchukulia kwa dharau**’. Tunapolitumia ovyo jina la Mungu, tunaonesha hatumheshimu; tunamdharau.

Bwana Yesu alilipeleka fundisho hili mbele zaidi. Alisema tusiape kabisa, tusiape kwa ‘vichwa vyetu’ (Mathayo 5: 33-37). Leo, kama watu wakitaka kuonesha kuwa wanachosema ni kweli kabisa, wanasema kwa ‘kuapa mbele ya Mungu’. Hili linakuwa hasa linatakiwa, kama inatokea mtu kaitwa kutoa ushahidi mahakamani. Kamwe tusikubali kufanya hivyo.

Kama ‘shahidi’ ni kweli tunaweza tukatakiwa kuapa kwa Biblia, kwamba lile tutakalosema ni kweli kabisa, lakini mfuasi wa Bwana Yesu Kristo hatafanya hilo. Ataomba tu athibitishwe kuwa atakachosema ni kweli. Andiko linasema:

“Lakini zaidi ya yote, ndugu zangu, msiape, wala kwa mbingu wala kwa nchi; wala kwa kiapo kingine chochote; bali ndiyo yenu na iwe ndiyo, na siyo yenu iwe siyo, msije mkaangukia hukumu” (Yakobo 5:12).

### **Maneno ya upuuzi**

Ni rahisi sana kutumia ulimi tuliopewa, kwa namna ya kipuuzi. Tunaweza kushawishika kusimulia habari chafu, yenye matusi ndani yake. Tunaweza kutoa mzaha unaochekesha, unaowafanya wanaocheka wawabeze watu wengine. Tunaweza kuingia katika mjadala usio na maana; usio na manufaa yoyote. Yote haya ni ‘maneno ya upuuzi’, hayatusaidii kuwa wafuasi walio bora zaidi kwa Bwana wetu Yesu, na hayatufanyi kuwa kielelezo kizuri kwa wengine. Neno linasema:

“Lakini uasherati usitajwe kwenu kamwe, wala uchafu wowote wala kutamani, kama iwastahilivyo watakatifu; wala aibu wala maneno ya upuuzi wala ubishi, hayo hayapendezi; bali afadhali kushukuru” (Waefeso 5:3, 4).

“...wasimtukane mtu yeyote, wasiwe wagomvi, wawe wema, wakionyesha upole wote kwa watu wote...lakini maswali ya upuuzi ujiepushe nayo, na nasaba, na magomvi, na mashindano ya sheria kwa kuwa hayana faida, tena hayana maana. Mtu aliye mzushi, baada ya kumwonya mara ya kwanza na mara ya pili, mkatae; ukijua ya kuwa mtu kama huyo amepotoka tena atenda dhambi; maana amejihukumu hatia yeye mwenyewe” (Tito 3: 2,9-11).

### **Mfano wa Yesu**

Tunapohitaji hasa kujua namna ya kuongea mmoja kwa mwingine, tunahitaji kumtazama Bwana Yesu Kristo. Alikuwa mkamilifu kwa kila hali; kila neno alilotamka lilikuwa ni la Kimungu na sahihi. Nabii Isaya alinena juu yake kuwa:

“Hatateta wala hatapaza sauti yake; wala mtu hatasikia sauti yake njiani. Mwanzi uliopondeka hatauvunja, wala utambi utokao moshi hatauzima, hata ailetapo hukumu ikashinda” (Mathayo 12:19, 20).

Yesu hakupiga kelele wala kugombana. Wazo la ‘mwanzi uliopondeka na utambi utokao moshi’ ni lugha ya kiushairi; anasemea wale walio wadhaifu kiimani. Yesu hakuizima au kuivunja imani yao kwa maneno makali; alifanya aliloweza kuwafanya waendeleo na imani yao kwa huruma yake.

Watu walimdhiki na kumbeza Yesu. WaliOLEWA (pombe) walitunga nyimbo mbaya juu yake. Watu walimcheka na kumkejeli alipokuwa akining’nia msalabani, ikawa hivi:

“Alionewa, lakini alinyenyekea, wala hakufunua kinywa chake, kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni, na kama vile kondoo anyamazavyo mbele yao wakatao manyoya yake; Naam, hakufunua kinywa chake...Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; na pamoja na matajiri katika kufa kwake; ingawa hakutenda jeuri wala hapakuwa na hila kinywani mwake” (Isaya 53:7, 9).

“...Kwa sababu ndio mliloitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo zake. Yeye hakutenda dhambi, wala hila haikuonekana kinywani mwake. Yeye alipotukanwa, hakurudisha matukano; alipoteswa hakuogofya (hakutishia). Bali alijikabidhi kwake yeye ahukumuye kwa haki. Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa. Kwa maana mlikuwa mmepotea kama kondoo; lakini sasa mmemrudia Mchungaji na mwangalizi wa roho zenu” (1 Petro 2:21-25).

Hivi ndivyo tunavyopaswa kuutumia uwezo wa ndimi zetu. Hatukupewa uwezo uliopo katika kusema kwetu ili kujitetea, au kufanya mabishano makali. Tumepewa kusema maneno ya Mungu, kufuata mfano wa Bwana Yesu alivyokuwa katika maisha yetu ya kila siku, kusudi maneno yetu yawe ya kheri wakati wote na ya kumpendeza Mungu.



## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## HUDUMA YA KUMEGA MKATE

**SOMO:** Mathayo 26

Katika somo la 31 tuliona kwamba, ubatizo ni mwisho wa maisha yetu ya kwanza, na mwanzo wa maisha yetu mapya katika Kristo. Tunakuwa sehemu ya familia ya Mungu; wanawe wa kiume na wa kike, na kwa hiyo tunakuwa kwa pamoja ni **ndugu katika Kristo**. Tunakuwa ‘wafuasi’ wa Yesu; neno lenye maana ya ‘wanafunzi’; watu wanaojifunza kumfuata mtu. Tunaweka maisha yetu katika kuyafuata maneno ya Yesu na mfano wake. Mwenyewe alisema:

“Hakuna aliye na upendo mwingi kama huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake. Ninyi mmekuwa rafiki zangu mkitenda niwaamuruyo. Siwaiti tena watumwa, maana mtumwa hajui atendalo bwana wake; lakini ninyi nimewaita rafiki, kwa kuwa yote niliyoyasikia kwa Baba yangu nimewaarifu” (Yoh. 15:13-15).

Hili ni jambo la maana sana. Uhusiano wetu na Yesu unategemea sisi kuyafanya mambo anayotuagiza tufanye. Mojawapo ya mambo ya maana sana aliyotuamuru tufanye, ni kukutana mara kwa mara kula mkate na kunywa divai kwa kumkumbuka:

“Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu, **fanyeni hivi** kwa ukumbusho wangu”.

Kwa namna hiyo hiyo alichukua kikombe baada ya kula, akasema:

“Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; **fanyeni hivi** kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu”  
(1 Wakorintho 11:24-26).

Ibada ya pamoja kwa Wakristo wa kweli ni kitu kirahisi na chepesi. Ukiiondoa Ubatizo, Kumega Mkate ni kitendo pekee cha kiitikadi Bwana Yesu Kristo alichotuagiza kufanya; mengine ni watu wameongezea tu. Ni lazima tukipe uzito wake unaostahili.

Tunafahamu ya kuwa baada ya Yesu kupaa, wanafunzi wake walikutana kila siku nyumba kwa nyumba kumega mkate na kunywa divai kumkumbuka (Matendo 2:46,47). Baadaye eklesia zilikutana kila siku ya kwanza ya juma (Jumapili), kufanya hili. Kwenye Matendo 20:7 wanafunzi walipokuwa **wamekutana** katika siku ya kwanza ya juma **Kumega Mkate**, Paulo aliwahubiria.

Chini ya Sheria ya Musa, Wayahudi walikutana Jumamosi, siku ya mwisho ya juma, kwa ajili ya pumziko; Sabato. Wanafunzi wa Yesu waliamua kukutana katika siku ya kwanza ya juma, kwa kuwa ndiyo siku Yesu aliyofufuka kutoka kwa wafu. Uamuzi huu wa kukutana kila juma kwa namna hii, pengine ulifuatia kipengere cha Kimaandiko kilichohusu chakula cha kila juma, kilichokuwa kikiliwa na makuhani katika Agano la Kale, kilichoitwa ‘mkate-wa-wonyesho’ (Walawi 24:5-9).

Yesu alipotumia neno ‘ukumbusho’, alitumia neno lisilo la kawaida katika lugha ya Kiyunani lililopo kwenye Walawi 24:7. Kama mkate-wa-wonyesho ulivyokuwa wa kipekee, na wa thamani kwa makuhani katika nyakati za Agano la Kale (na ni makuhani tu walioruhusiwa kuula), ndivyo ambavyo Kumega-Mkate kulivyo kitu cha kipekee, kitakatifu, na cha thamani kubwa kwa wanafunzi wa kweli wa Yesu, wanaoshiriki kitendo hiki leo. Hawakifanyi na watu wengine, hata kama wanajiita Wakristo. Ni wale tu ambao ni ndugu wa kweli wa Kristo.

Kila mahali walipo Wakristadelfia duniani, wanakutana kila Jumapili kushiriki mkate na divai kwa pamoja kwa namna hii. Wanafanya hivi kwa kawaida katika kumbi au vyumba vya kupanga, na mara nyingine nyumbani mwa muumini mwenzao; haijalishi ni wapi.

Huduma yenyewe haina mambo mengi, na inafanana popote pale inapoendeshwa katika dunia. ‘Kumega Mkate’ kama tunavyokuita, ni sehemu ya muhimu sana ya ushirika wetu wa pamoja, na Wakristadelfia wanajua hivyo. Popote wanapokwenda kama kuna Eklezia, wanaweza kwenda kwenye Eklezia ya pale na kushiriki mkate na divai na wale wanaoabudu hapo.

Yesu alitoa maelekezo kadhaa kuhusu huduma hii. Tuyajadili moja moja:

### 1. ‘Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu’ (Luka 22:19)

Ni Yesu ambaye anapaswa kuwa chumbuko la mawazo yetu tunapokutana Kumega Mkate. Ndiye msingi, kwa hiyo mawazo yote yanapaswa kuwa kwake. Kama fikra zetu zipo kwenye migogoro na ndugu wengine, au katika matatizo ya kimaisha ya kila siku tuliyo nayo, tunakuwa tumeshindwa kuizingatia amri hiyo.

Neno ‘ukumbusho’ halina maana hapa ya kukumbukia tu kitu tulichosahau; maana yake ni **kuijaza akili yetu Yesu**. Tunakumbuka kuwa alikufa katika kipindi cha Pasaka. Haya yalikuwa majira ya mwaka ambapo Waisraeli walikumbuka namna ambavyo Mungu aliwaokoa kutoka katika utumwa, Misri. Alimteua Musa kuwaongoza watoke alfajiri baada ya usiku wa Pasaka, walipomchinja mwana-kondoo kifamilia na kumla pamoja kusherehekea wokovu wa Mungu.

Biblia inatufundisha kuwa, Kristo ndiye Mwana-kondoo wa kweli; alikufa kuwa dhabihu ya kuzichukua dhambi zetu. Kwa hiyo tunashiriki mkate na divai kila juma kukumbukia kuwa, kupitia katika kifo chake, tunaokolewa kutoka kwenye utumwa wa dhambi na mauti:

“Kwa maana Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka, yaani, Kristo; basi na tuifanye karamu (tule mkate na kunywa divai), si kwa chachu ya kale, wala kwa chachu ya uovu na ubaya, bali kwa yasiyochachika, ndio weupe wa moyo na kweli” (1 Wakorintho 5:7,8).

Tunapokunywa divai tunakumbuka kuwa, dhabihu ya Yesu ilileta mustakabali mpya wa Agano Jipya. Huu ni uhusiano mpya kati ya Mungu na watu wake. Mustakabali huu mpya unakamilisha ahadi zote za Mungu alizozifanya na watu katika enzi ya Agano la Kale. Yesu ni Mpatanishi wa Agano hili, na kwa sasa yupo mbinguni kuwakilisha maombi yetu kwa Mungu, na kutuomba msamaha wa dhambi zetu tunapoomba kuzikiri:

“(Yesu) sasa amepata huduma iliyo bora zaidi, kwa kadri alivyo mjumbe wa agano lililo bora, lililoamriwa juu ya ahadi zilizo bora”

(Waebrania 8:6).

Haya ni mambo yanayomhusu Bwana Yesu, ambayo tunapaswa yatujae katika akili zetu, tunapokuwa katika Kumega Mkate. Lakini kuna lingine zaidi.

Mtume Paulo aliandika maneno haya:

“Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo”

(1 Wakorintho 11:26).

Ni nani tunayemwonesha au kumtangazia mauti ya Bwana? Kwa hakika ni Bwana Mungu, na sisi wenyewe kwa wenyewe. Mkate na divai vinapopita kutoka kwa mmoja kwenda kwa mwingine, muumini kwa muumini, kila mmoja wetu anaonesha kutambua haja tuliyonayo ya dhabihu ya Yesu kwa ajili ya ondoleo la dhambi zetu. Tunaonesha kutambua pia kwamba, Yesu alikufa kwa ajili yetu na ndugu yetu pia.

Hili linasaidia kutuunga tuwe kitu kimoja katika ushirika wa kiimani. Tunakuwa mwili mmoja na waumini wenzetu tunaishi na kuabudu nao pamoja, wakati tukimngojea Bwana Yesu arudi:

“Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja”

(1 Wakor. 10:17)

## 2. ‘Lakini mtu ajihoji mwenyewe’ (1 Wakorintho 11:28)

Yesu hakusema kwamba tuchunguzane! Hatuendi kwenye Kumega Mkate tukiwa tunachunguza makosa ya wafuasi wengine! Tunajichunguza wenyewe kuona kama makusudi na nia zetu zipo kweli kwenye ibada yetu kwa Mungu.

Tunamkumbuka Yesu na maisha yake makamilifu ya utii, na kisha tunajipima kwa kujilinganisha naye. Hili kwa vyovyote litatufunya tujisikie wadhaifu sana mbele ya Mungu, maana ndivyo tulivyo. Kama tuna fikra zozote za kujiona wema-zaidi au bora-zaidi kuliko ndugu zetu, ni lazima tuziondoe kabla ya kula mkate na kunywa divai. Kuna tahadhari anayoitoa Yesu katika Mathayo 5:23,24. Tafadhali isome.

Kuna wakati ndugu wanashindwa kufanya hili. Wanakuja na ugomvi katika Kumega Mkate, au hawaji; wanajitenga. Wanafanya hivyo kwa kuwa wanashutumiana. Mtume Paulo aliandika maneno makali sana juu ya hao wanaofanya hivyo:

“Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana. Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe. Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokupambanua ule mwili. Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, na watu kadha wa kadha wamelala’ (1 Wakor. 11.27-30).

Hana maana ya kwamba ‘walio hawawezi na dhaifu’ walikuwa kimwili wagonjwa, bali kwamba ni wagonjwa kiroho, wanaelekea kufa (kama hao kadhaa waliokufa). Kama ambavyo tunahitaji chakula halisi kuifanya miili yetu iendeleo kuishi, ndivyo ambavyo tunahitaji chakula cha kiroho kwa njia ya mahubiri katika Kumega Mkate, ili tuweze kuendelea kuwa na uhai kiroho.

Tuwe macho! Ni rahisi wakati wote kuona makosa ya watu wengine kuliko kuyaona ya kwetu wenyewe (Mathayo 7:1-5). Tunapokuja kula mkate na kunywa divai, tunapaswa kuwa wakweli kabisa juu ya nafsi zetu mbele ya Mungu. Hata Yesu alijipima kwa namna hii muda mfupi kabla ya kufa msalabani.

Katika bustani ya Gethsemane, alikuwa na uchungu mkubwa alivyokuwa akishindana na nafsi yake. Alimwomba Mungu kwa huzuni amsadie ili aweze kuyafanya mapenzi yake Mungu na kulitimiza kusudi lake; aliomba ashinde udhaifu wake. Hivyo ndivyo nasi tunavyotakiwa kufanya tunavyojichunguza kabla ya kula na kunywa kwa kumkumbuka Yesu.

### **Mkate na Divai**

Sasa tuutazame mkate na divai. Luka anaandika maneno yafuatayo kuuhusu mkate:

“Akautwaa mkate, akashukuru, akaumega, akawapa, akisema, Huu ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu, fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu’ (Luka 22:19).

Tunapouchukua mkate na kuula, haubadiliki kimuujiza na kuwa sehemu ya mwili wa Yesu. Hakuna kitu kinachoitwa ‘mkate mtakatifu’ unaopaswa kutumika; tunatumia mkate wa kawaida katika kuabudu kwetu. Mkate ni alama (au ishara) ya mwili wa Yesu. Unawakilisha kwetu maisha yake yote, jinsi alivyokuwa na hulka kama yetu na alivyojaribiwa kama na sisi tunavyojaribiwa, lakini hakukosea.

Yesu hakufanya dhambi yoyote katika mambo yote aliyofanya; alipenda kuyafanya mambo Mungu anayoyapenda (Zaburi 40:8). Hili lilimfikisha msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. Haya ndiyo mambo tunayokumbuka tunapokula mkate.

Kuihusu divai Bwana Yesu alisema: “Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu, inayomwagika kwa ajili yenu” (Luka 22:20).

Biblia inasema waziwazi kuwa, kumwagika damu ni kitu cha lazima kwa Mungu kuweza kusamehe dhambi:

“Na katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo”  
(Waebrania 9:22).

Katika Sheria kulikuwa na dhabihu za wanyama, lakini hazikuwa na uwezo wa kuondoa dhambi. Dhambi zilikuwa zikifunikwa tu. Ni kwa kifo cha Yesu, kwa kumwagwa kwa damu yake, ndipo Mungu aliporidhia ondoleo la dhambi. Kila wakati tunapokuwa tukinywa divai, tunakumbuka hili. Linatukumbusha juu ya gharama kubwa sana iliyolipwa kwa ajili ya dhambi zetu.

Tunavyokunywa tusiruhusu kiburi chochote kikae ndani yetu. Hakuna nafasi ya chochote kingine zaidi ya kujinyenyekeza kabisa kwa kutambua kuwa, Mungu alitupenda sana, hata akamtoa Mwanawe wa pekee kufa kwa ajili ya dhambi zetu kuzisamehe:

“Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu, bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na hila, asiye na waa, yaani, ya Kristo” (1 Petro 1:18,19).

### **Mpaka ajapo**

Mpaka sasa tumetazama jinsi ibada ya Kumega Mkate inavyotukumbusha juu ya kifo cha Yesu Kristo. Wale ambao wanakula na kunywa kwa namna hii mara kwa mara, wanazijaza akili zao kumbukumbu hii ya Kristo, na hili linawasaidia katika ufuasi wao siku kwa siku. Kuabudu kwa namna hii ni kwa muhimu sana, ili tuweze kuendelea kuimarika kiroho.

Hata hivyo, kuna kipengere kingine katika Meza hiyo ya Bwana, ambacho mara kwa mara tunakisahau. Yesu alikuwa akitazamia kurudi kwake, na kuusimamisha Ufalme wa Mungu katika dunia. Aliwaambia wanafunzi wake:

“Nanyi ndinyi mliodumu pamoja nami katika majaribu yangu. Nami nawawekea ninyi Ufalme, kama vile Baba yangu alivyoniwekea mimi; mpate kula na kunywa mezani pangu katika ufalme wangu na kuketi katika viti vya enzi, huku mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli” (Luka 22:28-30).

Bwana Yesu atakaporudi, atakaa na wanafunzi wake na kula na kunywa pamoja nao katika Ufalme wake. Kwa hiyo, tunapokutana Kumega Mkate, tunafanya jambo la muhimu sana kwetu, litakalokamilishwa katika Ufalme wa Mungu.

Kila mfuasi wa kweli anataka kuwa katika Ufalme huo siku hiyo, na ni muhimu asikose kuwa katika ushirika wa Kumega Mkate, katika maisha yake ya sasa. Ni ushirika wa namna hii unaotupa nguvu tunavyoendelea kumsubiri Bwana wetu arudi:

“Basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu, njia ile aliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo katika pazia, yaani mwili wake, na kuwa na kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu; na tukaribie wenye moyo wa kweli; kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya; tumeoshwa miili kwa maji safi. Na tulishike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke; maana yeye aliyeahidi ni mwaminifu. Tuangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane, na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia” (Waebrania 10:19-25).

## MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

Karatasi ya Maswali: namba 10

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa 'Kazi ya ziada', unaweza kulijibu swali kama ukipenda au kuliacha kama unaona huliwezi. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

### MASOMO: 37- 40

37. (a) Wa-Beroya walikuwa ni watu gani?  
(b) Yesu alikuwa na Biblia ya Agano Jipya?  
(c) Tunatakiwa tusome Biblia zetu mara ngapi?  
(d) Ni sehemu zipi katika Biblia tunazopaswa kuzikosa tunaposoma?
- Kazi za ziada  
(e) Tunatumiaje mpango wetu wa kujisomea Biblia (Bible Reading Planner)?  
(f) Tunaposoma kitu kwenye Biblia zetu kuhusu jinsi tunavyopaswa kufanya, tunapaswa tupokeeje?
38. (a) Ushirika ni nini?  
(b) Elezea 'kujitenga'.  
(c) Kanisa lako liko wapi?  
(d) Tunapaswa tuabudu kwa pamoja au mmoja-mmoja?
39. (a) Toa njia tatu njema za kutumia ndimi zetu kwa kuongea mambo ya kujengana.  
(b) Ni kwa namna gani maneno yetu ni muhimu? Yanaonesha nini kutuhusu?  
(c) Tufanyeje na tusemeje wakati watu wanapokuwa wametukasirikia na wanasema maneno makali?  
(d) Kukufuru ni nini? Kwa nini ni kubaya?  
(e) Toa mifano mitatu ya namna ambavyo Yesu aliongea na watu.  
(f) Mistari ifuatayo kutoka katika Kitabu cha Methali inatufundisha nini?  
(a) 10:21      (b) 16:32      (c) 18:21      (d) 21:23.
40. (a) Kwa nini ni muhimu kwa wafuasi waliobatizwa kula mkate na kunywa divai mara kwa mara?  
(b) Ni kwa nini 'wajipime' kabla ya kufanya hivi?  
(c) Mkate unawakilisha nini?  
Divai inawakilisha nini?  
(d) Ni kwa namna gani huduma ya Kumega Mkate inatazamia kurudi kwa Bwana Yesu Kristo duniani?  
(e) Waumini wanapaswa kufikiri nini wakati wakila mkate na kunywa divai?  
(f) Waebrania 10:19-25 inamaanisha nini?

*Kumbuka kuweka jina lako, anwani na namba yako ya kumbukumbu katika karatasi yako ya majibu.*

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## MAISHA YA KIFAMILIA KATIKA HUDUMA YA YESU

## SOMO: 1 Petro 3

Hili somo ni kwa ajili ya wafuasi wa Yesu ambao bado wanaishi katika familia na wazazi wao, au wameoa au kuolewa, na sasa wana familia zao wenyewe.

Somo hili linalenga katika kuangalia kwa umakini 'familia', kwa kutaka kuona mambo yale ambayo ni mazuri juu yake. Tutaangalia pia kuona baadhi ya hasara za kuishi kimakundi. Ni muhimu kutambua kuwa, ingawa jamii zetu zinafofautiana sana tunapoangalia zilivyo sehemu moja ya dunia na nyingine, watu wote walitokana na chanzo kimoja. Wote wana Muumba mmoja ambaye ni Mungu, na ni Mungu aliyeifanya iwepo familia ya kwanza.

Katika masomo ya nyuma tumeiangalia familia ya kwanza ya Adamu na Hawa, na vijana wao Kaini na Habili, na pengine kuona ya kwamba, Adamu hakuwa baba mzuri sana. Inaekekea hakuwafundisha wanawe kutofautisha mema na mabaya. Hakuona, kwa mfano, ubaya uliokuwa katika wivu wa Kaini kwa ndugu yake Habili, na ni Mungu, sio Adamu, aliyegundua uuaji uliotokea na kumwadhibu Kaini.

Kama ukimfikiria zaidi Adamu utakumbuka ya kuwa, hakuwa mzuri sana katika kuukataa uovu yeye mwenyewe. Alikula tunda lililokatazwa bila kujihoji. Hili linatuleta katika hoja yetu ya kwanza ya muhimu: wajibu na umuhimu wa baba na mama katika kuiongoza familia. Katika siku za awali katika Biblia, jukumu hilo lilikuwa ni la mwanamume, akiwa ndiye msimamizi au kiongozi.

Mfano mzuri sana ni wa Ibrahimu. Alijitoea kuiongoza familia yake na watumishi wake wote katika njia ya imani kwa Mungu. Hili linaweza kuonekana katika kitabu cha Mwanzo. Katika 1 Petro 3:1-6 mtume Petro anawaandikia wanawake. Nasaha yake inapoisha, anawageukia wanaume, na kuwaambia, wake zao ni: 'warithi pamoja wa neema ya uzima' (ms. 7).

Upendo ni kitu tunachoona kikizungumziwa katika familia za awali kwenye Biblia. Katika Mwanzo 22:2 Ibrahimu anaagizwa kitu juu ya Isaka akiambiwa, "...mwana wako wa pekee, umpendaye", na tunaambiwa juu ya Isaka 'kumpenda' Rebeka katika Mwanzo 24:67.

Familia ni kiungo kilichowekwa na Mungu, na kama wazazi wakiwalea watoto wao katika upendo, kumjua Mungu na kuliheshimu Neno lake, watakuwa wamewawekea msingi mzuri wa maisha ya watoto wao kukulia.

Upendo kati ya watu wa familia moja ni wa muhimu sana, kama familia hiyo inataka kuwa ya furaha. Hekima na mamlaka ya wazazi ni vitu vya muhimu pia kujengwa. Paulo alimwandikia Timotheo juu ya kuvunjika kwa familia ambako kungetokea baadaye (2 Tim. 3:2).

Katika Waraka wake wa kwanza Paulo anatoa ushauri mzuri kwa wanaume na wanawake walio wafuasi wa Yesu. Kuna mambo ya muhimu kiibada, ambayo sio tu yale yanayosemwa na mtu katika kuomba. Yapo yanayokuwa mtindo wa maisha, ambayo ni namna ya kweli na ya dhati ya kuabudu.

Sura ya tatu ina orodha ya hulka ambazo Timotheo alipaswa aziangalie katika kuchagua wanaume, ambao wangekuwa wazee na viongozi wa eklesia zinazoanzishwa. Aliambiwa, mtu wa namna hiyo ni lazima: "Awe mwenye kuisimamia nyumba yake vema" (1 Tim. 3:4).

Ushauri huu wa Kibiblia unaohusu 'nidhamu ndani ya familia' unaweza ukawa uliandikwa kwa Timotheo, lakini ni muongozo wa wazi kwa wafuasi wa nyakati zote. Mfumo huo wa kimwenendo, kwa sasa ni kama umekataliwa karibu wote na jamii za kisasa katika nchi nyingi. Kuporomoka kwa maadili na kwa uimara wa familia, kumekuwa kukiongezeka kwa kasi katika miaka ya karibuni kwa kiwango cha kutisha.

Serikali nyingi zimetambua makosa katika sheria ambazo zimeweka, kwa kuruhusu talaka kutoka kirahisi. Hili limechochea kutengana na kufanya wazo la uwepo wa familia za mzazi mmoja kukubalika. Tatizo kwa sasa ni kwamba, kwa sasa ni vigumu na pengine haiwezekani kuuvunja mwelekeo huu wa hatari.

Utumiaji wa madawa ya kulevya kwa vijana wadogo na kuongezeka kunakotisha kwa ugonjwa wa UKIMWI, ni mifano michache tu ya majanga ambayo yanatokana na ukosefu wa nidhamu ya kibinafsi. Nidhamu hiyo inanzia kwenye familia, na watoto wadogo wanatakiwa wajifunze kwa kuiona kwa wazazi wao.

Ni vizuri sasa kuelezea kwa umakini kanuni ya kiimani ya 'nidhamu katika familia', kwa kuwa hii ni rahisi sana kutumiwa vibaya. Fungua sasa Waebrania 12 na utazame msitari wa I mpaka wa II. Mababa wanaokuwa na watoto jeuri au wenye tabia mbaya, wanaweza kuwa wakali mno au wapole mno. Hili sio sawa. Busara na haki vinaweza kutumika, na mwongozo wa msingi upo katika amri za Yesu kwa ajili ya wafuasi wake.

Baadhi ya Nchi za Kimagharibi kwa sasa zina sheria zinazokataza wazazi wasiwaadhibu watoto wao. Katika kifungu hiki uhusiano kati ya Mungu na Mwanawe, Bwana Yesu Kristo, umetolewa kama kielelezo. Mungu alikuwa tayari kwamba Mwanawe wa pekee apate mateso kwa ajili ya dhambi za ulimwengu.

Yesu akiwa ni Mwanawe aliyempenda na mwenye kuwajibika, alikuwa tayari kuyapokea mateso hayo. Tunaweza kamwe katika familia zetu tusiweze kufikia kiwango hicho cha udhibiti na utii wa kujitoa, lakini ni vizuri tuyatafakari maneno ya Paulo kwa undani.

Angalia msitari wa 7 kwanza na ulinganishe na msitari wa 9 na 10. Biblia inachofundisha hapa ni kwamba, wazazi wadhibiti nidhamu ya watoto wao; ikibidi wawaadhibu. Hawatakiwi wafanye hivyo kuwakomoa au kuondoa hasira zao, bali kwa upendo kwa ajili ya kumfundisha mtoto kwa faida yake.

Tutaangalia mada ya mateso katika Somo la 47, lakini kwa sasa ushauri wa msitari wa 11 ni kwamba, adhabu itamnufaisha mtoto kwa kumfanya atambue kuwa yeye ni sehemu ya familia yenye sheria. Sheria au kanuni hizo ni sharti zitokane na mafundisho ya Biblia.

Kwa hiyo, kusoma Biblia kunapaswa kuwe mahali pa kuanzia. Kama hatujui mafundisho na miongozo ya Mungu, na ile ya Yesu na mitume wake, tutawezaje kuleta mambo yake katika maisha yetu? Kuna uheri na utulivu katika kuwa karibu na Neno la Mungu. Usomaji wa Biblia wa pamoja unaweza kuwa kitu cha kutuelimisha na kutuburudisha.

Ni muhimu watoto watiwe moyo kujiunga na hili, na wasaidiwe wanapoyakuta maneno magumu. Wazazi wanaweza kuufanya muda huu wa kusoma Biblia kwa pamoja kuwa wa kusisimua sana, kama mambo yale wanayoyakuta yanaelezewa, na muhimu zaidi yanajadiliwa ili wote wapate fursa ya kuchangia mawazo yao.

Nyaraka za Paulo hazikuandikwa kwa kundi dogo la waumini tu, bali zilikusudiwa kwa eklesia zingine pia (unaweza kuliona hili katika Wakolosai 4:16). Jukumu kubwa la kuleta Agano la Kale la Wayahudi na Injili, pamoja na maandishi ya mitume na kitabu cha Ufunuo lilifanywa ili wafuasi, wa nyakati zote waweze kujengeka kutokana na Neno la Mungu. Mtume Petro, akiandika katika wakati ambao wafuasi wa Yesu walikuwa na Agano la Kale tu kama kiongozi chao, alitoa maoni ya nguvu. Unaweza kuyasoma hayo katika 1 Petro 1:19-21. Anasema Neno lenye pumzi ya Mungu linaaminika kwa kuwa, Mungu alikusudia tulipate.

Neno hilo limeandikwa na wanadamu wa kawaida, wasiodumu, lakini waliandika kile Mungu alichowakusudia waandike. Paulo anasema kitu kama hicho katika 2 Timotheo 3:14-17. Anatuambia sababu mojawapo ya Neno la Mungu ni 'kuonya na kuongoza', ili, "Mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema" (ms. 17). Utatambua hapa ya kuwa, Timotheo alikuwa akisoma na kujifunza Biblia yake tangu utotoni.

Pamoja na ushauri na muongozo huu mzuri, wazazi ni wanadamu na wanakosea. Mara nyingine wanafanya makosa makubwa yasiyoweza kusahaulika. Kwa mfano: kujiachia mara nyingine hasira na kuchukia kujionesha, na kutumika dhidi ya watoto wao.

Maneno makali na vitendo vya kikatili vimefanya familia nyingi zisambaratike. Sheria ya upendo kwa jirani yetu ni lazima ianzie nyumbani kwetu wenyewe, kwa kuwa na upendo kati ya wanandugu, na inapaswa iendelee wakati wa hali mbaya na nzuri, katika kujielekeza kuushinda ubaya.

Endapo wafuasi wanaona shida kutumia upendo na kusamehe nyumbani katika familia zao wenyewe, watawezaje kwa furaha kufanya kazi pamoja katika familia pana zaidi, ya undugu wa Kikristadelfia duniani? Kanuni zile zile za nidhamu kibinafsi na moyo wa Yesu katika eklesia, ni vitu vinavyotakiwa kuanzia nyumbani kwenye mioyo yetu wote.



## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## TATIZO LA DHAMBI

**SOMO:** Warumi 7

## Ulevi wa Dhambi

Kuna nguvu katika maisha ya kila mmoja wetu inayotushinda. Ni ulevi unaozidi ulevi wa pombe, kamari au madawa ya kulevya, nao ni **ulevi wa 'dhambi'**. Ni tatizo linalotukamata vibaya; tunakuta tumekosea na inakuwa vigumu kujizuia, na tunavutwa kuendelea hivyo.

Watu wengi hawautambui, na wanakana hawako katika hali ya ulevi huu. Lakini, ni kama mlevi anavyoweza kukana kuwa sio mlevi, kwa kuwa hataki kulikubali tatizo lake. Dhambi, inaleweshwa!

Lakini matokeo yake ni mabaya mno. Biblia inatuambia kuwa, matokeo ya kulewa dhambi ni mauti. Dhambi inaua: 'Mshahara wa dhambi ni mauti'. Katika Waraka kwa Warumi, mtume Paulo anatuambia juu ya tatizo hili katika maisha yake mwenyewe, akisema:

"Mimi ni mtu wa mwilini, nimeuzwa chini ya dhambi. Maana sijui nifanyalo, kwa sababu lile nilipendalo, silitendi; bali lile nilichukialo ndilo ninalolitenda. Lakini nikilitenda lile nisilolipenda, naikiri ile sheria ya kuwa ni njema. Basi sasa si mimi nafsi yangu ninayetenda hilo, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu. Kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi; bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo... Ole wangu, maskini mimi!" (Warumi 7:14-24).

Hiki ni kifungu kimojawapo kinachouchunguza sana moyo katika Agano Jipya. Paulo anatuambia kuwa, akilini mwake anataka kuzitii sheria za Mungu, lakini vitendo vyake ni vya ki-dhambi. Ni kama yeye ni watu wawili tofauti: mmoja ni mtu mwenye akili inayoelewa kuwa anatakiwa amtii Mungu; na kwa dhati anatamani kufanya hivyo, lakini, mwingine ni mtu ambaye wakati wote hamtii! Hili ni mojawapo kati ya matatizo makubwa kabisa ya 'ufuasi'.

Mara kwa mara tunajua lililo sahihi, lakini hatulifanyi katika maisha yetu. Ni kwa nini tuko hivyo? Sehemu ya jibu ni kwamba, tunaweza kuwa tunafurahia kuwa hivyo; kutofanya lililo sahihi! Hakuna anayetulazimisha kutenda dhambi; tunatenda dhambi kwa kuwa tunajisikia vizuri kufanya hivyo, hata kama tunajua hili linaweza kutufikisha kwenye mauti ya milele. Lakini, juu ya Musa tunaambiwa:

"Kwa imani Musa alipokuwa mtu mzima, akakataa kuitwa mwana wa binti Farao; akaona ni afadhali kupata mateso pamoja na watu wa Mungu, kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo" (Waebrania 11:24,25).

Katika Warumi 6 Paulo aliandika juu ya watu kuwa 'watumwa wa dhambi'. Dhambi ni 'bwana', ni mtawala huyu. Dhambi inawatawala watu na kuwaongoza. Ni vizuri tutambue ya kwamba, ni mtawala jeuri sana huyu, anayewalipa wafanyakazi wake kifo. Anawazalia mauti! Ni mara nyingi Biblia inaionesha dhambi kwa namna hiyo. Ni nguvu inayotawala juu yetu, na hatuwezi kuikwepa kwa jitihada zetu wenyewe.

Sehemu ya pili ya jibu ni kwamba, tunaona vigumu kumtii Mungu. Hata tunapokuwa tunajua lililo sahihi na tunapojaribu kulifanya, mara nyingi tunashindwa. Nia ya kuwa wafuasi wa kweli wa Bwana Yesu Kristo inapaswa iwe ndani ya mioyo yetu. Kama tukijaribu kumfuata kwa kulazimishwa, kwa hakika, hatutaweza. Kama tukitaka kumfuata kwa sababu mioyo yetu imejaa kumpenda na Baba yake, kwa ajili ya wokovu uliowekwa mbele yetu, tutakuwa tumeanza ufuasi wetu vizuri; na kwa neema ya Mungu tutaendelea vizuri, kwa dhamiri iliyo sahihi. Andiko linasema:

"Na mmojawapo wa waandishi akafika, akawasikia wakisemezana naye, akatambua ya kuwa (Yesu) amewajibu vema, akamuuliza, katika amri zote ni ipi iliyo ya kwanza? Na Yesu akamjibu, Ya kwanza ndiyo hii,

Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote” (Marko 12:28-30).

### Dhambi ni nini?

Dhambi ni kuzikiuka sheria za Mungu, na adhabu yake ni kifo:

“Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti, na hivyo mauti imewafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi... Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki” (Warumi 5:12,19).

Tunahitaji kurudi nyuma kwenye Bustani ya Edeni ili tuweze kuona kilichokuwa chanzo cha dhambi. Hapo mwanzo, Mungu alipokuwa amemuumba Adamu, alimpa amri moja tu ya kutii. Adamu alikatazwa asile tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya (Mwanzo 2:17). Mungu alimuonya kuwa kama angekula, kwa hakika angekufa. Ni kwa nini alipewa sheria ya namna hiyo? Adamu na Hawa waliumbwa kumpa Mungu ‘utukufu’ kwa kulitii Neno lake. Waliumbwa wawe na matakwa huru; wachague wenyewe kama wamtii Mungu au wasimtii.

Sheria hii iliwapima walikuwa na moyo wa kujitoa kwa Mungu kwa kiasi gani; wangukuwa na imani ya kumtii Mungu au wangemkiuka. Mungu alikuwa sio tu Muumba-Mkuu aliyeiumba dunia, alikuwa pia ni YEYE aliyekuwa juu ya vitu vyote, ambaye Neno lake halipaswi kuvunjwa. Adamu alipomtii Mungu, alionesha kulitambua hili na kulikubali; alipomkiuka, aliukana uweza wa Mungu na mamlaka yake juu yake. Kifungu kwa Warumi kinasema:

“Kwa kuwa mambo ya Mungu yanayojulikana yamekuwa dhahiri ndani yao, kwa maana Mungu aliwadhihirishia. Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumba ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani uweza wake wa milele na Uungu wake: hata wasiwe na udhuru; kwa sababu walipomjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu wala kumshukuru; bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza. Wakijinena kuwa wenye hekima walipumbazika; wakaubadili utukufu wa Mungu asiye na uharibifu kwa mfano wa sura ya binadamu aliye na uharibifu, na ya ndege, na ya wanyama, na ya vitambaavyo. Kwa ajili ya hayo Mungu aliwaacha katika tamaa za mioyo yao, waufuate uchafu, hata wakavunjiana heshima miili yao. Kwa maana waliibadili kweli ya Mungu kuwa uongo, wakamsujudia kiumbe na kukiabudu badala ya Muumba anayehimidiwa milele. Amina” (Warumi 1:19-25).

Ingawa maneno haya hayakuandikwa moja kwa moja kuwahusu Adamu na Hawa, mengi yanayosemwa yanahusiana na maisha yao, na yanatusaidia kuona jinsi dhambi ilivyoingia ulimwenguni. Inaoneshwa kwamba:

1. Uweza wa Mungu ulioneshwa kwa watu, kwa vitu Mungu alivyoviumba (Zaburi 19). Adamu na Hawa walilipuuza hili.
2. Dhambi ilianza kwenye akili ya Hawa, alipoamua kuwa alichokitaka kilikuwa ni cha muhimu zaidi kwake kuliko kuitii amri ya Mungu. Kujaribiwa kwake na dhambi ili amkiuke Mungu, kulimwingia moyoni na akilini. Alilitamani lile tunda la ule mti, likamvuta kulila (Mwanzo 3:6).
3. Hawa alifikiri angeerevuka kwa ujanja wake mwenyewe, kwa kulila tunda lililokatazwa. Kwa kufanya hivi aliukana uweza uliopo katika Neno la Mungu wa kumhekimisha ‘hata apate wokovu’ (2 Timotheo 3:15).
4. Aliamua kuwa Sheria ya Mungu haikuwa hasa kweli, ila uongo; na kama akilila tunda asingekufa kikweli. Kwa hiyo alilila na kumpa mumewe ambaye naye alikula.
5. Kwa vitendo vyao walijiweka wenyewe mbele na kile walichotaka, kuliko kumjali Mungu.

Walikuwa wakipaswa kumwabudu Mungu, Muumba, kwa kuwa watiifu kwake. Ukweli huu wa mwisho (kipengere cha 5), unatupa ukweli wa muhimu sana. Ibada kwa Mungu ni **kumjali na kuwa watiifu kwake** katika maisha yetu ya kila siku; sio tu kwa kukutana pamoja kumsifu siku za Jumapili.

Kwa hiyo, dhambi sio tu kutozitia amri za Mungu; ni kukana pia uwepo wake kama Muumba aliyetuumba sisi wote. Tukilitambua hili na kulipokea, litabadili mtizamo wetu wote wa maisha.

### **Kumtupia mwingine lawama**

Adamu alijua nini kingetokea hata kabla ya kufanya dhambi, kwa kuwa: “Kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria” (Warumi 3:20).

Mungu alipompa Adamu amri hiyo moja, alimwambia dhambi yenyewe ilivyo na matokeo yake – kifo! Adamu na Hawa waliona shida kuwajibika kwa kitendo chao; na sisi ndivyo tunavyofanya. Sisi wote tunataka kumtupia mtu mwingine lawama kwa makosa yetu. Adamu alisema:

“Huyu mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala”. Na Hawa alijitetea, akisema: “Nyoka alinidanganya, nikala”.

Mafundisho potofu yaliyoenea juu ya ibilisi na shetani, yanatokana na hiyo nia ya kumlaumu mtu mwingine kwa ajili ya dhambi zetu. Tunapokosea, ni rahisi sana kulaumu ‘shetani’ badala ya kukubali kuwa tatizo liko ndani yetu. Tunajidanganya kuwa sisi tuko safi, hatuna dhambi; wa kulaumiwa ni ibilisi, anayesababisha. Nabii Yeria kwa kulitambua tatizo, alisema: “Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha” (Yer. 17:9).

Lakini Biblia haitaki tujiongopee, inasema:

- ✚ “(Yesu) Akasema, kimtokacho mtu ndicho kimtiacho unajisi. Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wivi, uuaji, uzinzi, tamaa mbaya, ukorofi, hila, ufasidi, kijicho, matukano, kiburi, upumbavu. Haya yote yaliyo maovu yatoka ndani, nayo yamtia mtu unajisi” (Marko 7:20-23).
- ✚ “Mtu ajaribiwapo, asiseme, Ninajaribiwa na Mungu; maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu. Lakini kila mmoja **hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa**. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti. Ndugu zangu wapenzi, **msidanganyike**” (Yakobo 1:13-16).

Nyoka alichofanya kwanza kilikuwa ni kuweka wazo la kula tunda lililokatazwa, kwenye akili ya Hawa. Tangu hapo, kwenye Biblia, nyoka amekuwa ishara ya ‘nguvu ya dhambi na matokeo yake’ katika maisha yetu. Tamaa hii ya kujifurahisha wenyewe badala ya kutaka kumfurahisha Mungu inatuvuta tusimtii; inatuvuta tufanye dhambi. Hebu angalia vifungu hivi vitatu vinavyofuata, vinavyotambua juu ya watu wasiomtii Mungu:

- ✚ “Mtu asiwadanganye kwa maneno yasiyo na maana, kwa kuwa kwa sababu ya hayo hasira ya Mungu huwajia wana wa uasi” (Waefeso 5:6).
- ✚ “Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu. Katika hili watoto wa Mungu ni dhahiri, na watoto wa ibilisi nao. Mtu yeyote asiyetenda haki hatokani na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu yake” (1 Yohana 3:9-10).
- ✚ “Hata alipoona wengi miongoni mwa mafarisayo na masudukayo wakiujia ubatizo wake, aliwaambia, Enyi wazao wa nyoka, ni nani aliyewaonya nini kuikimbia hasira inayokuja?” (Mathayo 3:7).

Katika mfano wa ‘Mpanzi’ katika Luka 8 Yesu anatuambia kuwa, ‘mbegu ni neno la Mungu’ (ms. 11). Kwa hiyo wale wanaolichukua Neno la Mungu katika mioyo yao na katika maisha yao, wanaweza kuelezewa kama wanaochukua ‘mbegu ya Mungu’; wanakuwa ‘uzao wake’. Ni kile Neno hilo linachofanya ndani yao ndicho kinachosaidia kuwafanya wawe ‘watoto wa Mungu’, na kuanza maisha mapya. Matokeo yake ni kwamba, wanaweza kujitoa kwa Mungu sasa, badala ya kuendelea kuwa ‘watumwa wa dhambi’.

Lakini mistari hiyo inatuambia pia juu ya daraja lingine la watu. Ni hao wanaoupuuza ukweli wa Neno la Mungu na kuendelea na namna zao wenyewe za maisha. Hao wanaelezewa kuwa ni ‘wana wa uasi’, ‘watoto wa ibilisi’ na ‘wazao wa nyoka’. Wako kama Adamu, aliyemwacha Mungu na kumkiuka kwa makusudi.

Tumeshaona kuwa, mauti ni adhabu inayotokana na dhambi. Kila siku tunavyoendelea kukua na kuwa wakubwa na kuzeeka, na miili yetu inapoanza kuchoka, tunaonesha lilivyo kweli Neno la Mungu. Hatimaye, tunakufa! Tunaweza kumkana Mungu kwa maneno na matendo yetu, tunaweza kujifanya hayupo, lakini hakuna tunachoweza kufanya kuyashinda mauti.

Mauti ni adhabu iliyowekwa juu yetu kwa sababu ya dhambi. Dhambi inatutenganisha na Mungu, lakini kuna lingine linalotokana na dhambi. Inatupeleka mbali na Mungu. Nabii Isaya, anasema: “Maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hata hataki kusikia” (Isaya 59:2).

Adamu na Hawa walipofanya dhambi, walihukumiwa kifo. Waliondolewa na Mungu watoke katika Bustani ya Edeni. Hili ndilo hasa balaa la dhambi. Adamu alipoondoka katika Bustani hiyo, alipoteza ushirika wake wa kila siku aliokuwa akiufurahia na Mungu. Nguvu ya Mungu na Neno lake katika maisha ya Adamu ilipungua siku baada ya siku.

Mawazo yake yaliendelea kirahisi zaidi kujaa tamaa zake, na hivyo ikawa rahisi zaidi kwake kuendelea kuanguka dhambini. Hii ndio maana ya Yakobo kuongelea, ‘kuvutwa na kudanganywa na uovu’. Maana yake ni kwamba, dhambi inatuvuta mbali na Mungu.

Tunapokuja kutambua mafundisho haya ya ukweli kuhusu ‘dhambi’ kama yalivyo katika Biblia, yatakuwa na mguso mkubwa katika maisha yetu. Tunaweza kuhitimisha kihivi:

1. Kwanza ni lazima tutambue kuwa, kwa mambo yoyote yale mabaya tunayofanyiana, hatimaye tunayekuwa tumemkosea ni Mungu. Ni Neno lake tunalolikiuka.
2. Kila kitu ambacho kinaikiuka sheria ya Mungu hakikubaliki kwake, na yote ni ‘dhambi’.
3. Kama tumeyaweka maisha yetu kwa Mungu kupitia kwa Mwanawe, Yesu Kristo, hatuwezi kuendelea katika dhambi.
4. Kuyaweka maisha yetu kwa Mungu hakuna maana kwamba tutakuwa wakamilifu, watu wasiokosea. Ni Yesu tu aliyekuwa hivyo!

Mungu hatawakubali watu wanaosema ni wafuasi wa Yesu, lakini hawafanyi jitihada zozote kumfuata kwa namna wanavyoishi maisha yao, wakati wamebatizwa. Maisha yetu ni sharti yabadilishwe na kumfahamu kwetu Kristo. Mwenyewe alisema:

“Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni” (Mathayo 7:21).

### **Kuipata tena Njia ya Mungu**

Mwanzoni kabisa mwa huduma yake, Yesu alipanda mlimani na kuanza kuwafundisha wanafunzi wake kwa maneno matamu ya mibaraka, akisema:

“Heri walio maskini wa roho, maana ufalme wa mbinguni ni wao” (Mathayo 5:3). ‘Maskini wa roho’ ni watu ambao wanajua wanavyomhitaji Mungu. Mahusiano yetu na Mungu ndipo yanapotakiwa kuanzia.

Ni hapo tunapotambua mioyo yetu ilivyo na jinsi dhambi ilivyo ndani yetu, na vile inavyotutenganisha na Mungu, ndipo tunapoelewa tunavyomhitaji Mungu katika maisha yetu. Ndipo tunapoweza kuwa tayari kuanza safari ya kumrudia na kumkaribia Mungu kwa maombi, na kuitaka rehema yake na msamaha.

Kama tunamkaribia kwa namna hii, tunajua kuwa atatupokea kama wanawe, kupitia kwa Bwana Yesu Kristo. Dhambi haitakuwa tena ‘bwana’ katika maisha yetu. Mwishoni mwa maneno yale machungu ya kujichunguza katika Warumi 7, mtume Paulo alisema:

“Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti? Namshukuru Mungu, kwa Yesu Kristo Bwana wetu!

(War. 7: 24,25).

Ujumbe mwema wa faraja wa Biblia, ni wa wokovu dhidi ya dhambi na matokeo yake, kupitia kwa Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Kwa hiyo Paulo aliendelea kusema:

“Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti” (Warumi 8:1,2).

Tunapaswa kwa mioyo yetu kumshukuru Mungu na kufurahi kutokana na hili. Hii ni Habari Njema, ni ujumbe wa Injili unaohitimishwa kwa msitari mmoja:

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3:16).

Tunapojitoa kwa Bwana Yesu Kristo kuwa wafuasi wake, tunaanza maisha mapya. Dhambi zetu zinasamehewa bure na Mungu aliyejaa huruma na rehema, ambaye hapendi yeyote apotee. Anapenda watu wote wamkubali Mwanawe na kutembea kuelekea Ufalme wake.

Sehemu iliyobaki ya kozi yetu hii inachunguza mafundisho ya Biblia yanayohusu maisha haya mapya katika Kristo, na kile yanachomaanisha kwa kila mmoja wetu. Neno la BWANA linasema:

“Sheria ya BWANA ni kamilifu, huiburudisha nafsi.

Ushuhuda wa BWANA ni amini, humtia mjinga hekima.

Maagizo ya BWANA ni ya adili, huufurahisha moyo.

Amri ya BWANA ni safi, huyatia macho nuru.

Kicho cha BWANA ni kitakatifu, kinadumu milele.

Hukumu za BWANA ni kweli, zina haki kabisa.

Ni za kutamanika kuliko dhahabu, kuliko wingi wa dhahabu safi.

Nazo ni tamu kuliko asali, kuliko sega la asali.

Tena mtumishi wako huonywa kwazo,

Katika kuzishika kuna thawabu nyingi” (Zaburi 19:7-11).

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## NENO LA MUNGU KATIKA MAISHA YETU YA KILA SIKU

**SOMO:** Kumb. la Torati 6

**Israeli wakiwa Nyikani**

Agano la Kale linatupa simulizi la ajabu la namna Mungu alivyowaokoa watu wake, Israeli, kutoka katika nchi ya Misri. Walikuwa wamekaa hapo wakiwa watumwa kwa zaidi ya miaka 200. Walikuwa wameteswa, na mfalme (Farao) alijaribu kuwaua watoto wa kiume wote waliozaliwa kwa Wayahudi. Israeli walimlilia Mungu wakimueleza taabu yao, na Mungu alisikia kilio chao na kumtuma mwokozi wao, Musa, kuwatoa katika Misri.

Wokovu wao ulitegemea kutii kikamilifu maneno ya Mungu kupitia kwa Musa. Kushindwa kuyatii kungewapelekea kuangamia. Waliambiwa kuiadhimisha karamu ya Pasaka kwa pamoja usiku mmoja. Waliagizwa wakae ndani ya nyumba zao mpaka Mungu awaite, alafu, katika usiku huo waondoke Misri kwa pamoja. Mungu aliwaambia kuwa, Musa angewaongoza kwenda kwenye nchi ya Israeli, nchi aliyokuwa amemuahidia Ibrahimu miaka mingi nyuma.

Walipoondoka walifuatiwa na majeshi ya Farao mpaka kwenye ukingo wa Bahari ya Shamu. Mmoja kati ya miujiza mikubwa kabisa katika Biblia ulitokea; Mungu aliyatenga maji ya Bahari ya Shamu ili Israeli waweze kuvuka kwenda ng'ambo, na alilizamisha jeshi la Misri lilipojaribu kuwafuatia. Mtume Paulo anatumambia kwamba, tukio hili lilikuwa mfano wa ubatizo:

“Baba zetu walikuwa wote chini ya wingu; wote wakapita kati ya bahari; wote wakabatizwa wawe wa Musa katika wingu na katika bahari” (1 Wakorintho 10:1,2).

Ndani ya miezi kadhaa, Israeli walikuwa wamefika Sinai kuzipokea sheria za Mungu. Kwa shauku walimuahidi Musa kuwa, wangemtii huyu Mungu aliyewaokoa:

“BWANA akamwita (Musa) toka mlima ule, akisema, Utawaambia nyumba ya Yakobo, na kuwaarifu wana wa Israeli, maneno haya... Sasa basi, ikiwa mtaitii sauti yangu kweli kweli, na kulishika agano langu, hapo ndipo mtakapokuwa tunu kwangu kuliko makabila yote ya watu; maana dunia yote ni mali yangu, nanyi mtakuwa kwangu ufalme wa makuhani, na taifa takatifu. Hayo ndiyo maneno utakayowaambia wana wa Israeli. Musa akaenda akawaita wazee wa watu, akawafunulia maneno hayo yote BWANA aliyokuwa amemwagiza. Watu wote wakaitika pamoja wakisema, Hayo yote aliyoyasema BWANA tutayatenda” (Kutoka 19:3-8).

Ilikuwa ni katika maisha yao ya kila siku ambapo sasa Mungu aliwajaribu, kuona kama walikuwa na maana kweli ya lile walilosema. Walipokuwa na njaa na kiu, Je, wangepakumbuka maneno ya Mungu na kumtumaini, au wangepasahau lile waliloitikia?

Mojawapo ya matukio ya kuhuzunisha sana katika Biblia, ni habari ya jinsi watu wazima wote (kasoro wawili), waliokuwa wametoa ile ahadi kwa Mungu, ‘walivyomwangusha’ Mungu. Walikufa humo nyikani kutokana na dhambi yao, kwa hiyo hawakuwahi kuiingia Nchi ya Ahadi.

Muda mfupi kabla ya Musa kufa, aliwafundisha wana wa hao walioangamizwa humo nyikani somo kubwa kwa ajili ya maisha yao, kusudi na wao wasianguke:

“Na hii ndiyo sheria, na amri, na hukumu, alizoziamuru BWANA, Mungu wenu, mfundishwe, mpate kuzitenda katika nchi ile mnayoivukia kuimiliki; upate kumcha BWANA, Mungu wako, kushika amri zake zote na sheria zake, ninazokuamuru, wewe na mwanao, na mwana wa mwanao, siku zote za maisha yako; tena siku zako ziongezwe. Sikiza basi, Ee Israeli, ukaangalie kuzitenda; upate kufanikiwa, mpate kuongezeka sana, kama BWANA, Mungu wa baba zako alivyokuahidi, katika nchi ijaayo maziwa na asali.

Sikiza, Ee Israeli, BWANA, Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja. Nawe mpende BWANA, Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote. Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako, nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako. Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako” (Kumb. La Torati 6:1-9).

Jambo moja liko wazi katika nasaha hizo; maneno ya Mungu yalipaswa yawe na sehemu muhimu katika maisha yao ya kila siku. Walikuwa wayaseme wakati wote, na kuwafundisha watoto wao juu yake. Ilikuwa tu ni kwa njia ya kuyafanya Maandiko kuwa sehemu ya kila kitu wakifanyacho, ndipo wangeweza kukumbuka umuhimu wa maneno ya Mungu na kuyatii.

Hebu ona ulinganisho kati ya Wana wa Israeli na sisi hapa. Maisha yetu yamekusudiwa yawe kama yao!

<b>Wana wa Israeli</b>	<b>Wafuasi wa Yesu leo</b>
Walikuwa watumwa Misri	Kabla ya ubatizo tulikuwa watumwa wa dhambi.
Mwana-kondoo wa Pasaka alitolewa na Mungu kuwa dhabihu ya kuwaokoa	Bwana Yesu Kristo ametolewa na Mungu kuwa dhabihu. Amekufa msalabani kutuokoa.
Israeli waliyaacha maisha ya utumwa Misri	Ni lazima tuyaache maisha yetu ya awali ya utumwa wa dhambi.
Israeli waliivuka Bahari ya Shamu	Tumebatizwa.
Waliambiwa maagizo hayo ni lazima yawe sehenu ya maisha yao ya kila siku	Ni lazima tuisome Biblia kila siku, na kuiruhusu itufundishe na kutuongoza katika kila kitu tunachofanya.
Israeli hawakumtii Mungu na wakafa nyikani. Hawakuifikia Nchi ya Ahadi	Kama Biblia haikuwa sehemu ya maisha yetu ya kila siku, hatutaufikia Ufalme wa Mungu.

### **Biblia inamaanisha nini kwako?**

Inashangaza mara nyingine kuona wafuasi ambao hawajali kuisoma Biblia, na kujifunza inachosema katika maisha yao ya kila siku, wakati wanategemea kuwa na sehemu katika Ufalme wa Mungu Yesu atakaporudi. Kama hatuoni jinsi Neno la Mungu linavyosisimua na kutuvutia sasa, kama hatutaki kujifunza kutoka kwake kila siku, tunawezaje kutegemea nafasi katika Ufalme huo ambao Biblia ndiyo msingi wake?

Tafadhali yafikirie maswali yafuatayo, na ujaribu kuyajibu kwa ukweli na moyo wako kwa ajili yako mwenyewe:

1. Ni kwa nini Biblia ni ya muhimu kwako? Inakufanya ujione ‘wa maana’ tu kuwa nayo, au ni sehemu ya muhimu ya maisha yako?
2. Unaifungua na kuisoma mara kwa mara kiasi gani: Kila siku? Kila juma? Mara moja-moja? Unaisoma yote au vile vifungu tu unavyovipendelea?
3. Unaweza kuifungua vizuri: Unajua Zaburi kilipo? Yuda kipo wapi? Mika je?
4. Unaweza kupata vifungu vya Biblia kuwaambia watu wengine unayoamini?

### **Kwa nini ni ‘ngumu’ kueleweka?**

Sehemu za Biblia ni ngumu kueleweka. Mungu hakuiandika kwa namna ambayo inatupa majibu mara tunapoisoma. Hebu yaangalie maneno haya:

“Mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu, asema BWANA” (Isaya 55:8).

Katika somo letu la nyuma tuliona ya kwamba, toba ni lazima ituongoze kwenye mabadiliko makubwa katika maisha yetu. Ni lazima tuache namna yetu ya kwanza ya maisha, na tuanze maisha mapya ambayo ni 'ya Ki-Mungu' (sio tena ya kiubinafsi). Hili ni gumu sana, na hasa mtu anapoanza. Anajikuta kama vile hawezi hasa kuyaelewa maneno ya Mungu. Mawazo na fikra za Mungu anazona safi na zakupendeza, lakini hazitui moyoni kwa namna ya kumfanya achukue hatua. Sababu ni kwamba, akili zetu sisi zinawaza zaidi dhambi!

Ni lazima tuanze kufikiri kwa namna nyingine; tuyafanye mawazo ya Mungu na njia zake kuwa zetu. Tunajifunzia wapi haya? Ni katika Biblia, lakini ni lazima tufanye kuyachimbua! Kama tutakuwa Wafalme; ni sharti kwa sasa tuyachunguze Maandiko kuona yote Mungu anayotufundisha kumhusu YEYE na kusudi lake. Hili ndilo litakalotupa ushirika na Bwana Yesu Kristo katika Ufalme wa Mungu, atakaporudi. Kwa kadri tutakavyofanya hivyo ndivyo imani yetu kwake itakavyojengeka. Andiko linasema:

“Ni utukufu wa Mungu kuficha jambo, bali ni utukufu wa mfalme kuchunguza jambo” (Methali 25:2).

### **Neno lenye pumzi ya Mungu**

Biblia ina madai ya kipekee juu yake yenyewe; inadai ni neno lenye, 'Pumzi ya Mungu'; ikiwa na maana tu ya kwamba 'imetokana na Mungu'. Kama ambavyo tunatumia pumzi (hewa) iliyoko kwenye mapafu yetu kuipa nguvu sauti yetu na kutufanya tusikike, ndivyo ambavyo Biblia inavyotupa picha ya Mungu kusema nasi maneno. Mtume Paulo aliandika juu ya hili katika Waraka wake kwa Timotheo, akimwambia:

“Bali wewe ukae katika mambo yale uliyofundishwa na kuhakikishwa, kwa maana unajua ni akina nani ambao ulijifunza kwao; na ya kuwa, tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu. Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema” (2 Tim. 3:14-17).

Kuna hoja kadhaa za maana sana zinazotolewa katika mistari hii:

1. Biblia yote kabisa ni Neno lenye pumzi ya Mungu. Tunapata maelekezo ya kutusaidia na kututia moyo katika vitabu vya Agano la Kale, kama tunavyofundishwa na kutiwa moyo na ujumbe wa Injili katika Agano Jipya. Bila ya 'kila Andiko', kukua kwetu kiroho kama wanafunzi wa Yesu kusingekuwa kamili.
2. Tunawezaje kujifunza juu ya 'tendo jema' tunalotakiwa tulifanye katika maisha yetu, bila ya kuyasoma matendo mema katika Biblia?
3. Timotheo alikuwa amejifunza juu ya Mungu katika Biblia. Kujifunza kwake kulimfanya aamini kwa dhati ukweli wa mambo hayo; alifundishwa na 'kuhakikishwa'. Imani yake ilikuwa imekua. Alikuwa akifundishwa juu ya Biblia tangu utoto wake. Tunapoangalia katika 2 Timotheo 1:5 tunaona kuwa, alifundishwa na mama yake na bibi yake. Hili ni somo la muhimu sana juu ya jinsi tunavyopaswa kuwafundisha watoto wetu na wajukuu wetu.
4. Sasa alikuwa akipaswa kuendelea katika mambo hayo aliyojifunza na kuyaamini. Hii ilikuwa nasaha ya muhimu sana. Hakupaswa kusema sasa amejua vya kutosha na hahitaji kusoma na kujifunza Biblia tena. Kusoma Biblia kulikuwa kuwe sehemu inayoendelea katika maisha yake ya kila siku. Katika hili Yesu alifundisha kuwa: “Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu” (Mathayo 4:4). Mtu hawezi kuishi kwa ugali au ubwabwa au ndizi tu. Mahitaji yake ya kila siku ni pamoja na chakula cha kiroho; Neno linalotoka katika kinywa cha BWANA.

### **Kwa nini ni muhimu kusoma Biblia?**

Tunajua kuwa, kama hatukula mara kwa mara tutakufa kwa njaa. Chakula cha kawaida ni cha muhimu sana kwa uhai. Chakula cha kiroho nacho ni cha muhimu hivyo hivyo. Bila ya chakula cha kiroho cha kila siku kutoka katika Biblia, tutakufa kiroho na kuukosa Ufalme wa Mungu. Kama tukijilisha Neno la Mungu kila siku, tutakua kiroho. Tunaambiwa, Neno la Mungu:



- ✚ Lina uhai na lina nguvu inayotusaidia kuipima mioyo yetu kiukweli, kuona kile hasa tunachodhamiria (Waebrania 4:12).
- ✚ Linatupa nguvu ya kukabiliana na tamaa za dhambi ambazo zipo ndani ya kila mmoja wetu (Zaburi 119: 9-11).
- ✚ Lina uwezo wa kutujenga na kutuimarisha kiroho (Matendo 20:32, 1 Petro 2:1-2).
- ✚ Linatuonya tunapokosea (2 Tim. 3:16).
- ✚ Linatusaidia kutufanya tujitenge na dunia iliyojaa uovu (Yoh. 17:14-17).
- ✚ Linajenga imani yetu (Warumi 10:17).
- ✚ Linatupa mifano ya namna tunavyopaswa kuishi maisha yetu kama watu tunaomcha Mungu (Wakolosai 3:1-17).
- ✚ Linatufunulia lengo alionalo Mungu kwa dunia yake, na kwa watu watakaoishi duniani katika Ufalme wa Mungu (Zaburi 72).
- ✚ Zaidi ya yote linatambia juu ya yote upendo wa Mungu katika kumtoa Bwana Yesu Kristo kwa ajili ya wokovu wetu, na jinsi tunavyopaswa kuuonesha upendo huo kwa wengine (1 Yohana 4:7-21).

### **Neno lililofanyika mwili**

Biblia inatufundisha juu ya Yesu Kristo. Anaelezewa kuwa ni ‘Neno aliyefanyika mwili’. Kwa hili tunaielewa kuwa, aliishi kulingana na Neno la Mungu muda wote siku kwa siku. Kwake yeye kwa kweli Neno la Mungu lilikuwa ni ‘taa ya miguu’ yake, na ‘mwanga wa njia’ yake (Zab. 119:105).

Ni Biblia yake iliyomuonesha namna ya kuishi masaa yote kila siku, kwa namna iliyompendeza Baba yake. Muda mfupi kabla ya kufa, Yesu alimwomba Baba yake kwa ajili ya wanafunzi wake. Tunapata maombi haya katika Yohana 17. Alisema ameikamilisha kazi ambayo Mungu alimpa aifanye. Alikuwa amewafundisha wafuasi wake juu ya Mungu; amewapa ujumbe wa Mungu kwa maneno yale yale Mungu aliyosema naye:

“Kwa sababu mimi sikunena kwa nafsi yangu tu; bali Baba aliyenipeleka, yeye mwenyewe ameniagiza nitakayonena na nitakayosema. Nami najua ya kuwa agizo lake ni uzima wa milele; basi hayo ninenayo mimi, kama baba alivyoniambia, ndivyo ninenavyo” (Yohana 12:49, 50).

Nasaha zake hizi zilikuwa za muhimu kwa kuwa, alikuwa akikaribia kuwaacha na kupaa mbinguni. Wangehitaji nini ili waweze kuendelea kwa nguvu wakati hayupo? Ni Neno la Mungu! Anawaombea: “Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli” (Yohana 17:17).

Maombi yake haya ni kwa ajili yetu hata leo. Ni kupitia katika Neno la Mungu katika maisha yetu kila siku ndipo tutakapoweza kukua kiroho kuwa kama Yesu. Litatusaidia kujitenga na uovu uliopo katika dunia, na litatusaidia kuweza kujiweka sawa kumpokea Bwana Yesu Kristo katika kurudi kwake.

### **Namna ya kukua kiroho**

1. Soma Biblia yako kila siku. Tumia Mpango wa Usomaji wa Biblia (Bible Reading Planner) au Mshirika wa Biblia (Bible Companion), utakaopewa na mkufunzi wako ili uweze kuhakikisha unasoma sehemu zote za Biblia.
2. Kabla ya kusoma, muombe Mungu akusaidia uweze kuelewa unachosoma.
3. Kama unayo familia, watie moyo musome wote.
4. Weka orodha ya maswali katika daftari lako juu ya kile unachokisoma lakini hukielewi. Unaweza baada ya hapo kumuuliza mkufunzi wako au Mkristadelfia yeyote kukusaidia majibu ya maswali hayo.
5. Tafakari kile unachosoma. Kama utajipa muda wa kufanya hivi, hili ni jambo jema sana. Lakini, uyafikirie pia mambo unayosoma katika Biblia katika maisha yako ya kila siku, na ujaribu kuyaweka uliyojifunza katika matendo.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## KANISA LA MUNGU

## SOMO: 1 Timotheo 3

Wanaume na wanawake wanapobatizwa katika Kristo, wanakuwa watu wa Mungu, na kuwa sehemu ya familia yake. Mungu aliamuru kuwa wanawe wawe katika jumua ya kiimani, kwa dunia yote, na ametueleza wazi jinsi ambavyo hili lingekuwa. Neno linasema:

“Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo. Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani...” (1 Wakorintho 12:12,13).

Katika Biblia ya Kingereza, umoja huu unaitwa ‘church’, kwa Kiswahili ‘kanisa’, na katika lugha ya Kiyunani, ambayo ndiyo iliyotumika katika kuandikwa Agano Jipya, neno maalumu lililotumika ni neno ‘Ekllesia’. Ekllesia ni kundi la watu waliokusanywa pamoja kwa lengo maalumu, na kuna matumizi ya neno hilo katika Agano Jipya yanayoonesha hili. Katika Matendo 19 tunasoma juu ya muda Paulo alioutumia katika Efeso, na matatizo aliyoyapata yaliyoletwa na baadhi ya watu wa mji huo:

“Wakati huo kukatokia ghasia si haba katika habari ya Njia ile. Kwa maana mtu mmoja jina lake Demetrio, mfua fedha, aliyekuwa akifanya vihekalu vya fedha vya Artemi, alikuwa akiwapatia mafundi faida nyingi. **Akawakusanya** hao, pamoja na wengine wenye kazi ile ile, akasema, Enyi wanaume, mnajua ya kuwa utajiri wetu hutoka katika kazi hii.... Basi wengine walikuwa wakilia hivi na wengine hivi, kwa maana ule **mkutano** (eklesia) ulikuwa umechafuka-chafuka, na wengi wao hawakuijua sababu ya kukusanyika kwao pamoja” (Matendo 19:24-25, 32).

Hao mafundi walikuwa wamekusanywa pamoja na mtu huyo mwovu, Demetrio, kumpinga mtume Paulo.

Mungu amewakusanya watu pamoja kuwa ekllesia yake; kuwa ‘mkutano’, kwa lengo la wao kumwabudu na kuwa watu wa familia yake.

Matumizi ya kwanza ya neno ‘eklesia’ katika Agano la Kale kwenye Biblia ya Kiyunani, yako katika kitabu cha Kumbukumbu La Torati. Lilitumika kuelezea vile ambavyo wana wa Israeli walivyokuwa tofauti na mataifa mengine yote yaliyokuwa yakiwazunguka. Walikuwa wametolewa Misri na Mungu, na alikuwa akiwaongoza kuiendea Nchi ya Ahadi. Walikuwa wameitwa kwa sababu hiyo, na hivyo walikuwa ni ekllesia yake; ekllesia ya Mungu. Hivyo ndivyo ilivyo kwa kanisa la Mungu hata leo. Linaundwa na watu walio tofauti na wengine, na wameitwa watoke katika dunia ili Mungu aweze kuwaongoza kuuelekea Ufalme wake.

Bahati ya kuwa sehemu ya kanisa la Mungu, ni ya wale tu ambao wamebatiziwa, “Habari njema za Ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo” (Matendo 8:12). Wafuasi wa kweli wanajitenga na ulimwengu, na wanatambua kuwa hawawezi kikweli kumwabudu Mungu na watu wengine wanaojiita Wakristo, wakati hawaelewi au hawaukubali ujumbe wa kweli wa Injili. Wito wa kuwa sehemu ya ekllesia ya Mungu ni wito wa kujitenga. Mtume Paulo aliandika juu ya hili kwa ekllesia ya Wakorintho na kusema:

“Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema ya kwamba, Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. Kwa hiyo, tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana, msiguse kitu kilicho kichafu, nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa kwangu wanangu, wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi” (2 Wakor. 6:16-18).

Ni heshima kubwa kuwa sehemu ya eklesia ya Mungu, na waumini waliobatizwa wanapokutana kuabudu, wakati wote wanalikumbuka hili. Mungu amewaitia mambo haya na wasiyapuuze. Wanaambiwa:

“Na mlishike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke; maana yeye aliyeahidi ni mwaminifu; tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri: wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia” (Waebr. 10:23-25).

Katika Waraka wake kwa Waefeso, Paulo alielezea eklesia kama ni mahali ambapo waumini wanakua kiroho. Akitumia neno lenye maana ya ‘kujengana’, aliandika kuwa, ndani ya mfumo wa eklesia, ndugu wangeweza:

- Kukua katika uelewa na ufahamu (4:13-15).
- Kukua katika upendo, na kwa hiyo kuimarisha na kuijenga eklesia (4:15,16).

Hata hivyo anatuambia kuwa, hili lingeweza kutokea tu kama kila muumini katika eklesia angejihusisha na kuichangia (4:16). Aliandika kuwa, watu walio ndani yake ni ‘mwili’ mmoja, na alitumia usemi huu kama mara kumi katika barua zake. Kwa mfano:

“Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja tuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja; vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo, kila mmoja kwa mwenzake”  
(Warumi 12:4, 5).

Usemi huu, ‘mwili mmoja’, unaelezea ukaribu unaokuwapo, ndugu wanavyokuwa wakiishi na kuabudu pamoja kama sehemu ya familia ya Mungu, na Paulo anaandika mambo yafuatayo juu yake:

1. Kama ambavyo tulivyo na viungo tofauti-tofauti vyetu wenyewe, ndivyo vilivyo viungo tofauti-tofauti kwenye mwili wa kiroho. Sio kila muumini wa kiume au wa kike anafanana na mwingine, au wanaweza kufanya kazi moja katika eklesia. Lakini, kila mmoja ni wa muhimu na anathaminiwa na Mungu, na ana jukumu lake la kutekeleza katika mwili wa Kristo. Sisi wote tunahitajiana, kama tunavyovihitaji viungo vyote vya miili yetu, kwa mwili kuweza kufanya kazi vizuri (Warumi 12:4,5; 1 Wakorintho 12:12,20).
2. Mkubwa wa mwili huu ni Kristo (Waefeso 4:15,16). Ni Yeye ndiye mwenye mamlaka juu ya mwili huo, na hakuna mamlaka ya kibinadamu duniani iliyo na mamlaka juu yake.
3. Tofauti za kirangi au kitaifa, au jinsia, hazina maana. Mungu anawathamini watoto wake wote na wote ni sawa (Wagalatia 3:26-29).
4. Ingawa kuna mwili mmoja (eklesia moja) ambamo Kristo ndiye kiongozi wake (Waef. 5:23), mwili huo unaelezewa kuwa una matawi mengi. Kwa hiyo Paulo aliliandikia: “Kanisa la Mungu lililoko Korintho” (2 Wakor. 1:1) na makanisa mengine. Popote pale wafuasi wa kweli wa Yesu wanapokutana kuabudu, ni eklesia ya Mungu.

Tunahitaji basi kuangalia majukumu mbali mbali yaliyopo katika eklesia, na kufikiria ni nini Biblia inachotambua juu yake.

### **Mikutano ya kikazi ya Eklesia**

Baada ya kupaa kwa Bwana Yesu Kristo, eklesia iliyokuwa Yerusalemu ilipanuka haraka, na haraka ikaonekana kuwa ilihitaji watu wa ziada wa kupanga mambo na kuisimamia. Maelezo juu ya hili yanapatikana katika Matendo 6:1-7, na hili linatuwekea utaratibu wa namna eklesia zinavyopaswa kujipanga leo. Tunaweza kuorodhesha vipengere vya msingi kihivi:

1. Jukumu kubwa la viongozi (mitume) waliokuwa wakisimamia lilikuwa kuhubiri, kuomba na kufundisha Neno la Mungu.
2. Hata hivyo walihitaji msaada, hasa-haswa kwenye mambo ya kiuchungaji (malezi na ushauri), kwa ajili ya kuwatunza ndugu walioko katika eklesia.

3. Viongozi hawakufanya maamuzi peke yao, bali waliwaita ndugu wote pamoja kwa mkutano wa kikazi kujadili.
4. Mitume walitoa miongozo au ushauri wa lile waliloona linapaswa kufanywa, lakini ni eklesia yote iliyofanya maamuzi, na kuwachagua wanaume waliofikiri wangepaa zaidi kuzifanya kazi hizo kwa niaba yao. Bila shaka kila mtu alipiga kura alivyoona, lakini kila mmoja alikubaliana na uamuzi wa wengi na kuuunga mkono.

Matokeo ni kwamba, kama kulikuwa na kutokuelewana katika eklesia, kulisuluhishwa, na kila mmoja alijisikia kwamba anathaminiwa. Hili lilifanya eklesia iendeleo kuhubiri, na hivyo Luka anasema, 'Neno la Mungu likaenea'.

Hili ni somo la maana sana kwetu. Kama kuna utaratibu mzuri katika eklesia unaomhusisha kila ndugu katika maamuzi yake, eklesia itajizatiti katika kulihubiri Neno. Uamuzi unapokuwa umefanywa kwa haki na walio wengi katika eklesia, washirika wote ni sharti wauunge mkono.

Tunasoma juu ya mkutano mwingine katika Matendo 15, ukiwahusisha mitume na wazee kutoka kwenye eklesia nyingi. Walikuja kukutana kujadili kitu ambacho wengi wao walikuwa wakikipinga. Kulikuwa na hoja nyingi, na tunaona tena kuna mambo ya sisi kujifunza juu ya namna ya kukabiliana na tofauti zinazojitokeza katika eklesia.

1. Walikutana kuliongelea jambo hilo; hawakutuma barua au kukaa tu nyumbani. Ingawa kulikuwa na hoja nzito, tena zinazopingana, lakini walisikilizana.
2. Kulikuwa na fursa ya kila mmoja kusema.
3. Wakati Petro na Yakobo walipoongea, kila mmoja alikaa kimya na kusikiliza kwa kuwa walikuwa viongozi.
4. Walilitumia Neno la Mungu katika kufanya maamuzi; sio maoni yao wenyewe.
5. Uamuzi ulipokuwa umefikiwa, wote waliukubali na kuishi kwa kuufuata.

### **Majukumu ya Wazee**

Mtume Paulo alipokuwa akienda katika mizunguko yake ya kuhubiri, alijali sana kuweka utaratibu katika eklesia alizozienenda. Alitambua kuwa, ndugu wa kike na wa kiume waliokuwa ndio wamebatizwa, walihitaji kuwa na mfumo wa ki-eklesia, kwa hiyo aliteua wanaume katika kila mji kuwa 'wazee' (Matendo 14:23).

Haina maana kuwa, moja kwa moja alichagua waliokuwa wakubwa zaidi kiumri, ndio wawe 'wazee wa eklesia'. Timotheo alikuwa bado kijana, lakini alikuwa 'mzee' wa eklesia ya Efeso, aliyechagulia kutokana na hali yake ya kiroho. Paulo anatuambia mengi kuhusu sifa tunazopaswa kuziangalia tunapochagua ndugu wa kuwa 'wazee' katika eklesia zetu.

Tutambue hapa pia kuwa, sio vibaya kupenda 'kuwa mzee' katika eklesia zetu. Ni sababu ya huko 'kupenda' iliyo ya muhimu zaidi. Paulo anasema:

- ✚ "Mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema. Basi imempasa askofu awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji, ajuaye kufundisha; si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu; bali awe mpole; si mtu wakujadiliana, wala asiwe mwenye kupenda fedha; mwenye kuisimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu; (yaani, mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje kanisa la Mungu?) Wala asiwe mtu aliyelongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi" (1 Tim. 3:1-6).
- ✚ "Maana imempasa askofu awe mtu asiyeshitakiwa neno, kwa kuwa ni wakili wa Mungu; asiwe mtu wa kujipendeza nafsi yake mwenyewe, asiwe mwepesi wa hasira, asiwe mlevi wala mgomvi, asiwe mpenda mapato ya aibu; bali awe mkaribishaji, mpenda wema, mwenye kiasi, mwenye haki, mtakatifu, mwenye kudhibiti nafsi yake; akilishika lile neno la imani vile vile kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga" (Tito 1:7-9).

✚ “Nawasihi wazee walio kwenu, mimi niliye mzee, mwenzi wao na shahidi wa mateso ya Yesu, na mshirika wa utukufu utakaofunuliwa baadaye; lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi” (1 Petro 5:1-3).

Neno ‘askofu’ maana yake ni ‘mwangalizi’. Vifungu hivi vinatupa picha nzuri sana kuhusiana na mchango wa mzee wa eklesia. Anapaswa awe:

- ✚ Mwanamume anayeijua Biblia yake vizuri na anayeweza kuwafundisha wengine ujumbe wa Injili.
- ✚ Mwanamume anayeishi kulingana na Injili.
- ✚ Mwanamume anayejitawala na mwenye kiasi katika mambo yote, anayeyashughulikia matatizo ya eklesia kwa namna ya utulivu na busara (hata yakiwa magumu kiasi gani).
- ✚ Mwanamume asiyekasirika na kulipuka.
- ✚ Mwanamume asiyelewa.
- ✚ Mwanamume mkarimu; anayewakaribisha watu wengine nyumbani kwake.
- ✚ Mwanamume asiyedai malipo kwa kazi ya kuwa mwangalizi, na asiyeiba fedha ya eklesia.
- ✚ Mwanamume asiye na maringo au kiburi.
- ✚ Mwanamume ambaye amejengeka kiroho; sio aliyebatizwa karibuni.

Wapo wazee wanaojiona wenyewe kama wenye-mamlaka au kama viongozi katika makusanyiko yao. Hili linawafanya wajisikie kuringa au kujiona ‘wa-maana’ zaidi kwa namna wanavyowachukulia wengine. Hili linatoa mfano mbaya sana kwa eklesia. Baada ya Yesu kuwaosha wanafunzi wake miguu katika chumba cha juu alisema:

“Nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo. Amini, amin, nawaambia ninyi, mtumwa si mkuu kuliko bwana wake; wala mtume si mkuu kuliko yeye aliyempeleka. Mkiyajua hayo heri ninyi mkiyatenda” (Yohana 13:15-17).

Mzee wa eklesia (Mwenyekiti au Katibu) anapaswa awe mtumishi wa eklesia yake. Anatakiwa awe kama mchungaji wa kondoo anavyowachunga kondoo, na kuwasaidia kwenye njia ya Ufalme wa Mungu.

### **Nafasi za wanaume na wanawake**

Paulo aliandika kwamba:

“Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu”  
(Wagalatia 3:27,28).

Haya ni maneno ya kulisimua na yanalithibitisha lile wazo la ‘mwili mmoja’. Rangi ya ngozi yetu, tu wanaume au wanawake, yote haya hayana umuhimu kwa Mungu tunapokuwa watu wa nyumba yake; watu wa familia yake.

Hata hivyo Biblia iko wazi kuwa, kuna majukumu yanayotofautiana ndani ya eklesia kwa wanaume na wanawake. Katika eklesia, wanaume ndio wanaoongoza maombi na ibada ya pamoja.

Ni wajibu wa wanaume kufundisha na kuongoza pia katika mahubiri ya hadharani. Wakina dada ni wa kuwasikiliza kimya-kimya wanaume, na kuwatii (1 Timotheo 2:8-15). Paulo anasema sababu ya hili ni kwamba, Adamu aliumbwa na Mungu kwanza.

Adamu alipaswa kuongoza katika kumwabudu Mungu akiwa na mke wake, lakini mwanamke, Hawa, alidanganywa na kula tunda lililokatazwa. Alipompa mume wake, naye alikula bila kujihoji, wakaivunja amri ya Mungu. Kwa kufuata mwongozo wa Mungu kuhusu majukumu yanayotofautiana kati ya wanaume na wanawake katika eklesia, Paulo anasema tunaurudia utaratibu ambao Mungu aliweka tangu mwanzo.

Hili halina maana kuwa, hakuna shughuli kwa ndugu wa kike. Namna yao ya kushirikisha ni ya muhimu kwa eklesia yoyote. Ni Lidia aliyeweka kielelezo cha ukarimu na wema uliojengeka katika eklesia ya Filipi (Matendo 16). Dorkasi alikuwa dada wa Yafa, aliyefahamika sana kama mfuasi aliyejaa ‘matendo mema’ kwa kuwasaidia maskini (Matendo 9).

Wakina dada wengi wanafundisha Shule za Jumapili katika eklesia zao, na mara nyingi wanao uwezo na watoto wadogo ambao wanaume hawana. Wanao pia miguso ya kushirikisha katika nyumba zao kwa namna wanavyofanya mambo, na wanaweka mfano mzuri wa ucha-Mungu kwa watoto wao na kwa waume zao (Tito 2:4,5).

Namna mojawapo inayotofautisha majukumu kati ya wanaume na wanawake hadharani katika eklesia imewekwa. Wanaume wanatakiwa wasali bila ya kufunika kitu vichwa vyao, na wanawake kufunika (1 Wakorintho 11).

### **Mikutano ya eklesia**

Kila eklesia inapaswa ikutane kila juma, Jumapili kama inawezekana, ili kula mkate na kunywa divai kwa kumbukumbu ya maisha na kifo cha Bwana Yesu Kristo (Somo la 40). Namna inayopendekezwa ya kuendesha huduma ya Kumega Mkate imeoneshwa hapo chini. Hata hivyo ni eklesia iliyo dhaifu tu inayoweza kukutana mara moja tu kwa namna hii kwa juma. Eklesia na waumini mmoja mmoja, wanapaswa kukua kiroho:

“...ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiunganishwa na kushikamanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili (eklesia) upate kujijenga wenyewe katika upendo” (Waefeso 4:14-16).

Ni usomaji makini katika kujifunza Neno la Mungu, kwa maombi, ndio unaotusaidia kukua (1 Petro 2:1). Eklesia inapaswa kukutana kwa ajili ya Somo la Biblia, na sio kukutana Jumapili tu. Hili ni lazima litawasaidia ndugu wote kukua-kiimani; kuendelea mbele kutoka kwenye kanuni za kwanza za kiimani, kwa kutafakari kile mwandishi kwa Waebrania anachokiita ‘chakula cha neno’; kukua kutoka ‘kunyonya’ na kufikia ‘kula chakula kigumu’.

Inapaswa pia kuwe na siku nyingine ya kukutana kwa ajili ya kuihubiri Injili, ambapo eklesia inaangalia nje kuwashirikisha watu wanaoishi jirani Habari Njema ya wokovu. Mikutano hii haiwi rahisi kuiandaa na kuiendesha, na hasa kama eklesia ni ndogo.

Hata hivyo msaada upo. Kitengo cha msaada kwa ‘walio kwenye mazingira ya upweke’ (Christadelphian Isolation League) kipo kwa ajili ya kuwatumia kwa njia ya posta mahubiri yaliyoandikwa, mihadhara, na makaratasi ya masomo ya Biblia, ambayo eklesia inaweza kufaidika nayo.

### **Ratiba ya Kumega Mkate kwa eklesia za Kikristadelfia:**

Wimbo

Maombi

Kusoma sura mbili za masomo ya siku kutoka katika Mshirika wa Biblia (Bible companion).

Mahubiri (yanayotoka katika Biblia, ili kuwaandaa waumini kumega-mkate)

Utangulizi kwa ajili ya Mkate na Divai

Maombi kwa ajili ya Mkate

Maombi kwa ajili ya Divai

Wimbo

Matoleo kwa ajili ya eklesia

Matangazo kuhusu mipango ya baadaye

Wimbo

Maombi

## MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

Karatasi ya Maswali: namba 11

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa 'Kazi ya ziada', unaweza kulijibu swali kama unapenda, au kuliacha kama unaona ni gumu mno. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

### Masomo: 41-44

41. (a) Tunaweza kujifunza nini kutokana na jinsi Adamu na Hawa walivyowalea watoto wao?  
(b) Ibrahimu anatupa kielelezo gani kuhusiana na maisha katika familia?  
(c) Paulo hakuwa baba yake Timotheo, lakini ni vipi anavyomchukulia? Hili linatufundisha nini?  
(d) Mzazi anaweza kumwasha-kibao mtoto?

Kazi ya ziada.

- (e) Msamaha katika maisha ya familia unatufundisha nini?

42. (a) Kwa nini tunatenda dhambi?  
(b) Dhambi ni nini? (Jibu lina sehemu mbili)  
(c) Tamaa ya kutenda dhambi inatoka wapi?  
(d) Nyoka anasimama badala ya nini katika Biblia, baada ya dhambi ya Adamu na Hawa?

Kazi ya ziada.

- (e) Matokeo ya dhambi ni nini?

43. (a) Ni kwa nini Biblia ni ya muhimu kwako? Inakufanya tu kujisikia vizuri kuwa nayo, au ni kitu chenye maana ya kipekee katika maisha yako?  
(b) Ni mara ngapi unaifungua na kuisoma? Kila siku? Kila wiki? Au mara moja-moja tu? Unaisoma yote au baadhi ya vifungu unavyovipenda tu?  
(c) Unaweza kuifungua mahali unapopataka kiurahisi? Unajua Kitabu cha Zaburi kilipo? Yuda kipo wapi? Mika, je?  
(d) Unaweza kuvipata vifungu ndani ya Biblia kuweza kuwaambia watu wengine unayoamini?  
(e) Unaweza kuisema baadhi ya mistari au vifungu kutoka kichwani (bila kusoma), ili kuonesha unachoamini?

Kazi za ziada

- (f) Biblia inakuvutia na kukusisimua kama ni Neno la Mungu?  
(g) Usomaji wako wa Biblia umekusaidia kubadili namna yako ya kufikiri na kuishi katika maisha yako? Kama ndio, kwa namna gani?

44. (a) Neno 'Eklezia' lina maana gani?  
(b) Watu wanapaswa kufanya nini ili waweze kuwa na sehemu katika Eklezia ya Mungu?

Kazi ya ziada

- (c) Wafuasi wanapaswa waweje wanapokutana kujadili masuala ya Eklezia?

*Kumbuka kuweka jina lako, anwani na namba yako ya kumbukumbu katika karatasi yako ya majibu.*

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## NAMNA TUNAVYOWAFIKIRIA WATU WENGINE NI MUHIMU KWA MUNGU

**SOMO:** Yakobo 2

Yesu alipojaribiwa siku moja na mmoja wa madaktari wa Sheria ya Kiyahudi, juu ya amri iliyo kuu kuliko zote, alijibu kuwa ni kumpenda Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, nguvu zako zote, na akili yako yote, na jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe. Kwa ajili ya kuelezea maana aliyokuwa nayo ya 'jirani', aliendelea kwa kutoa mfano wa Msamaria aliyekuwa mwema. Unaweza kusoma juu yake katika Luka 10:25-37.

Tutairudia sehemu hii ya mafundisho ya Yesu katika somo letu lijalo, lakini ni muhimu tuanzie hapa kwa sababu, tunataka kuutumia upendo wa Kikristo katika mahusiano yetu na watu wengine, kama Msamaria-mwema alivyofanya. Tukifanya hivi tutaona kuwa, maagizo mengine tuliyopewa na Yesu na mitume wake, yanaweza kuwa rahisi kuyaelewa na kuyafuata.

Ni rahisi sana kuwa mwema kwa matajiri na wenye nguvu, na kuwadharau na kuwabeza walio wanyonge, maskini au walemavu. Yakobo, mdogo wa Bwana Yesu, anasema, huku ni 'kuwapendelea watu'; akiwa na maana ya 'kutukuza watu'. Anasema ni kuwa na hitilafu mioyoni mwetu, na anatuonya dhidi ya kufikiri kwa namna hiyo (Yakobo 2:1-9).

Kuna mengi ya kufikiri katika maneno haya, na ni muhimu hasa katika nchi na jamii ambazo kuna michanganyiko wa watu walio na asili mbalimbali, makabila au rangi. Kumekuwa na migogoro mibaya na mapambano makali ya watu katika sehemu mbalimbali za dunia katika miaka ya karibuni, inayotokana na ubaguzi. Wapo wanaowaelezea wengine kama vile hawana thamani, sio wakweli, ni washenzi n.k. Ni namna ya kawaida ya kufikiri kibinadamu, lakini ni mbaya sana.

Biblia inachosema ni tofauti. Mawazo na mwelekeo wa kibaguzi ni tabia isiyopaswa kuwa na nafasi, katika mioyo na akili za wale wanaokuwa wafuasi wa Yesu Kristo.

Paulo, mtume wa Yesu, aliishi katika nyakati ambazo utumwa ulikuwa ni sehemu ya mifumo iliyokubalika katika Dola ya Kirumi. Kuna maelekezo na ushauri mwingi katika nyaraka za Paulo, kuhusu mahusiano kati ya mabwana na watwana, waliokuwa wameamua kumfuata Bwana Yesu. Mfano upo kwenye Wagalatia 3 msitari wa 26 mpaka wa 29.

Hapa Paulo anasema wazi wazi kuwa, wafuasi wa Yesu walikuwa wote sawa mbele ya Mungu. Hakukuwa na utofauti wa uasili, jinsia, rangi ya ngozi au hadhi ya kijamii.

Tunapongea na watu tunaishi nao au tunaofanya nao kazi, ni rahisi sana kutumia maneno makali au maneno ya kukosoa ambayo yanajeruhi au kuwakatisha tamaa wengine. Yakobo aliandika pia juu ya hili (Yakobo 3:5-11). Maneno makali yanapokuwa yametumika, hayawezi kufutika; huwezi kuyarudisha tena mdomoni. Kwa kuwa sisi sote tunatofautiana tulivyo, ni wale wenye hasira za haraka-haraka wanaopaswa kuwa makini zaidi. Mungu, kupitia kwa malaika zake, anajua yote tunayosema.

Kutumia uwezo wetu wa kuhukumu ni kitu cha muhimu kwetu, inapokuwa ni kuamua lililo zuri au baya, sahihi au kosa. Lakini tunapohukumu watu wengine, inatubidi tuwe macho zaidi.

Yesu anatupa ushauri wa maana juu ya hili, na umeandikwa katika Mathayo 7:1-5. Kutokana na maneno hayo, unaweza pengine kuamua usimhukumu tena mtu mwingine, lakini sio rahisi kushikilia msimamo huo. Yesu anakazia maelekezo yake hayo kwa kutoa mfano mdogo. Ufunguo wa kuyaelewa maneno yake ni usemi unaohusu 'kuona kibanzi katika jicho la ndugu yako'. Huku ni kukosoa wengine hapo kwa hapo, kunakopuuzia kushindwa kwetu wenyewe mbele ya macho ya Mungu.



Kuna wakati tunahitaji kufanya maamuzi kiuangalifu, na Yesu anatoa mfano wa haya katika Mathayo 7:15,16. Nasaha hii kwa vyovyote ilikuwa ya maana sana katika miaka za awali ya imani ya Kikristo, walimu wa uongo walipokuwa wengi mpaka wengine kuitwa 'Makristo'. Ni nasaha ya maana sana hata sasa, katika wakati huu ambao kuna makanisa mengi sana na walimu wengi. Namna ya kuwahukumu ni 'kuwapima kwa matunda yao'. Kwa kawaida, kile wanaume hao (na pengine wanawake) wanachofanya katika maisha yao, kinaonesha zaidi walivyo kuliko kile wanachohubiri.

Yesu alipokuwa amewachagua wanafunzi wake, alianza kuwafundisha namna ya kufanya mambo yanayoweza kumpendeza Mungu. Mafundisho hayo yaliyo mengi yapo katika Injili ya Mathayo, Sura ya 5, 6 na 7. Hebu tuangalie pamoja katika Sura ya 5, kuanzia msitari wa 21. Yesu hapa ananukulu kutoka katika Sheria ya Musa iliyotoka wakati taifa hilo lilipotoroka utumwa katika nchi ya Misri.

Hapa anaeleza kuwa, wakati sheria ya zamani ilidhibiti vitendo vya kitabia kwa Wayahudi, sheria yake mpya ingeendelea mbele na kudhibiti mawazo na matendo pia. Anaongelea hasira, lugha chafu, na mawazo ya tamaa. Anaongelea kuvunjika kwa ndoa, ambako mara kwa mara kunatokea kutokana na tamaa ya kufanya mapenzi na wengine nje ya ndoa.

Katika msitari wa 33 Yesu anaonya juu ya kuapa bila kufikiria. Kwa hili ana maana ya maneno watu wanayosema, ili kuwavutia wengine kuamini ukweli wa lile wanalosema. Kwa bahati mbaya, wanatumia maneno ya 'utakatifu wa Mungu' na hili lilikatazwa. Hata inapokuwa tunayafikiria tu maneno hayo katika akili zetu, ni muhimu tukumbuke wakati wote kuwa yalikatazwa (Kutoka 20:7). Mwongozo wa jumla wa Yesu ni kwamba: "Usiape kabisa" (Mathayo 5:34).

Ni vizuri zaidi kuepuka kabisa kuapa wakati wowote, na hili linahusu pia kwenye mahakama kama itatokea tukajikuta mahali hapo. Kwa kawaida kunakuwa na kipengere cha wafuasi wa Yesu 'kuahidi' kabla ya kutoa ushahidi; kinapaswa kitoshe. Matumizi ya viapo kama njia ya kuelezea tunavyowafikiria wengine, yameshughulikiwa na Yesu katika tahadhari yake kuhusu tunayosema, katika msitari wa 22.

Katika Mathayo 5:44 amri ya kumpenda jirani imepelekwa hatua kadhaa mbele. Yesu sasa anatuagiza tuwapende maadui zetu, tuwabariki wale wanaotulaani, tuwafanyie mema wale wanaotuchukia, na kuwaombea wanaotuumiza. Haitakuwa rahisi kamwe kuzifuata amri hizi kwa kuwa, tunavyojisikia kufanya wakati wote inakuwa kufanya kinyume cha hivyo. Lakini, kama Yesu alivyoweza kusamehe katikati ya maumivu makali ya mateso aliyokuwa nayo msalabani, wale kati yetu wanaotamani kuwa wafuasi wake kwa dhati, ni lazima wajifunze kufuata mfano wake.

Kiburi na maringo visiwe na nafasi kabisa mbele ya Mungu katika mambo tunayofanya, lakini, muhimu zaidi, katika mioyo na akili zetu.

Kwa kumaliza somo hili, hebu tuyaangalie kwa pamoja maneno ya nabii Isaya yanayotupa dokezo la mambo Mungu anayoyataka kutoka kwetu, na hulka zile katika ubinadamu ambazo zinampendeka. Baada ya kuelezea kazi kubwa ya uumbaji Mungu aliyofanya, anasema: "Mtu huyu ndiye nitakayemwangalia, mtu aliye mnyonge, mwenye roho iliyopondeka, atetemekaye asikiapo neno langu" (Isaya 1:1-2).

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## KUMPENDA JIRANI YAKO

**SOMO:** Luka 10

Katika somo hili tutaangalia zaidi maagizo ya Yesu kuwa, kama kweli tunataka tuwe wafuasi wake, ni lazima tuoneshe katika maisha yetu kiwango kisicho cha kawaida cha upendo kwa watu wengine. Mahali pa kuanzia pa somo hili ni mfano wa Msamaria-mwema uliotajwa katika somo letu lililopita. Tunapoangalia kwa ukaribu maneno ya Yesu katika Luka 10:30-37, tunaona mambo kadhaa ya muhimu.

Kwanza, Yesu alichagua kumweka Msamaria katika mfano huo, kwa kuwa Wasamaria walikuwa wakichukiwa na Wayahudi; walikuwa wakionekana kama watu wa kudharaulika.

Pili, mtu aliyeshambuliwa na wanyanganyi, hakisaidiwa na watu wawili waliokuwa wakistahili kwanza kumhurumia na kumsaidia. Makuhani waliokuwa wakitokana na kabila la Lawi, walikuwa wakiwajibika katika Sheria ya Musa kuangalia afya za Waisraeli wenzao na huduma kwa ujumla, lakini hakuna kilichofanyika.

Ni Msamaria aliyeonesha upendo na huruma, kwa kufanya mambo aliyofanya kusaidia. Alimwosha majeraha, akambeba mtu huyu aliyemizwa kwenye punda wake na kumweka mahali pa usalama kupumzika. Mwishoni, ndiye aliyeweka mpango wa msaada zaidi kwa ajili ya kuendelea kuhudumiwa.

Tunaposoma katika Injili juu ya matendo mengi ya uponyaji yaliyofanywa na Yesu, waandishi mara nyingi wanaongezea maneno, Yesu: 'Alimwonea huruma'. Mfano upo katika Luka 7:11-15.

Yesu alipokuwa amewateua wanafunzi wake wa karibu kumi-na-wawili, alianza kuwafundisha juu ya upendo, msamaha na huruma. Kama ukifungua sasa nyuma kidogo kwenye Luka 6:17 utaona hayo kwa pamoja. Umati uliomsikiliza Yesu siku hiyo ulikuwa mkubwa sana, na wengi walikuwa wamekuja kutoka mbali sana kumwona. Walio wengi walikuja ama kuponywa, ama kuona matendo ya Yesu ya kuponya. Walikaa hapo muda wote kusikia mafundisho yake kuhusu ufuasi wa Kikristo, na tutafanya na sisi hilo, tukitazama zaidi msitari wa 27 mpaka wa 36.

Hakuna hasa linaloshangaza. Tunalosoma katika Injili ya Luka ni kama lile lile tulilolisoma katika Injili ya Mathayo, katika somo letu lililopita. Ujumbe huu ni wa maana mno kiasi kwamba, unarudiwa mara nyingi katika Biblia. Kile kinachoanza kama wazo katika akili zetu, mara nyingi kinageuka kuwa tendo, kwa hiyo sheria ya Yesu inahitajika kwanza iongoze katika kufikiri kwetu, ndipo itakapoweza kutawala matendo yetu. Tunapoonisha upendo na huruma kwa mtu mwingine, tunafanya hivyo kwa matendo yetu.

Muda mfupi kabla Yesu hajaondoka katika kile Chumba cha Juu, alipofurahia mlo wa pamoja na wanafunzi wake kabla ya kufa, aliirudia tena hii amri ya muhimu kipekee kuhusu upendo. Tunaiona katika Injili ya Yohana 13:34,35.

Maneno yake yanahitaji kuzingatiwa kwa umakini kwa kuwa, upendo wa Kikristo unaooneshwa na wanafunzi wake, unatakiwa uwe mkubwa kama ule uliooneshwa na Kristo mwenyewe kwa hao wanaume na wanawake wa enzi yake, na wale wote ambao wangemfuata katika nyakati zote.

Alionesha upendo wake kwa kujitoa kwa hiari kufa msalabani, ili wote wanaomfuata, wanaonesha imani ya kweli, waweze kupata fursa ya kuwa na uzima usio na mwisho katika Ufalme wake unaokuja katika dunia hii. Hebu angalia Yohana 15:9-14 na uone vile amri hii inavyorudiwa katika msitari wa 12 na wa 17.

Petro alipojitetea kuwa kamwe hatamwacha Yesu (Yohana 13:36-38), Yesu alimwambia, kabla jongoo hajawika (yaani kabla hakujakucha), angemkana Bwana wake Yesu mara tatu. Lilipotokea hilo kama Yesu alivyotabiri, Petro alitahayari, lakini alijifunza somo kuwa, kumpenda Bwana Yesu hakuwi kitu kirahisi mtu anapobanwa.

Baada ya Yesu kufufuka, aliwakuta wanafunzi wake upande wa kaskazini katika Galilaya, mahali ambapo saba kati yao walikuwa wameamua kuchukua mashua na kwenda kuvua. Walijiunga na Yesu ufukweni mahali ambapo alikuwa ameandaa chakula cha mkate na samaki (Yoh. 21:9). Ni jambo la muhimu kuwa, Yesu alikuwa amewaonesha huruma yake umati ule wa watu elfu tano na baadaye elfu nne, kwa kuwalisha kwa muujiza mikate na samaki.

Baada ya kula hapo ufukweni mwa Bahari ya Galilaya, Yesu aliihitimisha somo lake la upendo kwa kumuuliza Petro mara tatu juu ya upendo wake kwa Bwana wake. Yesu aliendelea kwa kujazia maneno mengine kwenye maelekezo yake ya awali (ms. 15-18). Ilikuwa kwamba, kila mara Petro aliposema kuwa alimpenda Yesu, alipewa amri na majukumu ya: kulisha wana-kondoo, kuchunga kondoo, kulisha kondoo wa Yesu.

Katika miaka ya awali ya kanisa jipya (Ukristo), kulikuwa na wana-kondoo wengi (wafuasi wapya) wa kutunzwa. Eklesia nyingi zilipoanzishwa katika maeneo mengi ya Israeli na nchi zingine, majukumu yalibadilika kukawa na haja ya ulezi kwa jumua zilizokuwa zimeanza (kondoo). Paulo aliitumia lugha hii hii katika ujumbe wake alipokuwa akiwaaga wazee katika eklesia ya Efeso (Matendo 20:28,29).

Mtume Yohana naye alijifunza somo hili la muhimu sana la upendo kutoka kwa Yesu. Alipokuwa akining'inia msalabani, Yesu alisema na Yohana na kumpa jukumu juu ya mama yake, Mariamu (Yohana 19:26, 27).

Miaka kama 50 baadaye Yohana aliandika Waraka aliokusudia usomwe katika Eklesia zote. Katika huo alielezea kwa kifupi kunavyopaswa kuwa na sheria ya upendo wa Kikristo (1 Yohana 4:7-21). Soma mistari hii kwa makini maana ni ya muhimu sana, na hasa katika nchi ambazo kuna chuki za kutisha kati ya kundi moja la kijamii na kundi jingine, wazimu wa kuangamizana kati ya kabila moja na jingine, vita kati ya eneo moja na lingine, mji na mji, kijiji na kijiji, chuki kati ya familia na familia, ndugu na ndugu.

Maneno ya Yohana ni thabiti na hayaachi shaka lolote katika mawazo yetu. Haiwezekani kwa mfuasi wa Kristo kusema kuwa anampenda Mungu, na wakati huo huo akawa na chuki kwa Wakristo wenzake moyoni mwake. Kama mtu anasema anampenda Mungu na anamchukia ndugu yake, ni mwongo. Hakuna namna ya kuweza kuyakwepa maneno haya, na kwa wale wanaotaka kubatizwa au wale waliobatizwa hivi karibuni, hili ni fundisho la muhimu sana.

Kuna mambo mengi sana ya sisi kukumbuka kutoka kwenye maneno hayo kiasi kwamba, ningependa nitumie sehemu iliyobaki ya somo hili kuyaangalia kwa undani:

1. Msitari wa 7: “Pendo latoka kwa Mungu” – hili lina maana kuwa katika uumbaji, uwezo wa kuonesha upendo wa kujitoa ulijengwa ndani yetu kwa namna Mungu alivyotumba. Anatumia tuitikie upendo wake na upendo wa Yesu kwetu.
2. Msitari wa 10: Mungu alituma Yesu awe dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu. Hiki ni kipimo cha upendo wake kwetu.
3. Msitari wa 11: Kwa kuwa Mungu anatupenda, ni lazima tuoneshe upendo kwa wengine.
4. Msitari wa 12: Tunapouonesha huo upendo unaotoka kwa Mungu kwa watu wengine, kuna kitu kinachomhusu Mungu kilichopo ndani ya kila mmoja wetu.
5. Msitari wa 17: Kama ni kweli kwamba tunajisikia tumeweza kuonesha upendo huo wa Mungu kwa wengine, basi hatuhitaji kuwa na hofu ya hukumu siku ya kurudi kwa Yesu.
6. Msitari wa 10: “Pendo lililo kamili huitupa nje hofu”. Kuna thawabu ya uhakika kwa wale wanaoweza kuuonesha upendo wa namna hii.
7. Msitari wa 20 na 21- Hii ni mistari ambayo tumekwisha itazama, lakini kwa sababu ya kukua kwa chuki na mauaji kati ya watu katika nchi mbalimbali duniani, nataka hasa nisisitize umuhimu wa ujumbe huu.

Hatuwezi kumpenda Mungu na kumchukia kaka au dada yetu. Yohana hapa anaongea na wafuasi wa Yesu; watu waliobatizwa. Hakuna kabisa sababu ya kuwa na uadui kati yetu kama tumebatizwa.

Kama ambavyo 'jirani' wa mtu katika mfano wa Yesu alivyokuwa Msamaria, ndivyo ambavyo jirani yetu anavyoweza kuwa mtu yeyote anayehitaji msaada wetu. Kwa maana pana, majirani wanaweza kuwa watu tunaokutana nao kila siku, kwa hiyo tunalo jukumu lililo kubwa. Kwa bahati hatuhitaji kujihusisha na watu walio wengi tunaopishana nao kila siku, lakini, inapotokea kukawa na dharura, amri ya Yesu ni lazima tuiikumbuke: mpende Mungu na jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## MAFUNDISHO YA BIBLIA KUHSU MATEO

**SOMO:** Waebrania 12

Mateso ni tatizo katika maisha, na yanaweza kumpata mtu yeyote. Mtoto anazaliwa kipofu, au amelemaa na tunajiuliza, ni kwa nini? Mtoto hajakosea kitu. Wanaume kwa wanawake, vijana kwa wazee, matajiri kwa maskini, wote wanaweza kupatwa na maumivu ya magonjwa ya hatari yanayoweza tu kuishia kwenye kufa. Kwa nini wateseke?

Mateso, maumivu, mauti n.k. ni majanga ambayo yanaletwa kwa mamilioni ya watu na ukiritimba wa mwanadamu, na uharibifu mkubwa unaletwa na silaha za kisasa. Uhai unaangamizwa na vitendo vya ugaidi na jinai.

Matatizo ya namna hii yamekuwapo katika historia yote ya dunia, lakini kutokana na ongezeko la watu na ongezeko la uwezo wa silaha kuangamiza, kiwango cha majanga haya leo kinatisha. Watu wanajiuliza, ni kwa nini Mungu anaruhusu mambo haya kutokea?

Swali hili linaonekana angalau kukubali kuwa Mungu ni kweli yupo, ila anayeliuliza anamtegemea Mungu afanye mambo wakati wote kwa namna iliyo ya kheri. Kitu anachopuuza kabisa au asichokijua ni sababu ya 'uwepo wa mateso' katika dunia. Sababu zinaweza kuhitimishwa ifuatavyo:

1. Katika Bustani ya Edeni, mwanadamu alichagua kwenda njia yake mwenyewe badala ya kuifuata Njia ya Mungu, na kujiletea laana iliyoahidiwa ya kifo. Lakini hii ilikuwa ni sehemu tu ya adhabu. Maisha ilikuwa yabadilike na kuwa magumu sana kwa mwanadamu (Mwanzo 3:16-19).
2. Kwa sehemu kubwa, mateso wanayopata watu yamekuwa yakitokana na ukatili wa wanadamu wengine. Kuanzia kwenye uuaji wa kwanza, Kaini alipomuua ndugu yake Habili, Biblia inaonesha kulivyokuwa na vita na ugaidi, hila na mauaji, hali ya mambo ambayo tunaielewa vizuri sana. Katika kila kitendo cha ukatili, kunakuwa na shida zingine zinazofuatia. Matokeo ya mambo haya hayakwepeki.

Pamoja na hili kuna suala la mambo yanayofanywa na kizazi kimoja, kuwa na athari kwa vizazi vinavyofuata. Vitu kama vita vya madawa ya sumu yanayoharibu ardhi, bahari au hata urithi wa kimaumbile ya watu na kusababisha ulemavu, upofu, uziwi n.k. yote yametengenezwa na watu.

Tunapaswa kuelewa kwamba, mateso na maumivu tunayoyasababisha wenyewe, au yanayosababishwa na wanadamu wenzetu, hayawezi 'kutupiwa' Mungu. Mabomu ya kutegwa ardhi na silaha zingine za maangamizi zinazoua, zimetengenezwa na watu, na zinatumiwa na majeshi kwa amri zinazotolewa na Serikali za kibinadamu.

3. Mwanadamu anaishi katika dunia inayoongozwa na kanuni za kiasili na kimaumbile. Jambo moja linaleta matokeo fulani kwa lingine, na majanga ya asili makubwa kama volkano, matetemeko ya ardhi, mawimbi ya bahari, ukame na mafuriko, yote yanayoleta mateso makubwa kwa watu, hayachagui. Yanawapata wema na wabaya. Kama tunaona kuwa ni Mungu anayeongoza mambo hayo, tujiulize, tungependa kwa namna fulani ayatumie kwa namna ambayo wabaya wanauawa na wema wanaachwa?

Katika Injili ya Luka kuna kumbukumbu ya Yesu, akiulizwa juu ya uhusiano uliopo kati ya dhambi na mateso (Luka 13:1-5). Alichofundisha Yesu kinaeleweka hata kwetu hivi leo. Majanga hayawatafuti tu wadhambi na kuwatokea kwa kuwa, hayatokani na dhambi.

Katika visa hivyo katika Luka, ilikuwa ni ukatili wa utawala wa Kirumi uliosababisha mauaji ya kwenye hekalu na damu kuchanganywa na dhabihu. Kwa kuanguka Mnara wa Siloamu ambapo watu 18 walikufa, pengine ilikuwa ufundi usiokidhi haja, au tetemeko la nchi.

Yesu alikuwa makini kusema hapo hapo kuwa, wajibu wa mwanadamu mbele ya Mungu sio kujiwazia kishirikina mambo mabaya yanapotokea. Analosema ni kwamba, maisha ya mwanadamu ni mateke; yanakatika kirahisi. Hayana uhakika, anaweza kufa dakika yoyote! La msingi kwake lilikuwa 'kuifikia toba'. Kwa hiyo, kuamini na kubatizwa sio jambo la kuahirishwa.

Nataka sasa nigeukie upande mwingine wa mateso. Katika Methali 3:11,12 tunaambiwa kwamba, kuna majaribu katika maisha ya wale walio waaminifu. Mistari hiyo inasema:

“Mwanangu, usidharau kuadhibiwa na BWANA, wala usione ni taabu kurudiwa naye. Kwa kuwa, BWANA ampendaye humrudi, kama vile baba mwanawe ampendaye”.

Waaminifu wanajaribiwa na Mungu kwa kuwa Mungu anawapenda. Anawaadhibu kama watoto kwenye familia, mara nyingine wanavyoadhibiwa na wazazi wao wanaowajali. Mungu anawataka wanawe waerevuke na kuelimika kwa ajili ya maisha yao ya baadaye, kwenye Ufalme wake.

Paulo alinukulu mistari hiyo ya Methali katika kutoa hoja yake katika Waraka wake kwa Waebrania (Waebr. 12:5-13). Anachosema katika Waraka huo amekielezea vizuri hata zaidi kwenye Waraka wake wa pili kwa Wakorintho (2 Wakor. 12:7-10).

Paulo, akiwa mtume aliyeteuliwa kwa ajili ya watu wa mataifa (watu wasio Wayahudi), na akiwa mtu ambaye alipata maono ya moja kwa moja kutoka kwa Bwana Yesu akimfundisha na kumwelekeza, alikuwa na tatizo fulani la maumivu lililimpa kitu kama ulemavu. Lilimpa shida katika kufanya kazi zake.

Alimwomba Mungu mara tatu kwamba amponye. Jibu alilopewa lilikuwa:

“Neema yangu yakutosha, maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu” (ms. 9).

Kwa maneno mengine, hakuitikiwa; aliambiwa 'bakia hivyo-hivyo'! Ni wazi Paulo aliyakubali majibu hayo kutoka kwa Mungu na kuendelea na kazi yake ya kusafiri na kuhubiri mpaka siku alipokuwa mfungwa wa Warumi. Hatuambiwi aliwahi kupona.

Na sisi tunapaswa kujifunza somo hili kutoka katika maneno hayo ya Mungu. Udhaifu na shida ni vitu ambavyo ni lazima tuvikubali katika maisha yetu. Tusiviruhusu viyaharibu maisha yetu, na tusiviruhusu viingilie na kuathiri ibada yetu kwa Mungu na kwa Mwanawe, Bwana Yesu Kristo. Tunaweza hata kuyaelewa mateso kama ni njia ya kujivua anasa na mivuto ya dunia inayotuzunguka, ili tuweze kupata ukaribu zaidi kimahusiano na Mungu na Yesu.

Hivi kwa hakika ndivyo ilivyokuwa kwa wengi kati ya watumishi wa Mungu katika nyakati za Agano la Kale. Hili limeoneshwa sana katika Waebrania 11. Walijaribiwa sana katika maisha yao, na imani yao kwa Mungu iliimarika katika kujaribiwa kwao. Wengi kati ya watu tuliowaona katika masomo haya, wanaume kwa wanawake, walijaribiwa: Ayubu, Ibrahimu, Sara, Yusufu, Hana, Eliya, Danieli, Yeremia na wengineo.

Mpaka sasa tumeangalia tu zaidi mateso kwa wanadamu, na sasa nataka nikutake umfikirie BWANA Mungu mwenyewe. Aliumia wakati watu wake, Israeli, walipomkataa. Anaumia hata hivi leo kutokana na ugumu wa mioyo ya wanadamu, na ukatili wanaoufanya kwa wanadamu wenzao.

Hebu ifungue Biblia yako katika Injili ya Yohana 3:14-17. Hapa, kwa hakika tunaona mateso makubwa kwa Mungu, katika kuruhusu Mwanawe wa pekee apigwe na kuuawa kwa kuwambwa msalabani, ili dhambi za wanadamu ziweze kusamehewa, na watu wa-imani waweze kuwa na tumaini la ufufuo na uzima wa milele.

Yesu alikuja katika hali ya uanadamu, yalimpata yanayotupata na alivumilia majaribu kutoka ndani na dhiki kutoka nje. Ni hali ambayo ni ya kawaida kwa watu wote. Maisha yake ya kipekee aliyoyaishi kwa manufaa ya wengine; kwa manufaa yetu, yanaelezwa katika Waebrania 2:10-18.

Hapa tunaona somo lingine la maana sana kwa ajili yetu. Yesu alikamilishwa kupitia katika mateso (ms. 10), ili aweze kuwasaidia wale wote wanaojaribiwa (ms. 18). Katika Waebrania 5:5-8 tunasoma kuwa Yesu alijifunza kutii, kwa mateso aliyoyapata.

Kama basi Mungu aliteseka (na anaumia hata leo), na kama kwa kumtii Baba yake, Yesu aliteseka, tunaweza kulitazama tatizo lote la mateso ya mwanadamu kwa mwanga tofauti. Bila ya kuelewa kwamba Mungu alipata shida kwa ajili ya Kristo ili kutuokoa, kuna uovu mkuu unaotung'ang'ania.

Tukiwa na imani na mfano wa Yesu mbele yetu, tunaweza kuelewa kuwa, mateso yanaweza kuitakasa imani yetu. Inaweza ikawa njia ambayo Mungu anaitumia katika kumleta mfuasi anayeteseka karibu naye.

Kuadhibu kwa Bwana ni sharti tukuchukulie kama ni 'katurudi' kwa namna ya Ki-Mungu. Kama tunaona 'haturudi' tumshukuru na kumwabudu, na kama 'tunarudiwa', basi tuwe na subira, tuvumilie na kumkaribia Mungu wetu tukijua ya kuwa, naye aliteseka. Anatokusudia tuimarike na kumtii kwa yale yanayotupata.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

### KUISHI KWA HOFU

**SOMO:** Kumb. La Torati 26

Ni rahisi sana kwa wale wanaoishi katika nchi zenye serikali nzuri, zenye amani na utangamano, kusema kuwa hofu ni kitu unachopaswa tu kukikubali. Kuna useme wa kisasa unaosema, ‘kabili hofu zako’.

Katika miaka ya karibuni, hata watu waliokuwa wakiishi katika nchi zilizokuwa na utulivu, imewabidi wajifunze kuishi kwa hofu mchana na usiku. Kutegameana na wapi walipo duniani, kumekuwa na matukio ya kutisha: vita, majanga ya asili kama matetemeko ya nchi, milipuko ya kivolkano, mafuriko, vimbunga n.k.

Hofu inakuja kutokana na kutojua ni nini kitakachofuata; iwe ni kuweza kujiokoa mwenyewe, familia yako na marafiki, au mali. Matukio ya ghafla na mistuko yake ni hali inayoweza kutupata sisi sote. Somo hili limeandikwa kuonesha namna ya kuyachukulia mambo haya, na kuikabili hofu isiyoondoka. Hii ni hofu ambayo tunakuwa nayo mchana na usiku kwa siku kadhaa, miezi na hata miaka.

Kuna mifano mingi katika Biblia inayoweza kutuonesha watu walivyoikabili hofu. Mmoja upo katika Kutoka 14:10 wakati wana wa Israeli waliokuwa wameutoroka utumwa katika Misri, walipogundua ghafla kuwa, walikuwa wakifuatiliwa na jeshi kali la Wamisri nyuma yao. Bahari ilikuwa mbele yao, Wamisri nyuma; kwa vyovyote waliogopa sana.

Mfano mwingine, kwa sasa ni katika Kumb. La Torati 26:63-67. Unaposoma hapo utaona kuwa, maneno hayo yanaielezea ile hofu isiyokwisha. Mungu anawaambia watu wake kuwa, hofu hii itawapata kama wakimuacha na kuanza kuabudu miungu ya uongo; ya miti na mawe. Wayahudi walimuacha Mungu, na historia yao mpaka siku ya leo inaonesha walivyoishi miaka mingi maisha ya hofu. Katika Ujerumani kwa mfano, kati ya mwaka 1939 na 1945, Wayahudi milioni 6 waliuawa kwa sababu tu kuwa Wayahudi.

Hofu ni mbaya zaidi inapokuwa ni ya kitu kisichojulikana. Inaweza ikaathiri makundi makubwa ya watu. Inapenyezwa kutoka kwa mmoja hadi kwa mwingine kwa njia ya mazungumzo. Hili linapokupata, kitu cha kwanza unachoweza kufanya kibinafsi ni kutaka kujua chanzo cha hiyo hofu. Ni vizuri pia kujua, inaletwa na nini au na nani.

Ukifanya hivyo ndipo utakapoweza kuona ni nini ufanye juu ya chanzo hicho. Mara nyingine kuihama nyumba, kijiji, familia au marafiki zako inaweza kuonekana kuwa suluhu pekee ya maana pengine kwa muda.

Tangu mwanzo wa kanisa la Kikristo, wafuasi wa Yesu walikuwa wakiteswa kama inavyowatokea watu wengine hata sasa. Mara nyingi hili liliwapata kwa sababu ya kuwa Wakristo. Hata hivyo mateso hayakuwafanya waache kuwa wafuasi. Badala yake, inaonekana walikuwa shupavu zaidi kwenye imani yao na kwa utii wao kwa Yesu.

Kitabu cha Matendo kinatuambia juu ya kazi ya kuhubiri iliyofanywa na mitume, katika nchi za kaskazini ya Bahari ya Kati (Mediterranean Sea). Tunaoneshwa kuwa, popote walipokwenda walitishiwa na vikundi vya Wayahudi waliokuwa wakiishi maeneo hayo.

Mitume walipigwa, waliuawa kwa kupigwa mawe na kufungwa, lakini hatuoni wakirudi nyuma au kushindwa; tunachooni ni kinyume chake. Mungu kuna wakati aliwaokoa. Tunaona, kwa mfano, akituma malaika zake kufungua milango ya gereza (Matendo 16:22-29). Hebu jaribu kufikiri ilivyokuwa kwa Paulo na Sila, wakiwa wanaumwa kwa kipigo walichopata na kukosa usingizi, lakini wanaimba wakimsifu Mungu (pengine kutoka kwenye Zaburi).

Tangu mwanzo wa kanisa la Yesu, wafuasi walijua kuishi kwa hofu kulivyokuwa, lakini hawakuiruhusu iyatawale maisha yao; iwarudishe nyuma. Yesu alikuwa ndiyo nguvu iliyoyatawala maisha yao. Mfano wake



uliwapa nguvu. Katika siku ile ya kutisha, Yesu akijua ya kuwa watu wakatili wangekuja kumkamata na kumchukua akasulubiwe, alivyoendelea mbele, aliacha kielelezo kikubwa kwa wafuasi wake. Anaweza kuwa kielelezo hivyo hata kwetu leo.

Katika Luka 22:39-44 tunasoma wakati huo ulivyokuwa wa hofu kubwa kwa Yesu. Alijua kutokana na utabiri mwingi wa Kimaandiko lile ambalo lingempata, na kwa kuwa alikuwa mwanadamu kama sisi, alitishika sana. Kilichosaidia ni kuwa, alikuwa pia Mwana wa Mungu, akijua kifo hiki cha uchungu mkubwa kilivyokuwa gharama iliyotakiwa kulipwa kwa ajili ya dhambi za wanadamu.

Kwa moyo mkuu alisimama kutoka pale alipokuwa ameinama akiomba, na kuondoka mahali pale pa utulivu kwenda kuonana na wanaomshutumu, na kufa.

Yesu hakuwahi kuwaahidi wafuasi wake maisha yasiyo ya shida na hofu. Badala yake aliwaonesha kuwa, maisha tunayoishi sasa ni dhiki inayoutangulia Ufalme wa Mungu. Kuna baadhi ya wanaomfuata ambao wangekufa kwa sababu ya kuwa Wakristo, lakini katika kusudi la Mungu kamwe wasingehaulika; wasingepotea. Katika siku ya ufufuo, watasimama duniani pamoja na wale ambao wameishi na kufa katika hali ya amani.

Hebu yatazame maneno ya Yesu katika Luka 12:4-7. 'Jehanum' katika msitari wa tano hapo ni kaburi, na wale wasioupokea wito wa Mungu wa wokovu, wanakaa humo daima. Kama tukijiweka sisi mikononi mwa Mungu, tutakuwa tumeweka tumaini letu mikononi mwa Muumba, mwenye uweza wote. Ndiye Mungu aliyetuumba na kutuweka duniani hapa kwa ajili ya mpango wake mwenyewe wa ajabu.

Ili kutunyanyua juu zaidi ya matokeo ya hofu, tunayo maneno ya kututia moyo yaliyo katika Wakorintho wa kwanza, Sura ya 3 msitari wa 16. Msingi wa maisha yetu ni Yesu, kama tumebatizwa katika jina lake. Msitari wa 12 mpaka wa 15 upo kutuonesha wazi kuwa, hata kama mali zetu zote zinapotea, kama tunaishikilia imani yetu, bado tupo salama katika kusudi la Mungu.

Hebu sasa turudi tena kwenye Kutoka 14, tuone kilichowapata Wana wa Israeli. Kumbuka kuwa walikuwa kabisa katika hali ya kuangamia, wakiwa wamenasa kati ya Bahari ya Shamu na majeshi yanayokuja mbio ya Wamisri. Tazama sasa msitari wa 13 na endelea kusoma mpaka mwisho wa Sura hii. Umeona ushauri wanaopewa na Musa? Anawaambia: "Msiogope, simameni tu, mkaone wokovu wa BWANA" (ms.13).

Hebu tazama sasa 1 Yohana 4:15-19. Msitari wa 15 unatoa wito kwa wale wote walio na mawazo ya kubatizwa, lakini bado hawajaamua. Kama mtu yupo katika Kristo, anazungukwa na upendo wake mkamilifu, na upendo huo mkamilifu unaondoa hofu.

Kuna maneno kadhaa ya faraja katika Zaburi ya 34; hebu isome. Ni maneno yanayoweza kubadili kabisa mtazamo wetu wa maisha. Ufikirie hasa msitari wa 4 mpaka wa 8. Katika msitari wa 9 tumepewa wazo jipya: "Wamchao (Mungu) hawahitaji kitu". Kama kunakuwa na hofu katika maisha yetu, na iwe basi hofu ya namna tofauti, iliyo nzuri zaidi, hofu iliyo ya kutufaa...hofu ya kumcha Mungu. Kama unausoma msitari wa 11 utaona kuna wito unaotolewa na Daudi, aliyeandika Zaburi hii.

Alikuwa ni mtu ambaye, alipokuwa kijana, alitoka kwenda kupigana na Mfilisti 'kibonge', aliyeitwa Goliati, kwa manati, akiwa amejandaa na kokoto zake chache, na imani iliyojaa kwa Mungu wake. Daudi anatupa nasaha njema. Hofu ya Mungu ni nzuri na ni safi kwetu. Hili lina maana kwamba tutakuwa wakati wote tukitambua uwepo wake. Tutamheshimu Mungu wakati wote na kutambua jinsi alivyo karibu nasi kupitia kwa malaika zake. Daudi anasema kwenye Zaburi hiyo tuliyoisoma: "Malaika wa BWANA hufanya kituo, akiwazungukia wamchao na kuwaokoa" (Zab. 34.7).

Mambo tunayofanya katika maisha yetu yatakuwa ni kwa uaminifu na wema, na tunavyompenda Mungu, ndivyo itakavyokuwa rahisi kwetu kuwapenda wanadamu wenzetu kama alivyofanya Yesu. Kumbuka hapa ya kuwa, hata wakati alipokuwa akining'inia msalabani kwa uchungu mkali, alimwomba Baba yake kusamehe, akisema: "Wasamehe Baba, kwa kuwa hawajui walitendalo".

Mtume Yohana anatuambia mengi juu ya upendo katika maisha yetu, lakini anatuambia pia juu ya hofu ya mwanadamu: “Katika pendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu” (1 Yoh. 4:18).

## MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

Karatasi ya Maswali: namba 12

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa 'Kazi ya ziada', unaweza kulijibu swali kama unapenda, au kuliacha kama unaona ni gumu mno. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

### MASOMO: 45-48

45. (a) Amri iliyo kubwa kabisa ni ipi?  
(b) Tunaweza kutamani kuwa matajiri na wenye nguvu?  
(c) Utumwa unakubalika kwa Mungu?  
(d) Tunapaswa kufanyaje kama wakubwa wetu wa kidunia wanatutaka tufanye kitu?

Kazi ya ziada

- (e) Kama ndugu yetu anafanya jambo lisilofaa, tufanyeje?

46. (a) Yesu alimtumia Msamaria katika mfano wake wa Msamaria-mwema. Kwa nini?  
(b) Toa mifano ya mahali Yesu alipoonesha huruma.  
(c) Yesu alikuwa na maana gani alipomwambia Petro, 'chungu kondoo zangu'?  
(d) Upendo ni nini?

Kazi ya ziada

- (e) Mungu anasemaje juu ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na mauaji ya kimbari?

47. (a) Mateso ni nini?  
(b) Mateso yaliletwa katika Bustani ya Edeni, kwa nini?  
(c) Mungu anasababisha mateso?  
(d) Kwa nini Mungu 'anaturudi'?

Kazi ya ziada

- (e) Mateso yanatokea tu kwa bahati mbaya?

48. (a) Hebu toa mifano ya Kibiblia kuonesha mahali watu walipoishi kwa hofu.  
(b) Hebu elezea historia ya Wayahudi baada ya kutawanywa, mwaka 70 Baada ya Kristo.  
(c) Wakristo waliwahi kuteswa?  
(d) Yesu aliwahi kuahidi kuwa maisha yetu yasingekuwa na shida?

Kazi ya ziada

- (e) Hebu eleza matatizo uliyonayo katika maisha yako, na useme ni kwa nini unafikiri unayapata.

*Kumbuka kuweka jina lako, anwani na namba yako ya kumbukumbu katika karatasi yako ya majibu.*

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## NI SAWA KUPENDA MAKUU?

**SOMO:** Mathayo 18

Maelezo ya Mathayo juu ya maisha na mafundisho ya Yesu, ni pamoja na misemo kadhaa inayohusu tamaa za kibinadamu. Maelezo hayo yote yanalaani au kutuonya dhidi ya msukumo wa tamaa, ambao ni kitu chenye nguvu katika hulka yetu.

Wanafunzi wa Yesu walielekea kuwa na mjadala wa: nani angekuwa mkubwa zaidi katika kikundi chao (ukimwondoa Yesu). Inaonekana lilikuwa jambo waliloliona la muhimu kwao kwa wakati huo, na inaelekea walibishania mara nyingi.

Swala lingine lililowapa shida ni: nani ambao wangepata nafasi ya juu zaidi katika Ufalme ambao Yesu alikuwa akiwaahidia? Yesu alitambua mabishano hayo. Walipomuuliza wazi wazi, aliwajibu kwa kuwapa fundisho fupi linaloeleweka. Tutaanzia hapa uchunguzi wetu.

Angalia kwanza Mathayo 18:1-4. Swali lilikuwa: “Nini aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni?” Jibu la Yesu lilikuwa kuwapa kielelezo cha mtoto, aliyemweka mbele yao: Mpole, mkweli, mnyenyekevu mbele ya wakubwa, mwaminifu. Ujumbe wa Yesu kwao ulikuwa ni: ye yote ajinyenyekezaye mwenyewe akawa kama mtoto huyu, ndiye atakayekuwa mkubwa.

Sasa angalia linalofuata katika Mathayo 20:20 ambapo tunasoma juu ya mama mmoja wa wawili kati ya wanafunzi pale, aliyekuwa akiwaomba nafasi za heshima wanawe hao; Yakobo na Yohana.

Ni kitu cha kawaida mzazi kutamani lililo bora zaidi kwa ajili ya wanawe, lakini kwa mara nyingine tena Yesu anakuwa makini kujibu. Alitambua hiyo ilikuwa namna ya kawaida ya kufikiri kibinadamu, lakini haikuwa ikiwiana na mahitaji na malengo ya kanisa lake na Ufalme wake unaokuja. Mambo yote ya maana sana Mungu aliyoyaandaa kwa ajili ya wale watakaopata nafasi katika Ufalme wake katika dunia, watayapata atakaowaona wamestahili.

Hebu sasa pitia jibu lote Yesu analolitoa kwa mama huyo wa Yakobo na Yohana, katika msitari wa 22 na 23. Sio juu yetu kwa sasa kuwa na tamaa za madaraka katika eklesia au katika Ufalme unaokuja.

Katika msitari wa 24 tunasoma, kunatokea tatizo wale wanafunzi wengine kumi wanaposikia juu ya ombi hilo, na unaweza kuona wanavyokasirika. Yesu sasa anatumia uhusiano kati yake na wanafunzi wake hao 12 kuwa kielelezo. Yeyote anayetaka kuwa mkubwa ni lazima atumikie kwanza.

Mfano wetu mwingine uko katika Mathayo 23. Yesu anawaonya wanafunzi wake wawe macho, wasijifanye kuonekana kwa nje wasafi na watakatifu, wakati hasa misukumo waliyonayo katika mioyo yao ni ya kiburi na tamaa za kibinadamu. Kama ukisoma msitari wa kwanza mpaka wa kumi na mbili, utaipata picha ya lile analofundisha. Maelekezo hayo yanatuhusu na sisi leo, kama tunapenda kweli kuwa wanafunzi wake. Ni kwa ajili pia ya wote kati yetu ambao wamebatizwa.

Yesu aliwatumia viongozi wa dini wa wakati wake, kukosoa namna isiyo sahihi ya kumwabudu Mungu. Katika msitari wa kwanza tunaambiwa kuwa, wanafunzi wake nao walikuwa sehemu ya mkutano uliokuwa ukisikiliza mafundisho yake. Mafarisayo kwa vyovyote walichukizwa, hata hivyo ujumbe ulikuwa ni ule ule kama aliokwishatoa kwa wanafunzi wake. Yeyote anayetaka kuwa mkubwa katika Ufalme, ni sharti awe kama mtumwa kwa wengine kwa sasa.

Sasa fundisho hili lililo wazi kutoka kwa Yesu, sivyo namna wanadamu wanavyoenda mambo, sio? Wapo watu ambao kwa jinsi walivyo, hawana tamaa, wanatosheka na maisha tu yaliyo; wako mara zote tayari kutumikia; hawana tamaa ya kuwa wakubwa juu ya wengine.

Lakini wengine sisi wote tunakuwa na tamaa kazini kwetu au katika jamii zetu. Tunakuwa tunatamani kupata heshima katika jamii tunamoishi, iwe ni katika jiji, mji au kijiji. Katika sehemu hizi zote wapo watu wengi wanaojitahidi kwa nguvu zao zote kupata nafasi juu ya wengine. Mafundisho ya Yesu Kristo yanakuwaje kwa tamaa ya namna hiyo?

Sasa kumbuka kuwa, mafundisho yote ya Yesu yalikuwa ni kwa kuwalenga wanaume na wanawake ambao wamekuwa wafuasi wake. Chochote kile ambacho kilikuwa kikiingiliana na 'kuwa mwanafunzi' wa Yesu, kilikuwa na lazima kichunguzwe. Ndivyo inavyopasa hata leo. Hakuna mashaka kuwa, Yesu alijionesha kuwa mfano mzuri katika jambo hili alipowaosha miguu wanafunzi wake (Yohana 13:3-15).

Kama Yesu ambaye ni Mwana wa Mungu, aliweza kupiga magoti sakafuni mbele ya kila mwanafunzi na kumwosha miguu yake, kazi ya mtumishi wa chini kabisa, basi wanafunzi wake wote tangu wakati huu wanapaswa wawe tayari kutumikia, na sio kutoa amri.

Kwa kutegemeana na jamii tunamoishi na desturi za nchi hiyo, kuwaosha miguu wageni wanaoheshimika bado kunaweza kuwa kitu kinachofanywa. Kwa sehemu zilizo nyingi ambazo sio hivyo, somo hilo bado ni la muhimu; linahitaji kutafsiriwa kwa namna ambayo ni ya kuwatumikia wengine kwa njia zingine. Tunaweza kuzisaidia familia zetu, majirani, wafanyakazi wenzetu na watu wengine wowote tunaokutana nao njiani kila siku, kwa namna fulani fulani.

Kwa hiyo, tujiulize: tamaa zetu za kibinadamu ni mbaya? Jibu ni kwamba, inategemea kama kuna ambaye tamaa hizo zinatumizwa. Kama tunafanikiwa kupata kile tunachohitaji kwa kuwasukumia mbali wengine; kwa kutumia ujanja na mbinu zisizofaa, basi jibu ni lazima liwe 'ndio'; ni mbaya. Kama tunapata kazi kwa kuwaangusha wengine, au tunapanda cheo au hadhi kwa kuwafuata wengine, tunakuwa hatukutii mwongozo wa Yesu.

Ni wazi yote yanategemea kusudi letu hasa ni nini. Ni kujisikia tumepanda hadhi au kulipiza kisasi kwa wale wasiotupenda, au tunalotaka kufanya litawanufaisha wengine? Tunaweza kuwa viongozi wazuri wanaofoa? Tunaweza kuwa watu wanaoweza kuganga migawanyiko kati ya watu? Haya ni maswali tunayohitaji kujiuliza, na kuna mifano mingi katika Biblia inayoweza kutusaidia kufanya hivyo.

Angalia kwanza katika kitabu cha Esta, Sura ya 3, msitari wa 1 mpaka wa 9. Hapo utamkuta mtu aliyekuwa akiitwa Hamani, aliyekuwa mshauri wa kutegemewa katika Ikulu ya mfalme wa Uajemi. Hamani alikuwa kizalia cha Waamaleki na adui mkubwa wa Wayahudi. Alibuni mpango wa kuwafanya Wayahudi wote chini ya Dola ya Kijemi wauawe.

Matokeo ya mpango wake huo ulipogunduliwa, yapo kwenye Sura ya 4 msitari wa 3. Kwa jinsi alivyopanga hili litimie, inaonesha Hamani alivyokuwa na nia ya kiuovu ya kuwadhuru wengine. Kama utakuwa na muda wa kukisoma kitabu chote cha Esta utagundua kuwa, kinasisimua kusoma, na kitakuonesha mfano wa namna Mungu alivyokuwa akiwaangalia na kuwachunga watu wake kwa namna isiyotegemewa.

Mfano mwingine ninaotaka tuutizame uko katika Danieli; mtu wa imani kubwa sana kwa Mungu. Alikuwa mtu wa uwezo mkubwa na unyenyekevu wa hali ya juu. Katika maisha yake yote yasiyo ya kawaida, Danieli wakati wote alimpa Mungu sifa kwa miujiza yote iliyofanyika, na kamwe hakudai kuwa na uwezo wa kipekee yeye mwenyewe. Angalia sasa katika Danieli 2:26-30.

Tamaa ya kibinadamu inaweza kuwa na msisimko unavyojitahidi kwa kila njia kufanikisha unachokitaka, lakini ni muhimu kuufikiria mfano wa Sulemani, aliyekuwa mfalme mkubwa kuliko wote wa Israeli. Aligundua kuwa, unapokuwa umefikia hatimaye lengo lako, unalokuwa umepata haliwi la kutosheleza hasa! Unaweza ukawa umejaribu kila kitu na kupata kila kitu, lakini kamwe hutajisikia kabisa umetosheka.

Kuweza kutambua ilivyokuwa kwa Sulemani, angalia Mhubiri 2:1-11. Sulemani anasema katika msitari wa 26 kuwa, kitu kilicho bora zaidi ni kuifuata njia ya Mungu.

Kwa hiyo, Njia ya Mungu basi ni ipi? Ni njia ambayo imeoneshwa vizuri kabisa na Yesu. Ni njia ambayo wale wote watakaokuwa wakubwa, watacaoongoza, lazima pia wawe 'watumikaji'; watu wanaowatumikia wengine. Ni njia ambayo hulka ya mtu mume, au mtu mke, inaongozwa na upendo na huruma. Inaongozwa na moyo wa rehema na dhamira ya kuwasaidia wale wanaotuzunguka.

Mfano wetu wa maana kabisa utakuwa wakati wote ni Yesu mwenyewe, ambaye, ingawa atakuwa Mfalme mkubwa kabisa juu ya mataifa yote atakaporudi duniani, aliweza kuutumia muda wake na nguvu zake kuwahudumia maskini na wagonjwa. Alikuwa na muda na walemavu na vipofu, wakoma na waliokuwa na matatizo ya magonjwa ya akili.

Hatutaweza kuiponya huzuni inayotuzunguka kila siku, ya hali mbaya aliyonayo mwanadamu kama Yesu alivyofanya. Hata hivyo, tunaweza kuifanya nia yoyote tuliyo nayo, kuwa mpango unaotekelezeka, katika kuwasaidia wengine kwa njia yoyote tunayoweza.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## UAMINIFU MBELE YA MUNGU NA MBELE YA MWANAWA YESU KRISTO

**SOMO:** Matendo 5

Katika somo hili, nataka tuangalie kwa makini mambo tunayofanya kila siku. Baadhi yake yatakuwa ni kwa ajili ya Mungu na Yesu, kama kuhubiri kwa wengine au kuwasaidia wagonjwa na wazee, wakati mengine yatakuwa ni kwa kuhudumia familia au kuipa mwelekeo fulani, au wale tunaowajibika kwao.

Matendo mengine yote yatakuwa yakiwahusu watu tunaokutana nao kila siku kwenye shughuli, au safari au kwenye lolote linaloweza kutokea.

Uaminifu ni kitu kinachohusu kutii sheria au kanuni. Ni hivyo zaidi kwa sheria za Mungu, lakini pia kwa sheria za jamii tunayoishi ndani yake. Wakati mwingine kunapokuwa na vita au majanga mengine, sheria za kibinadamu zinavunjwa, lakini mfuasi wa Yesu hajiachii tu kuzivunja. Sababu ni kwamba sheria alizoziweka Mungu na kuelezewa kwa umakini sana na Yesu na mitume wake, zinakuja kwanza katika maisha yake.

Katika somo mojawapo la nyuma kuhusiana na hofu, tulitazama pamoja fundisho lililopo kwenye Zaburi 34:7. Haya ni maneno ya maana sana na ni faraja kubwa kwetu katika nyakati za shida, lakini maneno hayo yanafanya kazi kwa namna mbili. Kama malaika wa Mungu wapo karibu na watu wa imani katika maisha yao ya kila siku, basi wapo pia karibu kusikiliza na kuona tunapofanya ujanja na kukiuka maadili; tunaposema uongo au kuchukua kitu ambacho sio chetu.

Njoo nami sasa kwenye maneno ya Paulo juu ya mada hii, tuweze kuona anachotuambia. Tuanze na Waraka wake kwa Warumi, Sura ya 12, msitari wa 17. Paulo anaonekana kuzingatia hapa jinsi watu wasio Wakristo wanavyomtazama mtu anayemfuata Yesu. Kumbuka hapa kuwa, kuhibiri sio tu yale tunayosema kwa wengine; kunahusu pia yale tunayofanya na namna tunavyoyafanya. Paulo anaendelea katika Warumi 13:12-14 kusema juu ya 'matendo ya giza'; mambo ambayo watu wanayafanya kwa kuvunja sheria, wakifikiri kuwa hawataonekana.

Yesu alilitumia wazo hili alipokuwa akiongea na Nikodemo (Yohana 3:19-21). Kusudi analokuwa nalo mfuasi wa kweli wa Yesu, ni kufanya mambo yote kwa namna ambayo yanaweza kuonwa wazi na yeyote; na Mungu na wanadamu wengine. Hili ni fundisho lililo wazi kabisa, au siyo?

Katika Waraka wake kwa Wafilipi, Paulo anatushauri tuwekee mambo fulani-fulani kanuni katika maisha yetu (Wafilipi 4:8). Mambo kama: ukweli, staha, haki, usafi, mambo ya pendeza, yenye sifa njema n.k. ni mambo yatakayowaonesha wengine kuwa ni kweli unamfuata Yesu, na kwa wakati huo huo yatakuwa ni njia iliyo bora kabisa ya kuwahubiria. Kama tutakuwa tunawazungumzia majirani zetu habari za Yesu na Injili yake ya Ufalme wa Mungu tukiwa na hulka hizo, watakuwa tayari zaidi kuamini tunachosema.

Ni kitu kinachoshangaza kusoma katika nyaraka za Paulo na Petro ushauri wanaotoa, juu ya namna tunavyopaswa kuwachukulia wale walio na madaraka juu yetu. Serikali zinatofautiana duniani, zipo zilizo nzuri na zingine mbaya. Zipo zenye mifumo ya kisheria iliyo ya haki, wakati zingine sheria zake ni kali na za kikatili. Hata hivyo, mitume hao wanashauri utii kwa mamlaka zote. Hebu angalia waraka wa kwanza wa Paulo kwa Timotheo, Sura ya 2, msitari wa kwanza mpaka wa tatu.

Maneno haya yaliandikwa katika wakati ambao dola ya Kirumi ilikuwa ikiwatesa Wakristo. Ni lazima lilikuwa somo gumu kwa wafuasi kulipokea na kulitekeleza wakati huo, lakini ni somo lililopo hapo na kwetu pia kulifuata.

Yesu aliwafundisha wafuasi wake kulipa kodi zao kwa mfalme wa Kirumi na, kwa maneno yake, anatupa nasi kitu kingine cha ziada kukumbuka. Maneno yake katika Mathayo 22:17-22 ni maelekezo ya kulipa nchi kiuaminifu kodi na ushuru mwingine, na kumpa Mungu upendo wetu na maisha yetu yote kwa kumtumikia.

Paulo aliwapa Wakristo wa Kifilipi nasaha za maana sana. Kuna usemi: “Ikiwapo sifa nzuri yoyote...” (Wafilipi 4:8). Ulikuwa ukimaanisha nini? Haya ni mambo ambayo yalikuwa kwa ujumla yamekubalika kwa wafuasi wote wa Yesu kufanya. Hayakuwa tu kwa namna mtu anavyoona, bali wote walivyoona kwa pamoja, wakiwepo wale ndugu wa kutegemewa zaidi katika eklesia. Kwenye Matendo 6:3 kuna mfano kama huo ambapo maoni ya pamoja ya wafuasi wote yalitumika.

Ilikuwa ni muhimu kwa wakati huo kuwateua watu wakufaa zaidi waliokuwapo. Walikuwa wawe mashemasi; viongozi wa kuwaongoza wengine. Pengine ni uchaguzi mzuri waliofanya; tunayo taarifa ya wawili kati ya hao, walioonekana kuwa watumishi wazuri katika eklesia, wenye uwezo wa kuongoza na kuhubiri kwa bidii.

Kuna somo katika Agano Jipya linalorudiwa-rudiwa kuwa, tufuate mafundisho ya Yesu, na miongozo makini ya mitume wake. Ingawa kuna ushauri huu wa Kibiblia, kikawaida tunaelekea kuwategemea zaidi marafiki na jamaa zetu katika kupata ushauri wa mambo yetu mengi.

Uliwahi kufikiri ni nini hasa kilichopo kwa mtu mwingine, kinachokufanya wewe ufuata ushauri wake? Pengine imekuwa: ni mtu mzima, mwenye uzoefu na hekima, au ni mkweli. Hebu tuangalie mifano miwili ya watu waliotoa ushauri. Wa kwanza tunauona katika Hesabu 13, ukingoni mwa Nchi ya Ahadi. Musa alikuwa amewatuma wapelelezi 12 mbele ya taifa lote la Israeli kuipeleleza hiyo nchi na kuleta ripoti. Waliporudi taarifa zao zilitofautiana (ms. 26-33).

Kati yao kumi walirudi wakiwa wamejaa hofu na mashaka, na ni wawili tu waliokuwa na imani na uhakika kuwa, kwa msaada wa Mungu hakuna ambacho kisingewezekana.

Tunapoendelea kusoma kifungu cha 14 tunaweza kuona maneno ya Kalebu na Yoshua katika msitari wa 6 mpaka wa 9. Unafikiri wananchi waliwaamini nani? Ilikuwa, kwa bahati yao mbaya, ni wale waliowakatisha tamaa. Ghadhabu ya Mungu juu ya lile walilolichagua inatuonesha ni nani kati ya wale kumi na wawili, waliokuwa wakweli na wa kuaminika; watu wa imani. Ilikuwa ni Kalebu na Yoshua. Zawadi yao ilikuwa kuvuka na kuiingia Nchi ya Ahadi na familia zao, wakati wengine wote waliokosa imani waliangamia nyikani.

Mfano mwingine ni wa marafiki waliotoa ushauri kwa Ayubu, unaopatikana katika Kitabu cha Ayubu. Ayubu alikuwa amepoteza kila kitu alichokuwa nacho. Akiwa amekaa kwenye dampo la takataka za mji akijikuna, alitembelewa na marafiki watatu waliompa ushauri. Lakini haukuwa ushauri mzuri, na mwishowe tunasoma kuwa, Mungu aliwalaumu marafiki hao watatu kwa ushauri wao potofu (Ayubu 42:7-10).

Ilikuwa ni vizuri kwa Ayubu kwamba alipuza ushauri ule wa rafiki zake hao, na kuing’ang’ania imani yake kwa Mungu. Kitu cha muhimu cha kugundua hapa ni kwamba, watu hao watatu hawakujaribu kumsaidia Ayubu; walitumia muda mwingi kujaribu kumfariji tu katika huzuni yake (Ayubu 2:13). Hawakutumia kanuni za Mungu katika ushauri wao kwa Ayubu, badala yake walitumia hekima ya kibinadamu inayoshindwa. Huu ndio utofauti tunaohitaji kuuchunguza tunapotaka kupata ushauri kwa marafiki.

Mambo mengine yanayohusu uaminifu yanaonekana kuwa madogo sana na yasiyo na umuhimu, lakini tukumbuke kuwa, kwa Mungu mambo madogo madogo sana tunayofanya, yana maana sana. Tuangalie sasa unabii wa Mika 6:8. Baadhi ya mifano imetolewa katika msitari wa 10 na wa 11.

Hebu jaribu kuwafikiria wenye maduka walio na mizani, ambazo zimefanyiwa ujanja zito bidhaa pungufu kuliko kile mteja anacholipia. Mwenye duka anaweza kufikiri ni kawaida, ni ujanja mzuri, lakini Mungu anachukizwa na uovu huo uliojificha. Lakini unaweza usiwe na duka au genge, sasa maneno haya yanakuhusuje?

Katika maisha yetu, ni mambo mengi tunayofanya kwa ajili ya watu wengine. Tunaweza tukawa na ajira, kwa mfano. Tunaweza katika kufanya kazi tukawa tunajituma na kufanya kazi kwa bidii, au kufanya kidogo tu. Tunaweza kupata au kutopata mshahara wetu. Ni hivyo hivyo inavyokuwa tunapofanya mambo kwa ajili ya Mungu. Tunaweza tukajitoa sana au kidogo tu. Uongo unakuja tunapojifanya kwa Wakristo wengine kuwa, tumejitoe kwa yote tuliyonayo wakati sio kweli.



Tunapokuwa tumepewa wajibu wa kutekeleza kwa ajili ya wengine au kwa ajili ya kipato, ni lazima tulikumbuke somo hili. Bila kujali ni kwa kiasi gani tunajaribiwa kuzembea kutekeleza wajibu tuliopewa, Mungu anajua tunavyofikiri na kile tunachoweza kufanya kwa siri. Inaweza ikawa rahisi kuyaficha matendo yetu kwa wengine, lakini hatuwezi kumficha Mungu.

Kuna fundisho kali kuhusiana na hili, katika Matendo ya Mitume, Sura ya 5, msitari wa kwanza mpaka wa tano. Hapa mtu na mkewe walijaribu kusema uongo kwa mitume, lakini ilikuwa mbele ya Mungu wasiyemwona. Hukumu waliyopata ilikuwa ya kutisha. Unaweza ukaona kuwa, huu ulikuwa ni uovu kama ule wa kuwa na mizani batili, au mawe ya kupimia yasiyo sawa, na tunasoma katika Mika kuwa Mungu anachukizwa na hili.

Kitendo hicho cha Anania na Safira ni lazima kilionekana kibaya sana, kiasi kwamba hatua ya hapo kwa hapo ilibidi ichukuliwe. Hili ni tukio pekee katika Agano Jipya, ambapo uweza wa Roho Mtakatifu umetumika kuua. Kwingineko pote ulitumika kuponya na kurudishia uhai kwa wale waliokufa.

Yesu alipojiachia achukuliwe na wale askari, apigwe na kisha asulubiwe, alijitoa kwa kila kitu kwa ajili yetu. Alifanya hivyo ili watu waweze kufunguliwa njia ya wokovu kutoka katika mauti ya milele.

Hapakuwa na udanganyifu katika Yesu; alikuwa wakati wote mkweli kabisa na mwema kwa wote waliomjea. Katika hotuba yake juu ya kuishi Kikristo, ametupa vigezo kadhaa vya kipekee vya kulenga katika kumwitikia (Luka 6:35-38). Maneno ya mwisho katika msitari wa 38 yanatukumbusha haja ya kutoa kwa uaminifu, kama tunahitaji kupokea urithi wa milele.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

### MATUMIZI NA UDHIBITI WA HASIRA

**SOMO:** Mwanzo 34

Hasira ni hisia ya ajabu sana ndani ya uanadamu wetu. Pengine ina nguvu hata zaidi katika ulimwengu wa wanyama, ndege na samaki. Katika Biblia kuna ushauri mzuri unaotolewa wa namna ya kuidhibiti hasira, na kuna maonyo kadhaa ya wazi kuhusiana na nini kitatokea kama tukiiachia hasira itutawale.

Hasira imekuwa na mwanadamu tangu mwanzo wa historia yetu; sio kama ni tatizo la leo. Kama ukiangalia Mwanzo 4 utaona maelezo ya jambo la kutisha hasira inavyoweza kumpelekea mtu kufanya: “Kaini akaghadhibika sana, uso wake ukakunjamana” (Mwanzo 4:5). Matokea yake alimuua ndugu yake, Habili.

Kwa kawaida inawezekana kumtambua mtu akiwa na hasira kali, kutokana na kubadilika kwa sura yake. Mara nyingi, na hasa kama ni mweupe, kunakuwa na kubadilika hata kwa rangi ya ngozi yake usoni.

Kutokana na somo hilo katika Mwanzo tunahitaji kukumbuka kuwa, Kaini alikuwa ni mtoto wa kwanza wa Adamu na Hawa, na kwa hiyo alikuwa ni mtu wa tatu kuishi katika dunia. Kama angekuwa amechukia tu, isingekuwa neno sana. Lakini, kwa kuwa Mungu alikuwa ameikubali dhabihu iliyokuwa imetolewa na mdogo wake, Habili, na kuikataa ya kwake, chuki iliipandisha hasira na kuwa ghadhabu, iliyomfanya Kaini amuee Habili, ndugu yake.

Kwa hiyo ilikuwa kwamba, katika mwanzo kabisa wa historia yetu, uuaji ulifanyika kutokana na wivu na hasira. Tunajifunza hapa kuwa, hasira ni ya hatari! Katika tukio hilo, ilileta balaa kubwa katika familia yote. Iipelekea Habili kupoteza uhai wake, na Kaini kufukuzwa. Adamu na Hawa wakawa wamewakosa vijana wao wote wawili.

Mfano mwingine upo katika maneno ya unabii yaliyotamkwa na mmojawapo wa waasisi wa taifa la Israeli; Yakobo. Alipokaribia kufa aliiita familia yake pamoja na akatabiria hatma yao yote ambavyo ingekuwa. Kifungu cha Mwanzo 49:5-7 kinawaongelea wawili kati ya wana wa Yakobo, Simeoni na Lawi.

Hawa wanaume wawili walikuwa wamejionesha kuwa, walikuwa watu wa hasira kali isiyo na maana. Hebu kifungue kifungu hicho cha 34 ukisome mwenyewe. Haya yalikuwa matendo ya giza, na ya aibu katika siku za mwanzo kwa taifa la Israeli; yakivunja ahadi na kukiuka matarajio kimakusudi. Kilichofanya hili litokee ilikuwa ni hasira.

Kitu kinacholeta hofu juu ya haya yote ni kwamba, sisi wote tunapatwa na hasira mara kwa mara. Kama tusingepatwa, tungekuwa watu wa ajabu sana. Hasira inakuja kutokana na kutotimia malengo au matarajio, kushindwa, wivu, kuchukizwa, na mara nyingine hata kuchoka tu. Tunaweza tukapata hasira kwa ajili ya watu wengine na pia dhidi yao.

Kama tunajisikia mtu mwingine ametufanyia ubaya, tunaweza kujikuta tumechukia, na ni rahisi sana kujihesabia wenyewe sababu iliyotufanya tuchukie kuwa ni halali. Kwa namna hii tunaihalalisha hasira, lakini ni mbaya!

Kuna watu waliozaliwa na hasira za haraka-haraka, wakati wengine wanakwenda pole pole zaidi. Ni wazi kuwa wale wanaokasirika kwa kasi, wana wajibu wa kufanya la ziada kuishinda hiyo hulka. Maneno makali yanayosemwa kwa hasira hayawezi kirahisi kufutika. Neno linasema:

“Jawabu la upole hugeuza hasira, bali neno liumizalo huchochea ghadhabu. Ulimi wa mwenye hekima hutamka maarifa vizuri, bali vinywa vya wapumbavu humwaga upumbavu. Macho ya BWANA yako kila mahali, yakimchunguza mbaya na mwema” (Methali 15:1-3).

Katika mistari hiyo, kuna ushauri wa maana. Tunaonywa kuepuka maneno ya mashindano; ‘Neno liumizalo huchochea ghadhabu’. Hekima na upumbavu vina nafasi katika nafsi ya mtu. Kwa maneno mengine, kama tukifikiri kwa makini kabla ya kusema, tunaweza tukaepusha matatizo.

Hili sio jambo rahisi kufanya, lakini ni la maana sana kama tukijizoeza kufanya hivyo. Katika msitari wa 3 suala hili limewekewa uzito hata zaidi kwa kuwa tunaambiwa, macho ya BWANA yako kila mahali, ‘yakimchunguza mbaya na mwema’. Mungu anatambua yote tunayofanya na tunayosema. Hili lina mguso mkubwa, na hasa kwa wale kati yetu ambao tayari wamemweka vizuri Mungu mioyoni mwao, kwa kuwa Mungu anawajali sana wale wanaompenda.

Mahusiano kati ya hasira na upumbavu, yanayojitokeza tena katika Kitabu cha Mhubiri. Tunaambiwa: “Usifanye haraka kukasirika rohoni mwako, maana hasira hukaa kifuani mwa wapumbavu” (Mhubiri 7:9). Unajisikiaje juu ya maneno haya? Ni nasaha nzuri?

Ningependa sasa tugeukie Agano Jipya na kuifungua barua ya mtume Paulo kwa Wakolosai. Paulo anawaandikia wafuasi wa Yesu; watu waliobatizwa, walioahidi kuufuata mfano wa Yesu katika maisha yao. Katika Sura ya tatu, wasomaji wa waraka huu wanakumbushwa umuhimu wa ubatizo: “Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu” (Wakol. 3:1).

Kufufuliwa hapa kunamaanisha kuibuka kwenye maji ya ubatizo, kama ambavyo kutumbukizwa ndani ya maji kunavyowakilisha kufa na kuzikwa pamoja na Kristo. Paulo anatumia kielelezo hiki anaposemea hili katika Wakolosai 2:12.

Muumini anapobatizwa, anapaswa baada ya hapo ayatafute maadili ya kiroho, na sio kuhisi na kufikiri kama wale ambao hawamfuati Bwana Yesu Kristo katika maisha yao. Baada ya hapo Paulo anatoa orodha ya mambo ambayo mfuasi ni lazima ayaondoe akilini mwake. Hayo mambo, anasema Paulo, yanaweza yakatuletea ghadhabu ya Mungu (Wakol. 3:6).

Nataka tuangalie sasa msitari wa 8 ambapo hasira na mabaya mengine yanatakiwa yawekwe mbali na maisha ya Mkristo. Alilielezea hili vizuri zaidi alipowaandikia Waefeso (Waef. 4:17-24). Picha anayoitoa ni ya mfuasi-mpya anayeziacha namna zake za maisha ya awali, na kuvua utu mpya, ‘katika haki na utakatifu wa kweli’. Haya yanapaswa yawe ndiyo matokeo ya kubatizwa ndani ya muumini.

Paulo anatambua ya kuwa, hulka ya ndani ya mfuasi mpya inachukua muda kubadilika, kwa hiyo katika msitari wa 26 anaongelea hasira, akisema: “Mwe na hasira, ila msitende dhambi” (Waef. 4:26). Alikuwa anakubali kuwa kutakuwa na wakati ambapo hata mfuasi madhubuti kabisa wa Yesu atapatwa na hasira na kwamba, katika mazingira ya namna hiyo, itamfaa akasirike lakini ajidhibiti asitende dhambi. Hasira iwe akilini, lakini isimfanye afanye kitendo kiovu kinachotokana na kukasirika huko.

Ametuachia tufikirie wenyewe ni kwa wakati gani hali hiyo inatupata, na itakuwa ni zoezi la maana kwako kutafakari hili, na kuzingatia ushauri huo kulingana na maisha yako yalivyo. La muhimu lingine katika ushauri huo ni kwamba, hasira hiyo inapotujea, ni muhimu iwe ya muda mfupi; iondoke kabla ya jua kutua. Anasema Paulo: ‘Jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka’.

Huu hakika ni ushauri mzuri sana, na hasa kunapokuwa na karaha za kimahusiano kati ya mume na mke. Hasira isiachiwe ikaende siku ya pili; mmojawao ni lazima apende suluhu; atafute ‘upatanisho’.

Tumeshawafikiria watu wale ambao wanazaliwa na hasira za haraka-haraka; wenye uwezo mdogo wa kujidhibiti. Hebu sasa twende pamoja kwenye barua Paulo aliyomwandikia Tito, Mkristo kijana aliyempa jukumu la kufungua eklesia katika kisiwa cha Krete. Katika Tito 1:1-7 alimpa mwongozo wa kuweka waumini ambao wangukuwa ‘wazee’ wa eklesia hizo, na utaona kuwa mojawapo ya sifa za kuangalia ilikuwa ni wasiwe, ‘wepesi wa hasira’.

Ni Yesu mwenyewe aliyekuwa ametoa kanuni zote za maisha ya mfuasi. Katika hotuba yake ya Mlimani, mojawapo ya mambo ya muhimu aliyosema Yesu, ilikuwa ni kuhusu hasira. Hebu soma Mathayo 5:21-22 upate mwenyewe anachosema. Kama tukiyachunguza maneno yake, tutakuta kuna maswali kadhaa yanatujea.

Tunaweza tukawaelezea watu wengine kama ni 'wajinga' katika namna yetu ya kuongea ya kawaida, lakini mara nyingi ni maneno yanayosemwa kwa kilipuka au mzaha kidogo, na yanapokelewa kihivyo na mtu tunayeongea naye. Ni wakati maneno hayo yanaposemwa kwa hasira na kwa kukaziwa, ndipo yanapomuuma mtu wa pili na hayakupaswa kutumika.

Katika msitari wa 23 mpaka wa 26 Yesu anaruhusu hali ambayo, kama tumefanya vibaya au kusema vibaya kitu, tunaleta tena kuelewana. Ushauri wake uko wazi: "Upatane kwanza na ndugu yako" na "Patana na mshitaki wako upesi". Hili linafanya kazi kwa namna nyingine pia, maana kuna neno lingine la maana analilolitia Yesu katika kuwafundisha wanafunzi wake; neno 'msamehe' (Luka 17:3,4).

Mtu anapokuja kwako na kusema 'nisamehe', kubali ombi lake na usilifanye jambo hilo kuwa kubwa kwa kuwa mgumu. Katika Injili zote tunafundishwa kuwa, kama tunategemea Mungu atusamehe makosa yetu, ni lazima na sisi tuwasamehe wengine.

Nataka nimalizie somo hili kwa kuongea kidogo juu ya 'hasira ya haki'. Hii ni aina ya hasira au ghadhabu inayoonekana katika Biblia, na ipo kwa sababu nzuri. Hasira inayotokana na ujinga wetu, kutotii kwetu au dhambi zetu, ni hasira inayostahili kuwepo kwa Mungu aliyetuumba. Yeye peke yake ndiye aliye na haki kamilifu ya kukasirika, na tunasoma mengi juu ya hili hasa katika Agano la Kale.

Mungu alimuumba mwanadamu kwa namna ya kipekee, kati ya viumbe wengine wenye uhai katika sayari hii. Sisi ni watu tunaoguswa sana tunapofanyiwa ubaya, lakini ni wajanja-wajanja sana. Tunaweza kuwa na upendo, lakini tuna hila na tunalipuka-lipuka mara nyingine. Tangu Adamu na Hawa wafukuzwe katika bustani ya Eden kwa sababu ya kiburi, mwanadamu wakati wote amekuwa akimhuzunisha Mungu.

Agano la Kale linaongelea ghadhabu ya Mungu kwa taifa la Israeli. Hili halina maana kuwa haoni uovu walionao wanadamu leo; ni kinyume chake kabisa. Mungu alimtoa Mwanawe pekee awe dhabihu kwa ajili ya dhambi za watu, na kwa sababu hiyo anataka mwikio wa maana kutoka kwetu. Tumepata bahati ya kuwekewa mpango wote wa Mungu mbele yetu katika Biblia. Tunaitikia?

Historia ya taifa la Israeli imehitimishwa katika unabii wa Hosea, katika Sura ya 13, msitari wa 9 mpaka wa 11. Kitu kibaya kuliko vyote walichofanya Israeli kilikuwa kumkataa Mungu, na kuchagua kuabudu miungu ya miti na mawe (sanamu). Baada ya hapo walimtaka Mwana wa Mungu auawe, likatokea. Kwa sababu hizo, Mungu alipatwa na hasira juu ya watu wake.

Kuna fundisho la maana kwetu leo kwa kuwa, kama tukimwalia tena Hosea, kwenye Hosea 14:1-4, tunauona tena upendo wa Mungu kwa watu wake Israeli, kwa namna ambavyo atawabariki mbeleni. Katika somo la mbeleni tutalirudia tena somo hili la upendo wa Mungu kwa kuwa ni la muhimu sana.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## MFUASI NA NCHI

**SOMO:** Warumi 13

Mtume Petro alipokuwa akiziandikia eklesia zote katika Asia alisema kwamba, wafuasi wa Yesu ni lazima wamche Mungu na kumheshimu mfalme (1 Petro 2:13-17). Kwa wakati huo, mfalme pekee alikuwa Mfalme wa Kirumi, na kwa wakati huo wa mwisho-mwisho wa maisha ya Petro, mfalme huyo alikuwa Nero, aliyekuwa 'bala' kwa ukatili wake na kwa jinsi alivyowatesa Wakristo.

Tatizo la kuwa mfuasi wa Yesu, na wakati huo huo kuishi katika dunia ya watu iliyojaa ubadhilifu, ukatili na utovu wa maadili, ni lazima lilionekana gumu kwa Wakristo hao wa kwanza. Tatizo hilo halijapungua makali hata leo; bado lipo. Somo hili litaonesha maelekezo ya Kibiblia kwa ajili ya wafuasi wote wa Yesu waliobatizwa, na wale ambao wamekuwa wakiifuatilia kozi hii ya Biblia kwa njia ya posta.

Litajaribu kusaidia wote wale wanaoona shida kuelewa mahusiano yanavyopaswa kuwa, kati ya mfuasi wa Yesu na Serikali katika nchi anamoishi. Masuala tutakayoangalia ni:

1. Huduma za kijeshi.
2. Ushiriki katika shughuli za kipolisi, mgambo n.k.
3. Kutumikia mahakama au kuwa sehemu ya mfumo wa kisheria.
4. Kushiriki katika maandamano yoyote ya kupinga.
5. Kutumia haki ya kupiga kura.

Kwa kuwa somo hili limeandikwa kwa ajili ya kutumika katika nchi nyingi, ni lazima litoe maelezo kuhusu sheria za namna tofauti, na kanuni zinazowatawala raia wa nchi hizo. Ni muhimu pia lisemee uwezekano kwamba, nchi yako inaweza ikawa na tatizo la kivita kwa wakati huu. Katika baadhi ya nchi, vijana wanatakiwa kujiunga na jeshi kwa lazima na kupambana vitani. Inakuwaje kwa mfuasi wa Yesu?

Kusimama mbele ya maafisa wanaowaandikisha vijana kwa nguvu, au mbele ya mahakama kudai haki ya uhuru wa kutojiunga na jeshi la nchi yako, vyote vitahitaji moyo wa ujasiri wa hali ya juu. Lakini, vitahitaji pia kuzijua sababu za Kimaandiko za kwa nini ufanye hivyo. Mkufunzi anayekufundisha, anaweza kukupatia vijitabu vya Kikristadelfia vinavyoongelea mada hii kuifafanua zaidi, lakini sababu za kawaida zimeelezwa hapa.

Tuangalie kwanza katika Injili ya Luka, Sura ya 22, msitari wa 35 mpaka wa 38. Mtu anaweza akanukulu mistari hiyo kwako kuonesha sababu ya kupambana, lakini ni muhimu uangalie kwa umakini matukio yote katika usiku ule ambao Yesu alikamatwa. Wawili kati ya wanafunzi wake tayari walikuwa wamebeba silaha, na tunajua ya kuwa mmojawao alikuwa Petro (Yohana 18:10). Fundisho kwa wanafunzi wake na kwetu pia limeandikwa katika Injili ya Mathayo: "Wote waushikao upanga, wataangamia kwa upanga" (26:51-53).

Yesu alitaka kuweka wazi kwa wafuasi wake kuwa, hawakupaswa kutumia nguvu; hawapaswi kulazimisha. Alionesha kimatendo kulivyo 'kuwapenda maadui' kulingana na mafundisho yake, kwa kumponya askari yule wa Kuhani Mkuu aliyeshambuliwa na Petro, kwa kulirudishia sikio lake (Mathayo 5:44, Luka 33:50, 51). Ili uweze kuwashawishi wakubwa walioko madarakani kuwa ni kweli unafuata na kuitii miongozo ya Yesu, itakubidi uoneshe imani yako kwa namna unavyoishi. Ukiweza kufanya hivyo, watu wengine wataweza kutambua ya kuwa uko tofauti.

Yesu analielezea hili kwa namna nzuri sana akisema: "Nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni" (Mathayo 5:16).

Paulo alitoa maelekezo hayo kwa Wakristo waliokuwa wakiishi Rumi. Aliweka wazi jukumu la mfuasi la kuwa mtii kwa sheria za nchi yake, na wajibu wake wa kulipa kodi zote (Warumi 13:1-7). Katika waraka wake kwa

Timotheo anaamuru tuwaombe wafalme na wote wenye mamlaka, tukiomba waweze kuendelea kuturuhusu kumwabudu Mungu kwa namna anavyotutaka.

Miaka kama mia tano nyuma Mungu alikuwa ametangaza kuwa, ndiye aliyekuwa akiongoza katika falme za binadamu, na ndiye aliyekuwa akiwaweka watawala madarakani kulingana na anavyoona (Danieli 4:25).

Pamoja na jeshi, kuna kazi zingine zinazowataka watu wavae sare, wabebe silaha na kuapa viapo maalumu vya utii kwa taifa. Kutokana na sababu tulizozisema, na haja ya kuelezea kwa nini unapingana na kuingia vitani, isingekuwa jambo la busara kuipokea ajira ya namna hiyo; hata kama inatoa mshahara mzuri na marupurupu, kwa maisha bora zaidi ya familia yako.

Bwana Yesu alipokuwa akihukumiwa mbele ya mtawala wa Kirumi, Pilato, alisema kuwa Ufalme wake ungekuwa wa wakati mwingine. Haungekuwa wa kuwekwa kwa nguvu za kijeshi, na wafuasi wake wasingehitaji kupambana (Yohana 18:36).

Nchi zile zenye mfumo wa kisheria unaotokana na ule wa Waingereza, zitakuwa kwa kiasi kikubwa zikitumia 'wazee wa mahakama' kukaa katika mahakama ya kisheria na hakimu, kuamua hukumu ya mtuhumiwa aliyefikishwa mahakamani. Katika nchi ya Uingereza na Amerika, inachukuliwa kuwa ni haki na wajibu wa raia wote kufanya kazi hiyo wakitakiwa. Kama hili likikutoka, itakubidi kuamua kama ni sawa au sio sawa kuwa na sehemu katika baraza hilo. Hapa kuna mwongozo unaotoka kwenye Biblia, unaoweza kukusaidia.

Pamoja na Paulo kutoa maelekezo ya kuwa raia wema, la kwanza kukumbuka ni kwamba, wajibu wetu wa kwanza ni kwa Mungu; 'kumcha Mungu, na kumpa mfalme heshima' (1 Petro 2:17). Petro na wanafunzi wenzake kadhaa walipoletwa mbele ya baraza la Kiyahudi lililokuwa likitawala, wakishutumiwa kwa kumhubiri Yesu kinyume cha sheria, jibu la Petro lilikuwa: "Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu" (Matendo 5:28, 29).

Bwana Yesu yuko wazi katika maelekezo yake kwetu kuwa 'tusihukumu' (Mathayo 7:1). Maana yake hapa ni kuwa, tusilaani au kutolea adhabu makosa ya wengine. Hili liko wazi kutokana na maneno yake yaliyofuata na mfano mdogo aliotoa, kumhusu mtu mwenye boriti kwenye jicho lake (ms. 2-5).

Yesu anatutegemea tuwe na maamuzi yenye umakini, katika mambo na matukio mengi katika maisha yetu. Hatupaswi kuwa mahakimu. Yeye mwenyewe ndiye atakayekuwa mhukumu mkubwa wa wote, atakaporudi duniani. Sio juu yetu kuwatolea hukumu watu wengine; tunalohitajika kufanya ni kuwa waangalifu tu na wale wanaotaka kututenga na Yesu.

Katika waraka wake kwa Wafilipi Paulo anaeleza kuwa, kumfuata Yesu kulitakiwa kuwe kipau-mbele chao namba moja. Uraia wetu upo naye mbinguni kwa kuwa huko ndiko aliko kwa sasa. Hatuna sehemu katika michakato ya serikali za kibinadamu, na mifumo ya kisheria ya nchi yoyote ndio msingi wa taifa hilo. Kwa hiyo, hatuwezi kuwa na sehemu katika kuhukumu.

Hili lina maana ya kwamba, tutaona shida kujiunga na kazi ya uhakimu au kushiriki katika namna haki inavyotolewa. Kuwa 'mzee wa baraza' ni kushiriki katika namna haki inavyotolewa. Kuwa 'mzee' kunamuweka mtu katikati ya mchakato huo.

Kutokana na vifungu tulivyovitazama katika somo hili, inaeleweka kuwa, kama wafuasi wa Yesu ni lazima tujitenge wenyewe na dunia, na mengi ya mambo watu wanaotuzunguka wanaoyaona ya kawaida; ya kukubalika. Paulo alitoa nasaha nzuri kwa Wakorintho katika waraka wake wa pili kwa Wakorintho, Sura ya 6, msitari wa 14 mpaka wa 18. Kama tumekuwa wafuasi wa Yesu, ni kwa kuwa Mungu ametuita kwa ajili ya fursa hii ya ajabu ya kuwa watoto wake.

Watu walioko madarakani, kwa kawaida hawajihesabii kuwa wapo hapo kuyafanya mapenzi ya Mungu. Wanafuata sera za chama kilichopo madarakani. Katika mataifa ya magharibi na mengi mengine, watu wote wanapofikia umri fulani wanakuwa na haki ya kupiga kura, kwa ajili ya wanasiasa watakaokuwa madarakani katika serikali za mitaa na serikali kuu. Haki ya kupiga kura, kwa sehemu kubwa ni fursa iliyopatikana miaka

ya karibuni, na ilipatikana baada ya jitihada kubwa. Sasa ni nini anachopaswa kufanya mfuasi wa Yesu kunapokuja uchaguzi?

Tunafahamu kutokana na Mungu anachosema kuwa, YEYE ndiye anayeongoza na kudhibiti hatma ya mataifa; tumeona hili katika unabii wa Danieli. Tunajua ya kuwa, kama tunampigia kura mwanasiasa, tunawajibika kwa kile mtu huyo anachofanya. Lakini tunajua pia kuwa, wanasiasa walio wengi wanafuata maamuzi ya viongozi wa vyama vyao, na kwamba, maamuzi yanayofanywa na wanadamu, ni mara chache yanakuwa yakiizingatia Sheria ya Mungu. Sio vizuri kuishi kwa kuwatumainia.

Kwa hiyo hakuna sababu ya sisi kumpigia kura mwanasiasa, au kujihusisha na mambo ya siasa kiserikali za mitaa au kitaifa. Wala hatuwezi pia kujishirikisha katika maandamano yoyote yanayotokea kupinga sera ya serikali. Sheria ya Kristo kwa maneno ya Paulo ni: “Mwe radhi (‘mtosheke’) na vitu mlivyo navyo”, na, “Bwana ndiye anisaidiaye” (Waebrania 13:5,6).

## MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

### Karatasi ya Maswali: namba 13

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa 'Kazi ya ziada', unaweza kulijibu swali kama ukipenda, au kuliacha kama unaona ni gumu mno. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

#### MASOMO: 49 - 52

49. (a) Ni nani aliyekuwa mtume mkubwa zaidi?  
(b) Tunawezaji kutambua kama dhamira iliyopo ndani ya mtu ni kiburi au tamaa?  
(c) Kwa nini Yesu aliwaosha wanafunzi wake miguu yao?  
(d) Wale walio na majukumu mbalimbali kwenye Eklesia wanatambulika kuwa ni 'watumishi'. Fafanua.

Kazi ya ziada

- (e) Tunaweza kujifunza nini kulingana na mfano wa Hamani?

50. (a) Ni kwa namna gani Anania na Safira walikiuka utaratibu?  
(b) Wajibu wa 'nuru ya kweli' ni nini?  
(c) Tulipe kodi?  
(d) Mzee wa Eklesia (kanisa) aweje?

Kazi ya ziada

- (e) Ni nini malipo ya uongo?

51. (a) Hasira ni mbaya?  
(b) Mungu anachukia?  
(c) Mungu anafikirije juu ya kuvunja ahadi na kudanganya kwa makusudi?  
(d) Kama ukisema maneno makali kwa hasira, unasuluhishaje?

Kazi ya ziada

- (e) Yesu aliwatimua waliokuwa wakifanya biashara kwenye hekalu. Je, ilikuwa dhambi?

52. (a) Kama serikali yako ni mbovu, unapaswa kulipa kodi?  
(b) Tufanyeje kama tunatakiwa kujiunga na jeshi?  
(c) Ni sawa kwa Mkristo kujihusisha na siasa?  
(d) Mkristo afanyeje kama akitakiwa awe 'mzee wa mahakama'?

Kazi za ziada

- (e) Kama ukitakiwa kupiga kura kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa CBM, utachaguaje?  
(f) Unafikiri ni sawa kwa wanajumuia wa CBM kupata kura kwa kupiga kampeni?

*Kumbuka kuweka jina lako, anwani na namba yako ya kumbukumbu katika karatasi yako ya majibu.*



## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## KUJAMIIANA: tuzo ya Mungu

## SOMO: Mwanzo 19

Kama unaamini kwamba Mungu alimuumba mwanadamu awe kiumbe aliye bora zaidi kati ya wanyama wengine, utaamini pia kwamba ndiye aliyeubuni mwonekano wa miili yetu ya ajabu; ndiye aliyetupa miguu na mikono na viungio vyake na misuli. Alitupa akili yetu na uwezo wa kufikiri na kupanga kutii au kutotii.

Katika Mwanzo 2:7 tunaambiwa jinsi alivyomuumba mwanamume kutokana na udongo, na katika msitari wa 21 na 22 alivyomuumba mwanamke. Hakuna taarifa popote kwamba Mungu aliwabadilisha kimwili Adamu na Hawa baadaye, alipowafukuza watoke katika bustani ya Edeni kwa sababu ya kutomtii.

Kwa hiyo katika wakati wa kuumbwa, Adamu na Hawa ni lazima waliwekewa uwezo wa kupata watoto. Kwa sababu hiyo, waliwekewa via vinavyotofautiana vya uzazi kwa ajili ya kujamiiana, kufanya suala la watoto liwezekane. Sasa ni nini kingetokea, kama Adamu na mke wake wangekuwa wamejizua wasiangukie katika kulila tunda la mti uliokatazwa?

Kwa hakika hatujui, lakini kuna mambo mawili ya kuisimua ya kutafakari hapa. La kwanza lipo katika Mwanzo 1:28 ambapo amri ya “Zaeni, mkaongezeke”, inakuja kabla laana ya ‘kufa’ haijaja juu yao. La pili lipo katika Mwanzo 2:25 ambapo tunasoma kuwa: “Walikuwa uchi wote wawili, Adamu na mkewe, wala hawakuona haya”. Walikuwa wameumbwa na via vya uzazi na walikusudiwa wapate watoto, lakini hawakuoneana haya kwa kuwa uchi.

Lakini pamoja na kupewa uwezo huo, hawakuutumia mpaka baada ya kufukuzwa kutoka katika bustani hiyo. Ni mpaka tunapofika katika Mwanzo 4:1 ndipo tunaposoma juu ya wao kujamiiana, na Hawa kupata mimba ya mwanawe wa kwanza.

Ningependa nirudi nyuma kidogo na kuangalia kwa undani zaidi juu ya kitendo cha uasi kilichobadili mwelekeo na historia ya mwanadamu, na kuleta shida na maumivu, na mchakato wa kuzeeka, unaoishia kwenye mauti.

Kumbuka kuwa, mti waliokatazwa kuugusa ulikuwa ni, “mti wa ujuzi wa mema na mabaya” na ulikuwa na matunda yaliyoonekana kuvutia kuliwa (Mwanzo 3:6).

Sasa, katika nchi karibu zote duniani, kuna miti yenye matunda ambayo watu wanaweza kuyala bila wasiwasi wowote, lakini ipo pia miti michache ambayo inazaa matunda yenye sumu; matunda yanayoweza kuwaua wale wanaoyachuma na kuyala.

Tunda alilochuma Hawa na kuliwa na wote wawili, mume na mke, lilionekana zuri kwa kuliwa, lakini lilikuwa hasa na sumu ya namna fulani. Lilikuwa na uwezo wa kuibadili miili ya wanadamu na akili zao (Mwanzo 3:7). Adamu na Hawa waliona kila kitu kimebadilika walipolila; walipatwa na hisia tofauti za kuwasitua, na ghafla kuona mambo mengine mengi kwa wakati huo huo.

Hawakuwa na hofu kabla ya kulionja tunda, bali walianza kuogopa baada ya hapo (ms. 10). Utambuzi wao wa jinsi jambo walilofanya lilivyokuwa la hatari na la kutisha, uliwavunja-vunja kimwili na kiakili. Hawakuwa na la kufanya isipokuwa kujificha, kwa kuwa walijitambua wako uchi. Tunaambiwa walijitengenezea vizibao vya majani (Mwanzo 3:7). Walifanya hivyo kwa kuwa walijisikia iliwapasa wafunike via vyao; vilikuwa sasa vimekuwa sehemu zao za siri.

Kilichotokea katika miili yao wakati tunda la ‘mti wa ujuzi wa mema na mabaya’ liliposagwa miilini mwao, kilibadili kimaumbile mfumo wao wa hulka za kiurithi (‘kijenetiki’). Matokeo yake yakawa kwamba, laana

iliyowapata ilikuja pia kwa watoto wao, na juu ya vizazi vyote vya wanadamu. Watu wote wakawa baada ya hapo viumbe ambavyo vinakua na kuzeeka, na hatimaye kufa. Hapo ndipo kila mmoja wetu alipo.

Na sisi tunao pia ujuzi huo wa mema na mabaya na, ingawa mema yanaweza kutuongoza kwenye kufanya mambo ya maana na ya kupendeza sana, ubaya upo pamoja nasi wakati wote. Mitume wa Yesu walilazimika kulionya kanisa jipya la Yesu (waumini) kujichunga sana na huo. Maneno ya mtume Paulo kwa Warumi katika Warumi 3:9-12, ni maneno anayonukulu Zaburi 14:1-3. Paulo anachosema hapa hasa ni kwamba, katika wakati wake huo, hali ilikuwa ni ile ile kama ilivyokuwa katika enzi za Daudi, mfalme wa Israeli, aliyeandika hiyo Zaburi miaka 1000 nyuma. Ni hali inayoendelea.

Tazama pamoja nami sasa katika waraka wa kwanza wa Paulo kwa Wakorintho kifungu cha 6 msitari wa 9 mpaka wa 11. Paulo analosema hapa ni Habari Njema kwa wote wanaojisikia kuwa, uovu katika maisha yao ya awali unamaanisha kuwa hawawezi kusamehewa; hawezi kubatizwa. Hivi kwa hakika sivyo! Toba ya kweli na ubatizo vinayaosha yote ya kale, na kuwapa waumini wote mwanzo mpya kwa kuwa wafuasi wa Yesu.

Yesu ametupa msaada mkubwa katika mada hii ya kujamiiana. Alieleza kuwa, Mungu alikusudia mume na mke waungane kwa maisha yao yote. Alieleza kwamba katika Sheria Mungu aliyowapa watu wake, Israeli, kupitia kwa Musa, uzinzi ulipigwa marufuku (uzinzi ni kumchukua mume au mke wa mwingine).

Uzinzi katika Sheria ya asili, ulikuwa hukumu yake ni kifo, kwa hiyo kwa hao wafuasi wa awali, uaminifu katika ndoa ulikuwa ni kitu kilichoheshimiwa sana. Ili ndoa ivunjike, ilikuwa ni lazima kuwe na sababu nzito sana, na ikitokea ikavunjika, mume na mke hawakuwa huru kuondoka tu na kuo au kuolewa tena. Hakuna hata mahali katika Agano la Kale ambapo mume alikuwa na ruhusa ya wake zaidi ya mmoja, kwa sababu tu ya kuwapenda na kuwa na uwezo wa kuwatumia. Matala ni namna isiyo ya kinidhamu ya matumizi ya fursa ya kujamiiana Mungu aliyokataza.

Hebu turudi nyuma kwenye mafundisho ya Yesu katika Mathayo 5:27,28. Hapa aliirudia kwa uzingativu amri ya kale kuhusu uzinzi, lakini kwa ajili ya wafuasi wake alielezea kwa undani zaidi. Alionesha kuwa, uovu wote hasa unapoanzia ni kwenye fikra. La muhimu kukumbuka juu ya hili ni kwamba, Mungu anayatambua yote tunayofikiri, kama Yesu alivyowashangaza Mafarisayo waliokuwa wakimkosoa wakati wote, kwa kuyajibu mawazo yao, zaidi kuliko maswali waliyouliza.

Kama ukiangalia maneno yake katika Mathayo 5:29,30 utaona yakisemea kitu cha kufanywa, ambacho tungeona vigumu kukielewa cha, "Jicho lako ling'oe/mkono wako ukate". Hata hivyo anachoongelea hasa ni kuyakatilia mbali nasi mawazo mabaya na nia mbaya, na sio kujitia ulemavu. Vinginevyo, kungekuwa na idadi kubwa na wafuasi ambao ni chongo au wenye mikono vigutu, kama maneno ya Yesu yangukuwa ni ya kuchukuliwa tu alivyosema.

Anachokitaka Yesu tufanye, ni kuondoa katika maisha yetu mambo yale yanayotuweka zaidi katika majaribu. Hiki sio kitu kirahisi kufanya, lakini tunategemewa tukifanye kazi.

Kwa kawaida tunao uhuru katika maisha yetu, kama tuna Luninga, kuona kipindi tunachokitaka, kuona gazeti gani tusome, tuwe na ushirika na nani au kuwa rafiki wa nani. Hii ni baadhi tu ya mifano ya maeneo tunayopaswa kuwa waangalifu; unaweza kufikiria mingine. Ni rahisi sana kuvutwa kwenye dhambi kama tunakuwa 'limbuke' wa kila kitu.

Somo kutoka kwa Yesu kwa wafuasi wake na wale wanaofikiri kubatizwa; wanaotaka kumpendeza Mungu, ni kwamba, ni lazima wadhibiti tamaa zao za kufanya mapenzi. Ni lazima wakwepe mazingira ambayo wanajua yanaweza kuwavuta kwenda ovyo. Maneno hayo ya Yesu ya kung'oa jicho na kukata mkono, yamekusudiwa yawe kama kengele inayogonga akilini mwao majaribuni. Inapotokea ukajikuta umejaribiwa vikali, ni muhimu utafute msaada kutoka kwa Mungu kwa haraka kwa kuomba.

Katika maandishi ya Paulo, kuna ushauri mzuri mwingi unaohusu maisha ya kila siku, ingawa barua zake ziliandikwa kwa ajili ya Wakristo karibu miaka 2000 iliyopita. Mfano mzuri sana upo katika Warumi 1:26,27.

Kuna kelele nyingi zinazoendelea kukua, za makundi ya watu wanaofanya mapenzi ya jinsia moja, wanaodai haki yao.

Wakiwa wanaungwa mkono na serikali nyingi na sheria za haki-sawa, wanasema wakati wote kuwa, uhuru wa kufanya hivyo ni haki yao ya kawaida, na wale ambao hawajiingizi katika mambo hayo, ni wenye ukasoro fulani au wamepitwa na wakati.

Wanaposomewa Biblia inachosema, kunakuwa na michomo ya hasira na kukana, na hili ni kwa kuwa mafundisho ya Biblia yanasema wazi wazi kuwa, huo ni uovu (Warumi 1:28-32). Unaweza kuona hata zaidi umuhimu wa msitari wa 32. Kama unavyoona, Paulo anatuonya kuyaepuka mapenzi ya jinsia moja na ngono huria akionesha kuwa, ni kutokumwamini Mungu kunakowafanya watu wafuate namna ya kuishi inayoabudu tamaa.

Katika Walawi 18 kuna Sheria za Mungu kwa watu wake Israeli. Kwenye msitari wa 22 mpaka wa 24 kuna mwongozo unaokataza kukiuka ngono-halali. Mapenzi ya jinsia moja yanaelezwa kuwa ni 'machukizo' kwa Mungu. Kitu cha kukumbuka kutokana ni hili kipo katika msitari wa 24 ambapo tunaambiwa, mataifa yaliyokuwa yakiishi katika nchi ya Kanaani yalikuwa yakifanya machukizo hayo, na Mungu alikuwa amepanga kuyaadhibu vikali kwa hili kwa kuyafuta.

Ni muhimu kwa wote wanaokuwa wafuasi wa Yesu kukumbuka wakati wote kuwa, ngono isiyofuata nidhamu ni uovu mkubwa mbele ya Mungu. Mfano mmoja ambao ni rahisi kuukumbuka upo katika Mwanzo 18:20 na pia Mwanzo 19:-1-29.

Tangu wakati huo mpaka leo, neno Sodoma limekuwa likitumiwa kusemea mapenzi ya mwanamume na mwanamume mwenzake, na miji ya Sodoma na Gomora imetumiwa kuwakumbusha Waisraeli juu ya hukumu ya Mungu ya kutisha, inayowaonya wasifuate mtindo wa kimaisha kama huo unaoikiuka Sheria ya Mungu.

Imekuwa ni muhimu katika somo hili kutafakari matumizi mabaya ya kujamiiana, ambako ni tuzo inayotoka kwa Mungu. Sababu ni kwamba, ngono ni kitu chenye msukumo mkubwa katika maisha yetu, na ni rahisi kutumiwa vibaya. Tutaona katika somo linalofuata, uzuri wake.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## KUCHAGUA MWENZA

## SOMO: 1 Wakorintho 7

Mungu alipokuwa akiwaumba watu, alimuumba kwanza mwanamume. Baada ya hapo alimuumba mwanamke kwa namna aliyoona inafaa, baada ya kuona haikufaa mwanamume awe peke yake (Mwanzo 2:18). Kwa hiyo mpango wa uumbaji ni wa mume na mke kuwa wamoja katika maisha yao yote.

Adamu na Hawa walitakiwa wawe na ushirika katika utukufu wa bustani ya Edeni. Baada ya kumkiuka Mungu, walifukuziwa nje na kuwa na ushirika wa kimapenzi uliowafanya wapate watoto, kwa ajili ya kuendeleza kizazi cha mwanadamu.

Mahusiano yanayojengeka kati ya wazazi na watoto inabidi yabadilike watoto wanapokua, na wanapofikia utu-uzima wanaanza maisha kikwao kwa kuoa na kuolewa (Mwanzo 2:24). Yesu alifundisha kuwa, mahusiano hayo kati ya mwanamume na mwanamke yanapaswa yawe kitu cha kudumu. Ndivyo Mungu alivyotaka iwe tangu mwanzo (Mathayo 19:4-6).

Talaka iliruhusiwa iwepo tu kwa sababu ya udhaifu wa kibinadamu; wa mtu kushindwa kuitii Sheria ya Mungu.

Uhuru wa kutengana na kuoa au kuolewa tena, unatofautiana kati ya nchi na nchi. Katika nchi za magharibi ni mazoea yaliyoingia nyakati hizi, yasiyoruhusiwa kwa wafuasi wa Yesu, na ni pale tu mume anapogundua ya kuwa mke wake amekuwa akifanya mapenzi na wanaume wengine. Hakuna kinachogusiwa kusema kama ruhusa hiyo ya kipekee ilikuwa pia kwa upande mwingine; kama mke aligundua kuwa mumewe alikuwa akifanya mapenzi nje.

Mtume Paulo anayakazia mafundisho haya ya Yesu katika waraka wake wa kwanza kwa Wakorintho, Sura ya 7, msitari wa kwanza na wa pili. Ingawa Paulo hakuo na alipendelea kubakia hivyo, alitambua ya kwamba wafuasi wa Yesu walio wengi wangependa waoe au kuolewa, na ni wachache tu wangeweza kuwa tayari kuufuata mfano wake (1 Wakor. 7:8,9). Anasema wanapokuwa wamekwisha kuoana wasiachane (1 Wakor. 7:10,11). Ni pale mmoja wao anapokufa tu, ndipo aliyebaki anaweza kuoa au kuolewa tena (Warumi 7:1-3).

Dunia ya kisasa inapuuza haya yote na inaruhusu sio kutengana mara moja tu, bali kubadili wapenzi kunakoendelea. Hili ni wazi ni kinyume kabisa cha kusudi la Mungu, na ni kinyume cha mafundisho aliyotoa Yesu kwa wafuasi wake. Wanaume kwa wanawake wasio na imani na wanaoukana uwepo wa Mungu, kwa vyovyote hawaoni haja ya kufuata miongozo inayowabana wasifanye wanavyotaka.

Matokeo ya hili yamekuwa kuvunjika kwa maisha ya kifamilia na kuongezeka kwa matatizo yanayowakumba watoto, wanaokosa upendo wa wazazi wanaopendana. Kwa wanaume na wanawake wanaomwamini Mungu na wanaotamani kuwa wafuasi wa Yesu, kuna haja kubwa sana ya kuwa waangalifu juu ya mada hii ya ndoa.

Ujumbe wa Agano la Kale na Jipya unaosemea hili uko wazi, na unarudiwa-rudiwa mara nyingi. Hata hivyo, Paulo anauhitimisha kwa ajili yetu katika 1 Wakorintho 6:9-10. Hakuna lisiloleweka juu yake:

- Uasherati unakatazwa.
- Uzinzi unakatazwa.
- Mapenzi ya jinsia-moja yanakatazwa.

Haisaidii kitu kulalamikia makatazo hayo yaliyo wazi sana kwa kuwa, hayo ni mapenzi ya Mungu. Kama tunatamani tufufuliwe kutoka kwa wafu (kama tutakuwa tumekufa kabla Yesu hajarudi), na kuwa na sehemu katika Ufalme wa Mungu unaokuja, na kama tunatamani kuufurahia uzima usio na mwisho na maajabu ya kuwa na sehemu katika mpango wa Mungu kwa ajili ya dunia hii, ni lazima tushikamane na sheria zake hizi.

Tunaweza kuyapindisha maneno hayo na kuyageuza yasiseme kile yanachosema, lakini ipo siku tutatakiwa kusimama mbele ya kiti cha hukumu cha Bwana Yesu Kristo. Tusithubutu kuyapuuza maelekezo haya.

Tunapofikia wakati katika maisha yetu wa kutaka kuchagua 'mwenz' wa maisha, inatubidi tuwe macho sana. Msichana mrembo sana au mvulana mtanashati kabisa wanaweza kuonekana wazuri, lakini utahitaji kujiuliza kama watakuwa na ushirika nawe wa imani yako kwa Mungu. Jiulize kama mtaweza kwa pamoja kusaidiana katika njia ya Ukristo, kuufikia Ufalme wa Mungu!

Paulo alitambua kuwa, baadhi ya wanaume na wanawake wangukuwa wafuasi wa Yesu waliobatizwa, wakati 'wenz' wao watakuwa hawataki kubadilika. Ushauri wake kwa watu hao ni wa busara na wa wema sana (1 Wakor. 7:12-16). La muhimu analosema hapa ni kwamba, mume au mke asiyeamini anapaswa aridhike kwamba, mwenz wake amechagua kumfuata Yesu, na asimkwaze katika ibada yake.

Kuna tatizo lingine kwa muumini aliyebatizwa: afanye nini kama hawezi kupata mwenz wa umri wake, ambaye naye ni mfuasi wa Yesu? Kuna majibu ya namna mbili hapa. La kwanza ni kwamba, kuoana ni sehemu muhimu mno ya maisha ya furaha kwa muumini, katika kuweza kuishi kwa imani yake mbeleni, kiasi kwamba, inaweza kumbidi asafiri kwenda sehemu nyingine ya nchi, au hata nchi nyingine kumpata mwenz.

Hili kwa kiasi kikubwa ni rahisi zaidi kwa mwanamume kuliko kwa mwanamke, lakini kuna mifano ya kusisimua katika Biblia ambapo hili lilitokea nyakati za kale (Mwanzo 24 na Ruthu 1 na 2).

Katika Ruthu, Sura ya kwanza, tunamwona Ruthu akionesha tu nia yake ya dhati ya kuendelea kuwa na mama-mkwe wake, Naomi, lakini, tunapofikia Sura ya pili, ni wazi Naomi amemwongelea Ruthu juu ya ndugu yao katika ukoo (Boazi), aliyekuwa tajiri katika Bethlehemu, ambaye pengine angevutiwa kuiheshimu sheria yao ya mirathi na kumwoa mke wa ndugu yake aliyekufa.

La pili linalowezezana ni kutafuta mwenz ambaye ni msomaji wa Biblia, anayependa kuwa mfuasi ya Bwana Yesu Kristo. Kwa kusoma Biblia pamoja, inawezezana, sio tu kumpata mwenz wa kuoana naye, bali pia kupata furaha ya kumleta mtu mwingine katika ufahamu wa Ufalme wa Mungu unaokuja duniani. Hili kwa vyovyote ni mwendelezo wa kazi ya kueneza ujumbe wa Injili, ambao wafuasi wote wa Yesu wameamriwa kuifanya (Marko 16:15,16).

Kwa hiyo, ipo sababu nzuri sana ya kumpata mwenz na kufaa wa kuoana naye. Hata muumini ambaye amefiwa na mume au mke, ni muhimu sana kujali hivyo vigezo kabla ya kufikiri kuo au kuolewa tena (1 Wakor. 7:39).

Mada hii ya ndoa ilithaminiwa sana na mitume kiasi kwamba, Paulo alipokuwa akiandika waraka wake wa pili kwenda Korintho, aliirudia hiyo amri tena (2 Wakorintho 6:14-16).

Kuwafungia nira wanyama wawili wasio sawa kimwili au kihulka ili walime pamoja shambani au wakokote mzigo, ni kwa hatari, na kunaweza kuwa na matokeo mabaya sana. Ile nira, kwa kuwa haiwezi kukaa vizuri, itasugua ngozi na kuwatia wanyama hao vidonda (hasa mmoja). Wanyama hao watajikuta wakivutana na hata kuangushana, badala ya kuvuta jembe au mkokoteni pamoja.

Kwa hakika, hii ni namna iliyo sahihi kabisa ya kuelezea ndoa yenye migogoro, lakini inakuwa ni hivyo hivyo kwa mahusiano mabaya ya kikazi au kibiashara. Kwa hiyo Paulo anatuonya ili haya yasitokee.

Kwa upande mwingine kunakuwa na furaha kubwa katika kuwa na imani moja kati ya mume na mke, katika kusoma Biblia pamoja, na kama kuna watoto kuwafundisha kuziheshimu Sheria za Mungu na kumfuata Yesu.

Katika waraka wake kwa Waefeso, Paulo anafananisha uhusiano kati ya mume na mke na ule uliopo kati ya Yesu Kristo na kanisa lake. Dhabihu ya damu yake aliyokuwa tayari kuitoa kwa ajili ya wafuasi wake, ili waweze kuokolewa kutokana na mauti ya milele, inaonesha upendo unaopaswa kuwepo kati ya mume na

mke. Mfano huu wa nira, sio kielelezo alichokibuni tu Paulo, kwa maana Yesu alitumia mara nyingi mifano katika kuhubiri kwake Injili.

Mfano mzuri katika kuhitimisha upo katika Injili ya Mathayo, Sura ya 25:1-13. Hapa Yesu anaongelea kurudi kwake duniani anakokufananisha na 'ujio wa bwana-harusi', kitu kinachotufundisha kuwa macho wakati tukimsubiri. Pamoja na hilo, anatutaka tuwe makini juu ya kile tunachokuwa tukifanya wakati anapofika. Kwa wafuasi walio na wenza, hakuna namna iliyo bora zaidi, zaidi ya kusaidiana katika umoja wa kiimani na tumaini, katika kujiweka tayari kwa ajili ya siku hiyo njema ya ajabu.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## VIPENGERE KADHAA KUHUSU HUKUMU NA UFALME

**SOMO:** 1 Wakorintho 15

Mojawapo ya njia zilizotumiwa huko nyuma kuwashawishi watu wajiunge na Ukristo, ilikuwa kuwatisha juu ya Kiti cha Hukumu cha Kristo. Kusudi la masomo haya ni kukuelezea faida na haja ya wewe kubatizwa katika Jina la Yesu. Kwa hiyo ni muhimu tuangalie mada hii ya hukumu, kwa kuipitia mistari inayosemea jambo hili katika Biblia.

Mada ya hukumu ni mada inayotisha, lakini ni vizuri itazamwe kwa pamoja na ahadi alizotoa Mungu, za msamaha na rehema yake kwa wale wanaomtafuta.

Kwa kuwa tutakuwa tukiangalia jambo hili linalokuja, rejea zilizo nyingi tutazichukua kutoka kwenye unabii. Unaweza ukazitegemea zitoke kwenye Agano la Kale, lakini nyingi zipo pia kwenye maneno ya Yesu na mitume wake, na zingine katika kitabu cha Ufunuo.

Kwa yeyote ambaye, kwa bahati mbaya, ametakiwa kukabiliana na mashtaka katika mahakama ya kisheria, mara nyingi atataka kujua hakimu atakayeendesha kesi yake ni nani. Sababu ni kuwa, hata kama hakimu amesoma kiasi gani na ana uzoefu kiasi gani, ni binadamu, na hivyo anakuwa na mtizamo pia ambao ni wa kwake kibinafsi, juu ya kile kilicho haki au kosa mbele ya sheria.

Tunapotaka kuangalia mada hii ya hukumu kama ilivyo katika Biblia, tutataka nasi kufahamu kitu juu ya hakimu wetu. Hebu ifungue Biblia yako kwenye Zaburi ya 72. Hapo tunaambiwa: “Atawaamua watu wako kwa haki, na watu wako walioonewa kwa hukumu...Siku zake yeye mtu mwenye haki atasitawi, na wingi wa amani hata mwezi utakapokoma” (ms. 2-7).

Kumbuka ya kwamba haya ni maneno ya Mungu, yanayoongelea ‘haki’ iliyo ya kweli kama ilivyokusudiwa na Mungu, kwa ajili ya wanadamu, tangu mwanzo kwenye bustani ya Edeni. Maelezo mengine kumhusu huyu ‘mwamuzi wa kweli’ yapo kwenye unabii wa Isaya, Sura ya 11, ambapo utangulizi wake ni: “Basi litatoka chipukizi katika shina la Yese”. Maelezo kuhusu ‘tawi’ yanapolinganishwa na rejea kama hiyo yanaonesha kuwa, chipukizi hilo ni Bwana Yesu, Mwana wa Mungu.

Paulo aliondoa mashaka yoyote juu ya hili alipowaandikia, kwa uweza wa Roho ya Mungu, Warumi, na kuonesha wazi kuwa, ni Yesu atakayekuwa Mfalme wa dunia yote atakaporudi (War. 14:7-13). Katika maneno yake ya kumaliza kwa Timotheo, Paulo aliongelea juu ya tumaini lake kibinafsi na imani aliyokuwa nayo juu ya huyu mwamuzi wa kipekee sana (2 Tim. 4:6-8).

Gundua hapa ya kuwa hakuwa na hofu, badala yake ilikuwa kutamani tu kwamba hiyo siku ingekuja mapema. Hili linaweza kuwa hivyo hata kwetu kama tunayaishi maisha yetu kwa kuzingatia miongozo ya Yesu na kufuata mfano wake.

Petro alipokuwa akimfafanulia Injili akida wa Kirumi, Kornelio, alionesha pia kuwa, Yesu ndiye atakayehukumu (Matendo 10:38-43). Kuna taarifa zaidi hapa juu ya hukumu hiyo, kwa kuwa Petro anasema kuwa, Yesu, “Ndiye aliyeamriwa na Mungu awe Mhukumu wa walio hai na wafu” (ms. 42).

Yakobo katika waraka wake, Sura ya 5 msitari wa 8 na wa 9 anaandika akiwa na tumaini kuwa, kurudi kwa Yesu kungekuwa wakati wa uhai wake. Haikuwa hivyo, lakini, kwa kuwa maisha yetu ni mafupi sana, na wakati wa kufa inakuwa, utambuzi unaofuata ni wakati wa kufufuliwa kwetu, hatuwi mbali na siku hiyo ya hukumu; hata kama mamia ya miaka yamepita.

Mengi zaidi juu ya hili yapo katika Kitabu cha Ufunuo, na tutaangalia kwanza Ufunuo 11:18. Hebu yaangalie maneno hayo kwa makini na utaona kuwa, kusudi la Mungu kwanza ni kuwazawadia wale waliomtumikia, na

kuonesha imani kwake na kupenda kulitukuza Jina lake. Adhabu kwa wale wanaomkataa Yesu ni kitu ambacho sitaki kukijadili katika somo hili.

Tunapofungua mbele kwenye Ufunuo 20:11-13 tunaona kinachosemwa kinavyovutia. Ni lazima kivutie, na hasa tukilinganisha na mambo madogo madogo yanayoyazuga maisha yetu, na ujanja-ujanja wote wa mwanadamu katika yote anayofanya. Mwanadamu aliumbwa katika uso wa dunia ili amche Muumba wake; ampe Mungu utukufu kwa kuiakisi hulka ya Mungu, kwa kuwa alimuumbwa kwa mfano wake.

Mungu atawafanyaje upya waliokufa katika kuwafufua? Jibu ni 'hatukuoneshwa!' Lakini, kwake yeye mwenye hekima, uweza na maarifa makuu, aliyeviumba vitu vyote, itakuwa hakika ni kitu kirahisi kutufanya upya. Ni muhimu pia kuyaona maneno yaliyopo kwenye msitari wa 12: "Hao wafu wakahukumiwa katika mambo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao" (Ufun. 20:12).

Uthibitisho huu wa mambo tuliyojifunza katika masomo ya awali ni wa maana sana. Uhusiano uliopo kati ya kuwa na imani kwa Mungu na kuiweka imani yetu katika matendo katika maisha yetu, ni kitu anachokichunguza Yesu kila siku, akiwa ni Mpatanishi wetu na Mwamuzi ajaye. Hakuna kinachompita pembeni.

Nataka sasa kuiacha picha hii ya hukumu, tuweze kuangalia tena Ufalme wa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Tumekwisha soma undani wa Ufalme unaokuja, utakaokuja na Mhukumu wa Haki ambaye atakuwa Mfalme Mkuu sana. Wakati wa mwanzo wa enzi yake utakuwa, kwa vyovyote umejaa umwagikaji wa damu, na kipigo kwa mataifa ya dunia yatakayokuwa yakimpinga na kutaka kumwangamiza.

Lugha za manabii sio rahisi kuzielewa sana na kuna mifano mingi ya kuchagua, lakini angalia kwanza Isaya 24:21-23 ambapo tunaoneshwa picha ya adhabu. Sasa twende kwenye Zekaria 14. Isome Sura yote. Vita na uharibifu unaosemewa ni vitu visivyokwepeka, lakini ni lazima tutegemee hili kutokea kwa kuwa, ujio wa Yesu utakuwa ni ujio kwa dunia iliyojaa uovu.

Kitu kinachosisimua katika unabii huu ni jinsi Yerusalemu inavyosemewa mara kwa mara na Wayahudi. Hili kwa hakika lina jambo la muhimu katika kusudi la Mungu, na migogoro ya mara kwa mara katika Taifa la Israeli ipo kuashiria jinsi kurudi kwa Yesu kulivyo karibu. Kuna picha ya mibaraka Mungu aliyoihidi kwa wale wote watakaokubaliwa katika Ufalme wake katika Isaya 25:8 na 9, inayosemewa pia kwa kuelekezwa kwa watu wake.

Wafuasi wa Yesu ni wale wanaosemewa katika Ufunuo 20, kama watu walioandikwa katika 'kitabu cha uzima'. Ni watu maalumu na ni pamoja na Wayahudi kati ya mataifa yote, waliokusanywa katika nchi yao wenyewe na kubarikiwa na Mungu. Ni picha nzuri sana ya Mungu akiwa anawafuta machozi watu wake katika Ufalme huo unaokuja. Picha hiyo imerudiwa tena kwenye Ufunuo 21:3-5.

Mibaraka ya wakati wa Ufalme ni mingi, na imetajwa katika sehemu nyingi za Biblia kama tulivyokwishaona. Kwa sehemu kubwa undani wa haya upo katika maeneo ya unabii yanayosemea vita na uharibifu, adhabu itakayokuja juu ya wale wanaoitwa maadui wa Mungu na maadui wa watu wake, Wayahudi. Mfano wa hili upo katika Isaya 35 ambapo manufaa watakayoyapata watu wa kawaida (wanaokufa) wakati wa Ufalme yameoneshwa.

Kwa hiyo kutakuwa kuna watu wa kawaida (wanaokufa) katika kipindi cha Ufalme wa Yesu, na watakuwapo wale ambao wamepewa uzima wa milele, wasioweza kufa. Katika Isaya 35: 5 wanaongelewa vipofu na viziwi, na katika msitari wa 6 vilema na walio bubu. Huu ni ulemavu unaohusiana na baadhi ya watu wa kawaida na sio watakatifu wa Mungu wasiokufa. Urefu wa muda Ufalme utakaochukua umeoneshwa kuwa ni miaka 1000 katika Ufunuo 20:4-6.

Yanayosemewa mengine juu ya ibilisi na shetani katika msitari wa 2 na 'wafu waliosalia' katika msitari wa 5 yatakuwa katika somo la mbeleni; hatutayasemea hapa.



Habari zinazohusu Ufalme zimeenea katika Biblia yote, na utakuwa kwa sasa umepata mawazo ya jinsi utakavyokuwa. Paulo, katika waraka wake wa kwanza kwa Wakorintho, Sura ya 15, anatoa taarifa ya mchakato wa ufufuo, lakini pia analo la kusema kuhusiana na kazi ya Yesu, akiwa sasa ni Mfalme wa dunia. Ni vizuri kuisoma Sura hiyo chochote, lakini kwa sasa tuangalie msitari wa 20 mpaka wa 28.

Hapa tunaona ya kuwa, Ufalme wa Mungu ni wakati wa maandalizi ambayo dunia yote na watu wake, wakiongozwa na wale ambao wamekwisha pata uzima usio na mwisho, itaifikia hali ya amani, utulivu na ufanisi. Ndipo Yesu, Mfalme Mkuu, atakapoikabidhi dunia kwa Baba yake, Mungu, tayari kwa kipindi kinachofuata katika mpango wake, akiwa ni 'Yote katika Wote'.

Hatujui mpango huo ukoje na hakuna taarifa inayotolewa zaidi ya kwamba, kutakuwa na ufufuo mwingine (wa pili) kabla ya hapo na hukumu nyingine, na mauti kutokomezwa katika dunia. Hili lina maana kuwa, watu watakuwa hawafi tena kwa maana, adui wa mwisho atakayekuwa amebatilishwa ni mauti (1 Wakor. 15:26).

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

### ZAWADI YA HALI YA JUU YA TUMAINI KATIKA MAISHA YAKO

#### **SOMO:** Maombolezo 3

Tumaini ni mojawapo ya zawadi za maana sana zinazotoka kwa Mungu. Kwa upendo wake kwetu, alijua ni kwa kiasi gani mwanadamu angehitaji hili, na kwa namna alivyoshughulikia uanadamu wetu, ametuwezesha kuwa nalo hata katika mazingira yaliyo mabaya sana. Hebu funua Biblia yako usome waraka wa pili wa mtume Paulo kwa Wathesalonike, Sura ya pili, msitari wa kumi na sita na kumi na saba.

Kutoka kwenye kurasa za mwanzo kabisa za Biblia, tunaweza kuyafuatia maisha ya watu waliosukumwa na tumaini, katika kufanya mambo kadhaa katika maisha yao. Kuna mahusiano makubwa yaliyopo kati ya tumaini na imani, na tutaingalia imani katika somo la 57.

Katika Waebrania, Sura ya 11, msitari wa kwanza, tunasoma ya kuwa, imani ni uhakika wa mambo yatarajiwayo. Tunapokuwa tuna tumaini, tunaweka akilini mwetu picha za mambo ambayo tungependa yatokee, mambo ambayo tungependa kuyafanya, na kwa kuwa tu-wanadamu, vitu ambavyo tungependa kuvipata.

Tumaini ni mojawapo kati ya mambo matatu ambayo Paulo aliyaona kuwa ya msingi, katika hulka ya mfuasi wa kweli wa Kristo, anayosema ni: imani, tumaini, na upendo (1 Wakor.13:13). Kwa hiyo hebu twende sasa na kuwaangalia baadhi ya watu katika Biblia, waliokuwa na tumaini, na wachache waliokosa.

Tutaanza na Yesu kwa kuyatazama maneno ya Petro, aliyekuwa mmoja kati ya wafuasi wake wa mwanzo. Yapo katika Matendo 2:26. Petro alikuwa akimuongelea Yesu, lakini akitumia maneno ya mfalme Daudi yaliyopo katika Zaburi ya 16 msitari wa 9. Kama unaweza kujiweka katika nafasi ya Yesu alipojiachia mwenyewe akamatwe, na kuteswa, na kuuawa msalabani, utaweza kutambua jinsi unabii huo uliofanywa na Daudi katika Zaburi hii, ulivyokuwa wa muhimu kwa Yesu.

Sasa tutaangalia maneno kadhaa ya nabii Yereimia, aliyeteseka sana kwa sababu ya kusema bila kuogopa ujumbe uliotoka kwa Mungu, kwa watu katika Yerusalemu. Aliwaambia watu na mfalme wao kuwa, ili waishi iliwabidi wajisalimisha kwa jeshi la Babeli. Walimchukulia Yereimia kama msaliti, na kumtumbukiza katika handaki refu jijini hapo (Yereimia 38:6). Katika Maombolezo 3:1-6 Yereimia anaongelea hofu aliyokuwa nayo na hali yake ilivyokuwa mbaya sana.

Somo la maana sana kwetu ni kwamba, katika dhiki yake na hatari iliyomkabili, Yereimia aliweza kuyaona mambo kwa namna iliyokuwa nzuri zaidi (ms. 18). Tunaweza na sisi kujisikia hivyo wakati wa hali ngumu katika maisha yetu, lakini endelea kusoma sasa msitari wa 19 mpaka wa 21. Katika dhiki yake, Yereimia ghafla anakumbuka kuwa bado yupo hai, na maneno yake matamu ya sisi kukumbuka, yanafuatia:

“BWANA ndiye fungu langu, husema nafsi yangu, kwa hiyo nitamtumaini yeye. BWANA ni mwema kwa hao wamngojeao, kwa hiyo nafsi imtafutayo. Ni vema mtu autarajie wokovu wa BWANA, na kumngojea kwa utulivu” (Maombolezo 3:24-26).

Kwa hiyo, tumaini ni kitu kinachotaka kuwa na subira; tunahitaji kuwa watulivu tunapoungojea wokovu unaotoka kwa Mungu.

Mengi yameandikwa kuhusu kurudi kwa Yesu duniani, akiwa ni Mfalme. Tungependa hili liwe leo; kuna matatizo mengi mno katika dunia hii yanayohitaji ufumbuzi. Watu wanaonekana hawawezi kuyatatua hata wafanyeje. Ni hapa ndipo maneno ya Yereimia yanapokuwa ya muhimu kwetu kukumbuka. Tuna wajibu wa kuungojea kwa utulivu wakati ambao Mungu ameuweka.

Sasa hebu tu tafakari mfano wa Abram, aliyehama mji na kuacha kila kitu, kufuata maono aliyopewa juu ya wakati wa mbeleni. Mungu alipokuwa amemuahidi mambo ambayo yalikuwa mbali sana mbeleni, ilikuwa wazi kwa Abram kuwa, angehitaji mwana wa kuendelea baada yake, na hata mjukuu na kitukuu pia! Hebu angalia uone ni kwa muda gani ilimbidi Abram angojee kabla ya Isaka kuzaliwa. Abram alikuwa na miaka 75 alipoondoka Harani, na miaka 100 Isaka alipozaliwa; ni miaka 25. Ni muda mrefu kusubiri kwa imani!

Ni vibaya kiasi gani kuishi bila tumaini! Kwa kipindi kifupi Ayubu alikuwa hivi (Ayubu 7:3-7). Kama ukisoma juu ya mabaya yote yaliyompata yeye na familia yake, ni rahisi kuelewa ni kwa nini alijisikia hivyo. Hata hivyo, baada ya kupima namna ya kufikiri ya kibinadamu ya marafiki zake, namna yake ya kuyaona maisha iliboreka. Katika Ayubu 19, pamoja na hali yake kuwa mbaya sana, ghafla anabadilika katika maombolezo yake, na kusemea mambo ambayo nasi tunayaamini hata leo kuhusiana na mada ya kifo na ufufuo.

Ni sawa tushangae jinsi ilivyomjema picha nzuri ya ajabu, na tumaini zito ambalo lilikuwa liwe muhimili wa hulka ya mtu huyu wa imani sana. Anasema, anajua ya kuwa mtetezi wake yu hai na kwamba, hatimaye atasimama katika nchi na kumhesabia haki (Ayubu 19:25-27). Haya ni maneno matamu sana ya kuyageukia, tunapokuwa kwenye taabu na maisha yenyewe yanapokuwa hayaeleweki.

Kwa hiyo, tumaini ni kitu cha maana sana cha kuwa nacho; tumaini juu ya kutimia kwa Ahadi za Mungu kwa dunia hii, kwa namna ambayo maisha ya watu wote yataboreka sana. Lakini kuna namna nyingine ya ajabu zaidi ya vile tunavyoweza kulielewa hili neno 'tumaini'.

Mitume wa Yesu walilitumia neno 'tumaini' kwa namna iliyoelezea mambo yote waliyoamini, kumhusu Yesu na Ufalme wake unaokuja. Maneno waliyotumia ni: "Kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu" (Tito 3:7), "tumaini la wokovu" (1 Wathes. 5:8) na, "tumaini la utukufu" (Wakolosai 1:27).

Paulo aliandika hata kwa Warumi katika Warumi 4:18 kuwa, tunaokolewa kwa njia ya 'tumaini'. Katika 1 Wakorintho 15:19 anatumia wote tutulie na kufikiri. Kama katika maisha haya matumaini yetu ndipo yalipo tu, anasema, basi sisi ni watu wa kusikitisha sana. Kutegemea kuwa wanasiasa, wanadiplomasia, majeshi, mashirika ya misaada ya kimataifa n.k wataibadili dunia iwe mahali bora zaidi pa watu wote kuishi, ni kitu ambacho hakitakaa kitokee.

Paulo anasema kuwa, ni tofauti sana na kuwa na tumaini kwa Yesu maana, Yesu alifufuka kutoka kwa wafu, yupo hai na atarudi duniani. Atakaporudi, atausimamisha Ufalme wa Mungu, na wafuasi wake wote wa enzi zote katika historia yote, watafufuliwa kutoka maadini, na kama waliishika imani, watapeleka uhai utakaoendelea daima katika dunia iliyoboreshwa sana, yenye amani.

Bwana Yesu Kristo atakuwa Mfalme juu ya mataifa yote, na atatawala kwa mamlaka inayotoka kwa Mungu, kwa haki na hekima na upendo.

Kubatizwa katika Jina la Yesu kunaifungua njia ya mambo haya mazuri sana, na mtume Petro anaandika katika waraka wake wa kwanza, kuwa:

"Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili, tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu" (1 Petro 1:3).

Kubatizwa ni kuzaliwa upya ili kuwa mfuasi wa Yesu. Hili kwetu leo ni tumaini lililo hai, na moja ambalo tunaweza kujisikia vizuri sana kuwashirikisha wengine.

## MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

Karatasi ya Maswali: namba 14

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa 'Kazi ya ziada', unaweza kulijibu swali kama unapenda, au kuliacha kama unaona ni magumu mno. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

### MASOMO: 53 – 56

53. (a) Mti wa ujuzi wa mema na mabaya ulikuwa na sumu?  
(b) Ni sawa kuwa na wake zaidi ya mmoja?  
(c) Mungu anafikirije kuhusiana na mapenzi ya jinsia moja?  
(d) Mungu ana maoni gani kuhusiana na picha za ngono?

Kazi ya ziada

- (e) Ungemshaurije mtu mwenye wake wawili kuhusiana na ubatizo?

54. (a) Kufanya mapenzi kabla ya ndoa ni sawa machoni pa Mungu?  
(b) Kama 'mwenz' wako anakufa, ni sawa kuoa/ kuolewa tena?  
(c) Mungu anatazamaje talaka.  
(d) Kuna ulinganisho gani kati ya mume na mke, na Bwana Yesu Kristo na Eklesia?

Kazi ya ziada

- (e) Mungu anatazamaje kutooa/ kutoolewa?

55. (a) Tuiogope hukumu ya Kristo?  
(b) Tutakuwa watu tusiokufa mbele ya Kiti cha Hukumu cha Kristo?  
(c) Utawala wa Yesu utachukua muda gani?  
(d) Adui wa mwisho ni nani?

Kazi ya ziada

- (e) Mpangilio wa matukio utakuwaje wakati wa kurudi kwa Kristo duniani?

56. (a) Elezea uhusiano uliopo kati ya tumaini na imani.  
(b) Yesu aliwezaje kuvumilia kifo cha kuwambwa msalabani?  
(c) Ni kitabu gani katika Biblia kinachoongelea tumaini alilokuwa nalo Yeremia?  
(d) Ni nini kilichomsukuma Ibrahimu aondoke Uru, na aliacha nini nyuma?

Kazi ya ziada

- (e) Tumaini ni nini?

*Kumbuka kuweka jina lako, anwani na namba yako ya kumbukumbu katika karatasi yako ya majibu.*

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## IMANI NA KUUFANYIA UKRISTO KAZI

**SOMO:** Waebrania 11

Mara nyingi katika masomo yetu haya, tumetumia neno 'Imani'. Sasa ni wakati wa kutazama na kuona ni nini waandishi katika Biblia wanachotutaka tuelewe juu ya neno hili. Ni neno linaloweza kutumika katika lugha yetu ya kawaida kwa namna mbalimbali.

Mfumo wowote wa kiibada unaweza kuitwa 'Imani'. Kama tunalazimika kuvuka kikorongo au kijito kwa kupita juu ya kigogo, tutahitaji kuwa na imani kuwa kidaraja hicho kina uwezo wa kuuhimili uzito wetu na kimewekwa vizuri; vinginevyo hatutathubutu.

Paulo katika waraka wake kwa Waebrania, Sura ya 11, anatupa maelezo juu ya imani. Anasema, imani ni kuwa na uhakika wa kitu tunachokitarajia, tusichokiona. Ni hili lililowafanya watu waaminifu wa kale wasifiwe.

Unajua kutokana na masomo haya mengi uliyopitia kuwa, katika Agano la Kale Mungu alionekana kuwa karibu sana na Ibrahimu na familia yake, kuja mpaka wakati wa manabii. Watu waliokuwa wakiishi enzi hizo, hawakuwa mbali na mojawapo ya matukio makubwa ya kutisha. Pengine ilikuwa ni rahisi zaidi kwao kuwa na imani kwa Mungu na kwa ahadi zake. Mungu aliwatarajia watu hao wawe na imani na alipendezwa nao na kuwazawadia walipokuwa nayo.

Katika wakati wa Yesu, ni miujiza iliyowafanya watu katika nchi ya Israeli waamini kuwa, Yesu alikuwa Mwana wa Mungu na Masihi wao walioahidiwa (angalia Yohana 11:44, 45, kwa mfano).

Leo hatuna miujiza ya waziwazi kama maji ya Bahari ya Shamu kutengana, yaliyowaachia wana wa Israeli walitoroke jeshi la Kimisri (Kutoka 14 na hasa msitari wa 13). Hatuna manabii wa Mungu wanaozunguka katika nchi zetu, na hatuna uwezo wa kusimama na kuiona miujiza iliyofanywa na Yesu.

Ulichochacho ni Biblia yako ambamo matukio haya yote, na ahadi na maonyo yameandikwa humo kwa uwezo wa Mungu, kwa ajili yetu wote kusoma. Ni ili tuwe na kumbukumbu ya wakati wote ya kusudi la Mungu kwa dunia hii, na 'ofa' anayoitoa kwako kibinafsi, ya wewe kuwa na sehemu katika mambo yanayokuja.

Kwa hiyo, imani kwa leo ni ridhaa ya moyoni utakayokuwa nayo moyoni na akilini mwako. Utakuwa nayo kutokana na mambo unayoyasoma kwenye Biblia yako au kufundishwa na wengine, ambao nao wana imani na Neno la Mungu.

Ninalotaka kufanya sasa ni kukuonesha kuwa, Mungu anatutaka tuweke imani yetu katika matendo. Mtume Yakobo katika waraka wake analielezea hili (Yak. 2:14-18). Kuna uhusiano mkubwa unaopaswa kuwepo, kati ya imani na matendo. Mungu anatutazama na kuyapima matendo yetu; kwa hiyo kile tunachofanya kwa sababu ya kuwa na imani, ni cha muhimu sana kwake.

Mungu anajua tunahitaji msaada kuweza kufanya hili, na ametupa katika Neno lake mifano mingi jinsi imani inavyoweza kuwa matendo.

Kuna mifano miwili katika Sura tuliyoisoma katika waraka kwa Yakobo. Ilikuwa ni Sura ya pili, na sasa tuangalie msitari wa 21 mpaka wa 24. Kama ukirudi nyuma kwenye Mwanzo 22: 1-18 unaweza kuyapata maelezo yote hapo. Ili kuweza kutambua sawasawa imani ya Ibrahimu ilivyokuwa, ni vizuri ukumbuke kuwa, Mungu alikuwa amempa Ibrahimu ahadi ya muhimu sana alipomtoa katika mji wa Uru katika Ukaldayo (Mwanzo 12:1-3).

Ahadi hiyo kutimia, ilitegemea Ibrahimu kupata mtoto wa kiume, na familia yake kukua na kuwa taifa kubwa. Tunajua, hatimaye Ibrahimu aliweza kumpata mtoto huyo, Isaka, wakati yeye na mke wake wakiwa wazee waliopitiliza muda. Hili linatusaidia kuelewa jinsi Ibrahimu alivyokuwa na imani kubwa kwa jinsi alivyoiamini ahadi hiyo ya Mungu, na vile alivyojaribiwa alipotakiwa amtoe Isaka kuwa sadaka.

Paulo anatuambia kile Ibrahimu alichokuwa akiwaza, wakati alipokuwa akipanda na Isaka kwenda mlimani Moria (Waebrania 11:17-19). Isaka alikuwa kijana wa muhimu sana katika ahadi Mungu aliyokuwa ameitoa; bila ya Isaka hakuna ambao lingeweza kutimia. Mungu alipomtaka Ibrahimu amtoe Isaka afe, Ibrahimu aliamini Mungu angeweza kumrudishia tena uhai.

Kwa vyovyote hili lilihitaji kuwa na imani sana. Lingine la muhimu sana kuhusiana na tukio hili ni kwamba, Mungu hakulifanya hili ili kumpima Ibrahimu tu. Alikuwa tayari akijua imani ya Ibrahimu ilivyokuwa, na unaweza kuliona hili katika Mwanzo 15:3-6. Amri yake kwa Ibrahimu kwamba amtoe Isaka, ilikuwa ni kumfundisha Ibrahimu jinsi yeye Mungu alivyokuwa akikusudia kuleta wokovu kwa wanadamu, kwa njia ya dhabihu ya Mwanawe.

Tendo hili lilimfundisha Ibrahimu kuwa, siku moja mbeleni, yeye Mungu, akiwa ni Baba, angemwachia Mwanawe Yesu awe sadaka kwa ajili ya dhambi za dunia; awezeshe msamaha kwa ajili ya dhambi kupatikana, ufufuo na uzima wa milele kwa watu wenye imani kwa Mungu, na kwa Mwana wake, Yesu Kristo.

Mfano mwingine uliotolewa na Yakobo ni wa Rahabu. Huyu alikuwa, kwa kumwona haraka, mtu asiyefaa. Hakuwa Myahudi na inasemwa alikuwa kahaba, akikaa katika mji wa Kikanaani wa Yeriko. Alikuwa ni mtu pekee hapo aliyekana kuwa na imani juu ya Mungu wa Wayahudi.

Kwa namna fulani alikuwa amefahamu kuwa, umati mkubwa wa watu waliokuwa wamepiga kambi upande wa pili wa mto Yordani, wangukuja na kuidai nchi yao ya zamani, nchi Mungu aliyokuwa amempa Ibrahimu (Yoshua 2).

Kuta za mji huo zilipoanguka kwa muujiza, ni Rahabu tu na familia yake waliookolewa kwa kuwa, Rahabu alikuwa amejihatarishia maisha yake kwa kuwahifadhi wapelelezi wa Kiisraeli. Tukio hili kwa vyovyote lilikuwa la kipekee sana, kiasi kwamba Yakobo na Paulo walimtumia Rahabu kama kielelezo cha mtu wa imani.

Waebrania 11 imejaa mifano ya imani kwa matendo, na ninataka sasa kuutazama mmoja tu zaidi. Nuhu aliishi katika nyakati ambapo kulikuwa na uovu mwingi sana kati ya watu, wakati wa enzi ya ustaarabu wa kale (Mwanzo 6, 7 na 8 na hasa Mwanzo 6:5-7). Tunaoneshwa miaka ilivyopita, Nuhu alikuwa akijenga meli kubwa, kwa kuona kinachosemwa kwenye Mwanzo 5:32 na Mwanzo 7:6. Kwa hiyo alichukua miaka 100 kujenga hiyo Safina; ambao ni muda mrefu sana kwetu. Kwake yeye haukuwa, kwa kuwa aliishi miaka 950.

Kuna mashaka kama kuna mtu aliyewahi kujenga mashua kubwa kama hiyo nyuma. Kwa miaka hiyo yote Nuhu alilazimika kujifunza kutengeneza misumeno, kukata miti, kupasua mbao na kuzisawazisha zinyoke ziweze kufaa kiviipimo, zikipigiliwa maji yasiyenye.

Safina hiyo ilipaswa iwe kubwa sana, iwe mahali pa usalama kwa wanadamu na wanyama, ndege na wadudu, kwa zaidi ya mwaka mmoja. Kwa jitihada yote hii na kwa miaka yote hiyo ya kujenga, kilichomsukuma Nuhu kufanya yote ilikuwa ni imani yake kwa Mungu. Paulo anahitimisha mfano huu wa hali ya juu wa Nuhu katika Waebrania 11:7 akisema, "Aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake....akawa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani".

Tulicho jifunza ni nini mpaka hapo? Tumejifunza:

- Kwamba imani ni kuwa na uhakika kuwa Mungu yupo, na kwamba kwa wakati wake atatimiza kile alichohidi.
- Kwamba haitoshi kusema kuwa tunaamini; Mungu atakuwa akijua wakati wote kama ni kweli.

- Kwamba imani peke yake haitoshi, tunahitaji kuifanyia kazi katika maisha yetu.
- Kwamba Mungu anatumarajia mara nyingine tuendelee na kitendo cha kiimani tunachokifanya kwa muda mrefu.

Kama unafikiria kuamua kubatizwa au kama umeshampokea Yesu kwa njia ya Ubatizo, utahitaji kujua kama hili lina maana gani kwa maisha yako ya siku kwa siku. Unaiwekaje imani yako katika matendo? Yafuatayo ni mapendekezo kadhaa kutoka kwa Paulo, katika waraka wake kwa Warumi, kwenye Warumi 12:9-18.

Yasome kwa umakini na utafakari jinsi yanavyoweza kuyagusa maisha yako. Paulo anatuambia kuwa, tunapaswa kuiheshimu Serikali katika nchi tunamoishi, hata kama ni mbaya. Hili lina maana kuwa, ni lazima tuviheshimu vyombo vya dola (Warumi 13:1-5). Hili linahusu pia kulipa kodi kiuaminifu (ms. 6,7).

Masharti muhimu mengine yanatoka kwa Yesu mwenyewe, katika Mathayo 25. Anatuambia hasa namna ya kuyaweka mafundisho yake katika matendo maishani mwetu (ms. 31-40). Ni muhimu sana kuyakumbuka maneno hayo.

Yesu anaongelea siku ya hukumu kuwa, katika siku hiyo, hatatupima sisi kulingana na mambo tuliyoyajua, bali kwa namna tulivyojitahidi kuyaweka aliyofundisha katika matendo katika maisha yetu. Kwa hiyo atakachoangalia ni jinsi tulivyoifanyia kazi Ukristo wetu.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## NEEMA YA MUNGU

## SOMO: Wafilipi 3

Tunavyokaribia mwisho wa kozi hii, inafaa tuyaangalie masomo yote na kukumbuka kile ambacho tumetaka kukipata. Tumeona kutoka katika Biblia kuwa, maisha mapya katika Kristo ni tofauti sana na maisha watu wanayoishi kabla ya kubatizwa. Ufuasi unataka kujizatiti kuufuata mfano wa Bwana Yesu Kristo, na anawataka watu wajipime kwanza kabla hawajafanya uamuzi wa kumfuata. Anasema:

“Maana ni nani katika ninyi, kama akitaka kujenga mnara, asiyeketi kwanza na kuhesabu gharama, kama anavyo vya kuumaliza? Asije akashindwa kuumaliza baada ya kuupiga msingi, watu wote waona wakaanza kumdhihaki, wakisema, Mtu huyu alianza kujenga, akawa hana nguvu ya kumaliza. Au kuna mfalme gani, akitaka kwenda kupigana na mfalme mwingine, asiyeketi kwanza na kufanya shauri, kwamba yeye pamoja na watu elfu kumi ataweza kukutana na yule anayekuja juu yake na watu elfu ishirini? Na kama akiona hawezi, hutuma ujumbe kutaka sharti za amani, mtu yule angali mbali. Basi, kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa wanafunzi wangu” (Luka 14:28-33).

Kuchagua kuwa mfuasi wa Bwana Yesu, ni uamuzi wa maana kuliko uamuzi mwingine wowote tunaoweza kuufanya katika maisha yetu ya sasa. Ni uamuzi utakaokuwa na matokeo kwetu kwa sasa, na katika enzi ya Ufalme unaokuja.

Mara nyingine watu wanakataa kufanya uamuzi wa namna hii kwa kuwa, wanasema hawawezi kuishi kulingana na inavyotakiwa. Hili linasikitisha sana. Ufuasi sio mzigo mzito tunaoubeba wakati tunapobatizwa; ni kinyume chake kabisa. Bwana Yesu ndiye anayetubebea mzigo mzito tunaoubeba kwa sasa. Mwenyewe anasema:

“Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsi ni mwenu. Kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi” (Mathayo 11:28-30).

Mfuasi anapobatizwa, hali ya ajabu ya uhuru na amani inamwingia katika maisha yake. Mizigo inayomvunja ya dhambi inakuwa amepokelewa; sasa anakuwa sehemu ya familia ya Mungu. Kwa lolote linalomtokea katika maisha haya, anajua Mungu amesema:

“Msiwe na tabia ya kupenda fedha; mwe radhi (‘mridhike’) na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa. Hata twathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiaye, sitagopa; mwanadamu atanitenda nini?” (Waebrania 13:5, 6).

Kujisikia kwa namna hii kunakuja, kwa sehemu, kutokana na kujitambua kuwa umekuwa huru mbali na dhambi. Ni karama inayotoka kwa Mungu; ni kitu kinachotokana na ukarimu wake. Hakitokani na kazi; sio malipo kwa namna yoyote. Ni kitu tunachokipata kwa neema tu ya Mungu. Paulo anasema:

“Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu, alituhisha pamoja na Kristo, yaani, tumeokolewa kwa neema.... Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu” (Waefeso 2:4-9).

Neno ‘neema’ (au ‘rehema’) ni gumu kulitafsiri. Hata hivyo tunatambua, linamaanisha ‘upendeleo’ wa namna fulani. Hatukustahili kuokolewa kutokana na dhambi zetu; ni upendeleo tunaofanyiwa. Wokovu unaotujea unatokana na upendo wa Mungu ambao ni mkubwa kwetu; tunaokolewa kwa neema iliyopo katika upendo huo. Hakuna wokovu bila ya imani katika hiyo neema.



Neno 'neema' tunalikuta kwa mara ya kwanza, katika maisha ya Nuhu: "Lakini Nuhu akapata neema machoni pa BWANA" (Mwanzo 6:8).

Tugundue hapa ya kuwa, Nuhu **alipata** neema. Kinachomaanishwa hapa ni kwamba, neema ni kitu tunachopaswa kukitaka (au kukitafuta). Kwa hiyo, sio kitu kinachopatikana tu hivi-hivi. Hili ni jambo alilolielewa vizuri mtume Yohana, kwenye Injili yake anafundisha kuwa, tunaipata neema hasa tunapouangalia mfano wa Bwana Yesu Kristo:

"Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama kwa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli" (Yoh. 1:14).

Yesu mwenyewe aliwaambia Wayahudi wenzake:

"Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia. Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima" (Yoh. 5:39, 40).

Tunaipata neema; huo upendeleo tusioustahili kwa Bwana Mungu, tunapolisoma Neno lake, na zaidi tunapoyaangalia maisha ya Bwana Yesu Kristo, na kumwona mtu huyu aliyekuwa kweli na huruma, aliyejua rehema, aliyekuwa tayari kufa kwa ajili ya wengine.

Tunajua kuwa Sauli wa Tarso alikuwa adui mkubwa wa waliokuwa wafuasi wa Bwana Yesu. Alishiriki katika kifo cha Stefano; aliyekuwa mfuasi wa kwanza wa Yesu kuuawa kwa ajili ya imani yake. Sauli alitaka kuzivunja eklesia kwa kuwaweka wafuasi gerezani (Matendo 8:3). Tunaambiwa katika Matendo 9 jinsi alivyopanga safari ya kwenda Dameski kutoka Yerusalemu, ili aweze kuwakamata wafuasi waliokuwa huko.

Alipokuwa safarini, Yesu aliyefufuka alimtokea, na mchakato ukaanza, kwa mamlaka na utukufu kumbadilisha Sauli, na kuwa mtume Paulo tunayemfahamu. Paulo alitiwa upofu katika jambo hili, baada ya hapo Yesu akamwelekeza kuendelea mbele kwenda Dameski. Akiwa huko aliunganishwa na mfuasi mmoja aliyetitwa Anania, aliyempa kuweza kuona tena; na ikawa kuona kweli-kweli. Neno linasema:

"Anania akaenda zake, akaingia mle nyumbani; akamwekea mikono akisema, Ndugu Sauli, Bwana amenituma, Yesu, yeye aliyekutokea katika njia uliyojia, upate kuona tena, ukajazwe Roho Mtakatifu. Mara vikaanguka machoni pake vitu kama magamba, akapata kuona, akasimama, akabatizwa" (Matendo 9:17, 18).

Kuna mawazo mengi ya kuvutia katika taarifa hii. Hebu ona vile neno la kwanza kabisa analosema Anania kwa Paulo linavyokuwa, 'Ndugu'. Huyu ni mtu ambaye alikuwa akija Dameski kuwatia nguvuni Anania na wafuasi wengine! Lakini, Anania anajua kuwa Yesu amemwita awe mfuasi, na kwa hiyo, kwa kuwa anakuwa mshirika katika familia ya Mungu, ni 'ndugu' katika Kristo kwa Anania.

Neno 'ndugu' kwa kawaida, kiimani, ni kwa ajili ya wale tu waliobatizwa. Hapa Anania analitumia kwa kuwa amepata ufunuo wa moja kwa moja kutoka kwa Mungu juu ya Paulo. Na inaelekea, upofu wa Paulo ulipokuwa ukimwondoka, mtu wa kwanza wa kumwona mbele yake alikuwa Anania, aliyemfanyia muujiza huo. Jina Anania maana yake ni, 'Mungu amekuwa wa neema'.

Kwa hiyo kitu cha kwanza Paulo alichokiona kilikuwa ni mtu huyu, aliyekuwa akisimama badala ya 'neema' ya Mungu! Paulo alielewa sasa ya kuwa, angeweza kuokolewa kutokana na dhambi zake **kwa neema tu** kwa kuwa, sio kwamba alikuwa amewezeshwa kuona tena kwa macho yake tu, ila kuona mambo yalivyo kiroho pia. Hili lilipomtokea, jambo la kwanza lilikuwa kubatizwa.

Tunaambiwa na Paulo kuwa, baada ya hapo alipata matatizo alivyokuwa akisafiri kuihubiri Injili. Alikuwa na maumivu yaliyokuwa yakimpa shida katika kutembea. Alimwomba Mungu mara tatu amwondolee tatizo hilo, lakini jibu la Mungu kwake lilikuwa:

"Neema yangu yakutosha, maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu" (2 Wakor. 19:9).

Inawezekana Mungu alikuwa akimtaka Paulo amkumbuke Anania, na jinsi alivyopewa kuona sawasawa mambo kiroho. Katika mazingira yote Paulo alitakiwa kuukumbuka upendeleo asioustahili alioupata, umpe nguvu ya kuweza kukabiliana na changamoto zote za kimaisha na za ufuasi. Baadaye, akiwa amefungwa, aliweza kuandika akisema:

“Zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu, ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nimpate Kristo; tena nionekane katika yeye, nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani; ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake, ili nipate kwa njia yoyote kuufikia ufufuo wa wafu” (Wafilipi 3:8-11).

Alikuwa ni mtu aliyeacha kazi yake, marafiki, mali, madaraka na afya, kwa ajili ya Bwana Yesu. Anatuambia, vitu hivyo havikuwa na maana yoyote tena kwake. Tunaelewa hapa kuwa, ujasiri alioupata Paulo kwa kuielewa ‘neema ya Mungu’, alibakia nao kwa maisha yake yote. Sehemu ya maneno yake ya mwisho aliyoandika yanatuambia hili:

“Kwa maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa, nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa, tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na mwokozi wetu, ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomoe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema” (Tito 2:11-14).

Kwa neema, kama Anania alivyomtokea Paulo, ndivyo ambavyo Mungu amekuwa wa neema pia kwetu. Tumemjua Bwana Yesu Kristo, ambaye katika yeye tumepata neema.

Tunamshukuru Mungu kwa mambo haya yanayojaza mioyo yetu, na kutupa nguvu katika jitihada yetu ya kumfuata Bwana Yesu, kama wafuasi wake wa kweli. Ni neema ya Mungu tuliyopewa, inayotunesha namna ya kuishi na namna ya kusema na wengine, ili tuweze nasi kuwa watu wa neema kwa wengine (Wakolosai 4:6).

Tunajua ya kuwa mara nyingine tutashindwa, lakini tunajua pia kuwa, kama tukizikiri dhambi zetu kwa Bwana Mungu, yeye ni mwaminifu na wa haki wa kutosamehe. Hatuna nguvu au uwezo, hatuna haki iliyo ya kwetu wenyewe mbele ya Mungu. Ni neema yake inayotufundisha kugeuzia migongo maisha haya, na kumfuata Bwana Yesu Kristo tukiwa ni wanafunzi wake. Ni neema yake inayotufanya tupende kufanya lililo sahihi na ndiyo itakayotuleta kwenye Ufalme wake:

“Yeye mwenye kuyashuhudia haya asema, Naam, naja upesi. Amina; na uje, Bwana Yesu. Neema ya Bwana Yesu na iwe pamoja nanyi nyote. Amina!” (Ufunuo 22:20, 21).

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

## MUHTASARI WA MAFUNDISHO YA BIBLIA

**1. Injili**

Hii ni Habari Njema inayohusu Ufalme wa Mungu utakaoanzishwa hapa duniani, Yesu akirudi. Ni ujumbe unaopatikana katika Agano la Kale na Agano Jipya. *Mwanzo 22:17, 18*  
*Mathayo 4:23*

**2. Biblia ni Neno la Mungu**

Waandishi wote 40 wa vitabu 66 vya Biblia waliandika waliyoandika kwa kuongozwa na Mungu. *Zaburi 68:11*  
*2 Petro 1:21*

**3. Mungu ndiye aliyeiumba dunia**

Kila kitu katika dunia kiliumbwa na Mungu kwa manufaa ya wanadamu, kwa lengo la dunia kuweza kujazwa na Utukufu wake. Yesu Kristo ni msingi wa lengo hilo la Mungu. *Mwanzo 1:1*  
*Hesabu 14:21*  
*Zaburi 103:8-11*  
*Isaya 45:18*

**4. Yesu atarudi duniani**

Yesu alikuja miaka 2000 iliyopita kuihubiri Injili na kutoa uhai wake akiwa kama “Mwana-kondoo aliyechinjwa tangu kuumbwa kwa ulimwengu”. Kwa sasa yupo mbinguni, lakini atarudi na kuwa Mfalme wa dunia. *Mathayo 25:31-34*  
*Matendo 1:10-11*  
*Matendo 3:20, 21*  
*Ufunuo 22:20*

**5. Kurudi kwa Yesu kuko karibu sana**

Unabii wa Biblia unaendelea kutimia na kuna ishara nyingi leo kuwa, kuja huko kwa Yesu kumekaribia sana. Mifano: Wayahudi na uwepo tena wa Taifa la Israeli; kuporomoka kwa maadili; ugaidi; njaa; magonjwa na matetemeko ya nchi. *Luka 21:10-11*  
*Luka 21:24-33*  
*2 Timotheo 3:1-5*

**6. Ufalme wa Mungu utakuwa duniani**

Huu ni ujumbe wa msingi katika Biblia. Ufalme tunaouomba katika ‘Sala ya Bwana’ utakuwa na makao makuu yake katika Yerusalemu, Israeli, ambapo Bwana Yesu atatawala kwa miaka 1000 juu ya mataifa yote kwa amani. Baada ya hapo hapatakuwa na dhambi na mauti tena duniani. *Yeremia 3:17*  
*Mika 4:1-8*  
*Ufunuo 11:15*

**7. Mungu alitoa Ahadi kwa Ibrahimu**

Kwa sababu ya utii wake wa kiimani, Ibrahimu alipewa ahadi na Mungu kuwa, yeye na familia yake wataimiliki nchi ya Kanaani (Israeli), na kwamba mmoja kati ya uzao wake (Yesu), atakuwa Mfalme wa dunia. *Mwanzo 12:1-3*  
*Mwanzo 15:5-6*  
*Mwanzo 22:15-18*  
*Wagalatia 3:8,16,29*

**8. Wayahudi ni Watu wa Mungu**

Waliwekwa wawe mashahidi juu ya uwepo wa Mungu na uweza wake. Lakini hawakumtii, kwa hiyo walitawanywa duniani mwote. Biblia ilitabiria kuwa, katika ‘siku za mwisho’ watarudi tena katika nchi ya Israeli. *Isaya 11:11, 12*  
*Isaya 44:8*  
*Ezekieli 37:21-22*  
*Warumi 9:3-5*

- 9. Yerusalemu itakuwa ni Makao Makuu ya dunia**  
 Yesu alikuwa Myahudi. Wengi kati ya uzao wa Kiyahudi uliomsulubisha utamkubali kama Masihi (Mwokozi) wao. Yerusalemu utakuwa Makao Makuu ya Ufalme wa Mungu, na Israeli itakuwa 'kichwa cha mataifa yote'. Wasafiri kutoka katika kila nchi watakuwa wakienda Yerusalemu kuabudu.  
*Yeremia 3:17*  
*Mika 4:1-2*  
*Zekaria 14:16*  
*Mathayo 5: 34-35*
- 10. Mungu alimpa Daudi ahadi**  
 Mfalme Daudi aliambiwa kuwa, angekuwa na mzao (mwana) ambaye angekaa katika Kiti chake cha Enzi milele. Huu ni unabii uliokuwa ukimhusu Yesu.  
*2 Samweli 7:12-16*  
*Luka 1:30-33*
- 11. Yesu ni Mwana wa Mungu**  
 Alizaliwa kwa uweza wa Roho Mtakatifu na mama yake, Mariamu. Kwa namna hii alikuwa ni 'Mwana wa Mungu' na pia 'mwanadamu'. Yesu alisema wakati wote kuwa, Baba yake (Mungu) alikuwa ni mkubwa kuliko yeye. Hakuna tunapoambiwa kwenye Biblia kuwa Yesu alikuwa ni Mungu.  
*Mathayo 1:20-25*  
*Yohana 14:28*  
*Warumi 1:3-4*  
*Wagalatia 4:4*
- 12. Yesu hakutenda dhambi**  
 Ingawa alikuwa mwanadamu, Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, na kwa hiyo aliweza kuyashinda majaribu yote na kuishi maisha makamilifu. Aliweka kielelezo kwa ajili ya wafuasi wake wote.  
*Isaya 53:5, 12*  
*2 Wakorintho 5:21*  
*1 Petro 2:22*
- 13. Yesu alikufa msalabani kwa ajili yetu**  
 Ilikuwa ni lazima afe kama inavyokuwa kwa watu wote, kwa kuwa alikuwa uzao wa Adamu kama sisi sote. Lakini kwa kuwa hakutenda dhambi, alikuwa dhabihu kamilifu katika kufa kwake. Kwa sababu hii ameweza kuzichukua dhambi za wale 'wanaokufa naye' kwa njia ya ubatizo.  
*Yohana 1:29*  
*Yohana 3:16*  
*Wagalatia 1:4*
- 14. Yesu alifufuliwa kutoka kaburini**  
 Kwa kuwa hakufanya dhambi, kaburi halikuweza kumng'ang'ania. Mungu alikuwa sawa kumrudishia uzima mtu huyu mmoja pekee aliyekuwa wa haki. Kwa kufufuka, Bwana Yesu Kristo ni 'limbuko' la waliokufa (tunda la kwanza la waliokufa). Huu ni uthibitisho wa kwamba wale walio katika Kristo, watafufuliwa kutoka kwa wafu, atakaporudi.  
*Matendo 2:24*  
*Matendo 17:31*  
*1 Wakor. 15:22-23*
- 15. Roho Mtakatifu ni uweza wa Mungu**  
 Uweza wa Mungu unaonekana kwa yale yote aliyoumba. Mungu anapoitumia Roho yake kwa kusudi maalumu, uweza wake huo unaitwa 'Roho Mtakatifu'. Roho Mtakatifu sio kitu kilicho nje ya Mungu; kilicho na uweza wa kufanya kazi chenyewe; sio nafsi. Ni uweza wa Mungu ule ule. Neno sahihi zaidi lingekuwa Roho Takatifu (Holy Spirit), na sio Roho Mtakatifu. (Herufi 'M' inaleta kufikiri kama ni nafsi, visivyo).  
*Isaya 61:1-3*  
*Luka 1:35*  
*Matendo 10:38*  
*2 Petro 1:21*

**16. Mshahara wa dhambi ni mauti**

Kifo ni adhabu inayotupata wanadamu wote kwa sababu ya dhambi. Tangu Adamu amkiuke Mungu kwa kutomtii mwanzoni, watu wote wameangukia kwenye dhambi (tukimwacha Yesu), na kwa hiyo wote tunakufa. Wanaume kwa wanawake, wote wataishia makaburini kama hawakulifahamu kusudi la Mungu na kuuitikia mwito wa Injili.

*Mwanzo 3:17-19*

*Warumi 5:12*

*Warumi 6:23*

**17. Karama ya Mungu ni uzima wa milele**

Uzima wa milele sio malipo; hakuna anayeweza kuustahili. Lakini Mungu, kwa upendo wake ameahidi kuwapatia huo wale wanaoliamini Neno lake, wanaoweka matumaini yao katika Bwana Yesu na kujitahidi kuyafanya mapenzi yake.

*Yohana 17:1-3*

*Warumi 2:6-8*

*Warumi 5:1-5*

*Warumi 6:23*

**18. Kutakuwa na ufufuo wa wafu**

Lakini sio kila mtu atafufuliwa. Yesu atawatoa makaburini wale tu waliopata fursa ya kuweza kuuitikia ujumbe wa Injili kwa ajili ya wokovu wao.

*Yohana 5:28-29*

*1 Wakorintho 15:12-19*

*2 Timotheo 4:1*

**19. Kutakuwa na hukumu**

Wale wote waliouelewa wito wa Injili, ni lazima watasimama mbele ya Mfalme atakaporudi duniani, ama kuadhibiwa kwa mauti ya pili (na ya mwisho), ama kukirimiwa uzima usio na mwisho. Kutakuwa pia na hukumu kali kwa watu wa dunia watakaompinga Yesu katika kurudi kwake.

*Danieli 12:1-2*

*Yohana 5:28-29*

*2 Wakorintho 5:10*

*2 Wathesalonike 1:7-9*

**20. Uzima wa milele**

Wale watakaopatiwa uzima wa daima watapata fursa ya maana sana ya kumtumikia Bwana Yesu duniani, na chini yake watawatawala watu wengine (watu wa dunia ambao hawajapata uzima huo; watu wanaokufa). Watu hao hatimaye watakufa na kufufuliwa tena kwa hukumu mwishoni mwa miaka 1000 ya Ufalme wa Mungu. Watakatifu (wale waliopewa uzima wa milele) wataifurahia afya bora kabisa na kila kitu, wakati wakiihubiri 'Injili ya milele' na kuifanya dunia kuwa mahali pazuri kabisa pa kuishi kwa kila mtu.

*Zaburi 37:9-11,22*

*Danieli 7:27*

*Ufunuo 20:4-7*

**21. Malaika ni Watumishi wa Mungu**

Mungu aliumba malaika wawe watumishi wake anaowatuma milele. Hawafi na wanatekeleza maagizo ya Mungu kama yalivyo, katika ulimwengu wote. Wanawachunga pia wale katika dunia walioitwa na Mungu kuwa 'watakatifu' wake.

*Kutoka 23:20-21*

*Zaburi 103:20*

*Waebrania 1:13, 14*

**22. Ibilisi na Shetani**

Katika Biblia 'ibilisi' ni neno lililotumiwa kuelezea nguvu ya dhambi iliyopo ndani ya watu wote. Wote wanaoyapinga mapenzi ya Mungu mara nyingine wanaitwa 'shetani'. Hakuna kitu katika Biblia kinachohusu uwepo wa malaika mwovu nje ya mtu, anayemfanya mtu akosee.

*Mathayo 16:23*

*Yohana 8:44*

*Matendo 10:38*

*Yakobo 1:14*

**23. Sisi sote tunapaswa kutubu**

Mungu anatutaka tuzitambue dhambi zetu, tuzijutie, tutubu na tujitahidi kuishi maisha ya kuikataa dhambi. Hatuwezi kuwa na tumaini la wokovu mpaka tuwe tumefanya hili. Maisha ya toba ni maisha mapya ya kumfuata Yesu; maisha ya kupingana na dhambi.

*Zaburi 51:1-10*  
*Mathayo 4:1-7*  
*Luka 13:1-5*  
*Matendo 3:19*

**24. Ubatizo wa mtu mzima kwenye maji**

Huu ni wa muhimu sana, lakini ni lazima tuelewe na kuyaamini mafundisho ya Biblia na amri za Yesu Kristo kabla hatujataka kubatizwa. Ubatizo ni ishara ya kufa pamoja na Kristo kwa ajili ya dhambi zetu, na kufufuka tena kwa ajili ya maisha mapya.

*Mathayo 28:19-20*  
*Marko 16:16*  
*Matendo 2:38*

**25. Wakristo hawapambani**

Mfuasi wa Kristo hawezi kutumia nguvu au kujiunga na huduma za kijeshi au za kipolisi. Ni sharti awapende maadui zake kama anavyowapenda rafiki zake.

*Mathayo 26:52*  
*Luka 6:27-29*  
*Luka 22:25*  
*Warumi 13:1-2*

**26. Ndoa ya Kikristo**

Biblia iko wazi kabisa kuwa, Mungu alimkusudia mwanamume awe na mke mmoja, na kwa pamoja wailee familia yao katika njia za Mungu. Kwa sababu hii, Mkristo hapaswi kutengana na mwenza wake.

*Mwanzo 2:21-24*  
*Mathayo 19:3-6*  
*Waebrania 13:4*

**27. Wajibu wetu kwa Taifa**

Wakristo wanazitii sheria zote za nchi zao, mpaka zinapokuwa zikipingana na amri za Mungu. Kwa kuwa wao ni raia wa Ufalme wa Mungu unaokuja, hawawezi kuutoa muda wao na nguvu zao kwa siasa za serikali yoyote ya kidunia. Mkristo akifanya hivyo anaweza kujikuta akipingana na Mungu.

*Mathayo 22:21*  
*Warumi 13:1-7*  
*1 Petro 2:17*

**28. Wakristo wanaweza kuomba msamaha wa dhambi zao**

Hii ni fursa ya bahati ya kipekee ya kuwa katika Kristo (yaani, ya kuwa umebatizwa). Bwana Yesu yuko mbinguni, akiwa Mpatanishi kati ya wafuasi wake na Mungu; akimwomba Mungu asamehe udhaifu wao.

*Wafilipi 4:6*  
*1 Timotheo 2:5*  
*Waebrania 7:24-26*  
*1 Yohana 1:9*

**29. Kusoma Biblia kila siku ni muhimu**

Kusoma Biblia ni kama kula; ni kitu cha kila siku. Mwenyezi Mungu anasema nasi kupitia katika Neno lake. Tunajifunza kutoka katika mifano ya Kimaandiko, ambapo kuna vifungu na mistari inayotufaa kwa matatizo yetu na mahitaji yetu.

*Zaburi 119:89-112*  
*Matendo 17:11-12*  
*2 Timotheo 3:16-17*

**30. Ushirika na kifo cha Yesu**

Wakristo-wa-kweli wanakikumbuka kifo cha Bwana Yesu kwa 'kumega mkate' na 'kunywa divai' kila juma, kama Yesu alivyoagiza katika chakula kile kwenye chumba cha juu. Kumbukumbu hii ina ahadi kwa wafuasi wake, ya kula pamoja naye katika Ufalme wa Mungu.

*Marko 14:22-25*  
*Luka 22:14-20*  
*1 Wakorintho 11:23*

### **31. Ushirika wa Kweli**

Hiki ni kitu kinachowaleta pamoja wale tu walioamini, wanaotaka kuyafanyia kazi mambo ya kweli waliyojifunza kwenye Biblia, yaliyofundishwa na Bwana Yesu na wanafunzi wake, katika karne ya kwanza. Wakristadelfia wanao ushirika wa hali hii na maelefu ya ndugu zao waliopo katika nchi nyingi duniani.

*Yohana 17:16-18*  
*Matendo 2:41-42*  
*Waebrania 10:24-25*

### **32. Wito wa Injili**

Mungu anawaita watu kutoka katika mataifa yote wamfuata Yesu na kujiandaa kwa ajili ya Ufalme wake unaokuja.

*Mathayo 16:24-26*  
*1 Wakorintho 1:26-27*  
*Wagalatia 3:27*  
*Matendo 15:14*

**Je, utaupokea wito huo?**

**Mstari wa mwisho wa kujifunza:** Matendo 17:30-31

“Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu. Kwa maana, ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu”.

## MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA

### HATUA INAYOFUATA

#### SOMO: Matendo 2

Imekuwa ni furaha kushirikiana nawe katika kozi hii ya kujifunza Biblia. Kwa sasa tumefikia mwisho wa masomo haya, na pengine unajiuliza: Nini kinafuata, au kitu gani nifanye? Kabla hatujajaribu kukusaidia kwa maswali haya, ni muhimu kukumbuka kozi hii ni kwa ajili ya nini. Tumekuwa tukikuonesha mafundisho ya msingi ya Biblia.

Lakini ujumbe unaoupata kwenye masomo haya, haukuwa ujumbe wetu. Kila wakati ulipofunua na kuisoma Biblia yako, ulikuwa ukilisikiliza Neno la Mungu. Hivi ndivyo Mungu anavyowafundisha wanawake kwa wanaume juu yake mwenyewe, na kusudi lake kwa dunia hii. Ni kwa kuwa ulikuwa ukiliheshimu Neno la Mungu, ndio maana amekuwa akiongea nawe na akitegemea umwitikie.

Biblia yote ni Neno la Mungu; ni neno la pumzi yake, na lina nguvu ya kuweza kuyabadili maisha yako. Kama kwa kukuhubiria Injili kupitia katika kozi hii tumeweza kukusaidia, kwa kukufanya kuyaangalia Maandiko kwa undani mwenyewe, basi tumefanikiwa na tunashukuru.

#### Masomo haya yamekugusa?

Unaweza ukawa umejifunza mambo kadhaa ambayo hukuyajua kabla. Utakuwa umewafikiria ‘wakuu’ kama Ibrahimu na Daudi, na kuona vile ambavyo:

- ✚ Injili inavyopatikana katika Agano Jipya na pia katika Agano la Kale.
- ✚ Wayahudi walivyo mashahidi wa Mungu kati ya mataifa.
- ✚ Bwana Yesu Kristo alivyozaliwa na kuishi ili kuwaokoa wanaume na wanawake wanaomwamini.
- ✚ Kifo na ufufuo wa Yesu vinavyotoa uthibitisho wa mpango wa Mungu kwa nyakati zijazo.
- ✚ Bwana Yesu Kristo atakavyorudi duniani kuusimamisha Ufalme wa Mungu.

Lakini kuyafahamu mambo haya sio kitu kinachotosha kwa chenyewe. Tunajua, wapo watu wengi tu wanaokwenda katika vyojo kujifunza dini ili kupata vyeti, au kupata ajira na kuwa wachungaji, lakini hili haliwafanyi kuwa Wakristo. Ukristo pia sio jina; hakuna anayekuwa Mkristo mbele ya Mungu kwa sababu ya jina watu wanalomwita. Jumua yetu ya Kikristadelfia haitoi vyeti, diploma au digrii kwa kuifahamu Biblia. Tunaihubiri tu Injili kwa kuwa tunajua, Mungu anataka kuifikisha neema yake kupitia kwa Kristo, kwa wote wale wanaotamani kuokolewa na dhambi zao.

Mungu anamwalika kila mtu anayeweza kuipokea Njia yake ya Wokovu, kuwa na sehemu katika Ufalme wake unaokuja duniani.

#### Kuwa Mkristo kuna maana gani?

Wakristo-wa-kweli ni watu wanaoziamini ahadi za Yesu, na ambao wamechagua wabatizwe na kuishi maisha ya kumfuata, wakijiandaa kwa huduma pamoja naye atakaporudi kuwa Mfalme wa dunia.

Wakristo-wa-kweli ni watu walio tofauti na watu wengine kwa kuwa, wako katika kuitwa na kuandaliwa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu katika dunia. Muumba anao mpango mmoja tu na dunia yake, na namna ya kuuitikia wito wake na kushiriki katika mpango huo ni mmoja, popote pale tunapoishi duniani.

Mungu hana kanuni fulani-fulani kwa watu walio India, na nyingine kwa nchi za Kiarabu au Afrika au Amerika au visiwa vya Pasifiki. Yupo Mwokozi mmoja tu, na namna moja ya kuweza kuokolewa: Mtume Petro alisema:

“Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hakuna jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo” (Matendo 4:12).



### **Kwa nini Mekanisa ni mengi sana?**

Unaweza ukajiuliza: “Ni kwa nini, basi, kuna makanisa mengi sana na vikundi vingi vya kidini?”

Hili ni suala linalowapa mashaka watu wengi, wanapofikiria kujiunga na jumua yoyote ya ‘Ukristo’. Lakini ni hivi: sio Mungu aliyeyagawa makanisa katika Ukristo kuwa Wakatoliki, Waprostanti au Walokole. Kwa sehemu kubwa ni tamaa za watu waliopenda kuwavuta watu wawafuate kuanzisha makundi mpya, kulikoyafanya yawe mengi. Wengi walikuwa wajanja mno kuweza kusikiliza au kuyapokea mafundisho ya kawaida sana, tena ya kueleweka, yaliyopo kwenye Injili, kama yalivyofundishwa na Yesu na mitume wake.

Walifanya kile alichotabiria mtume Paulo, akisema: “Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima, ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi-makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti (masikio ‘yanayowawasha’), nao watajipusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo” (2 Timotheo 4:3, 4).

### **Mimi, Je?**

Wakati wa kuitafakari KWELI unakuja tunapoanza kuelewa kuwa, sisi wote ni wadhambi mbele ya Mungu na kwamba, ni Mungu tu, kupitia kwa Yesu, anayeweza kutusaidia: “Kwa sababu, wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu” (Warumi 3:23).

Lakini, Andiko linasema: “Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu” (Warumi 5:8).

‘Hatua inayofuata’ kwako itategemea haya mambo uliyojifunza kuhusiana na Neno la Mungu, yamekugusa kiasi gani. Sisi sote tupo katika njia ya kuutafuta wokovu, tunapokuwa tumeanza kuujuu ukweli unaotuhusu sisi wenyewe. Nabii Yereimia alisema:

“Ee Bwana, najua ya kuwa njia ya mwanadamu haimo katika nafsi yake; kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu” (Yer. 10:23).

Unajisikia hivyo, sijui? Neno la Mungu limeanza kukuvuta ufanye kitu, kuhusu kuutafuta Ufalme wa Mungu na haki yake? Kwa sasa au kwa baadaye, kila mtu anatakiwa aone haja ya kufanya mabadiliko katika maisha yake. Ni mabadiliko ya kuacha kuwa mtu anayeendelea tu na dhambi; yaani, kuwa katika Adamu tu, na kufa na kutokomea milele, badala yake kuwa ‘mtakatifu’ katika Kristo, mtu mwenye tumaini la ufufuo atakaporudi Yesu na uzima wa milele katika Ufalme wake.

Wanaume fulani katika Yerusalemu, walipokuwa wameanza kuelewa ukweli ulivyo, walichomwa mioyo yao: “Wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu?”

Jibu la Petro lilikuwa: “Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu” (Matendo 2: 37, 38).

Ni tumaini letu kuwa, utakuwa ukijifikiria kwa umakini. Unaweza ukawa bado na mashaka kidogo hapo ulipo; huhitaji mtu akusukume, na hatufanyi hivyo. Unahitaji muda kutafakari; tunalielewa hilo!

Pengine unaweza kuwa unataka kuendelea bado na kujifunza kwako Biblia kwanza, au kukutana na Wakristadelfia fulani na kuongea nao kwanza juu ya mambo haya. Unaweza pia ukawa umeyaridhia mafundisho haya na unataka kubatizwa.

### **Kuna ushauri hapa wa kukusaidia**

1. Tafadhali yapitie tena masomo yote, somo la 1 mpaka la 59, ukiandika kwenye karatasi ugumu wowote unaouona, na kuwekea alama mistari ya muhimu katika Biblia yako.

2. Mwandikie mkufunzi wako umwambie jinsi unavyojisikia juu ya mambo uliyojifunza katika Biblia. Uliyafurahia masomo? Kulikuwa na mada zilizokuwa ngumu kwako, na ungependa kupatiwa maelezo zaidi juu ya baadhi ya mada?
3. Tunategemea umekuwa ukitumia mpango wetu wa kusoma Biblia wa kila siku (Bible Reading Planner), na umepokea Mshirika wa Biblia (Bible Companion). Huu ni utaratibu wa kusoma angalau Sura tatu kwa siku, na utakuchukua kuimaliza Biblia yote kwa mwaka mmoja (Agano la Kale mara moja/ Agano Jipya mara mbili). Endelea kuisoma Biblia yako kila siku. Sio kitabu cha kusoma na kuweka mbali, na kama utaisoma mara kwa mara, itakugusa moyo, akili na maisha yako.
4. Utapenda uunganishwe na Wakristadelfia walioko karibu na wewe (kama wapo)? Unaweza ukapenda kuwaandikia au kuwapigia simu kama unaona inafaa, au hata kuwatembelea kwa majadiliano zaidi ya Biblia. Kama wapo karibu ya kutosha, ungependa kuhudhuria baadhi ya mikutano yao?
5. Ungependa kupata masomo zaidi kuhusiana na Biblia? Kama ni hivyo mwandikie mkufunzi wako, umwambie unataka kujifunza zaidi juu ya nini. Tunavyo vijitabu na machapisho mengi ya maana sana kuhusiana na mada nyingi.
6. Kama unataka kuendelea mbele ubatizwe, lakini unajisikia kuhitaji muda zaidi wa kujifunza, tuna kozi zingine. Mwambie tu mkufunzi wako.
7. Kama unakubaliana na mafundisho yote uliyoyapata katika Kozi hii ya Biblia kwa Njia ya Posta na unafikiri kubatizwa, tuandikie utuambie.

#### **Unawezaje kubatizwa?**

Kama ulivyojifunza katika somo la 31, ni muhimu kuwa uielewe vizuri Injili. Ubatizo ni kitu kikubwa, ni vizuri utambue na kuyakubali mambo yanayoendana nao katika maisha yako kwanza. Ni jukumu letu kuhakikisha kuwa unaelewa hili kabla hatujakusaidia uweze kubatizwa.

Kwa hiyo kwanza tutakutumia maswali ya kujibu kwa Posta, maswali juu ya mafundisho ya msingi ya Biblia, na baadhi ya mambo ya kuzingatia kimaisha katika kuishi maisha ya Kikristo. Baada ya hili, kama utakuwa umefanya vizuri, tutapanga ili mmoja wetu au zaidi, kati ya waumini wenzetu akutembelee. Kama kweli umekuwa tayari kwa kubatizwa, mtapanga iwe wapi panapofaa, penye maji ya kutosha.

Kama kuna ndugu wa Kikristadelfia hapo jirani, utakuwa sehemu ya eklesia hiyo. Kama hakuna, bado tutahakikisha kuwa unapata wakati wote machapisho mbalimbali ya kusoma, na kama ni mengi utaweza kuwapa pia rafiki zako. Tutakutumia pia makaratasi ya mahubiri kwa ajili yako kuyatumia, katika Kumega kwako Mkate kila Jumapili nyumbani kwako. Ni mahubiri yanayoendana na masomo ya Jumapili kila mwezi, kwa walio kwenye upweke dunia nzima, kulingana na Mshirika wa Biblia.

Kama utakuwa umeamua kubatizwa, hilo litakuwa tukio la muhimu kuliko yote katika maisha yako. Kuwa Mkristadelfia ni kuzaliwa katika familia ya Yesu Kristo, yenye ndugu duniani pote, walio na imani moja na ushirika wa hali ya juu na wewe.

#### **Hatua yako inayofuata ni rahisi**

Mwandikie tu mkufunzi wako, uambatishe kuponi iliyokamilishwa utakayoiona pamoja na somo hili.

#### **MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA - KARATASI YA MWISHO YA MASWALI**

Jaribio hili la mwisho linauliza maswali kuhusiana na kozi yote. Tafadhali jibu sehemu ya A, B, C na D katika karatasi yako ya maswali kwenye nafasi zilizowekwa, na sehemu ya F katika karatasi nyingine tupu, na baada ya hapo utume majibu yako kwa mkufunzi wako. Usisahau kujaza jina lako, anuani, na namba yako ya kumbukumbu.

SEHEMU YA A: Jibu kwa neno moja- Ni nani?

1. Ni nani aliyeiumba dunia? .....
2. Ni nani aliyeumbwa kwa mavumbi ya nchi? .....
3. Ni nani aliyeahidiwa urithi wa nchi ya Kanaani? .....
4. Ni nani aliyepewa mwogozo wa kujenga Hema la Kukutania? .....
5. Ni nani aliyeahidiwa kupata 'mwana' atakayetawala badala yake katika Kiti chake cha Enzi? .....
6. Huyu 'mwana' (kwenye swali la nyuma) ni nani? .....
7. Yesu alimwita nani 'shetani'? .....
8. Yesu alimfufua nani kutoka kwa wafu? .....
9. Ni nani atakayeihukumu dunia? .....
10. Ni nani aliyewapa watu kuiandika Biblia? .....

SEHEMU YA B: Jibu kwa neno moja- Wapi?

1. Ibrahimu aliishi wapi mwanzoni? .....
2. Yusufu alifanywa kuwa mtawala wapi? .....
3. Musa aliipokelea wapi Sheria Mungu aliyowapa Israeli? .....
4. Kiti cha Enzi cha Daudi kilikuwa wapi? .....
5. Danieli alikuwa katika utumwa wapi? .....
6. Mlima Sayuni upo wapi? .....
7. Yesu alizaliwa wapi? .....
8. Yesu alibatiziwa wapi? .....
9. Kuzimu ni wapi? .....
10. Makao-makuu ya Ufalme wa Mungu unaokuja yatakuwa wapi? .....

SEHEMU YA C: Jibu kwa kifupi:

1. Taifa ambalo Mungu aliliteua liwe watu wake maalumu ni -----
2. Neno 'Injili' maana yake ni -----
3. Neema au Rehema ni -----
4. Kurudi kwa Wayahudi kwenye nchi yao wenyewe kunaashiria -----
5. Roho ni -----
6. Ahadi waliyotoa malaika Yesu alipokuwa akipaa kwenda mbinguni ni kwamba -----
7. Ubatizo ni -----
8. Ibilisi ni -----
9. Pepo ni -----
10. Roho Mtakatifu ni -----

SEHEMU YA D: Jibu kwa kifupi-Ni kwa nini:

1. Mungu aliiumba dunia? -----
2. Mungu aliigharikisha dunia siku za Nuhu? -----
3. Ibrahimu alibarikiwa na Mungu? -----
4. Tunahitaji kuisoma Biblia? -----
5. Wayahudi walichukuliwa utumwani? -----
6. Mungu aliruhusu Yesu afe msalabani? -----
7. Yesu alifufuliwa kutoka kwa wafu? -----
8. Tunafanya dhambi? -----
9. Karama/ Zawadi za Roho Mtakatifu zilitolewa? -----
10. Wakristo wanapaswa kuoana wenyewe kwa wenyewe? -----

SEHEMU YA E: Sema 'Ndio' au 'Hapana'.

1. Yesu alikuwapo wakati wa Agano la Kale? -----
2. Wakristo wanapaswa kujishughulisha na siasa? -----
3. Wakristo wanapaswa kuzipigania nchi zao? -----
4. Neno 'shetani' linaweza kutumiwa kuelezea watu wema? -----
5. Ufalme wa Mungu uliwahi kuwapo wakati wa Agano la Kale? -----
6. Karama/ Zawadi za Roho Mtakatifu kama kuongea kilugha, zipo leo? -----

7. Mungu na Yesu wako sawa? -----
8. Wakristo wanapaswa kuiadhimisha Sabato? -----
9. 'Utakatifu' una maana ya kujitenga? -----
10. Wakristo wanaruhusiwa kufanya ngono kabla ya kuoana? -----

SEHEMU YA F: Jibu kirefu (Tafadhali tumia karatasi nyingine).

1. Ni kwa nini waumini wa kweli lazima wabatizwe?
2. Kinachotutokea ni nini tunapokufa?
3. Nini kitatokea wakati wa hukumu?
4. Ni kwa nini Yesu ilibidi afe?
5. Kwa nini Biblia inazungumzia ibilisi?
6. Ufalme wa Mungu unaokuja utakuwaje?
7. Ni kwa nini Agano la Kale ni la muhimu?
8. Kwa nini ni muhimu kwa waumini waliobatizwa kukutana mara kwa mara Kumega Mkate?
9. Kwa nini ni muhimu kwa Wakristo wa Kweli kushiriki mkate na divai?
10. Dhambi zinawezaje kusamehewa baada ya kubatizwa?

Tuma majibu yako kwa: -----  
-----  
-----  
-----

Kumbukumbu yako ni namba: -----